*ME & YOU*1_6

Na
Mamuh mohd
(0716730000)

Tuanze..... SEHEMU YA 1

Assalam walleykum.... habari za wakati huu mpenzi msomaji wa mamuh na simulizi zake.

Alhamdulilah kiafya nipo salama hofu kwako wewe msomaji Wangu.

Kwa  furaha na bashasha nakukaribisha katika Simulizi hii nzuri ya kusisimua...inayowahusu wapendanao ambao walipambana kufa na kupona kupambania upendo wao wa dhati...Ilikuwaje ungana nami mtunzi wako maryam(mamuh) nikusimulie.

************

Ni katika familia ya Mr makuka aliekuwa Tajiri si haba,
Alikuwa ni baba mwenyewe watoto wawili Ambao walifuatana hawakupishana sana.
Kijana wake mkubwa aliitwa Hansy (24) na kufuatiwa na Mdogo alieitwa Erick (22)

Hawa walikuwa watoto wakishua Tokea kuzaliwa kwao hajui kitu kinachoitwa shida.

Siku hiyo Mr makuka alikuwa nyumbani na mkewe bibie Maina wakizungumza. Kubwa walikuwa wakizungumza biashara zao, walikuwa wakimiliki kiwanda cha utengenezaji wa vinywaji ivyo ni watu waliokuwa na jina jijini Daresalam.

"Mmewangu tumeishi hapa na vijana wetu hawa wakiume pasina Binti wa kike.
Natamani hansy   hata sasaivi afunge ndoa nipate mkamwana".

" Mhhh sijui ujue hansy yupo bize sana sio kama Erick ambae tushawahi hata kusika ana wanawake tokea anasoma wanamgombania.
ila hansy yupo  bize"
" Ni kutokana na hayo masuala analiyosomea mpaka sasa kaanza kazi mwanangu.
Yupo bize...ili akili yake itulie lazima apate mwenzake ndo itakuwa afadhali".
" Haya shida sio kuoa.. shida atamuoa nani? Maana wanawake Wengi sasa wana tamaa.
Kuona Matajiri watajileta kiurahis sana".
" Nililijua hilo Ndio maana tokea siku nyingi Sana nilikuwa nikiandaa mchumba kwa ajili ya kijana Wangu wa kwanza".

" Waoooo!!! Vizuri umemchagua nani? "
" Mhhh yupo Binti mrembo na msomi anaitwa Ester.
Anamaliza elimu yake ya masters mwaka huu huko India".
" Very intrest kwa hizo sifa tu zimeugusa moyo Wangu anaonekana anafaa.
Sikutamani eti kijana Wangu apate mwanamke wa uswahilini kina chausiku huko mala Shida sijui semeni".
" Hahaha jamani baba hancy una vituko sana...ni mtoto wa rafiki Yangu mama yake na mimi ni business partner tulikuwa mala nyingi tukienda china na uturuki pamoja"..
Walifurahi wazazi hao Maongezi yao yalikuwa mazuri.

ilikwenda mpaka usiku muda wa chakula wanafamilia wote walikuwa mezani.
Hancy alikuwa akizungumza na simu kuashiria kuna Safari anatakiwa kwenda.
" Ok wee kesho Asubuhi njoo hom tukutaneni na wengine tuende ni muhimu sana... Okay okay".
Kisha alikata simu Ndipo mama yake akamuuliza,
" Mhhh mnaenda wapi wenzetu".
" Mama tunaenda kufanya utafiti vijijini ni Muhimu kazini".
" Hongera sawa nenda ila ukirudi tuna mazungumzo na wewe".

" Sawa wazazi Wangu dua zenu katika Safari yetu hii".
" Kila la kheri ".

Waliendelea kula pale na kifurahi ilikuwa ni familia yenye upendo na furaha.

***********

Basi kweli siku iliyofuata waliungana hansy akiwa na wenzake wengine watatu ivyo jumla wanne wakaanza safari kuna utafiti wanakwenda kufanya vijijini.

Kijiji ambacho walidhamiria kwenda kwa mujibu wa ramani waliyokuwa wakiifuata ilikuwa ni safari ya masaa 7 Ndipo hatimae wakifika.

Waliacha gari sehemu ya Barabara na kubeba vitu vya muhimu kisha wakaendelea na safari.
Waliingia msituni Kabisa Ambapo mbele palikuwa na mto mkubwa walitakuwa kuuvuka Kisha Ndipo wafike mahali wakipotaka kwenda.

Jua mpaka lilizama wakiwa safarini hapo na hatiamae waliufikia mto huo.

Mmoja wapo alitoa ushauri kwamba walale Asubuhi Ndipo wavuke Mto... Kwa kuwa walikuwa na vifaa vyao watengeneze makazi ya mda mfupi".
" Ni kweli maana kwa Ramani inavyoonesha kweli tukivuka huu mto ndo tumefika hapo kijijini husika inaposadikika kuna watu wanaoishi tofauti na sisi tujue wanaishi vipi ".
" Sawa afadhali ili kesho tukivuka tukafanye kazi na tuwahi kugeuka".

Walikubaliana ivyo Ndipo wakakaa mahali na kufungua mabehewa yao ya lailoni kila mmoja alikuwa na la kwake lililomuwezesha kujiegesha.

Walikuwa na vyakula vyao wakala huku wakizungumza tu wala hawakupata hata lepe la usingizi.

Mpaka usiku ulipokuwa mkubwa kiasi saa 9 Ndipo walianza kusinzia na baadae usingizi wote uliwapitia.

*******

Palikwenda mpaka Asubuhi katika kijiji kilochofahamika kwa jina la mtakuja. Alikuwepo mfalme alieitwa mfalme mzota.

Huyu alikuwa kiongozi wao ambapo wanakijiji waishio hapo walikuwa wakimuheshimu sana.

Basi mala walinzi wa mfalme walifika na kumpa taarifa,
" Mfalme Vane ametoroka na kijakazi wake haijulikani alipo".
" Ujinga gani huo mnaniambia haraka kamtafuteni kabla hajavuka mto akatoroka".

Kweli walinzi waliamza mchaka mchaka kumtafuta Binti Ambae aliitwa Vane haijulikani kwa Sababu zipi lakini ilibidi wamkimbilie kumtafuta.

Upande wa vijana wanne akiwemo Hansy Asubuhi hiyo walianza kuvuka mto.
Mto ulikuwa una kina kirefu sana.

Kadri walivyozidi kutembea Ndipo maji yaliwazidi na kuwa mengi.

Hansy alielemewa Zaidi kuliko wenzie kwani ndie alikuwa mwanzo.
Mala alijikuta amesombwa na maji yale Ndipo wenzake wakashtuka lakini hakuna Ambae angeweza kumsaidia kwani na wao walikuwa katika hali Mbaya.

Waliishia kushuhudia Hansy akiondoka Ndipo na wao kwa uwoga ikabidi warudi kunusuru nafsi zao.

Hansy alijikuta anakunywa maji ya kutosha alilegea kabisa huku akiwa anapelekwa mbali.

Ndipo mala alishtukia amenasa mahali. Hakuwa amenasa tu bali alipogeuka aligundua kuna msichana mrembo Ndie aliemshika.

Hansy ilibidi nae amkamate vizuri msichana yule Ambae alionekana hodari katika masuala yale ya maji. Binti Alirudi nae Hansy mpaka nchi kavu lakini wakiwa Upande mwingine sio ule ambao Waliokuwepo wenzake na hancy.

Binti kufika alimlaza hansy na kuanza kumkamua kamua Maji ili yatoke.
Ndipo hansy walau alipata afuheni akafumbua macho yake vizuri na kujionea uumbaji wa Mungu.

Msichana yule mrembo baada ya kumuona hansy kaamka Ndipo akawa anaondoka zake lakini hansy akamvuta mkono Binti mpaka akaanguka na kumuangukia Hansy.

"Samahani unaweza kuniruhusu niondoke nafuatwa watu wale pale wakiniona watanichukua".
"Sijapata muda wa kukushukuru asante sana unaitwa nani? Hatokuchukua mtu bila kuongea na mimi".

Kabla Binti yule hajajibu Ndipo mala gafla akaona walinzi Kutoka himaya yao Wakiwa wanavuka mto ule Binti akaona akifanya masihara atakamatwa Ndio alitoka  mbio kuelekea kule msituni kutafuta namba ya kujificha wasimkamate.

Hansy nae alijikaza kiume akainuka na kumfuata mrembo yule kule alipoelekea inamaana hawakuwa wameachana mbalimbali Ivyo alikaza buti mpaka akamfikia.

"Nisikilize mimi kukutorosha hapa wasikuone maisha yao yote wala sio shida lakini niambie wanataka Nini kwako?"

"Ndoa.... Hii ni familia yangu wanataka niolewe na kaka yangu ili ukoo usiende mbali.

Baba yangu Ndie mfalme na ndugu zetu wengine wapo huko ni ukoo wetu tunaishi peke yetu na mila Ambazo sizipendi".

"Sawa umenisaidia nami naomba nikusaidie ila hautaonana na hawa ndugu  zako"

"Nipo Tayari sitaki kabisa".

Hansy Ndipo alimshika mkono mrembo yule Ambae aliitwa Vane na kufuata njia Upande mwingine.

Vane pia alikuwa hodari katika suala la mbio ivyo hakumuangusha hans, walifanikiwa wote  kukimbia msituni mule.

ilikuwa Asubuhi ikaenda mpaka Jioni Ndipo walinzi walirudi katika himaya yao ya mfalme mzota.
"Mfalme tumetafuta siku nzima lakini hatujamuona vane"
"Mnaongea upuuzi gani?!! Kwanini kwanini ujinga huu Binti Yangu lazima apatikane nitamtafuta pande zote nne lazima apatikane hakuna kulala namtaka Binti Yangu".

Alikasirika Mfalme watu wote waliitwa na kuamuriwa kuwasha moto Safari kumtafuta Vane Binti wa mfalme.

Upande wa mjini sasa nyumba  Mr makuka usiku huo walifika wale marafiki zake na Hansy ambao alikwenda nao safari.
Kufika walielezea hali halisi kuwa hansy alisombwa na maji na hawakumuona hawajui kama atakuwa mzima au laa".

Mama hansy aliangua kilio, Mr makuka alichanganyikiwa familia yote iliingiwa na hofu, Simanzi wakijua fika kijana wao atakuwa katika hali Mbaya.....

Siijui itakuwaje?

Tukutane sehemu ya 2*ME & YOU*

Na
Mamuh Mohd
(0716730000)

SEHEMU YA......... 2

Tuliposhia......

Mama hansy aliangua kilio, Mr makuka alichanganyikiwa familia yote iliingiwa na hofu, Simanzi wakijua fika kijana wao atakuwa katika hali Mbaya.....

SONGA NAYO......

Erick Mdogo wake na Hansy alikuwa mkali, akaanza kuwakalipia wale marafiki zake na Hansy,

"Na nyinyi mlikuwa wapi mpaka mwenzenu anapatwa na matatizo au ndo mlienda kumtoa kafara ili mpandishwe cheo?".

Baba yao Mr makuka ikabidi amtulize Erick kubwa akawaomba vijana wale wawapeleke hiyo Sehemu Ambayo kijana wao inasadikika amepotelea hapo.

Vijana hao walikubali lakini wakaomba kwanza na wao walifike makwao Kisha pakipambazuka wataweza kwenda na wafuatane na polisi kwa ajili ya uchunguzi.

Mama Hans alilia jamani mpaka majirani zake Walifika na kujaribu kumfariji.
"Hansy Wangu haijulikani hali yake jamani uwiiiii mwanangu hansy jamani eeeeh awe mzima jamani mwanangu mimi?".
Hakika yalikuwa ni maumivu ya aina yake.

Basi palikwenda mpaka Asubuhi Ambapo polisi walifika nyumbani kwa Mr makuka na wale vijana wenzake Tayari kwa kuanza safari kuelekea kijijini kule katika msitu wenye mto Ambapo Ndipo Hansy alisombwa na maji hapo.

Lakini wakiwa katika harakati hizo za kuanza safari mala getini aliingia Hansy akiwa na msichana yule vane.

Wote walishagaa hawakuamini.
Mr makuka na mkewe haraka walimkimbilia kijana wao na kumlaki kwa furaha.
"Hansy ohhhh Asante Mungu jamani hujui tu vile wazazi wako tulivyokuwa. Karibu mwanangu jamani tumeambiwa umesombwa na maji".

"Asante Wazazi Wangu  ni kweli Nimekumbana na hiyo dhoruba lakini ashukuriwe Mungu kwa kumtuma mja wake huyu msichana anaitwa  vane kanisaidia nipo salama wazazi Wangu".

Mama hansy alimtazama huyo msichana vane lakini kwa muonekano aliokuwa nao vane alijikuta anamnyari Pasina hata kumpa neno la shukurani.
Vane alikuwa amevalia  khanga tu juu na ingine amefunga chini yalikuwa ndio mavazi  waliyozoea kuvaa kwao.
Nguo za kawaida alikuwa akiziona kwa vijiji vingine majirani lakini sio familia yao waliojitenga.
Pia alionekana kabisa ni mshamba vitu kama vile kwake vilikuwa ni vya maajabu alibaki tu anashangaa.

Mr makuka Ndipo akamsogelea vane na kumuambia,

"Asante unaweza kusema nikulipe bei gani kwa kumsaidia kijana wangu".
"Hapana vane hajanisaidia kwa kutaka kulipwa baba na nimekuja nae hapa kuwaomba wazazi wangu akae hapa kwetu kwa muda nitawaeleza  kila kitu".

Mama hansy kusikia vile Ndipo akamtazama kijana wake.
" Hansy unaongea nini? Look.... Msichana haeleweki hata alivyo ukute ni mchawi kakusaidia kimazingaombwe ili apate nafasi ya kuja kutuangamiza hapa unajuaje? Usiamini watu kiurahisi baba... Wewe ni msomi kwanini unafanya haya? ".

" Mama.... Baba tafadhali naomba mnielewe katika hili huyu hayupo ivyo mnavyodhania nimejikuta namuamini Tafadhali".

Alikuwepo Erick Mdogo wake na Hansy Ndipo akajibu.
" Baba na mama mimi naona mnakuza mambo kumjadili mtu kama huyu tunauhitaji wa wafanyakazi hapa shida nini nadhani muhimu kaka amerudi salama hayo mengine si muhimu kwa sasa tutazungumza".

Hata hansy akakazia kwa kuwataka wazazi wake kwanza Kabisa wampokee vane pale nyumbani.

Basi Vane aliruhusiwa kubakia pale nyumbani huku waliagana na wengine waliokuwa wamejitokeza kisha wana familia wakaingia ndani kuendelea na mazungumzo yao.

Binti Vane alikuwa alishangaa jinsi nyumba ile ilivyokuwa nzuri. Mfanyakazi wa ndani pale alimkaribisha ndani Tayari kwa kunkirimu kama mgeni.

Hansy aliwaeleza Wazazi wake kila kitu kuhusu Vane hivyo akawaomba waishi nae pale nyumbani kama kulipa fadhila kwa wema alioufanya kwa kumsaidia Hansy.

Wazazi walikubali kwa kuwa lilikuwa ombi la Mtoto wao kwa vile alivyowaelezea.
Walimpa kazi mfanyakazi wao wa awali aleitwa mwasifa kumfundisha kazi Vane ili awe msaidizi Mwenzake pale nyumbani.

Mwasifa alikubali kupata mwenzake wa kusaidiana nae kazi na hata Hansy aliona sawa kubwa awe anamuona vane pale nyumbani.

***********

Basi maisha yaliendelea ambapo ilipita miezi kadhaa Vane alianza kuzoea mazingira ya mjini kule ivyo akawa nae hodari kwa kazi pale nyumbani ivyo akaozeleka.

Basi siku hiyo mama Hansy akiwa zake Nyumbani, alikuwa akisuguliwa miguu na bibie Vane Ndipo mala akapigiwa simu.
Aliempigia alikuwa ni Rafiki yake Ambae alionesha kufurahi kuzungumza nae. Waliongea na kucheka mpaka wakamaliza Ndipo akakata simu.

Alipomaliza kuzungumza na simu ile Ndipo akamuambia Vane.

"Mda wowote Hansy ataoa  uzuri nae amemaliza project yake iliyokuwa inampa ubize na huku mpenzi wake Ester amerudi hivyo weekend  watakuja hapa na mama yake aonane na Hansy".
"Ni vizuri mama".
"Yah naamini hansy atampenda maana ni msichana mrembo sana aiseee".
Vane alikuwa akiitikia tu Ndipo alipomaliza akatoka zake Kwenda jikoni kuendelea na kazi zake zingine.

Alikuwa amezoeana na yule msichana wa kazi mwenzake alieitwa mwasifa ivyo akamsimulia kila alichoambiwa na mama Hansy.

"Mwasifa kumbe Hansy ana mchumba wake anakuja hapa wiki hii mama kasema".
"Mhhh ndo nayasikia leo maana sikuwahigi kumjua mchumba wa kaka Hansy.
Ujue Hansy yupo serious sikuhisi hata kama atakuwa na mpenzi bola aje tumuone"
"Kwa kweli".
Waliendelea kupiga story zao pale huku kazi zikiendelea".

Majira ya usiku siku hiyo wanafamilia walikuwa Pamoja wamekaa Ndipo mama hansy akawapa taarifa za ujio wa Ester na atakuja nyumbani hapo weekend.

Mr makuka yeye alifurahi hata Hansy na Erick walidhania ni mgeni tu kama Wageni wa kawaida ivyo walionesha kufurahishwa na ugeni huo.

Baada ya mazungumzo hayo Ndipo Hansy alikwenda eneo la jikoni na kumkuta Vane akiwa anaosha viombo usiku huo.

"Bila shaka sasa umekuwa mwenyeji huku mjini japo nilikuacha kidogo kuna project iliniweka bize ila hatiamae nimamaliza sasa nipo free nitakutembeza uujue mji"
" Wala usijali Hansy natembeaga Mwasifa huyu huwa ananitembeza.

Kubwa nafurahi kukuona umerudi na nashukuru kwa kunikutanisha na Familia yako yenye upendo wakati wote upo bize walikaa nami vizuri".
" Usijali Vane... Nilituma mjumbe Kwenda kule kijijini kwenu akaangalie hali ipoje nilimpa Raman kila kitu.
Alirudi akasema amekuta  maisha yao yanaendelea sawa tu nadhani wameshakata tamaa ya kukupata".
" Mhhh sina hata Mpango wa kurudi huko nitakaa Zangu hukuhuku Hansy..... Pia in pongezi kwa Kupata mchumba tunasubiri wiki hii kumuona kwa hamu zote".

Hansy alishangaa Kusikia vile.

" Wewe Vane unasemaje? Mchumba gani tena sina mtu mimi weee nani kakuambia?".

Hata vane Alishangaa kuona Hansy kumbe hafahamu chochote.
" Basi Hansy si kitu usiku mwema nilidhania ni ivyo".

" Hapana Vane inaonesha kuna kitu unajua niambie?"
" Sifahamu kitu Hansy nilivyosikia ugeni basi nikajua atakuwa ni mpenzi wako ndie anakuja" .

" Mhhh vane Ondoa hofu na hayo mawazo... mwanamke Ambae walau anaaanza kuingia akilini mwanga wala hayupo mbali nasubiri tu azidi kufiti akilini mwangu wote nyie mtamjua...usiku mwema Vane".

Hansy aliondoka zake hata Vane alibaki haelewi kwamba Hansy ana maana gani kumuambia maneno yale.....

Sijui itakuwaje?
Tukutane sehemu ya 3*ME & YOU*

SEHEMU YA.... 3
Na
Mamuh mohd
(0716730000)

Tuliposhia.......

Hansy aliondoka zake hata vane alibaki haelewi kwamba Hansy ana maana gani kumuambia maneno yale......

SONGA NAYO......

Basi siku ilifika Ambapo  wageni Familia ya mwanamama Bi Rose akiwa na Binti yake wa pekee Ester walifika nyumbani kwa Mr makuka na kupokelewa kwa ukarimu kutoka kwa Familia hiyo. Waliketi wote Sebleni huku wakiandaliwa vinywaji mbalimbali na wafanyakazi wale mwasifa na Vane.

Maongezi yalikuwa ni kumtambua ambapo mama hansy alimtambulisha katika familia yake rafiki yake Bi Rose Pamoja na Binti yake Ester.

"Haaaa!!!! Nimefurahi sana kukuona bi Rose mkewangu alikuwa akikuongelea sana lakini hatukupata wasaa mzuri wa kukutana"

"Ni kweli shemeji...mala baada ya mumewangu kupoteza maisha na kuniachia mtoto akili Yangu ilikuwa bize kupambana na maisha.

Kiukweli sikuwa mtu wa kutembea sana Zaidi ni Safarini kufuata mzigo ili maisha yasonge nimsomeshe mtoto".

"Ni jambo Zuri sana hatimae umekuwa na Binti msomi hongera sana".

"Asante... hongereni na nyinyi kwa kuwa na vijana wazuri na wasomi pia".
"Asante huyu mkubwa anaitwa Hansy na mdogo wake pale anaitwa Erick"
"Nawafahamu kupitia mama yao huwa akiwazungumza".

Wote pale walifurahi Ndipo hawajakaa sawa vyakula viliandaliwa mezani na wote wakaenda kula chakula kile.

Wafanyakazi baada ya kuandaa chakula walikaa pembeni kama kawaida kuwaangalia maboss hao ili kama kitahitajika chochote basi watumwe.

Ester alionekana kumtazama kila Wakati Hansy.

Akimpakulia chakula katika sahani pamoja na kinywaji.
Hansy hakuwa na hiyana alimshukuru tu na chakula kikaendelea.

Basi baada ya chakula pale na Maongezi ya kujuana Ndipo Walirudi Sebleni Ambapo mama Hansy akamueleza kijana wake.
"Hansy mwanangu umekuwa baba unahitajika kuwa na mwenzako.
Huyu Ester ndie binti ambae sisi wazazi wako tumemchagua kwa ajili yako.
Bunti Mdogo msomi mrembo pia nadhani na wewe Ester mama ameshakuambia kuhusu hansy".

Hansy aliinamisha kichwa chini pasina kuzungumza kitu Ndipo Erick Mdogo wake Hansy akapiga makofi.
"Wooow!!! inapendeza sana Karibu Ester kwenye familia yetu"
" Hata Binti Ester alikuwa zake amenyamaza kimya akiangalia chini kwa aibu aibu".
Hansy alimtazama Ester kisha akamuomba kuzungumza nae faragha kidogo".

Walitoka nnje wakawaacha wazazi bado wakiwa wanajadiliana.

"Ester Binti msomi mrembo kwanini unakubali kuchaguliwa mchumba?"

"Hansy naelewa kuwa Mapenzi hayalazimishwi kama hujaridhika na mimi sawa wala sitaingilia hili japo mimi kiukweli nilikupenda sana".
" Hapana mimi bado sijafikilia chochote kuhusu wewe kwanza ndo kwanza na kuona Leo naomba mueleweshe mama yako  nami nitaongea na Wazazi wangu kwamba Hapana kuhusu hili ".
" Sawa Hansy nimekuelewa wala Usijali ".

Basi Wakati wanazungumza nnje kumbe vane na mwenzake mwasifa walikuwa dirishani wakiwaangalia.

Wao hawakujua hata kilichokuwa kinazungumzwa ila walichoamini wao ni kwamba wapendanao wameamua Kwenda kuzungumza nnje.

" Hansy kapata Mwanamke mzuri sana jamani Kama nawaona walivyoendana". Aliongea mwasifa lakini Vane yeye alikuwa kimya tu.

Alijikuta anakumbuka siku ya kwanza yeye kukutana na Hansy.
Jinsi alivyomsaidia kumtoa kwenye maji mpaka sehemu kavu.
Walivyotazamana kwa mala ya kwanza mpaka wakafanikiwa kutoka kijijini kule na kufika mjini.

Binti alijisemea ndani ya moyo wake, "Hansy sitakiwi kuwa Karibu na wewe tena... Umeshakuwa mwanaume wa mtu Asante kwa kunitoa kijijini katika tamaduni zenye kukandamiza na ukanileta huku mjini.
Hii ni Zawadi Ambayo sitaisahau kutoka kwako nakutakia maisha mema".
Alijisemea Binti huyo kisha alikwenda chumbani ni kama alijikuta ameumia kiasi Fulani.

Basi usiku ulipofika wageni waliondoka Ndipo Hansy alipata wasaa wa kuzungumza na wazazi wake kuwaeleza.

"Baba na mama kama mlivyoona nilipata wasaa wa kuzungumza na Ester tumekubaliana kuwa tupeane muda mwingi Zaidi kama tunaweza kuingia katika mahusiano ila kwa mala moja hii upande Wangu imeniwia vigumu sana".

" Unaongea nini Hansy? Kumbe ndo umemuambia ivyo binti wa watu? Uwiiii sijui nitamtazama vipi bi Rose mimi. Umefanya nini? Hansy Ester ni Binti mzuri anakufaa Karibu kuelewa ".
" Sio kwa sasa huo uzuri mnaouzungumza mimi bado sijaona nipeni muda tafadhali tafadhali ".

Alimaliza kuzungumza hayo Hansy kisha akaelekea zake chumbani kwake aliacha amewachanganya wazazi wake kwelikweli.

Vane alikuwa zake chumbani amekaa ametulia Ndipo nwasifa ajamfuata.
"Shoga vipi unaumwa au? Naona umejilaza tu jamani?"
"Tumbo linanisumbua sijui hata mwanini?"
"Ahhh pole Usijali pumzika mimi nitamalizia kazi.
Lakini nikupe umbea... Hansy kamkatas huyo mwanamke kasema amemuambia ampe muda hajaona uzuri wake".
Vane mpaka aliamka kusikia ivyo,
"Weeeee mwasifa kweli?"

"Habari ndo hiyo shoga umelala umepitwa na Mengi haya nakuja ngoja nikamalizie kazi".
Mwasifa alitoka na kumuacha vane nae akiwa ameshangazwa kwelikweli na Habari hizo.

Hansy nae alikuwa Chumbani kwake ndipo Mdogo wake Erick akamfuata.
"Kaka unazingua na hauheshimu hata mawazo ya wazazi wewe utaishi vipi bila kuoa.
Mke mzuri acha zako buana".
" Ni kweli lakini mimi sijamuwazia kuwa mkewangu yani sijapata hisia zozote juu yake".
" Haya basi labda yupo tayari una mchumba au?".

Hansy alitabasamu Ndipo akainuka na kushika begani Mdogo wake.

" Hakika yani hisia Zangu  kuna mahali zimeelekea kadri siku zinazidi kwenda najikuta napenda".
" Mhhh wapi huko? Kazini kwako alikuwa Classmate au? Kumbe kaka Tayari una chombo na husemi... Kama ni ivyo nami nakuunga mkono asilimia ya mia oa kitu roho inapenda japo I can't wait kuonana na shemeji Yangu ".

" Usijali hivi Karibuni kwanza nizungumze nae yeye mwenyewe bado sijasema chochote nahisi uwoga sijazoea ujue alafu nampenda balaa ".

" Hahahaa... Sasa hayo mambo niachie mimi Mr malavi davi nakupa Maneno hayo mtoto hatoki".
Walicheka pale kwa Sauti wenyewe Erick akawa anamuambia Maneno flani flani kaka yake ya kwenda kuzungumza kwa huyo mtarajiwa wake ambae hajajulikana ni nani bado.

Upande wa bibie Ester usiku huo alikuwa Chumbani kwake Ndipo mala aliingia mama yake.
"Hyyy darling hujalala bado unamfikilia mchumba bila shaka".
"Mhh acha tu mama... Hanitaki nawaza nimekataa wengi chuo kwa ajili yake leo hajaridhika na mimi".

"Hilo limewezekana vipi lakini? Amekwambiaje?"
"Kasema nimpe muda na nisikubali kuchaguliwa mwanaume ni wazi anaonesha hakunipenda".
"Ohhh mbona mama yake aliniambia kijana wake hana shida kabisa sasa iweje hilo?"
"Ndo hivyo huwenda Tayari ana Mwanamke wake hatuwezi kujua".
"Ni kweli lakini hapana nitahakikisha mwanangu unakuwa na furaha".

Eater alijilaza katika kifua cha mama yake na kumuambia,

"Mama najua unanipenda, hata siku moja haukuwahi kuonesha ishara zozote nijihisi  Sina wazazi umekuwa mama bora si wakati baba Yangu yupo hata akiwa hayupo unepambana kwa ajili Yangu na bado unataka kupambana kwa ajili Yangu".

"Wewe ni Binti Yangu Ester hata kama sijakuzaa... Kwa magumu niliyoyapitia na baba yako akaja kuwa mkombozi Wangu sina shukurani kwake Zaidi ya kukupenda kwa dhati.

Nilijifungua mtoto nikiwa kijijini na hali ngumu, baba wa Mtoto alimchukua mtoto huyo ikiwa ni siku moja tu nimeshinda nae wakaondoka.

Nilichanganyikiwa sana kijijini niliishi kama chizi sikujua hata muelekeo wa maisha Yangu utakuwaje.

Ndipo baba yako alikuja kijijini kwetu na kunichukua akanipeleka mjini milembe.. huko nilikaa mpaka afya Yangu ikatengamaa kama haitoshi akanipokea nyumbani kwake na kuniruhusu niwe mama yako hakika alinipa heshima kubwa sana.
Sijui mwanangu atakuwa na hali gani huko alipo lakini wewe sasa ndie nakuona kama yeye.
Kwaiyo nipi Tayari kulinda Furaha yako kwa gharama yoyote Ester ".

" Asante mama na pole sana kwa kukukumbusha machungu.
Lakini huyo baba yake haukujua kwao ni wapi haukwenda kumuulizia? "
" Sikupafahamu kwao yeye alinidanganya ni wa kijijini kwetu lakini kumbe haikuwa ivyo inaonesha alitokea mbali ".

" Basi mama nakupenda sana lakini ukweli nampenda Hansy nimejikuta nampenda kweli".
" Atakuo utakuwa mkewe ngoja nitazungumza na Mama yake tutajua cha kufanya ".

Ester alifurahi akamkumbatia mama yake huyo ambae pia tunapata kufahamu kumbe si mama yake mzazi ni mama wa Kufikia tu kwake......

Siijui itakuwaje?
Tukutane sehemu ya 4*ME & YOU*

SEHEMU YA..... 4
NA
Mamuh mohd
(0716730000)

Tuliposhia.......

Ester alifurahi akamkumbatia mama yake huyo ambae pia tunapata kufahamu kumbe si mama yake mzazi ni mama wa kufikia tu kwake.....

SONGA NAYO......

Asubuhi bibie Vane aliamka Ndipo kufika Sebleni alimkuta Hansy akiwa amekaa anaperuzi vitu katika laptop yake.
Vane aliamsalimia kisha akawa anaelekea zake jikoni  kuanza majukumu
Yake ndipo hansy akamuita.

"Vane kuna Zawadi yako hii tokea siku nyingi lakini nilisahau kukupatia"
"Zawadi? Zawadi gani kaka hansy?"
Hansy Ndipo aliishika ilikuwa ni simu.
Vane alishangaa awali alikuwa hajui hata kama ulimwenguni kuna simu lakini alipofika mjini ndipo akazijua na kazi yake baada ya kuona watu wakiwa wanatumia.
"Hansy kwanini umeniletea zawadi kama hii na ukizingatia mimi sina hata wa kuzungumza nae"
"Usijali nimekuwekea line kwa ajili ya mawasiliano".
" Asante sana Hansy nimefurahi"
" Karibu usijali".
Binti alitabasamu Ndipo akaenda sasa jikoni huku akiitazama simu yake hiyo.

Alikuwa hajui hata abonyeze wapi Ndipo mala akakutwa na yule mwasifa mfanyakazi mwenzake.
" Heee wewe vane simu ya nani hiyo? "
" Nikikwambia sijui kama utaamini kanipa hansy leo".
" Mhhh acha utani? Kaka hansy hapana hanaga mazoea na sisi mbona.
Japo yeye ndo alikuleta hapa lakini namuona kabisa hana mazoea na wafanyakazi "
" Niamini kweli amenipa"

" Bahati yako shoga Angu hongera nitakufundisha kutumia  najua bado hujui... Na kuna mkaka mmoja nnje huwa anakutakaga mala kwa mala ananiomba namba zako za simu sasa nitampatia"
" Mhhh hapana hata sitaki habari za wanaume sijazoea"
" Kwani kuna anaezoea basi? Mwanzo tu huo baadae wewe mwenyewe utataka".
Mwasifa alikuwa akiiangalia angalia simu ile Ya Bibie vane jinsi ilivyo nzuri.

Basi majira ya jioni mama Hansy alikwenda hotelini Ambapo aliitwa na rafiki yake yule bi Rose mama yake na Ester.

"Nimekuita hapa swahiba kiukweli kaa zungumza na kijana wako Hansy ulinihakikishia kuwa mmeshazungumza na anafahamu kuwa anatakiwa kumuoa vane sasa shida iko wapi?"

"Amesema apewe muda kwanza nadhani hawajazoeana lakini lazima hansy amuoe Ester"

"Na iwe hivyo maana kiukweli Ester amempenda sana hansy maana nilimuaminisha kuwa ni kijana mzuri nae anaridhika na kumuona ndo kazini kumpenda Kwaiyo naomba msimpe maumivu binti Yangu".

"Wala haina haja ya kuongea yote hayo swahiba hansy amelala katika tumbo langu miezi 9 lazima atamuoa ester".
Walifurahi wamama hao wawili Ndipo wakaagiza vinywaji kwa ajili ya kumwagilia moyo.

Basi majira ya usiku vane akiwa chumbani Ndipo simu iliita.
Kuangalia aliempigia ni namba ngeni yeye hata hajui ni nani.
ikabidi akuambie mwasifa amuelekeze maana hajui hata jinsi ya kupokea.

Mwasifa aliipokea simu ile kisha akaweka sauti na kumpatia Vane.
"Haloo"
"Haloo mumy umelala?"

"Hapana... Hansy mbona umenipigia simu Wakati upo chumba cha jirani tu"

"Mhhh nahitaji kukuomba kitu vane"

"Kitu gani?"

"Mtoko... Kesho naomba kutoka na wewe kuna Maongezi ambayo nahitaji tukakae tuzungumze".

"Hansy Maongezi gani hayo? Na nitatoka vipi hapa nyumbani? "

" Ukishakubali basi kutoka kwako sio shida utatoka kupitia mimi".

" Sawa".

" Wooo!!!! Nafurahi ukiamka Asubuhi nenda jikoni pale Kwenye kabati kuna mzigo nitakuwekea kwa ajili yako Kisha nitakupigia simu kukupa Maelekezo ya kufika mahali nitakapokuwa".

" Sawa".

Vane aliitikia tu ndipo waliagana na kukata simu.

Mwasifa alisikia kila kitu Ndipo kwanza nae alibaki anashangaa.
" Heee!!! Mtoto wa boss jamani mbona siamini? Vane hii nafasi mama sijui ningeipata mimi ingekuwaje?.
Sasa ndo napata picha kwanini Hansy kakulet katika hii nyumba na alionesha kukataa mchumba aliechaguliwa anakupenda wewe vane changamka".

" Hapana anipende mimi kwa kipi jamani?"
" Anajua yeye kakupenda kwa kipi.

Shoga huo mzigo wa Asubuhi usinitoshe kisha vaa upendeze... Yani waoneshe kwamba hata sisi wasichana wa kazi ni wazuri umetuheshimiwa wafanyakazi wote tukupe maua yako".

" Yani mwasifa ujue mimi hata sielewi unachomaanisha badhani umefika mbali sana hakuna kitu kama icho"
" Mhhh tusiandikie mate wewe kesho nenda ukamsikilize kubwa tugawane hayo mazuri atakayokupa".
Vane hakuwa na chakujibu aliamua kupanda zake kitandani kuutafuta usingizi.

Basi siku iliyofuata Asubuhi bibie Ester aliwasili katika kampuni moja iliyofahamika kwa jina la Jj limited company.
Binti alikwenda kwa ajili ya kuanza kazi. Alionesha kuwa anasubiriwa kwa hamu maana alipofika tu wafanyakazi wote waliitwa katika ukumbi wa mikutano kutambulishwa.

Ester alifurahi sana kwa mapokezi yale.
"Tulikuwa tukimtafuta sana mtu mwenye elimu kama yako katika fani hii lakini hatiamae naamini kampuni Yangu itazidi kuwa na sifa nzuri kwa ujio wako".
" Nafurahi kusikia ivyo kubwa ushirikiano wenu ni muhimu Sana ili tuzidi kufanya kazi".

Walipiga makofi wafanyakazi wote Ambapo waliagiza na chai wakanywa Pamoja na mgeni wao huyo.

Asubuhi hiyo vane aliamka na Kwenda jikoni kama jinsi ambavyo Hansy alimuambia.
Kufika Ndipo akakakuta kiasi cha pesa.
Walizihesabu wote na mwasifa ilikuwa shilingi laki 5.

Mwasifa alimuita Vane chumbani akamuambia,
"Hapa shoga angu jiandae bahati imekuangukia usichezee nafasi vibaya.
Nenda umependeza shoga nakuombea kila la kheri.

Hansy amekupenda wewe na sio huyo mwanamke aliekuja kwanza mbaya ana mashauzi khaaa".
"Acha buana naogopa ukute hata hansy haendi kuniambia kitu kama icho japo mwili Wangu unasisimka sana".
" Acha nakwenda kukununulia nguo utakayovaa leo shoga angu".
Vane alikuwa kimya tu bado hakuwa mzoefu wa mambo kama hayo lakini mwasifa alionekana kuwa anafahamu fahamu mambo hayo kwa kuwa alikulia sana mjiji Tofauti na bibie vane.

ilikwenda mpaka jioni Ndipo Bibie Vane alitoka nyumbani na Kwenda mahali Ambapo ndipo alitakiwa kwenda kukutana na Hansy.

Kufika alimkuta Hansy ameshafika na akampokea eneo la parking ambapo Ndipo gari aliyokwenda  nalo Vane lilisimama hapo.

Binti alishuka Ndipo akamkuta hansy akampokea.
Bunti alikuwa amevalia gaoni lake refu la rangi  nyekundu.
Alipendeza lilikuwa vazi Ambalo mwasifa alimchagulia kuvaa.

"Karibu... Umependeza sana Vane"
"Asante mimi sikujua hili ni mwasifa ndie kaniandalia hili vazi"
"Mhhh tumpe maua yake na atakuwa mbunifu wako wa mavazi"

"Mhhh wewe buana... Naogopa sana kama mama akijua nimetoka"
" Usijali madam mwasifa anajua hili atasawazisha na ukamuambie nimefurahi kwa ajili yake".

Hansy alimshika mkono Vane na kwenda nae eneo la Ndani Ambapo ajabu walikuwa wao wawili tu na pamepambwa sehemu Hiyo.

Vane alikuwa akishangaa tu huku mwili ukimsisimka.

"Vane kuwa huru haya  yote ni kwa ajili yako.
Naomba kabla ya yote nizungumze haya yaliyokaa kifuani Mwangu.

Vane tokea siku ya kwanza tunaonana nilikutazama tofauti na vile ambavyo huwa naangalia wanawake wengine.
Si kwamba ulinisaidia katika maji yale lakini naamini ile ilikuwa njia ya sisi kuonana.
Nilifurahi kuishi na wewe tabia zako, zikathibitisha kwamba yaliyomo katika muonekano wa nnje pia mpaka Tabia ni nzuri.
Nakupenda Vane naomba nipe nafasi ya kutangazia ulimwengu kuwa nimempata mwanamke".

Vane Machozi yalikuwa yakimtoka,
" Hansy kwanini unaniambia haya hali ya kuwa unajua fika unae mwanamke mwingine"

" Ester sijampenda na nishamuambia ukweli wote  moyo Wangu umekupenda wewe naomba nikupe muda nawe wa kujiridhisha kama nakufaa".

Vane alitazama chini tu kisha akamjibu hansy.
" Sina haja ya kukuangalia mala mbili huna baya Hansy nakufahamu.
Naomba muda nitakujibu kwa sasa najihisi mzito ulimi ni kama umepigwa ganzi".

" Basi usijali kuna vinywaji na Chakula maalum kwa ajili yako naamini utakaa sawa".

Basi kweli Hansy alitoa maagizo kwa Wahudumu wakaipamba meza ile kwa vyakula vya kila aina  ni yeye na Hansy kufurahia chakula kile.

Usiku kiasi saa 4 Ndipo Walirudi nyumbani wakiwa pamoja Hansy na Vane.

Vane hakutaka makubwa aliposhuka kwenye gari akapitia mlango wa jikoni kisha Hansy yeye akapita mlango wa Sebleni kama kawaida.

Vane moja kwa moja aliekuwa chumbani lakini kabla hajaingia mala akasikia akiitwa.

"Vane umetoka wapi?"
Bunti alishtuka Ndipo akaangalia aliemuuliza hivyo akakuta si mwingine ni Erick Ndugu yake na Hansy.

"Hapana kaka nilitoka tu kuangalia mji"
"Usinidanganye nimekuona umerudi na kaka Yangu nilikuwa juu gorofani nijibu kabla sijakuzingua Sasaivi ulikuwa wapi na kaka Yangu?"

Vane alimtazama Erick kisha akamjibu,
" Kama umeniona na kaka yako basi hata Hilo jibu lako kaka yako anaweza kukujibu kamuulize".

Alijikaza binti Vane hakuwa mpole kiivyo kwa mtu anaemuendea tofauti alijibu na kisha akafungua mlango na kuingia ndani.

Erick hasira zilimshika Ndipo akaona asipoteze muda akatoka kumfuata kaka yake Hansy....

Sijui itakuwaje?
Tukutane sehemu ya...5*me & you*

sehemu ya.... 5

na
mamuh mohd
(0716730000)

tuliposhia.......

erick hasira zilimshika ndipo akaona asipoteze muda akatoka kumfuata kaka yake hansy...

songa nayo.......

hansy alikuwa zake chumbani akijiandaa kwenda kuoga ndipo mala aliingia erick chumbani huku akiwa na hasira.
"kaka umefanya nini kaka yangu? yani kweli wewe.... ni wa kufuatana na kale kasichanana eti vane huoni hata aibu? usiniambie kuwa ndie mwanamke uliempenda.

kwamba kuzungumza kote kule kumbe mwanamke mwenyewe alikuwa ndie vane.

" yes.... ni vane na unamuona hana hadhi ni kwa vile tu si mtoto wa mjini lakini mpe muda atakaa sawa"

" tokea lini jogoo wa shamba akawika mjini kaka!!! kumbe ndo maana ulimtetea abakie kuishi na sisi hapa mwenyewe umemkubali sio?"

" sijui hata unazungumza nini mdogo wangu na sijaona kosa la vane...ni moyo wangu umempenda na wazazi wataelewa tu".

" umezingua yani nilikuwa nakuona kaka yangu msomi mwamba kama mwamba ila sio sili umeniangusha sana.

vane hana hadhi hata ya kuwa kilaka aiii".
erick aliondoka chumbani humo akionekana kuwa na hasira.

hansy kwanza ilibidi akae kitandani kwake na kuanza kumkumbuka tena vane.
alimkumbuka tabasamu lake pindi binti alipokuwa akitabasamu.
moyoni alijisemea hapana ana urembo kama wengine hawauoni basi yeye ameuona.

wakati huo vane alikuwa zake chumbani akimsimulia mwasifa kila kilichotokea huko.

"yani kama nawaona... hongera shoga angu siku si nyingi utaepukama na kusugua masufiria hapa".

"hapana sio kwa haraka ivyo bado nipo tunachunguzana kwa ukaribu kisha tutafikia hatua inayofuata.... lakini huyu erick alituona nikiwa na hansy tunarudi.

hee!!! mwenzangu ile naingia ndani si kanifuata kuanza kuniuliza.

alinitia hasira nikamjibu kamuulize kaka yako".

" safiiii ivyo ivyo umemuwezea.

ujue tena asikuzoee hajui wewe shemela".

" hahahahaha!!!! jamani".

walicheka wenyewe na kufurahia maongezi yao hayo.

*************

tukirudi kijijini katika himaya ile ya mtakuja chini ya mfalme mzota ndipo siku hiyo mfalme alikuwa na waganga wengi katika nyumba yake hiyo.

walikuwa wakifanya msako kwa njia ya kimiujiza kujua wapi binti yake alipo. hiyo ni kutokana na kwamba muda mrefu umepita wamemtafuta binti pasina mafanikio.

waganga walikuwa wanne ndipo kila mganga alipiga shabaha lake kujua wapi binti alipo.

baada ya kama dakika 10 ndipo mganga wa kwanza akatoa majibu.

"mfalme wa hii himaya kwenye ramli yangu simuoni kabisa binti wa mfalme vane.
lakini sioni kiza kinachoonesha amepata matatizo ila naona mwanga ni wazi yupo sehemu salama ila mbali na hapa".

mganga wa pili nae alipiga ramli yake ikamuonesha majibu,
"binti wa mfalme anaonekana kuwa upande wa kusini ila mbali na hapa".

wa tatu nae alitoa majibu,

"namuona binti mfalme akiwa amezungukwa na maua mazuri ishara ya kwamba yupo sehemu salama".

na mganga wa nnje wa mwisho alitoa majibu kuwa,
"bunti mfalme yupi uelekeo huu wa kusini mbali na hapa inashindwa kuonekana vizuri sababu ya umbali".

mfalme alizidi kuchanganyikiwa, alisimama kwanza na kutembea tembea.

"nataka binti yangu arudi huku nyumbani.
nahitaji mfanye kitu kitakachomfanya arudi huku nyumbani.

nimeshamtafuta sana nahisi siwezi kukaa bila binti yangu namtaka aje tujenge himaya hii aolewe na binamu yake saidiy wawe viongozi wa ukoo wetu".

" nataka kwanza mfanye mfanyavyo kuhakikisha binti yangu anakuwa mzima.
asiingiliwe na mwanaume yoyote isipokuwa mume niliemuandalia.
kila mwanaume atakaetembea nae asifanikiwe augue na ikiwezana apoteze maisha.
najua hiyo hali pekee ndiyo itamshtua vane itamfanya arudi huku nyumbani ".

" sawa tunahitaji nguo yake yoyote aliyokuwa akiivaa tufanye kazi".
basi hilo halikuwa shida ililetwa nguo ya vane aliyokuwa akivaa na sasa kazi inaanza.

wanamuwekea ulinzi mfalme hataki binti yake atembee na mwanaume yoyote tofauti na yule aliemuandalia sasa ikitokea kuna mwanaume atalala nae basi huyo mwanaume augue na kupoteza maisha.
waliamini hali ile itamfanya vane kushtuka na atarudi nyumbani yeye mwenyewe ipo siku.

hii ni baada ya kuambiwa kuwa anaonekana yupo sehemu salama na aliambiwa kuwa alionekana akikimbia na mwanaume ivyo akaona mtego huo ndio utakuwa sawa.

baada ya maagizo hayo mfalme aliingia ndani ya nyumba yake na kuwaacha waganga waliendelea na kazi.

huko alikuwepo mkewake malkia, alimpatia kikombe cha chai mumewe.
"vipi mmefanikiws kujua wapi alipo binti yetu?"
"hapana ila tunaweka mtego atarudi tu, nina amini binti yangu atarudi".

"ni binti yetu... hata kama mimi si mama yake mzazi lakini ndie nimemlea nina uchungu nae.
isitoshe ndoa tulikuwa tumeiandaa...sawa lakini mnaweka mtego gani? "
" mfalme ndipo alimueleza mkewe kila kitu na wote wakawa na matumaini kuwa hali ile ikimtokea vane atarudi nyumbani tu kwani amelelewa akiamini sana masuala ya kimila.

lakini mwanamama huyo kimoyoni alikuwa akijizungumza,

"sasa itakuwaje mimi ndie nilimsaidia vane kutoroka hapa... lengo langu atoke maana yeye ndo alikuwa kipenzi  cha baba yake akitoka hapa anipe nafasi mimi malkia sasa nipendwe na baba yake lakini anataka kumrudisha.... hapana hapana ".
alijisemea mwanamama huyo kwake aliona vane akirudi itakuwa kikwazo tena na alimsaidia kutoroka pia.

basi siku iliyofuata asubuhi bibie vane aliamka mapema na kukaa kitandani. alionekana kuwa anawaza sana ndipo mwasifa nae alimuona akainuka.
"mrs hansy kulikoni?"
"heee mimi?"

"ndio mrs maana yake mwanamke wa hansy"
"hahaha... una utani wewe hapana mimi bado vane ujue simuamini hansy ni mwanaume wa tofauti sana"
"shoga ndo uamini umeshapendwa pendeka shika simu nikuelekeze muandikie sms nzuri".
"mhhh naona aibu buana acha anitumie yeye"
"wee acha ushamba wako".

"kuna kitu nimekumbuka kinanisumbua sana"
"kitu gani?"

"kikwetu mtu akipata mwanaume kama hivi ili kuondoka mikosi na mabalaa lazima wafanyiwe tambiko sasa naanza nitarudi vipi nyumbani na hansy kufanyiwa tambuko hawatakubali maana kuna mwanaume walitaka anioe ndugu yangu".

"achana na hizo habari za matambiko hizo za kijijini muamini mungu mtegemee mungu swali omba dua"
"hata jinsi ya kuswali sijui kwetu tunakuwa na miungu tu n waganga".

"nitakufundisha wala usiwaze kwa ulivyonielezea mazingira ya kwenu mhhhhh sio rahisi kurudi tena na hansy".

" ni kweli asante sana mwasifa wewe ni rafiki mzuri sana".
" bibi yangu alinilea na kunifunza niishi na watu ili nivae viatu usijali twende tukafanye kazi".

waliinuka wote lakini kabla hawajatoka simu ya bibie vane iliita na hansy ndie alikuwa amempigia.
mwasifa ikabidi aingie bafuni kuoga kisha akavaa sare zao za jikoni akatoka akamuacha vane akiongea na hansy.

asubuhi hiyo kijijini kule waganga walimaliza kazi yao ndipo waliandaliwa chai na nyama choma kama shukurani kwa kazi waliyoifanya.

lakini malkia alimfuata mganga mmoja na kumuita.
"samahani mfalme anakuita".
mganga yule ikabidi ainuke lakini kufika nnje ni malkia akamsimamisha.

"hapana ni mimi ndie nimemekuita na sio mfalme kuna jambo ataka unisaidie "
" Malkia jambo gani tena? "
" Nataka upangue hiki mlichofanya ili vane asirudi huku".
" Malkia jambo zito hili hatuwezi kulizungumza hapa tafuta wakati mwingine "
" Sawa nitakuja kwako lep usiku"
" Sawa hayo Maneno".

Mganga  yule akarudi ndani malkia nae akaondoka sehemu Hiyo nae ana sababu zake ndio maana hataki vane arudi.

Upande wa Bibie Ester siku hiyo aliamka na Kwenda nyumbani kwa kina Hansy.
Kufika alikaribishwa mpaka ndani haswa na mama hansy alimpokea kwa shangwe.

"Mama nilikuwa naenda kazini nikaona nije kuwasalimia"
"Asante mwanangu jamani una upendo sana wewe...Hansy nadhani ametoka mapema sana"

"Ok sawa haina shida kubwa nyie wazazi Wangu wazima nimefurahi".

Eater Ndipo kuinuka ili aondoke na bibie Vane ndo alikuwa akitoka chumbani.

Mama hansy akamuita,
"Vane.. njoo mbebee pichi Ester mpaka nnje Kwenye gari".
Vane akatii amri akabeba picho ya vane kumsindikiza mpaka nnje Kwenye gari lake.

"Asante Vane ila kuna kitu naomba nikuulize kama hutojali"
"Sawa".

"Mhh eti hasny huwa anarudi saa ngapi? Na huwa wanazungumza chochote kuhusu mimi? Na pia nyie mnaishi nae mnavyohisi labda ana mwanamke?".

Vane alishtuka kwa maswali yake mpaka akapata kigugumizi kwanza.
"No usiogope nijibu sio kwa nia mbaya mumy relax".

"Hapana sifahamu chochote kuhusu hansy...uwe na kazi njema Karibu".

Vane aliamua kuondoka akakimbia kabisa mpaka ndani.....

Sijui itakuwaje?

Tukutane sehemu ya 6*ME & YOU*

SEHEMU YA.... 6
Na
Mamuh mohd
(0716730000)

Tulipoishia......

"Hapana sifahamu chochote kuhusu Hansy... Uwe na kazi njema Karibu".

Vane aliamua kuondoka akakimbia kabisa mpaka ndani....

SONGA NAYO......

Ester hakuelewa kitu alimchukulia vane kama uwoga tu Ndio umemfanya asijibu kitu ivyo akapanda kwenye gari lake na kuondoka.

Sasa Vane alirudi mpaka ndani eneo la jikoni na kuonekana Kabisa hajafurahishwa na Ester kumuuliza vile.
"Hansy hampendi Ester ananipenda Mimi  anatakiwa kukubali.
Na Mimi Tayari nimeshampenda Hansy sijui itakuwaje jamani".
Alijiuliza Vane Ndipo akaona ayaaache kwanza aendelee na kazi zake za pale ndani.

Siku Hiyo Ester alifika Kazini,alikuta kuna mgeni akimsubiri.

Binti Ndipo akamkaribisha mpaka ndani ofisini kwake kuzungumza nae.

"Karibu sana ant emmy mama kaniambia ujio wako"

"Asante sikutaka kusubiri ndio maana nikaulizia ulipo na kufika.

Kwanza hongera sana kwa kumaliza masomo yako salama salmini, ni mabinti wachache sana ambao huwa wanakwenda shule kufanya kile ambacho mzazi amemtuma.

Wengine huishia Kupata wanaume na kuharibu maisha yao".

" Ni kweli anty emmy katika hilo namshukuru sana Mungu.

Mama Yangu amepambana sana haijalishi alikuwa peke yake katika ulezi lakini niseme amepambana kuhakikisha nafaulu masomo Yangu".

" Sawa sawa...haya niambie mimi ni mshauri katika mahusiano kama eneo hili salama tuzungumze na kama majukumu yakiofisi yamekubana basi nikupe muda tutaongea nnje na hapa"
" Hapana anty emmy hili ni la muhimu Kwangu sana kwa sasa.
Nimemaliza masomo Yangu nahitaji kuwa katika mahusiano.
Mwanaume huyu ni Wazazi wetu walikaa wakashauriana kuwa tutaoana.
Binafsi nimependa Tena sana lakini yeye ni kama ananikwepa".

" Pole sana.... Wazazi wenu hawakutakiwa kuwazungumzia hayo mngeyazungumza nyie.
Lakini unatakiwa kufahamu amekukataa kwa Sababu zipi je anae Mwanamke mwingine au kuna vitu kwako havijampendeza?.
Ungepata wasaa wa kuzungumza nae"
" Katika hilo hayupo tayari kabisa.
Hataki kuzungumza na mimi.
Kubwa mimi nachotaka anipende nipe mbinu gani nifanye ili anipende hata kama anae mwanamke wake basi amuache kwa Sababu Yangu.
Nampenda sana huyo kijana ant emmy".

" Kwanza uwe Karibu na mtu wake wa Karibu huyo ndie utamtumia kukuweka Karibu na huyo Mwanaume mambo yenyewe yatakwenda kwenye mstari.
Daima kitu unachokipenda basi kipambanie kwa namna yoyote uwezayo usiache kiende kirahisi.

Ester kusikia ivyo alipata faraja ni kama nguvu zilimjia mala dufu kupambania Mapenzi yake kwa Hansy.

Vane alikuwa zake eneo la nnje akifanya usafi Ndipo sasa alitoka Erick nae alikuwa akielekea zake chuo.
Vane alimsalimia lakini Erick hakuitikia salamu.
"Nisikilize wewe achana na kaka Yangu.

Ukitaka uishi kwa amani katika hii nyumba achana na Hansy sitarudia tena kukuambia hili ila nitawaeleza wazazi ndo utaona nini kinafuata".
Erick alimuambia Binti maneno hayo makali kisha akaondoka zake.
Vane alibaki akimtazama Erick huku ameduwaa sasa asijue cha kufanya.

Mala alitoka mwasifa Ambae alikuwa amesikia kilichotokea.
" Vane achana nae Na mpigie simu Hansy muambie.
Silioni gari lake naona amewahi kutoka leo muambie kila kitu na asikuzee huyu hajui kama wewe shemeji yake?"
" Muda utaongea Mwasifa lakini sikufichi nampenda Hansy.

Yani kadri siku zinavyozidi Kwenda nauona Kabisa upendo Wangu kwake. Alafu ma huyu ndo kaanza vituko vyake"

" Achana nae hata asikusumbue kelele za chura hizo hazimzuii tembo kunywa maji".

" Asante sana unanifariji Mwasifa ngoja awaambie hao wazazi wakw tuone itakuwaje ila kumuacha Hansy sio rahisi leo nimeamka na upendo wa ajabu kwake.

Pengine angekuwepo hata ningemkumbatia"

" Hahaha!!! Wachaaaa mahaba niue".

Walicheka wenyewe kama kawaida yao kisha Ndipo wakaendelea na kazi zao.

Majira ya usiku malkia alikwenda nyumbani kwa mganga yule Ambae aliitwa mganga Ndomo.
"Nimekuja kwa lile jambo Langu.
Mimi nilishiriki kumfanya Vane atoroke maana hakuwa Tayari kuolewa na Ndugu yake alitaka kuishi maisha huru na sio ya kitumwa ya huku kwetu.

Nataka asirudi huku hiyo kazi mliyofanya mnataka kuhakikisha anarudi basi ipangue ili akae hukohuko asije na mimi nataka kumzalia Mtoto mfalme anipende mimi tu".
"mfalme umri umeenda utaweza vipi kumzalia Mtoto? "
" Mimi bado nina uwezo wa kupata ujauzito naweza kuzaa nae".

" Mfalme hana uwezo wa kuzalisha Mwanamke kwa sasa.
Alijigundua hilo tatizo akiwa Tayari ameshampa ujauzito mwanamke Ndipo alipata matatizo hayo.
Aliamua kwa kuwa hana tena uwezo wa kupata Mtoto basi amchukue mwanae aishi nae mbali kabisa.
Sasa wewe kupata ujazito ni ngumu sana mimi ndie naejua siri  Sababu baba Yangu alikuwa  ni mganga wao wa siku nyingi tokea enzi za Wazazi wake mfalme nilijua hii siri na mpaka nachukua mikoba ya baba Yangu naishi huku nafahamu hili".
" Sasa mganga utanisaidiaje jamani? Nataka anipende mimi.

Angalia anataka binti yake aje aolewe  ili awe mtawala wa Himaya na mimi je? ".
" Mhhh naweza kukusaidia kitu"
" Kitu gani? "
" Uzae na mimi... Nitamuaminisha mfalme kuwa ni mtoto wake amepona".
" Hii ni hatari sana vipi nikijifungua Mtoto anafanana na wewe si itakuwa balaa hili".
" Mpaka anajua wakati mnalea mimba utakuwa Karibu nae tutaizubaisha akili yake.
Hata mimi nahitaji kupata Mtoto.
Mkewangu hana uwezo wa kuzaa tusaidiane".

Malkia alinyamaza kimya kwanza akitafakari  Kisha akajibu,

"Sawa nipo Tayari tutakutana wapi mkeo asijue?"
"Hapahapa mimi mganga kama hivi atajua ni mteja na kama wewe Malkia anakuheshimu sana tutafanya mambo Yetu".
"Sawa nitakuja siku mbili izi ila iwe siri asijue mtu yoyote"
"Katika hilo nakuhakikishia".
Walikubaliana ivyo Ndipo bi malkia alitoka na kuondoka zake.

Upande wa Ester alikuwa zake nyumbani akizungumza na mama yake. Alimueleza kile alichoambiwa na ant emmy ambae alienda kumtembelea ofisini kwake.

"Mama nahitaji kuwa Karibu Zaidi na mtu yoyote pale nyumbani kwa kina Hansy iwe Rahisi anikutanishe na Hansy nimepata wazo nitembee nae labda nikibeba ujauzito atanikubali nampenda sana".

"Ester mwanangu mbona kama unahangaika sana... Mama Hansy nimezungumza nae ataweka mambo sawa shida nini?"

" Mama ni kweli lakini hawezi kumshawishi hansy anipende kitu ambacho kinaweza kumshawishi ni ukaribu wetu ndio nataka kuuweka. Niwe nae Karibu anikute sehemu mbalimbali na nikipata nafasi hata ya kutembea nae sawa"

" Sawa nakuelewa Binti Yangu ni sawa.... Sasa nani atakuwa Karibu yako kukuunganisha na Hansy".
" Ni wale wafanyakazi kuna mmoja Leo nilianza kumuuliza akawa na uwoga uwoga nadhani nitaenda nae Huyo huyo".
" Sawa naamini ni mwanzo tu mgumu kila kitu kitakuwa sawa".
Ester alifurahi kuona mama yake nae kamuunga mkono katika hilo.

Upande wa Nyumbani kwa tajiri Mr makuka ulikuwa ni muda wa wanafamilia Kupata Chakula.
Walikuwepo wazazi na kijana Erick, Hansy alikuwa bado hajarudi.

Wafanyakazi Mwasifa na vane walikuwa pembeni wamesimama kama kawaida yao.

Mala alifika Hansy akaingia mpaka ndani na kusalimiana na Wazazi wake.
"Hansy mwanangu upo bize sana unatoka mapema kurudi ndo kama ivi hatupati wasaa wa kuzungumza".
"Ni kweli baba kazi kuna program imetuweka bize sana lakini tunakamilisha... mhh sitawahi kuja kuungana nanyi hapa ivyo naomba Vane uniandalie chakula na matunda niletee chumbani plzzz".
Alitoa maagizo hayo Hansy kisha akaelekea zake chumbani kwake.

Bibie Vane ilibidi aende jikoni kuandaa kama alivyoagiza Erick ambae anaelewa mchezo unaondelea alimtazama kwa hasira vane mpaka alitoondoka mbele yao.
Erick alitamani kuwaambia wazazi wake Lakini alishindwa hata aanzie wapi.
Akapata wazo na kuchukua simu akamuandikia ujumbe Mama yake.

Vane alifika chumbani kwa Hansy Ndipo Hansy akampokea chakula kile akakiweza mezani kisha akamkumbatia Vane.
"Nimekumiss yani haielezeki umeshindaje mumy"
"Niko sawa pole na kazi? Upo bize sana mpaka napata wivu"

" Ondoa wasiwasi ni Mipango mizuri kwetu... Haya njoo ukae".
Hansy alikaa kitandani na kumuweka Vane juu na miguu yake.

" Natamani kukuambia kitu Hansy ila naona aibu!! "
" Aibu gani haya nafumba macho niambie".
" Nakupenda hansy yani nakupenda".
" Sidhani kama unanizidi mimi vane Kama nawe umenitamkia ivyo maana yake unaniruhusu kuomba uchumba kwako".
" Hapana bado mapema hansy Sitaki kukufanya uwe na haraka ya mambo nenda polepole mimi nitabaki wako.

Wasiwasi Wangu ni Ester leo alikuja akaniuliza kuhusu wewe naona bado anakupenda ".

" Achana nae huyo hata kumuwaza simuwazii kabisaa Tena asikuzoee alafu toa hizo habari tuongee yetu zawadi zako hizi nimekuletea naomba kukuomba kitu".

" Asante kitu gani Hicho".

" Nashindwa hata kusema ila natamani uje ulale chumbani Kwangu leo si kwa nia Mbaya lakini nina shauku na wewe".

" Hansy naogopa sijawahi Kabisa naogopa sana".

" Ok sawa utanizoea ipo siku kama si sasa kwa hiyari basi kwa lazima nikishakuoa".

Vane alihisi aibu Ndipo akachukua zawadi zake na kutoka huku anakimbia kutokana na aibu tu.

Lakini ile anatoka Ndipo mala akakutana Uso kwa uso na mama Hansy akiwa mlangoni pale.
Vane alishangaa Ndipo mama  Hansy kwanza alimpokonya ule mfuko aliokuwa amepewa.

"Kumbe wewe ndo kazi yako kumchekea chekea mwanangu eti".

Hadi Hansy alisikia ikabidi  haraka atoke....

Sijui itakuwaje?

Tukutane sehemu ya 7*ME & YOU*7_11

SEHEMU YA..... 7
Na
Mamuh mohd
(0716730000)

Tuliposhia.....

Kumbe wewe ndo kazi yako kumchekea chekea mwanangu eti? "

Hadi hansy alisikia ikabidi haraka atoke....

SONGA NAYO......

" Mama tafadhali tuzungumze mimi na wewe naomba usimkalipie vane"
" Unanifundisha cha kufanya mimi mama yako? Hansy hapa ni nyumbani kwangu na nyie ni watoto Wangu naweza kufanya chochote nachotaka. Vane nijibu usipoangalia utalala nnje usiku huu sitavumilia ulale ndani kwangu ".

" Mama huwezi kufanya ivyo ukimfanyia ivyo vane basi hata mimi pia nitaondoka humu ndani "

" Unanijibu ivyo mimi mama yako hansy umeamua kunivunjia heshima? ".

Mr makuka(baba hansy

alifika nae baada ya kusikia mzozo huo unaendelea.
" Mkewangu sio vyema kubishana na Mtoto namna hii.. na wewe hansy hutakiwi kubishana na mama yako haya wote mje Sebleni tuzungumze".

Vane alikuwa alitetemeka Ndipo kabla hajaenda Sebleni alipitiliza jikoni alipo mwenzake yule mwasifa.
" Yamenikuta mwenzako sijui itakuwaje mama hansy hatoniacha salama mimi".
" Hakuna huo Ndio mwanzo ilitakuwa lazima waujue ukweli.
Naamini hansy anakupenda na atasimama na wewe.

Usizungumze chochote kuwa msikilizaji Hansy atajibu maswali yote yatakayohitajika sawa? "

Vane alipata walau afuheni ya moyo ndipo akaenda nae Sebleni kusikiliza.

Mr makuka alianza kwa kumuuliza kijana wake Hansy,
"Nini kinaendelea kati yako na vane?"
"Baba vane ni mwanamke ambae namtarajia awe mkewangu.
Bado tupo katika hatua ya kuridhiana ndio maana sikuwaweka wazi ila huo Ndio ukweli Ambao lazima ningewaambia".
"Una uhakika Hansy kwamba huyu Ndie Mwanamke utakaemuoa?"

"Hakika baba Ndio maana sikuridhika na huyo Mwanamke mliemleta sijui Ester yule Sababu mimi nampenda Vane".

Mr makuka alimtazama vane na kumpa ruhusa aondoke awapishe wazungumze kifamilia maana alihofia Maneno mengine yasije kumuumiza Binti.

"Hansy mwanangu elimu yote uliyonayo ni wa kwenda kusema kwa ujasiri eti vane Ndie Mwanamke uliempenda utakwenda kumuoa serious?.... Nimekupeleka shule nikalipa na ada si tu upate kazi uje kuwa na maisha Mazuri lakini pia uwe na uelewa wa kujua kipi kizuri na kipi kibaya.

Haihitaji hata tochi kuangalia kati ya vane na Ester tofauti waliyokuwa nayo inaonekana wazi.
Tunataka upate mke na sio goli kipa.
Utapita nae wapi huyu vane".
Aliongea baba Hansy hadi Erick akapiga makofi kuonesha amemuunga mkono baba yake alichokisema.

" Yani baba sema wewe .. mimi nilimwambia mwanao huyu.
Baba sio bule kuna namna... Huyu msichana mchawi buana haiwezekani Kaka hansy naemfahamu mimi Hapana".

" Basiiiiiii!!! Nimewasikiliza inatosha msiendelee kujichosha kuzungumza kitu ambacho hakitawezekana.
Uzuri wa Vane naujua mimi sio lazima wote nyie muuone.
Huyo Ester sijampenda akilini Mwangu hayupo kabisa.
Nendeni mkalale huku mkitafakari nachotaka kwenu kesho ni jibu moja tu mtamkubali Vane au yeye na mimi tuondoke hapa".
Hansy alipomaliza kuzungumza hayo aliondoka zake.

Mama hansy alishika kichwa alihisi mpaka kinauma.

" Mtoto mpuuzi huyu anaongea nini mbele yetu? Umemuona mwanao baba hansy hana adabu wala heshima".

Mr makuka alikosa cha kuongea aliamua nae kuinuna na Kwenda zake chumbani kwanza akatulize akili yake na alimtaka mkewe watulie kwanza watajua cha kufanya.

Upande wa bibie Vane alikuwa Chumbani akilia sana.
"Mwasifa hansy amewajibu kwa ukali wazazi wake kwa Sababu Yangu. Amediriki kuwakosea heshima wazazi kwa Sababu Yangu naumia sana jamani".

"Hajawakosea heshima bali kawaonesha msimamo wake.
Wala isikupe shida huo ni msimamo wake wala sio ujeuri.
Vane Hansy anakupenda yani tena anakupenda kwelkweli Mshikilie kama kaweza kukutetea kwa ujasiri anakupenda tulia roho yako".
"Nahitaji kuona anaelewana na Wazazi wake ndio Furaha Yangu"
"Wataelewa lakini wacha kwanza awaoneshe msimamo wake weee tulia".
Mwasifa alijitahidi kumuweka sawa vane ambae alikuwa akilia tu.

Punde simu ya bibie Vane iliita Ndipo Binti akaipokea.
"Haloo Hansy"

"Unalia vane? Subiri nakuja huko chumbani kwako muambie mwasifa atupishe kama upo nae".
"Hapana Hansy mama yako asije akatukuta tena tafadhali".
"Usiogope kila kitu kitakuwa sawa. Natetea upendo Wangu wala Usijali. Jiandae tunaweza kuondoka hapa muda wowote sawa"
"Tutaenda wapi Hansy sipo Tayari kuona unakosana na wazazi wako kwa Sababu Yangu"
"Unamaanisha haunipendi sio? Sema kama haunipendi najisumbua"
"Nakupenda hansy tena sana nakupenda".

"Basi mimi na wewe  tutakuwa Pamoja utakaa napokaa, utakuwa nami pamoja kipenzi kuwa na amani".

Maneno yale yalimpa faraja sana vane akajikuta anaachia tabasamu mwanana katikati ya Simanzi alizokuwa nazo.

Siku ile ilipita siku iliyofuata Asubuhi Wazazi waliamka mapema na kukaa Sebleni wakionesha kumsubiri kwa hamu  Hansy wazungumze nae jambo lao.

Kweli Hansy nae alitoka akionekana kuwa na jazba.
Aliwasalimia wazazi wake na kuwaambia.

"Wazazi wangu sihitaji mazungumzo marefu sana ya kuwapotezea muda.
Msimamo wangu ni uleule ambao haubadiliki.
Nampenda vane nahitaji kumuoa.
Kama mmeridhia nambieni na kama hamumtaki nitaondoka nae Sasaivi".

Mr makuka alifurahi kwanza.
"Nimependa ujasiri wako Hansy Mwanangu hakika unasimamia katika msimamo wako.
Tumekaa na mama yako jana usiku tukazungumza mengi na tukaona basi wewe ni mkubwa una haki ya kuchagua.

Kama umeona vane anafaa basi tumekubali lakini isiwe haraka haraka kuingia katika ndoa mnahitaji kujuana Zaidi".

Hansy alijikuta anafurahi kusikia vile,
" Siamini hiki nachokisikia kutoka kwenu wazazi wangu.
Asanteni sana kwa kujali Furaha Yangu.
Asante baba... asante mama.
Nawaahidi nanyi ipo siku mtafahamu kuwa vane ni mwanamke mwema".

Hansy alimkumbatia baba yake hakika alifurahi sana.
Lakini Erick Alishangaa kwamba imekuwaje wazazi wake wamekubali kiurahisi hansy awe na kijakazi vane.

Moyoni Alijisemea si bule huwenda Vane ni mchawi kuna namna amefanya sio bule.
Alibaki anatikisa kichwa hakutegemea kama wazazi watakubali.

Aliitwa na bibie Vane na kupokelewa sasa kwa wema kama mkwe wao mtarajiwa.
Binti aliambiwa kuwa aache kuvaa sare za kijakazi hata kama atafanya kazi lakini awe anavaa mavazi ya kawaida tu.

Vane alifurahi sana akamkumbatiana na mama mkwe wake na kupeana mkono na baba hatiamae walipata ushindi yeye na Mpenzi wake Hansy.

Chai iliandaliwa pale na Vane akawekwa mezani kunywa na wanafamilia kama kumpokea huku Mr makuka akiwapa nasaha mbalimbali.
Muda wote huo Erick alikuwa amehamaki tu Ndipo mala sms ikaingia katika simu yake.

Ni mama yake Ndie alimtumia sms iliyosomeka,
"isikushangaze Erick huu ni Mpango tumepanga na baba yenu hakuna aliempokea huyu kijakazi".

Erick alitabasamu Ndipo akatazamana na mama yake walau alipata nguvu nae ya kwenda kunywa chai.

Basi baada ya tukio hilo Ndipo watu walitwanyika nyumba nzima wakabakia mwasifa na vane.
Vane alikuwa akifurahi sana Ndipo Mwasifa akamuambia,
"Shoga kuna kitu nimekiona kwa mama Hansy Wakati ule mnakunywa chai alitazamana na Erick wakacheka napata wasiwasi".
"Mhhh kweli?"
"Kweli kuwa makini nao usiwaamini sana" .
"Asante mwasifa kwa kuwa upande Wangu umenishtua ngoja tuone".

Vane mwenye aliendelea zake na majukumu hakuwa na hiyana licha ya kuwa ametambulishwa kama mchumba wa Hansy.

Basi mama Hansy alikwenda mpaka nyumbani kwa Bi Rose mama yake na Ester.
Kufika alipokelewa vizuri na mwanamama huyo, walisalimiana na Kuingia ndani....

Siijui itakuwaje?
Tukutane sehemu ya..... 8*ME&YOU*

SEHEMU YA.... 8
Na

Mamuh mohd
(0716730000)

Tulipoishia......

Basi mama hansy alikwenda mpaka nyumbani kwa Bi Rose mama yake na Ester.
Kufikia alipokelewa vizuri na mwanamama huyo wakasalimiana na Kuingia Ndani....

SONGA NAYO.....

"Swahiba mguu huu ni wako... Nimekuja kukuambia hayo yanayoendelea juu ya Hansy".

"Mhhh amekubali atamuoa Ester au?"
"Mwenzangu kumbe kukataa kwake Sababu ni kijakazi mmoja yupo pale nyumbani anaitwa Vane.
Wana mahusiano ya kimapenzi jana usiku ndo nimepata Habari rasmi Kutoka kwa mwanangu Erick.
Jamani nimefoka mimi na baba yake lakini cha ajabu Hansy kawa mkali hafai.
Yaani amefikia hatua anasema eti kama Hatumtaki huyo vane basi ataondoka nae si balaa hilo".

Bi Rose alishangaa kusikia vile,

" Jamani hili mbona balaa kwanini lakini? Yani anamkataa Ester Sababu ya kijakazi? Kwaiyo umekuja hapa kuniambia nini mama Hansy kwamba Hatamuoa Ester si Ndio ".
" Hapana... Baba Hansy alisema kwamba tujifanye tumekubali ili Hansy asihitishe zoezi lake la kutaka kuondoka, alafu sisi tudili na Huyo vane kimya kimya".
" Mhhh mbona mazito? Afadhali hata mwanangu hayupo maana angekuwepo angejisikia vibaya sana.
Mama hansy au mwanao amerogwa jamani kweli?"
" Yani hata mimi sielewi mwenzako habari ndo Hiyo hapa sasa tupange Cha Kufanya".

" Mama Hansy wewe ni Rafiki Yangu wa siku Nyingi, bila shaka unanifahamu vizuri nikitaka Langu basi mpaka litimie.
Ester anampenda Hansy sipo Tayari kumuumiza Binti Yangu.
Tutakula sahani moja na huyo mwanamke kijakazi ".
" Sawa sawa...mimi. nachotaka aondoke tu aniachie mwanangu Hansy ili amuoe Ester"
" Hii kazi ndogo Rafiki Yangu Subiri atafurahia shoo.
Ametoka kijijini kwao huko anajua mjini kuna wanaume wa kirahisi tu kama Hansy mbona ameula wa chuya".

Mama hansy alifurahi kuona mama Ester kamuunga mkono ivyo kazi itakuwa rahisi.

Upande wa Hansy alikuwa zake ofisini na rafiki yake mmoja aliletwa Amon. Alikuwa akimsimulia kuhusu vane kuwa ni mwanamke waliekutana nae Wakati wameenda katika utafiti ivyo anampenda.
Amon kwanza alicheka.
" Aisee kweli kukutana kwa watu ni siri ya Mungu.
Tulikwenda kufanya utafiti lakini Sababu kuu ilikuwa ukutane na mwenza ws maisha.
Niwapongeze tu na ututambulishe rasmi sasa shemeji yetu".

Walikuwa wakicheka hapo Ndipo mala Aliingia mgeni chumbani humo.
Mgeni Huyo alikuwa si mwingine ni bibie Ester.

Hansy Alishangaa kumuona, Amon kuona ivyo akaamua kuaga na kutoka zake nnje kuwapa nafasi wazungumze.
" Ester umekuja kufuata nini hapa?"
" Ni wewe Hansy  nimefanya jitihada mpaka nimefika.
Nimekuletea zawadi hii saa nzuri sana nimeinunua laki 3".

" Ester mbona unajisumbua yote haya kwanini? Kumbuka nimeshakwambia suala la mimi kuwa na wewe haliwezekani.

Sasa nikuambie tu ukweli mimi ninae mpenzi Wangu Tayari.
Tunapendana sana hata wazazi Wangu wanafahamu na wametubariki".

Ester aliumia kusikia vile,
" Hansy naomba usiniumize kiasi icho kama wazazi wako walikuwa wanafahamu hilo kwanini wamenipokea na mimi? "
" Hawakujua mwanzo ila Tayari nimeshawaelewesha kama hauamini nenda hata Sasaivi nyumbani kamuulize mama atakuambia.
Kwaiyo Ester wanaume ni Wengi utapata wa kupendana nae na mwema Zaidi Yangu wala usijali".

Ester aliumia sana Ndipo akatoka Pasina hata kuaga mpaka nnje Kwenye Gari lake akaondoka zake.

Baada ya Ester kuondoka Ndipo Alirudi yule amoni rafiki yake na Hansy katika ofisi ile ya hansy.

" Vipi mbona mrembo kaondoka kwa hasira ndo shemeji yetu nini? "

" Kwani wewe haumfahamu Vane?.."

" Namjua ile siku mmerudi tupo Pamoja lakini si unajua mjini hapa huwenda kabadilika na hata ivyo sikumkalilia vizuri".

" Hapana huyu ni Ester mwanamke ambae wazazi Wangu walimtarajia nimuoe".

" Ahhh kwaiyo umekaidi amri ya wazazi wako au? Mbona kama sikuelewi ila tu usiniambie kuwa huyu umemkataa Sababu ya huyo Vane".

" Huu Ndio ukweli amon.

Nampenda sana Vane kiasi kwamba sioni hata ambacho huyu amemzidi na simaanishi labda Ester huyu ni mbaya Hapana ila Moyo Wangu umempenda Vane".

" Mhhh sawa ila ungefikilia mala mbili Hansy unajua kuchagua hakutaki haraka au kuzingatia matamanio mke mwema ana vigezo vyake Ndio maana hata Wazazi wameamua kukusaidia ungewasikiliza".

" Mhhh ebu tuachane na hayo amon tuzungumzia kazi zetu kwanza". Walicheka hapo na kweli wakabadili mada na sasa wakazungumzia habari zingine.

Ester kumbe alipotoka kule ofisini kwa Hansy akarudi nyumbani kwao. Kufika ndo kama bahati akamkuta na mama Hansy bado hajaondoka.

" Mama mmenidanganya nyote nyie wawili mama unapanga na huyu anakudanganya tayari kumbe Hansy ameshawatambulisha mwanamke mwingine na wamempokea.... ".

Bi rose ndipo akasimama na kumtuliza binti yake.
"Haswaaa hicho ndicho kilichomleta hapa kaa nikuelezee sasa".
Ester kweli alikaa akaelewa kila kitu kuwa ni mpango waliopanga ili kumtuliza Hansy sasa wana kazi ya kufanya kuhakikisha wanatenganisha wale wawili

Ester alitafakari kwa muda kisha akawajibu wazazi wao wale.
"Sidhani kama itakuwa rahisi kuwaachanisha watu wanaopendana kwa dhati. Lakini nina Mapenzi ya dhati kwa Hansy sitamani kuachana nae".

"Hilo ndo tunalotaka sisi hapa lazima tumuoneshe hii kazi niachie mimi mama hansy.
Wewe jioneshe mwema kama mlivyokubaliana kisha mimi nitajua cha kufanya".
Alijibu mama Ester Ndipo wote wakakubaliana haijulikani ni kitu gani icho watakachokifanya.

Basi siku zilizidi Kwenda ambapo mwanzo vane alikuwa na wasiwasi alipoambiwa na Mwasifa kuwa Awe makini.
Cha ajabu alishangaa kwamba Familia ya Hansy hawaoneshi chuki nae.

Hata Erick alianza kusalimiana nae vizuri hapo ndo aliweka imani kabisa kwamba Wameshamkubali familia hiyo yote.

Basi  kutokana na hivyo hansy aliona asichelewe akawaeleza wazazi wake kuwa anahitaji  kumvalisha Pete Vane kama ombi la kutaka kufunga nae ndoa. Kwa wakati huo Mr makuka alikuwa amesafiri nnje ya nchi kikazi Ndipo walikubaliana wamsubiri akirudi Ndipo shuhuli hiyo itafanyika.

Mama Hansy kuona Mipango hiyo imeanza Ndipo akampigia simu Bi rose.

"Naoma mambo yanakawia Hansy yupo serious anataka kumuoa huyu sasa endeleeeni kuchelewa.
Hapa baba yake amesafiri Akirudi anamvalisha Pete simtaki huyu kijakazi kuwa mkamwana Wangu fanya kitu bi rose".
" Sawa niachie mimi huyo nitampoteza hatokaa amuone kamwe katika maisha yake subiri".
" Haya jitahidi baba Hansy anarudi wiki ijayo fanya haraka".
Basi walikubaliana bi rose akaahidi kwamba atafanya kitu haraka kuzuia.

Basi  siku mbili zilipita ndipo siku hiyo majira ya Asubuhi  vane aliamka kama kawaida kuanza majukumu yake.

Mala gafla alisikia geti linagongwa ndipo akaenda yeye kufungua geti.

Alimkuta kijana Ndipo wakamuuliza,
"Samahani namuulizia Vane"
"Mimi ndie Vane pana shida?"
"Nimetumwa kuja kukuchukua na Hansy kasema mnatakiwa kwenda kufanya shopping ya maandalizi ya shuhuli yenu".
Binti alitabasamu Kusikia vile,
" Kwa sasa si yupo Kazini au? Hata mimi ni majukumu nafanya lakini sawa naheshimu Zawadi yake wacha nikajiandae nakuja".
Vane akaingia ndani sasa na kumpa habari zile Mwasifa.

" Hansy katuma usafiri niende tukanunue nguo za shuhuli ya Pete "
" Wacha weee... Usinikose na Mimi kagaoni rafiki Yangu"
" Naachaje kwa mfano... Ngoja niwahi kipenzi ".
Binti vane alivaa na kushika simu akamuandikia sms Hansy kwani nae sasa alikuwa mtumiaji mzuri wa simu.

" Nakuja mpenzi".
Kisha Ndipo alitoka mpaka nnje Kwenye Gari alilokuja nalo kijana yule akaondoka nae.....

Sijui itakuwaje?
Tukutane sehemu ya 9*ME&YOU*

SEHEMU YA.... 9
Na
Mamuh mohd
(0716730000)

Tuliposhia.....

Binti vane alivaa na kushika simu akamuandikia sms Hansy kwani nae sasa alikuwa mtumiaji mzuri wa simu.

"Nakuja mpenzi".
Kisha Ndipo alitoka mpaka nnje Kwenye gari alilokuja nalo kijana yule akaondoka nae....

SONGA NAYO......

Vane akiwa kwenye gari Ndipo malaa akaona simu inaita.
Kuangalia alikuwa ni Hansy Ndie kampigia.
Bibie akapokea simu ile,
"Haloo"
" Nimeona sms yako Umesema unakuja mbona hujaniambia mapema nikuelekeze".
Vane Alishangaa kusikia vile Ndipo mala gafla simu ya vane ilikatwa na kuzimwa na Binti alizibwa mdomo Ndipo sasa alielewa wale sio watu wazuri kwake.

Wakati huo Hansy nae alibaki ameduwaa Ndipo akawa anapiga tena namba za Vane lakini simu ikawa haipatikani tena.
Basi aliona wacha Asubiri akifika watazungumza maana alimuambia kuwa anakwenda.

Vane alipelekwa mpaka katika nyumba moja akashushwa na kuingizwa ndani.
ilikuwa ni nyumba moja ambayo haijaisha vizuri (gofu).
Huko alimkuta mwanamama mmoja ambae alikuwa si mwingine ni bi rose mama yake na Ester.

Vane alishangaa akamtazama kwa hofu.

"Shikamoo mama sina makosa mimi naomba nisaidie"
"Mhhh sina shida na shikamoo kutoka kwako.
Wewe mtu Mdogo sana mbaya, mshamba huwezi kuharibu Furaha ya mwanangu.
Hiki nachokufanyia Leo ni utangulizi tu najua hautakuwa na Hansy tena na ukileta za kuleta nakumalizia kabisa".

Mama yule alikuwa ameshika chupa yenyew dawa kali kiasi kwamba yaye mwenyewe kuna miwani aliivaa alafu akampulizia vane Machoni.

Bunti alipiga kelele huku mwanamama yule bila huruma alimpulizia yote kama ni dawa basi alioverdose.
"Niliambiwa inatumika kidogo lakini nimekupulizia yote mjinga ukafie mbali".
Vane mpaka alipoteza fahamu kwa maumivu aliyoyapata pale.
Kisha mwanamama bi Rose kuna kitu aliwaambiwa vijana wake wale wa kazi wafanye.
Kweli walifanya wslichukua simu ya Vane na kumpigia simu Hansy kwani walipewa namba ya Hansy na bi rose.
Walipoandika tu namba ile likaja jina kwa kuwa Binti vane aliisave.

" Haloo Vane umefika wapi nakupigia simu haupokei? "

" Sikiliza vane yupo na sisi, tunahitaji Tsh milioni 20  Ndipo tutamuacha salama tunakupa saa moja tu"
" What? Mnaongea Nini nyie mmempeleka wapi vane? Ni watu gani nyie? Kwanini mmefanya hivyo? "
" Tunakupa saa moja Hansy".
Kisha watu wale walikata simu.

Sasa wanataka  kutengeneza mazingira ya kwamba ionekane vane alitekwa na watu Wengine kabisa ili wasimshuku mtu yoyote.

Hansy alichanganyikiwa alitoka ofisini akiwa amevulugwa kwelikweli.

Alifika mpaka nnje Kwenye gari lake Ndipo akawapigia simu baba na baba yake kuwapa taarifa zile.
Wote walikubaliana wakutane nyumbani.
Mama hansy yeye alikuwa nyumbani sasa Hansy na baba yake ndipo nao walikubaliana warudi nyumbani kuzungumza.

Kweli baada ya muda mchache walikutana Ndipo Baba Hansy akamuambia kijana wake.
"Huyu hatoki mbali lazima anafahamu kuwa vane ana mahusiano na wewe Ndio maana wakamteka na kupiga simu kwako na walikuja kumchukua kwa jina lako.

Wanajua kuwa hela zipo hapa kwanini nae vane alikuwa anawaambia waambia watu huko mtaani ona sasa".

" Baba kwa sasa ni mapema kulaumu nachoona ni hizo pesa zipatikane nimpate vane.
Account Yangu baba ina milion 10 tu Ndio kwanza mishahara yangu  ya miezi 6 hii naitunza kwanza naomba nifanikishie zilizobakia nikamtoe vane Wangu alipo".

" Mwanangu Sijui kama utaniamini ila kampuni iliyumba kidogo na bila shaka unafahamu hilo  tulitumia ela Nyingi sana kuiweka sawa ivyo sina balance hiyo.
Azima Popete mwisho wa mwezi huu zinaingia takriban milioni 50 kwenye kampuni tutalipa".
" Baba naazima wapi bado milioni 10 tu... Ok wait nikaandike barua ofisini nitapata hizo pesa".
Hansy alitoka huku amechanganyikiwa machozi yanamtoka.

Mama hansy walitazamana na mumewe wakafurahi kwa maana wanajua kila kitu.

" Bi rose apewe maua yake kamuweza kajua kucheza mchezo sijui kampeleka wapi?"

" Mhhh yani alinipigia simu akaniambia kuwa wamemuambia atoe hela tujikaushe na hata ofisini anapokwenda bi rose na huyo manager wana mahusiano ivyo lazima atamzuia asimpe hizo ela".
" Bi rose hatari jamani mhhh".
Walikuwa wakinong'ona wazazi hao".

Basi Hansy Alifika  mpaka ofisini tena Ndipo akaenda kuzungumza na mkurugunzi wao Ambae huwa anamuamini sana Hansy katika kazi.

Hansy alimueleza kila kitu Ndipo mkurugunzi yule alieitwa Dk Solomom akamjibu hansy.

"imekuwa gafla sana kuomba kiasi kama hicho.

Juzi tu mushahara imetoka bado hatujakaa sawa".

Hansy alipiga mpaka magoti kwa mkurugenzi wake huyo.

"Naomba nielewe Tafadhali Nipo Kwenye hali Mbaya  sana  Tafadhali".

" Hansy wewe si wa kunipigia magoti kwanza naumia kukosa kukupatia mtumishi Bora kabisa.

Naomba nipe muda Leo nipambane hata kwa watu wangu wa Karibu nitakufanikishia".

Hansy aliamua kuinuka na kuondoka zake akiwa amechanganyikiwa.

Basi mala alipigiwa simu na mama yake,
" Hansy uko wapi mwanangu? "
" Mama acha tu sijielewi Wazazi wangu naumia mimi mtoto wa watu jamani ahhhh".
" Sikiliza tumepata wazo hapa na baba yako... Ongea na Ester anaweza kukupatia mama yake mfanyabiashara mkubwa".

Hansy hakuuliza mala mbili alikumbuka namba za ester anazo mala kwa mala alikuwa akimtumia sms basi  alimpigia.

" Haloo Ester nina shida Tafadhali naomba msaada wako? "

" Hansy shida nini mbona naogopa "

" Naomba milioni 10 niazimie hata kwa mama yako... Tafadhali nakuomba Ester"

" Haina haja ya kumuambia mama Yangu ninazo hizo pesa nitajie account namba yako bank nikuwekee au nikuletee ulipo".

" Sawa niwekee Kwenye account Yangu nakutumia Sasaiv nitoe pamoja asante sana Ester"

" Sawa maliza changamoto  uliyokuwa nayo kwanza kisha tutaongea".

" Asante Ester".

Alijibu hansy kwa heshima ya hali ya juu kwa kuwa alikuwa na shida siku hiyo alikuwa mpole kwa Ester.

Kweli baada ya dakika 10 Pesa iliingia katika account ya Hansy kutoka kwa bibie Ester.
Hansy kwa Haraka haraka alipiga tena namba ya Vane ikapokelewa.

"Tayari pesa ipo Tayari yupo wapi vane".
"Sawa  njoo mahali nakutumia ujumbe fika Haraka sana bila kuchelewa ukiwa na pesa hizo ".
Hansy ni kama alikuwa mjinga kwa Wakati huo kila anachoambiwa anafuata alianza safari.

Mala alipigiwa simu tena na baba yake akiwa njiani kwenye gari.

" Hansy nimeshawaambia polisi habari hizi inabidi tukawakamate".

" Baba usijali pesa si kitu Mbele ya utu namfuata vane kuna mahali wameniambia niende"

" Usiende peke yako tuelekeze na utusubiri twende wote na askari".

" Sawa".

Hansy alimpa Maelekezo baba yake anapoeelekea inamaana wanamfuata yeye anatangulia kwenye kumchukua vane.

Alifika katika jengo lile akaambiwa jinsi lilivyo akaona bila shaka ni hapo.

Hansy alishuka Kwenye gari akiwa na begi alililoweka pesa na Kupiga tena namba ya vane.
Alisikia simu ikiita kutokea ndani pale lakini haikupokelewa.
Hapo hansy alipata uhakika kuwa Ndipo pale alijikaza mwanaume akaingia mpaka ndani.

Kufika Ndipo alikagua chumba kimoja kimoja Ndipo alifanikiwa kumkuta Vane akiwa amelala yupo kimya.

Wale vijana hawakuwepo alikuwepo vane peke yake.
Hansy aliinama na kumgusa Vane huku akimuita,
"Vane...vane...".

Binti alikuwa akihema lakini akionekana kuwa hoi taabani.

Hansy haraka alimbeba Vane na kutoka nae nnje mpaka kwenye gari lake nia amuwahishe hospital.
Lakini Ndipo baba yake akiwa na askari nao walifika na kumkuta Hansy akiwa analia sana huku kabeba vane mikono mwake...

Sijui itakuwaje?
Tukutane sehemu ya 10*ME&YOU*

SEHEMU YA..... 10
Na
Mamuh Mohd
(0716730000)

Tuliposhia......

Lakini Ndipo baba yake akiwa na askari nao walifika na kumkuta Hansy akiwa analia sana huku kambeba vane mikoni mwake...

SONGA NAYO......

Baba hansy alimsogelea kijana wake kwanza akamtazama, kisha alimtazama vane aliekuwa kimya hazungumzi chochote.

"Baba vane Wangu baba naomba niwahi hospital tumechelewa pamoja na kwamba nimepambana sana ila naamini atakuwa mzima"
"Sawa kijana Wangu twende Hospital... Polisi watabakia hapa wanafanya uchunguzi huku sisi tunawahi hospital".
Basi kweli hansy aliondoka akiwa na na baba yake kwenda sasa hospital.

Wakiwa njiani baba hansy aliwasiliana na mkewe na kumueleza kuwa wamempata vane akiwa kwenye hali Mbaya na sasa wanampeleka hospital.

Walifanikiwa kufika na Binti alipokelewa na kuanza kufanyiwa Uchunguzi huku hansy na Familia yake wakiwepo nnje Kusubiri kuona hali itakuwaje.

Zilipita siku tatu Ndipo Majibu yalionekana kuwa Vane alipuliziwa tindikali kali sana ivyo kwa kiasi fulani imeharibu macho yake Kiasi cha Binti kufungwa bandeji usoni kwa maana hawezi kuona Kabisa.

Taarifa zile zilikuwa mbaya kwa hansy, aliumia kupita kiasi moyo ulimuuma, alipokwenda nae kumuona vane akiwa katika hali ile ndipo alichanganyikiwa hansy.

Hansy alipata mpaka uchizi kiasi cha kwamba akawa hajielewi kwa Maumivu yale aliyokuwa nayo.

ilibidi nae aanze kufanyiwa Matibabu lakini Bado hali yake haikuwa sawa na kila mala alikuwa akumuita vane.
Kila mtu aliekuwa Mbele yake yeye alimuita vane hakika alichanganyikiwa sio kawaida.

*BAADA YA MIEZI 6*

ilipita Miezi sita tokea   majanga hayo yatokee.
Vane alirudi nyumbani pale lakini akiwa katika hali ile ya kutokuona.

Kwa wakati huo Hansy alikuwa nnje ya nchi akipatiwa Matibabu, kutokana na kuchanganyikiwa kwake baba yake alimpeleka kijana wake nnje ya nchi kuhakikisha anakuw salama salmini.

Basi siku hiyo nyumbani kwa  kina Hansy alikuwepo bi rose pamoja na mwanae ester.
Walikuwa wakifanya maandazi ya kurudi kwa Hansy na baba yake.
Hakika haikuwa rahisi Kabisa kwa hansy kuupokea ukweli ule.

Mama hansy alimfuata Ester ambae alikuwa amejipamba na kupendeza kwelikweli.

"Hansy anarudi leo baada ya kutokea makubwa sana.
Kiukweli sikutegemea kama mwanangu angepitia haya tulifanya kosa kubwa sana Ambalo hatukumuwazia hansy angelipokeaje?.
Yote kwa yote anarudi akiwa mzima Ndio Furaha yetu... hansy amekaa na wanasaikolojia huko wakalifuta kabisa jila la vane halikumbuki tena hivyo hatakiwi hata kutajiwa.
Kwa sasa ni kama anaanza upya ni Wakati wako wewe kumuonesha upendo akuone Mwanamke wa pekee kwake"

" Asante sana mama kwa hili nafurahi sans kuona wazazi Wangu mmenipambania japo kuna muda ni kama ilikuwa vigumu kwetu tukahisi tunampoteza hansy  lakini si haba.... kwaiyo atakuwa hanikumbuki kabisa?"

" Ndio kwa sasa hakumbuki chochote Zaidi ya sisi wazazi wake na kazi yake Sababu amesoma sana.

ilibidi wanasaikolojia wamuoneshe picha za Familia yake ndipo alianza kutukumbuka na tulituma picha za ofisini kwake na wafanyakazi wenzake akakumbuka ila kuhusu vane hatakiwi kugusiwa kabisa".

" Sawa mama hakika nimeelewa kila kitu kitakuwa sawa".

Walikubaliana hayo na kwa Wakati huo Vane alifungiwa katika chumba kimoja wapo Ndani ya nyumba hiyo.
Alikuwa hatakiwi kutoka nnje.
Chakula alikuwa akipelekewa na mwasifa.

Mwasifa alikuwa akiumia sana lakini kwa kuwa alikatazwa asiseme chochote anyamaze kwa ajili ya kulinda kazi ilibidi afanye ivyo.

Lakini siku hiyo mwasifa akiwa amekaa na Vane akimlisha Chakula huku akilia sana.
Ndipo walifika wamama wale wawili chumbani humo mama hansy na mama Ester.

"Haya Mwanangu Hansy anarudi wewe vane tumekaa na wewe hapa bila shaka umepona.
Mwanangu asije kukukuta hapa likawa balaa jingine unatakiwa Kwenda mbali sana na hapa".

Mwasifa aliumia kusikia vile,
"Mama tafadhali naomba msimtoe hapa angalia hali yake atakwenda wapi vane nakuomba mama".
"Wewe unanipangia kama nani? Hii ni amri Yangu aseme yeye mwenyewe kwao ni wapi afikishwe stendi apandishwe basi kwingine atafikaga tu haya muinue atoke aondoke".

Mwasifa Alizidi kulia, hata vane aliishia kulia tu hajui aseme nini hansy amemkosa na bado amembulia matatizo makubwa sana.

Walimtoa vane mpaka nnje Kwenye Gari na kupewa Maelekezo dereva akampandishe basi la Kwenda mkoa atakaochagua aondoke zake huko. Walijua kwa hali aliyokuwa kurudi itakuwa ngumu kwake...vane aliondoka na kumuacha Mwasifa akiwa analia sio kawaida.

Hata Ester alikuwa ndani akiangalia kupitia dirishani, kiubinadamu iliumiza lakini hakuwa na jinsi maana Mpango ule waliupanga wote ili kuhakikisha anakuwa na Hansy.

Mwasifa aliingia mpaka ndani Ndipo kufika Sebleni akamkuta Ester. Walitazamana sana Ndipo Mwasifa hakusema neno akaenda mpaka Chumbani Ambapo alikuwa akilala na vane Wakati bado ni mzima. Alikumbuka kwamba waliishi maisha Mazuri ya Furaha na amani. Alikumbuka mpaka siku ambayo Vane alitoka akisema amefuatwa na gari kwenda kwa Hansy na Ndipo ukawa mwanzo wa majanga na matatizo.

"Hii sio sawa, kwa jinsi walivyo hawa ndio wamemfanyia vane Mipango yote hii.
Mama hansy amejifanya kama hajui kitu lakini muongo wanajua hawa".

Mwasifa aliangalia eneo ambapo palikuwa panakaa nguo za vane pia simu yake ilibakia.
"Nitahakikisha Hansy anamkumbuka tu vane.

Sio watumie hali aliyokuwa nayo, hizi nguo na humu kwenye simu kuna picha za vane na Hansy nitahakikisha namuonesha ipo siku atamkumbuka vane na atamtafuta, hansy najua atampata vane na atajitahidi kwa gharama zake atampeleka akatibiwe". Alikuwa akijiambia mwasifa yani ni kama anajenga taswira yake jinsi inavyokuwa kuwa hansy atampata vane na atamtibia atapona jambo ambalo kwa sasa sio Rahisi kabisa kupokea.

Hakika mwasifa alikuwa ni rafiki mzuri wa vane walipendana sana Ndio Sababu japo Vane  kaondoka lakini alijiapiza kuwa atahakikisha hansy anamkumbuka vane.

Basi muda ulipowadia Kweli Hansy na baba yake Walifika nyumbani na kupokelewa vizuri.
Walifika marafiki zake wa kazini na familia yake kama kumpa pole pia kwa hali aliyopitia.

Hansy alipowatazama  marafiki zake aliwakumbuka maana alikuwa akiona picha zao, pia wazazi wake aliwakumbuka.
Lakini mapokezi ya bibie Ester yalimpa maswali mengi kuwa ni nani kwake.
Ndipo mama yake alimuambia kuwa ni mchumba wake wanatarajia kufunga ndoa.

Hansy kwenye akili yake hakumbuki kama aliwahi kuwa na mchumba mpaka wakataka kufunga ndoa.
ikibidi aitikie tu maana alichojua alikuwa anaumwa ivyo alijisemea kidogo kidogo atazoea.

Basi muda wa Chakula ilipofika, mwasifa aliandaa vizuri na alikuwa amevaa sare za mpishi huku amejifunga khanga ambayo Vane alikuwa akiivaa mala kwa mala.
Pia walikuwa na taratibu za kusimama pembeni mpaka wanafamilia wamalize kula chakula.

Mwasifa alisimama upande wa jaribu na Hansy Ambapo alikuwa akipenda kusimama vane.
Binti alitumia akili ya ziada nia amkumbushe Hansy kuwa aliwahi kumpenda mwanamke anaitwa vane ndie chanzo mpaka akapata ugonjwa wa akili.

Kweli Wakati wanafamilia waliendelea kula, hansy yeye alikuwa akiangalia Mbele yake anamuona mfanyakazi yule, sasa jinsi alivyovaa kama vane na sehemu aliyosimama alikumbuka kama aliwahi kupitia maisha hayo.
Alianza kuvuta kumbukumbu kwamba kuna Mwanamke alikuwa akisimama sehemu hizo mwenyewe nguo hizo.

Hansy alibaki akimtazama mfanyakazi huyo Ambae ni mwasifa huku wengine hawaelewi wao wanaendelea tu kula chakula.

Upande wa Mfalme mzota usiku huo alikuwa nyumbani na mkewe Malkia "Nuu" ambae alimpa taarifa mumewe kuwa ni mjamzito.

Mfalme alishangaa maana anajua hanaga uwezo wa kuzalisha Mwanamke sasa imekuwaje.

"Umri huu nipate tena mtoto kwa Sababu zipi? Kesho tutakwenda kwa mganga mkuu mguu wako na mguu Wangu kuna kitu utakijua".
"Mmewangu mbona unanitisha kuna nini?"
"Usijali utajua tu".
Basi wakati wamekaa hapo mala kuna kimbunga kilipita mpaka mfalme akashangaa na kuinuka.

"Nini tatizo hakika kuna kitu hakipo sawa? Sijui hali ya mwanangu vane sijui ni mzima? Sijui yupo kwenye hali gani?".
Alijiuliza mfalme mzota kwani hali ile ilimshtua sana.

Sasa upande wa mjini baada ya chakula Ndipo watu walitawanyika.
Ester alimfuata Hansy na kumuinua,
"Haya twende chumbani kwako ukaoge upumzike Mpenzi Wangu?"
"Asante nitakwenda mwenyewe napakumbuka".

Hansy aliondoka zake sehemu hiyo. Aalipoitazama tu nyumba ile kumbukumbu zilikuwa zikimjia kuwa chumba chake kulikuwa sehemu gani.

Lakini alipofikia katika chumba ambacho Alikuwa akilala bible vane ni kama kuna harufu fulani ilimjia Ndipo alibaki anajiuliza mbona kama kuna kitu anakikumbuka.

Aliunganisha tukio la yule msichana alivyoovaa na Sehemu aliyosimama na pale mlangoni kuna ishara ilimjia Polepole.

Wakati huo mama hansy na bi Rose walimtaka Ester aende chumbani kwa hansy akamtege ili akubali  kutembea nae kupata Sababu ya kuwahisha harusi.

Kweli Ester alikwenda chumbani kwa hansy na kuwaacha wazazi wale wakichekelea.
Mwasifa alikuwa akiwasikiliza machozi yakimtoka,

"Wamama wabaya nyie kama ester akitembea na Hansy basi atatumika na kuachwa hakuna ndoa hapa mpaka hansy amkumbuke Vane ndicho kitu pekee nachoweza kufanya kama kumlipia vane kwa mlichomfanyia". Alijisemea mwasifa alikuwa na hasira kwelikweli....

Sijui itakuwaje?
Tukutane sehemu ya 11*ME&YOU*

SEHEMU YA..... 11
Na
Mamuh Mohd
(0716730000)

Tuliposhia.......

"... Hakuna ndoa hapa mpaka hansy amkumbuke Vane ndicho kitu pekee nachoweza kufanya kama kumlipia vane kwa mlichomfanyia".
Alijisemea Mwasifa alikuwa na hasira kwelikweli....

SONGA NAYO....

Ester alikwenda mpaka Chumbani kwa Hansy akakuta bado yupo bafuni anaoga.
Ester aliangaza kabatini Ndipo akaangalia na kuchagua nguo Ambazo ni za kulalia.

Aliziweka kitandani kisha nae alibadili nguo akajifunga taulo ambalo alikuta chumbani kule.

Baada ya muda Hansy Alitoka kuoga ndipo akamkuta Ester akiwa katika hali kama ile.
"Mpenzi vaa nguo hizi za kulalia... Nitalala na wewe leo kwa ajili ya kukuangalia hali yako"
" Hapana mbona nipo sawa? Wanasema kuwa tuliwahi kuwa katika mahusiano lakini sikumbuki chochote hata kama niliwahi kuwa Karibu na wewe"

" Ndio maana nasema haupo sawa Hansy maana ungekuwa basi walau unanikumbuka ningesema kweli umepona... Lakini angalia bado unasema haukumbuki chochote ni wazi kwamba haupo sawa.
Ni wazazi ndio wametaka nilale na weee hapa ili kukuangalia jwa ukaribu".
" Lakini angeweza kuja hata Mdogo Wangu erick kwanini wewe?"
" Sababu mimi ni mpenzi wako Hansy".

Hansy Kusikia vile alibaki kimya kwanza nae akijaribu kukumbuka kama aliwahi kuwa Karibu na  Ester lakini kumbukumbu haikuwepi Kabisa.

Basi siku ile ilipita Ndipo palipambazuka Asubuhi na mapema.
Hansy aliamka mapema akajiandaa Tayari kwa kuelekea kazini.
Alimtazama Ester alikuwa amelala basi akaona haina haja ya kumuamsha akamuacha tu nae akaondoka zake.

Kufika jikoni alimkuta Mwasifa akiwa anafanya usafi huku amevaa gaoni Ambalo aliwahi kulivaa Vane siku anakwenda kuonana na Hansy nnje na nyumbani pale.

Hansy alipita pale akamtazama Binti yule hakika kumbukumbu ile ilimjia Kabisa kuwa kuna siku  aliwahi kumuona mwanamke ambae alimvutia machoni mwake akiwa amevaa nguo ile.
Hansy aliona Hapana akawa akamsogelea mwasifa.
"Samahani ivi unaitwa nani?"
"Mimi naitwa mwasifa umenisahau msichana wenu wa kazi nilikuwa rafiki kipenzi na vane".
Hansy alishtuka sasa kusikia jina lile,
"Unasema rafiki yake na nani?"
"Sasa kabla hajajibu tena Mala Mwasifa alisikia akiitwa na mama Hansy.
" Nenda Kazini Hansy mama asije akatukuta hapa lakini naomba tupate muda tuongee".

Kisha mwasifa haraka akakimbia kwanza Kwenda chumbani kubadilisha nguo.

Hansy nae Ilibidi aondoke zake  wazo la bibie mwasifa kwamba amtafute wazungumze Zaidi aliona linafaa kabisa.

Mwasifa alikwenda chumbani akabadili nguo Kisha Ndipo akarudi kuitikia wito wa mama Hansy.
"Wewe nimekuita muda mrefu sans ulikuwa wapi ndo unakuja Sasaivi?"
"Samahani mama nilikuwa nnje kidogo kule nafanya usafi"
"Jiangalie sana wewe... Andaa chai haraka tuna mgeni anatakiwa kula haraka"

" Sawa mama".
Mwasifa alitoka Na kurudi zake jikoni.

Mama hansy alibakia hapo Sebleni Ndipo mala alitoka bibie Ester.
" Shikamoo mama"
" Marhaba mwanangu umeonaje usiku wako wa kwanza kulala na mwanaume unampenda bila shaka umetumia vizuri uanamke wako"
" Mhhh ni kweli mama lakini nahitaji muda  wa kuwa nae Zaidi kama hamtojali naomba niendelee kubakia hapahapa nikae nae huku tukiikaribia ndoa"
" Sawa mwanangu hata mimi jana niliongea na mama yako kabla hajaondoka kuwa iwe ivyo.

Ndoa yenu itakuwa ya Haraka tumepanga weekend hii Mvalishane Pete.... Hapa kuna mtu tumemuandaa atakwenda huko ofisini kwa Hansy atamshawishi naamini atakubali stakuzoea tusimpe nafasi Kabisa ya kukakumbuka kale ka vane".

" Sawa mama nafurahi"

" Haya jiandae unywe chai si unaenda kazini? "

" Ndio nakwenda  mama ngoja nikajiandae kabisa".

" Haya mwanangu".

Mama hansy alifurahi sana aliona hakika mambo yanakwenda kama alivyotaka.

***********

Basi Siku hiyo mfalme Mzota alikwenda kwa mganga wake yule Ambae huws anafahamu mambo yake tokea zamani. Mganga huyo walizoea kumuita mganga mkuu.

"Mganga mkuu nimekuja hapa kwa mambo mawili...kwanza mkwangu  ni mjamzito na unafahamu fika mimi sina uwezo wa kumpatia Mwanamke ujauzito tokea nipate mwanangu yule mmoja tu. Nataka ajue hapa na aseme hiyo mimba ameitia wapi?"

" Mhhhh hiki kitu nilitaka kukuambia siku Nyingi sana lakini tulikuwa tukichenganga....nimegundua kwa sasa una uwezo huo tokea siku nilipokushika nikaona".
" Mganga mkuu una uhakika na hiki unachoniambia? "
"Kabisa hata nikikuangalia Sasaivi naona kabisa hakuna tatizo lolote upo sawa Kabisa hongera".

Mfalme mzota alifurahi kusikia vile,
" Sawa nafurahi Kupata Mtoto wa uzeeni lakini jana kuna hali ilinijia ni kams Binti Yangu Vane yupo matatizoni ebu angalia piga ramli umuangalie"
" Vane kuonekana ni kazi kwa sababu yupo Mbali sana na hapa.

Kumbuka tulifanya kazi kwa ajili yake sidhani kama kuna chochote kibaya kitampata"
" Sawa lakini nahitaji arudi mwanangu... Nataka nimuone Binti Yangu"
" ipo siku Atarudi mfalme lakini kwa sass usimuwaze sana bali muwaze huyu mwanao kijacho aliepo njiani.
Bila shaka atakuwa mtoto wa kiume mrithi wako mkuu akisaidiana na dada yake Vane".
Mfalme kusikia Ivyo alijikutaa anafurahi lakini sisi tunaujua ukweli kwamba kuna asilimia kubwa ujauzito huo usiwe wa Mfalme bali ni wa huyo mganga Ambae alipanga na malkia.

Upande mwingine tena mitaani alionekana msichana Vane Ambae kwa Wakati huo alikuwa hana uwezo wa kuona.

Vane alikuwa akihangaika na kutembea tembea pasipo kujua wapi anatoka wala anapoelekea.
Kulia ilikuwa ndio sehemu ya maisha yake.

Watu mbalimbali wa mtaani hapo walianza kuulizana kuwa Binti yule ametokea wapi? "
Kuna wengine walipata wasiwasi wakadhania labda ni mchawi au mwizi anaetafuta namna ya kuiba na katumwa na wachawi wenzake kwa jinsi alivyo.

Lakini kadri siku zilivyozidi kwenda walianza kumuelewa kuwa ni kweli anaonekana hana uwezo wa kuona na ni kama msichana tu wa mtaani.

Wamama majirani siku hiyo walimuwinda alipopita tena Ndipo wakamfuata na kumshika mkono kwenda nae nyumbani.
"Kina nani nyie naomba msinidhuru Tafadhali"
"Wala usijali ebu sema wewe umetokea wapi na unaishi wapi?"

"Nimetokea Daresalam ambapo niliwaambia wanipandishe mabasi ya kwenda morogoro ili nikifika huko niendelee kuomba nifike nyumbani lakini wamekuja kunishusha huku nasikia ni dodoma niliuliza watu".
"Ohhh pole sana jamani unakula na kulala wapi sasa?"
"Hata sielewi napolala mimi popote tu najilaza sehemu nitakayohisi ni nyumbani kwa mtu nnje nakaa.
Sina hali namuachia muumba tu Ndie ajuaje hatma Yangu".

" Huko ulipokuwa unaishi Daresalam ni kwa nani?"

" Nilikuwa mzima wa afya hakika binadamu sisi ahhh😢😢😢 yamenikuta makubwa sana.. naumia mimi".
Vane aliishia kulia tu alijikuta anaishiwa Maneno hata ya kuzungumza.

" Sisi tunataka kukusaidia maana huku unapohangaika kulala nnje unaweza kukutana na vibaka wakakufanyia kitu kibaya hapo tupu ushukuru... Sisi tutakupeleka mpaka kwenu sawa? "
" Asante niwashukuru sana kwa yalinikuta kweli nahitaji kurudi nyumbani".

Wamama wale Ambao walikuwa ni ndugu waliishi Pamoja walikubaliana wamchukue kwanza ambapo walimuogesha na kumvalisha nguo, walimlisha chakula kwani kwa Wakati huo Vane alikuwa akifanyia kila kitu kutokana na hali yake ya kuwa haoni kitu Chochote.

Siku hiyo Hansy alikuwa akitoka zake kazini Ndipo kuna mtu alimkuta kasimama pembeni ya Gari lake.
Mtu huyo alipomuona Hansy akamsalimia kwa kumchangamkia kana kwamba anamfahamu vizuri.

"Pole kwa matatizo hansy tunashukuru pia kwa sada upo sawa... Mimi ni mwanasaikolojia wakati upo hapa nchini ndo nilikuwa nikikusaidia Saidia mpaka ukaondoka"

"Ohhh sawa nashukuru japo sikukumbuki maana nahisi nakumbuka vichache nina vingi sivukumbuki"

"Ahhh nenda Polepole utakumbuka usilazimishe akili Mwishowe ukazua matatizo Zaidi"

"Ndio nakubali shukurani"

"Nimekuja hapa kuna jambo nataka kukuambia"

"Jambo gani tena?"

"Kuhusu wewe ili uzidi kuimarika unatakiwa ufunge ndoa... Muoe yule mchumba wako Ester utakuwa sawa"

"Kwani hata wewe unafahamu kama Ester alikuwa mpenzi Wangu binafsi sikumbuki hata"

"Ohhh Ester alikuwa mchumba wako tena mlikuwa mnaelelekea katika hatua nzuri ya Kufunga ndoa ndo gafla ukaangukaga ukapoteza kumbukumbu".

" Mhh sawa naendelea kukumbuka ila nahisi kipo kitu kikubwa sana nikikumbuka Hicho kitafanya nikumbuke na mengine yote kinakuja kabisa akilini Kwangu ila daaah".

" Hapana usilazimishe iwe ivyo Hansy... Kwa sasa ishi maisha yako sawa".

" Sawa nashukuru "

" Haya nikutakie jioni njema ".

Basi Hansy alipanda zake kwenye gari na kuondoka.
Yule mwanasaikolojia alibaki akimtazama tu huku akijisemea,
" Tayari kazi ya mama hansy nimeifanya bila shaka atakubali kumuoe Ester.... ".
inamaana hapo Ndipo tunapata kujua kuwa huyi mtu alitumwa na mama Hansy.

Upande wa ofisini kule kwa hansy alibakia yule rafiki yake wa kuitwa amon akiwa anazungumza na muhudumu wao wa mapokezi.
"Hansy amerudi lakini hajanichangamkia kama tulivyozoeana bado buana hayupo sawa daa!!"

"Kupoteza kumbukumbu si mchezo inaonesha huyo mwanamke alimpemnda sana"

"Acha kabisa yani siku tuamue hapa kumchana ukweli kuhusu vane nahisi atakumbuka kila kitu sema ndo ivyo tumekatazwa na familia yake ila inauma"

"Kwani ilikuwaje mpaka akapoteza fahamu"

"Alitekwa vane wakamfanyia unyama akawa haoni na haijulikani ni watu gani?"

"Aiseee pengine wangemuacha tu Hansy Akirudi amkute ingesaidia akae sawa"

" Sidhani labda wamefanya kumtoa pale ili amsahau maana kwa hali aliyokuwa nayo huyo vane wazazi wa Hansy ilijuwa ngumu sana kumkubalia kuwa mkwe wao.
Sasa hana budi kumuoa Ester yani nikifikilia kwa undani nahisi kama njama ilitengenezwa sasa ndo hawakujua kama ingemuathiri na Hansy ".

" Mhhh mbona kazi haya ngoja tuone".
ilikuwa ni gumzo ofisini hapo juu ya ujio wa Hansy ofisini hapo baada ya kuwa mbali na hapo kwa muda mrefu.

Basi usiku wanafamilia walikuwa mezani wakipata chakula, Hansy Ndipo aliambiwa kuwa ajiandae siku mbili izi wanavalishana pete na Ester kujianda kufunga ndoa.
Hansy yeye alikuwa akimtazama Mwasifa tu ambae alikuwa amevaa nguo kams ya vane na nguo ya kazi kwa juu.
Hali ile ilimtesa Hansy Ni kama kuna kitu anataka kukumbuka.
Alijisemea kuwa watu wakishalala basi atakwenda kuzungumza na mwasifa.

Chakula kilimalizizika Ndipo watu walikwenda kulala.

Ester kama kawaida aliekwenda chumbani kwa hansy.

"Ester ni sawa wewe unaweza mpenzi Wangu lakini hatujafunga ndoa na nipo sawa unaweza kwenda kulala chumba kingine"
"Hansy kwanini? inamaana hauna hisia zozote juu yangu.
Nipo hapa pia hata ukihitaji kufurahi nitakupatia".
Aliongea hayo Ester huku akiwa anamtega hansy kwa ukaribu akiamini ni mwanaume hawezi kuutegua mtego ule.

Sasa ilikwenda mpaka Asubuhi Ndipo Hansy aliamka na kuona pamekucha.

Alikumbuka kuwa alikuwa na mpango wa kwenda kuzungumza na mwasifa usiku lakini Tayari alirubuniwa na Ester mpaka wakalala pamoja na baada ya hapo alipitiwa na usingizi mzito.

Alimtazama Ester akaona saws huwenda kweli alikuwa Ndie mpenzi wake wazazi na watu wake wa Karibu hawawezi kumdanganya.

Alitoka sasa akamuacha Ester amelala akatoka kumfuata mwasifa.
Alimkuta Binti anafanya usafi jikoni,
"Kaka Hansy mbona upo hapa na nguo hizi za kulalia?"
"Niambie ulichotaka kuniambia unajua nini?"

"Mhhh kwanza umelala na Ester kama mke na mume?"
"Ahhh mambo ya faragha hayo achana nayo".
"Pole umeshamsahau kabisa vane... Vane wako ameumizwa kwa Sababu yako mpaka amekuwa haoni na kutolewa hapa kama mnyama... Usingemfanyia hivyo".

Mwasifa alichukua simu ya vane na kumuonesha picha,
"Angalia hii picha yenu mlipiga siku umetoka nae vane wako".

Hansy alishtuka hadi kichwa kilimuuma,.

Mwasifa akawa anasikia ujio wa mtu anakuja akaona ile kesi akakimbia na simu yake akatoka nnje.

Alikuwa ni Ester akimtafuta Hansy.
Alimkuta ameinama chini ameshika kichwa, anakumbuka sasa kweli Mwanamke yule wa kuitwa vane alimpenda sana.
Matukio yalianza kurudi tokea siku anakutana nae kule ndani ya maji mpaka akaja nae nyumbani kwao.
Yote hayo sasa yalirudi kichwani kwa Hansy .....

Sijui itakuwaje?
Tukutane sehemu ya 12*ME & YOU*12_16

SEHEMU YA..... 12
Na
Mamuh mohd
(0716730000)

Tulipoishia.......

Matukio yalianza kurudi tokea siku anakutana nae kule ndani ya maji mpaka akaja nae nyumbani kwao. Yote hayo sasa yalirudi kichwani kwa Hansy.....

SONGA NAYO......

Ester alifika na kumuona Hansy akiwa katika hali ile,
" Bby.. bby Nini shida jamani... Mamaaaa.. mamaaaaaaaa".
Alipiga kelele vane Ndipo alitoka mama hansy.
Wakati huo Hasny alikuwa amepoteza fahamu.

" Nini tena hansy Mwanangu amekuwaje?"
" Mama hata sielewi Hansy wangu jamani yani nilikuwa namtafuta ndo nimemkuta huku sijui nini shida".

Mama Hansy alimuita mwasifa ambae alifika nae akajitia kushangaa kama hajui kilichotokea.

" Lete maji na wewe Ester mpepee jamani mwanangu uhhh".

Mala alitoka na erick Ndipo akatoa wazo bola wampeleke Hospital wasije kuchukulia simple.

Kweli walimtoa pale mpaka kwenye gari na safari Kwenda hospital ilianza.

Mwasifa alibaki nae akilia mpaka alijilaumu,
" Eehh Mungu Wangu mjalie apone hansy nisije kuwa nimemshtua mimi jamani kwanini lakini uhhhh".

Upande wa Vane kule alipohifadhiwa Ndipo siku Hiyo wamama wale wawili walikubaliana wampeleke nyumbani kwao.
Vane aliwaambia mkoa, wilaya mpaka msituni ambapo Ndipo kuna ule mto wa kuweza kufika kwao.

Basi vane alimuambia mama mmoja wapo kama ana simu yenye salio. Walikuwa nayo Ndipo akawaomba wamuandikie namba fulani Ambazo aliwatajia zilikuwa kichwani kwake. Simu ile iliita pasina kupokelewa na haikujulikana ilikuwa ni namba ya nani.

Basi Safari ilianza wote kwa pamoja kuelekea mkoani morogoro.

Walifika baada ya masaa matano Kisha tena safari ikaanza Kuelekea huko kijiji ambacho vane aliwaambia kuwa Ndipo Nyumbani kwao.

Safari hiyo ilichukua tena masaa matatu Ndipo kufika kuna eneo Ambalo ilibidi watumie usafiri wa baskeli Binti alieleza eneo Ambalo walitakiwa Kwenda. Walipata usafiri huo walishukia sehemu Ambapo ni msituni hata baskeli ilikuwa haipiti.

Vane aliwaeleza Wale waendesha baskeli mahali wanapotakiwa Kufika ni katika Mto wa mpaka wa kwenda kwa mfalme mzota.

Walikuwa dereva watatu wa baskeli ivyo walikubali kuwasindikiza mpaka sehemu hiyo na kuwavusha maji pia mpaka wakafika Nyumbani kwa Kina vane ikiwa ni jioni imeingia.

Aliekuwepo nnje malkia na kijakazi wake Ndipo kumuona Vane akiwa ameshikwa na watu alishtuka akapiga kelele kumuita mfalme Aliekuwa ndani.

Wote walitoka Ndipo kumuona Vane amerudi lakini si kama alivyoondoka. Mfalme alimsogele Binti yake na kumtazama machoni.
"Vane umepatwa na nini mwanangu inamana hauwezi kuniona? Ni kweli hili nachokiona au naota"

" Ndio baba nisamehe sana kwa kuondoka bila kuaga nisamehe baba Yangu".
Alilia sana vane mfalme alimkumbatia mwanae kisha akaagiza Vijakazi wake kuwakirimu wale wageni waliofuata nao.

Vane aliwashukuru sana kina mama wale kwa wema wao walioufanya.
Hata Mfalme mzota aliaguza wageni wale wachinjiwe kuku kama shukurani kwa kumleta Binti yake kwa jinsi vane mwenyewe alivyowaelezea.

Usiku sasa ndipo Hansy alizinduka na kunikuta yupo hospital alianza kuita, "Vane... Vane.... Vaneee".

Daktari aliekuwa nae Ndipo akatoka nnje walipokuwa wanafamilia.

"Mgonjwa wetu ameamka lakini anamuita vane naomba kama yupo hapa huyo vane aanze kuingia kisha na wengine mtafuata".
Mama hansy alitazamana na Ester pamoja na bi rose na Erick ambao Ndio walikuwepo hapo.

"Hili tatizo mbona kama limerudi jamani mwanangu".
Alilalamika mama Hansy Ndipo Ester akamjibu,
"Wacha niende mimi bila shaka atanikumbuka maana alikuwa na mimi kwa mala ya mwisho na sio huyo vane".

Kweli Ilibidi Ester aingie kule wodini. Hansy kumtazama ester aliinuka,
"Ester upo hapa kwani nilikuwa naumwa sana mpaka nanyi mmekuja?"
"Ndio Hansy ulianguka lakini unaendeleaje? "
" Mimi mzima vipi hali ya vane emeweza kuona? Kweli mala ya mwisho nilianguka baada ya kupata taarifa kuwa vane Wangu amepoteza macho yake na sasa je  anaendeleaje? ".
Ester kusikia vile akaona hiyo tena kasheshe ikabidi aondoke wodini pale.

Alikwenda mpaka nnje ambapo walibakia wazazi wamekaa.

Binti alianza kulia hali iliyowashtua Wazazi.
" Mama hansy amekumbuka kila kitu mama amemtaja vane kama amepona? Kumbukumbu yote imemjia mama mbona hata hatujafunga ndoa nampoteza Hansy mamaaa".
Alilia sana Ester Ndipo mama hansy na Erick nao wakaenda wodini kumuona Hansy huku bi rose sasa akibaki kumbembeleza binti yake .

Mama Hansy akimtazama kijana wake, "Hansy upo sawa?"
"Mama vane anaendeleaje? Yupo wodi gani nikamuone?"

"Hansy mbona vane hayupo alishaondoka zamani sana na wewe unaishi na ester kwa sasa hata jana mlilala chumba kimoja".

" Hata sielewi mama ilikuwaje lakini sasa nina akili Zangu timamu huyo Ester kama alifanya ushirikina wake muambie kwa sasa nipo  sawa.
Vane alitekwa kwenda kumuokoa tutakuta amejeruhiwa machoni mwili mzima tukamleta Hospital nini kimeendelea vane Wangu unaniambia amendoka kwamba alipona au? "
Mama Hansy alikosa cha kumjibu mwanae huyo.

Erick nae Ndipo akamtuliza kaka yake,

" Kaka ebu tulia kwanza... Huyo vane hayupo alitorokaga huko  huwezi kulazimisha mambo".
Hansy aliamua kumnyamaza tu kwani bado kichwa kilikuwa kinamuuma muuma kwa mbali  basi ilibidi daktari amchome sindano ya usingizi kwanza atulie.

Siku iliyofuata Asubuhi Wasamalia wema wale wamama wawili waliaga na kuanza Safari ya Kurudi kwao mkoani dodoma.
Walisindikizwa na walinzi wa Himaya ya mfalme mzota hadi walivushwa mto na Kuondoka zao.

Mfalme mzota aliagiza waitwe waganga wote wa Himaya mpaka wa nnje ya Himaya kwa ajili ya kuandaa dawa ambayo itamponya Binti yake.

Upande wa Hansy aliruhusiwa kurudi nyumbani lakini huku akiwa mzima amerudisha kumbukumbu zake zote.

Basi Kufika kwanza alikwenda kuoga na kujiweka sawa Kisha Ndipo akarudi Kuzungumza na mama yake.

"Mama mliruhusu vipi vane atoroke akiwa katika hali ile ua upofu atakwenda wapi? Mlifikilia atakula nini huko alipo au laa?"

"Hansy Mwanangu hakuna aliemuona tulishtukia tu.
Ebu wacha hilo lipite endelea na Ester mbona mlishakuwa  Pamoja? "
" Mama huyo Ester simtaki wala simuhitaji. Kabisa mmeniumiza moyo Wangu kwa sasa niacheni mwenyewe nijue nini nafanya.
Nafunga kuanzia sasa sitakula chochote wala kunywa kumuomba Mungu anioneshe wapi vane alipo na ikishindikana basi nami sina umuhimu njaa itaniamulia maisha".

Aliongea kauli nzito Hansy kisha aliinuka akaondoka zake hakusema hata wapi anakwenda.

Mama Hansy alibaki kimya  Ndipo Erick akamtuliza,
"Mama wala usijali hizi ni mbio za sakafuni huyo vane kwa sasa hawezi kumpata ni hasira tu yataisha".
"Kweli inashangaza huyo vane kampa nini mwanangu mpaka Amemkaa kichwani jamani tulijua kamsahau lakini wapiii".
Aliumia sana mama Hansy.

Wakati huo Bibie Ester alikuwa nyumbani kwao na mama yake.
Baada ya hansy kukazania anamtaka vane basi ilibidi arudi nyumbani kwao.

"Mama nina gundu gani mimi wa kukataliwa kiasi hiki? Huyo vane hanipati hata nukta imekuwaje ananikataa.
Nimemlazimisha tukalala usiku mmoja lakini bado huyo vane kampa nini Ambacho kwangu hajakiona? ".

" Mwanangu ni suala la muda tu, hansy atasalimu amri maana vane kapelekwa mbali Kabisa hatompata wala usijali ".
Bi rose alimkumbatia Mwanae huyo Ndipo Binti alinyamaza akaona ajiandae na Kwenda zake Kazini.

Upande wa mwasifa Alirudi chumbani kwake akainama chini na kusujudu kama shukurani.

" Mungu asante hansy amemkumbuka vane, hakika huyu Ndie Hansy halisi. Sasa nami namuombea ampate vane jamani sijui atakuwa wapi".

Binti alifurahi Ndipo siku hiyo alipata hata kushika simu yake maana wakati hansy anaumwa nae alikosa raha akihisi chochote kikimpata yeye angekuwa ndie chanzo.

Bunti kushika simu yake alikuta misscall mala tatu namba ikiwa ngeni. ilimpigia muda wa masaa takriban 23 yaliyopita Karibia siku nzima.

Binti aliamua kuipiga namba ile Ndipo ikapokelewa.

"Haloo"
"Haloo habari"
"Salama nani mwenzangu?"
"Wewe ndo umenipigia niulize nani?"
"Mimi nimekuta misscall yako jana umenipigia mala tatu sema nilikuwa na mgonjwa jana sikushika simu kabisa".
"Ohhhh ile jana Asubuhi?"
"Ndio...nani mwenzangu?"
"Mimi nilitajiwa namba zako na Binti mmoja alikuwa anataka kuongea na wewe kama unamfahamu anaitwa vane haoni".

Mwasifa alishtuka kusikia vile mpaka mwili ulisisimka,

"Ndio vane yuko wapi? Upo nae hapo?"....

Sijui itakuwaje?
Tukutane sehemu ya 13*ME&YOU*

SEHEMU YA.... 13
Na
Mamuh mohd
(0716730000)

Tuliposhia......

Mwasifa alishtuka kusikia vile mpaka mwili ulisisimka,

"Ndio vane yupo wapi? Upo nae hapo?"...

SONGA NAYO.....

"Hapana tumemrudisha nyumbani kwao morogoro hapa sisi tupo njiani tunarudi nyumbani"
"Sawa nashukuru sana kwa wema wenu mliomfanyia mungu awalipe nafurahi sana kusikia yupo kwao mikono salama"
"Ndio maana kwa hali yake ile alikuwa anatembea tu mitaani Tunashukuru tuliwahi kumsaidia"
"Sawa Asanteni sana".
Mwasifa Ndipo alikata simu na kushusha pumzi.

"Bila shaka kaka Hansy anapafahamu kwa kina Vane itakuwa rahisi ataweza kumfuata.
Natakiwa kumuambia habari hizi haraka".

Alijisemea mwasifa huku amafungua mlango atoke nnje.
Lakini kufika mlangoni alimkuta mama Hansy akiwa amesimama ni kama mtu Ambae alikuwa amesikiliza yalliyozungumzwa.

" Huyo unaeongea nae amekuambia vane alipo ni nani? Au wewe ndo umesababisha mpaka wanangu amemkumbuka vane?.

Anhaa sasa ndo napata picha siku mbili nyuma, ulikuwa unavaa mavazi ya vane bila shaka ulikuwa unamkumbusha si ndio?.
Kama haitoshi ni wewe Ndie ulimuambia.
Kwanini alikutwa jikoni amepoteza fahamu kule alikuwa na nani kama sio wewe? "
" Hapana mama mimi sijamuambia chochote"
" Kelele.. huko unavyozungumza inaonesha kabisa inajieleza kile kilichotokea.
Mjaa laaana mkubwa wewe sasa Subiri nahakikisha nakupoteza hutakaa uamini".

Mwasifa pozi lilimuisha bahati Mbaya amekamatwa na mama Hansy.
Mama Hansy Ndipo alimuita kijana wake Erick na kumtaka amkamate mwasifa wampeleke Polisi.

"Mama kuna shida gani tena? Amefanya nini huyu?"
Mama hansy Ndipo akamsimulia kijana wake kila kitu.

Mwasifa alikamatwa alichezea kipigo kwanza kutoka kwa Erick kisha walimchukua na kumpeleka Katika kituo cha polisi.

Kufika Huko Mama hansy alimfungulia kesi ya wizi kuwa kaiba milioni 5 zilizokuwa ndani.
Akawapatia na pesa polisi kuhakikisha hatoki wanamfunga jela.

Mwasifa alikabidhi simu kila kitu na kuingia lumande, nyumba mbovu ilimuangukia.

"Yani mama umefanya la maana sana ungechelewa kidogo angeonana na kaka akamuambia alichokijua"
"Ndo ivyo amejua vane alipo anajisemea eti atakuambia hansy aiseee mbaya sana huyu.
Basi hapa hansy hatojua huyo vane alipo atamuoa Ester".

" Tena mama huyu faini ya milioni 5 hana ataambulia kifungo miaka 3 mpaka atoke hansy na ester wana watoto".

" Enhee lakini sasa iwe siri yetu hansy asijue kama mwasifa tumemuweka ndani akiulizia tuseme kaenda kwao kwisha Habari".

" Ni kweli mama".

Basi walipanga mipango yao Erick ambae alikuwa ni kama Mtoto wamama mambo Mengi anapanga yeye na mama yake.

Hansy alikwenda zake mpaka kww rafiki yake amoni kama kutuliza kichwa chake.

"Kwa sasa itakuwa ngumu Hansy kujua Wapi vane alipo kama alitoroka tu na hali yake labda urudi kws yuleyule mwasifa akuambie huwenda anajua alipo".

"Na hapo Ndipo Kwenye matumaini Yangu.

Natakiwa kuzungumza na mwasifa ila nawaza akiwa pale nyumbani hatuwezi kuzungumza vizuri maana mama mda mwingi anakuwepo itakuwa shida nadhani labda nipate nae kutoka Kwenda sehemu Nyingine na Nyumbani.

Sio siri sina hamu ya kula wala kunywa namuwaza vane Wangu.

Sijui anakula maskini huko alipo daaaah!!! ".

Hansy aliongea kwa uchungu huku machozi yakimtoka.

" Basi Hansy ebu tulia kisha jioni rudi ukajue namna ya kuzungumza na Huyo mwasifa".

Kweli Hansy Alitulia zake nyumbani pale kwa amoni huku akiwa anamuwaza mwasifa na hali yake ya kuwa haoni atakuwa anafananaje.

Kijijini kwa mfalme mzota waganga walifika wa kijijini pale mpaka wa upande wa ng'ambo.

Bibie vane alitolewa nnje na kuzungukwa na waganga wale Tayari kwa kuanza kazi ya kumponya.

Kila mganga alionesha uwezo aliokuwa nao lakini Vane hakupata nafuu. Masaa na masaa yalikwe nda mpaka giza liliingia hakukuwa na mabadiliko.

Mfalme mzota alichefukwa akafukuza waganga wote aliona kama hakuna walichomsaidia juu ya binti yake.

Alikasirika sana kila akimtazama mwanae jinsi anavyoteseka na hali ile. Upande wa malkia munaa kwake aliona ni sawa.

Aliwaza kama vane akipona basi hata Mtoto atakaemzaa hatokuwa na nafasi ya kupendwa upande mwingine kwake ni kama alifurahia hali ile ya vane ili mwanae atakaemzaa yeye ndie aje kuwa mtawala wa kijijini pale.

Sasa taarifa ziliwafikia familia ya bi Rukia akiwa na kijana wake saidy.
Bi rukia na mzee mzota walikuwa ni ndugu kabisa ambao Ndio walitaka watoto wao waowane kwa ajili ya kudumisha undugu wao.
Jioni hiyo bi rukia alimaliza kupika chakula Ndipo akamuambia kijana wake,

"Nakwenda kwa kaka kumtazama vane nasikia amerudi akiwa kipofu".

"Mama hapewi pole mwenyewe kiranga ameyataka.

Yeye si alikimbia hakutaka kuolewa na mimi ... Wacha limkute jambo huko shauli yake na mimi simuoi tena kwa sasa nipeni ruhusa nikaoe ng'ambo ya mto Binti mrembo na Ndie tutakuwa watawala wa kijiji siwezi kuoa kipofu mie".

" Haswaa nakuunga mkono mwanangu ujue kaka alikuwa kama ang'ang'ania tu ili mwanae asitoke kwenye madaraka hataki kuachia Wakati hiki kijiji waasisi ni Wazazi wetu wote... Wee nyamaza kimya ngoja nikawasikilize".

Kweli bi Rukia alikwenda mpaka kwa kaka yake na kuikuta hali ya vane si mwenye kuona anaekuja Zaidi ya kusikia Sauti.

"Asiesikia la mkuu huvunjika guu vane. Ulikumbia kwanini mwali wewe? Ona sasa ulipokwenda umeharibikiwa mwanangu?".
Aliongea bi rukia Ndipo mfalme mzota akamnyamazisha,

"Dada Hapana naomba usimtolee maneno hayo Binti Yangu.

Kwa sasa anahitaji faraja Zaidi nakuomba... Nimesikia kuna bibi mtama kijiji cha tatu nakwenda kuonana nae nikamuombe aje amtibu binti Yangu nipo katika hali ya kujaribu".
"sawa kaka lazima tuhangaike kwa ajili yake".
Mfalme mzota alijuandaa na usiku ule alitoka na walinzi wake kuanza safari inatuchukua takriban masaa2 kwa usafiri wa baskeli.

Hansy Alirudi nyumbani Ndipo kwanza alifikia jikoni kumtafuta Mwasifa lakini akamkuta mama yake Ndie yupo anapika.

Hansy hakumsemesha kitu akapita kutaka kuingia ndani lakini mama yake akamuita,

" Hansy baba tafadhali badili msimamo wako uliosema Asubuhi.
inamaama sisi wazazi wako tuliokuzaa... Na kukulea hatuna faida kwako mpaka unataka ujitese kwa Sababu ya vane umetufikilia sisi familia yako? "
" Sawa mama naomba unisamehe ni hasira.
Wewe ni mama Yangu sikufaa kukuambia vile nakiri kosa.
Basi niseme kwamba sitaoa mke yoyote endapo nitamkosa vane.

Nitamtangaza sehemu mbalimbali asipopatikana basi kama hali ya kushare nae maumivu ni kutokuoa.
Yeye amepoteza macho yake akiwa na mimi, nitakuwa na Furaha gani eti kuoa mke mwingine Hapana.
Ni vane tu mama sina furaha mama namtaka  vane Wangu kwa hali yoyote aliyokuwa nayo".
Aliongea hansy huku machozi yakimmiminika mpaka mama yake ikabidi ambembeleze kwanza.

"Na hapa nyumbani Mwasifa ametoroka gafla kabeba nguo zake zote".
Hansy alishagaa akaona sasa hilo balaa,
"Mama kwanini imekuwaje?"

"Hata hatuelewi hapa ndo manaa napika Mwenyewe ".
" Naomba namba zake za simu tokea mnibadilishie laini nadhani sinaga namba zake".
" Hapatikani hata ukimpigia".
" Hansy aliumia moyoni akaona kweli amepoteza mtu wa muhimu sana.

Usiku huo bibie mwasifa alikuwa zake polisi amefungiwa Ndipo alikuwa akilia tu.
Muda wote alikuwa akilia tu mpaka macho yalivimba.
Kwa siku hiyo hapakuwa na mtuhumiwa mwingine wa kike ivyo alibaki yeye peke yake.

Kuna askari mmoja wa zamu Ndipo akamfuata na kusimama mlangoni.
"Pole sana dada unalia mda mrefu hata chakula hujala kwani nini shida?"
"Nimesingiziwa kaka sijaiba ela amenisingizia".
"Pole sana MUNGU atakuwa upande wako ndo maisha acha kulia".
"Kaka naomba nisaidie Kakangu nipo chini ya miguu yako nakuomba".
" Ni kweli hata mimi nakuhurumia lakini Sina la kufanya yupo kiongozi wa kituo Ndie kaongea na mshtaki wako mimi ni ngumu zaidi nakuombea tu".

" Sawa naomba nisaidie kwa kilicho ndani ya uwezo wako.... Naomba dakika5 tu nikueleze ukweli wote".

Basi askari yule alitulia Ndipo mwasifa akamsimulia kila kitu mwanzo hadi Mwisho.

"Aiseee pole sana kwaiyo huyo boss wako ni kama amekata mzizi kijana wake asijue kitu ndo maana kakusingizia".
"Huo Ndio kweli nipo Tayari kukaa jela kwa muda nitakaopangiwa nisaidie kuandika barua imfikie hansy nimueleze tu ukweli vane alipo kisha basi najua kunitoa huwezi nnje ya uwezo wako lakini nimuambie hansy ukweli. Napafahamu ofisini kwake naomba niandike barua unisaidie hata kumlipa Boda boda aipeleke ofisini kwa hansy basiii".

Aliongea mwasifa huku akiwa analia sana.

Wahenga husema wastara daima haumbuki nia safi siku zote hairogwi utu na wema aliokuwa nao bibie mwasifa umekuwa kinga kwake katika mazito ambayo yamemzunguka.

Askari yule alimtazama mwasifa,
"Wewe ni binti wa aina gani? Upo katika matatizo kama haya lakini bado unampigania huyo vane chaguo lako la kwanza si kutoka hapa bali ni kusema ukweli.

Ni wanawake wachache sana dunia hii ambao  hawana tamaa na kuwatakia mema wenzao.
Nitasimama na wewe katika hili utaandika hiyo barua utanipa Maelekezo itafika nipo na wewe kwa kila hatua".

Mwasifa alifurahi sana uso wake uliokuwa umejaa Machozi ulipambwa na tabasamu mpaka askari yule alitoka Kwenda kumtafutia Karatasi na peni lakini huku akimfikilia hammalizi mwasifa.

Palikwenda mpaka Asubuhi Mfalme mzota Alirudi kijijini kwake akiwa na bi mtama alifanikiwa kumchukua na Kuja nae.

Bi mtama alimtazama vane Machoni Ndipo alitikisa kichwa.

" Huyu kawekewa sumu machoni ipo dawa ambayo inaweza kumponya lakini hiyo dawa inapatikana mbali sana. Kijiji cha saba kutokea hapa lazima atumwe mtu ambae atakwenda kuichukua na aniletee".

" Niambie nina vijana hapa watakwenda".

" Anatakiwa kijana shujaa ndie ataweza maana kuna vikwazo vingi sana kufikia huko kuna kupona au laa".

Mfalme jasho lilimtoka,

" Watakwenda toa Maelekezo nachotaka ni Mwanangu apone".

Basi bi mtama akatoka kwanza nnje ambapo alipewa sehemu  ya kukaa.
Alikuwa akichora njia ya kupita kwa hao watakaokwenda mpaka kufikia.
Alichora viashiria ambavyo watakutana navyo njiani n.k.

Walitumwa vijana watatu wa kwanza na kupewa Karatasi ile haraka walianza Safari ya takriban siku nzima masaa 12 kufika na masaa 12 kurudi jumla inatumia masaa 24.

Upande wa Hansy Alifika ofisini akiwa hayupo sawa.
Amon alikwenda kuonana nae.

"Vipi Hansy umefikia wapi?"

"Ni majanga tu mwasifa nimekuta katoroka nyumbani.
Usiku kucha natangaza mtandaoni kumtafuta vane lakini kimya sielewi ndugu Yangu".
"Daaa!!! Pole sana Hansy hakika ni mtihani kumpata itakuwa ngumu sana inabidi uanze kuzoea Hansy".
"Sio Rahisi sio rahisi amon".

Basi wakiwa hapo Ndipo mala aliingia secretary ofisini hapo.
"Samahani Mr Hansy kuna ujumbe wako huu umeletwa Sasaivi?"
"Kutokea wapi?"
"Sijajua".
Hansy alipokea ujumbe ule Haraka na kuufungua.....

Sijui itakuwaje?
Tukutane sehemu ya 15*ME&YOU*

SEHEMU YA..... 14
Na
Mamuh mohd
(0716730000)

Tuliposhia......

Basi wakiwa hapo Ndipo mala aliingia secretary ofisini hapo.
"Samahani Mr Hansy kuna ujumbe wako huu umeletwa sasaivi?"
"Kutokea wapi?"
"Sijajua".

Hansy alipokea ujumbe ule Haraka na kuufungua...

SONGA NAYO........

Amoni alikuwa kimya akimtazama Hansy akifungua na kuanza kuisoma barua ile.

" Habari yako kaka Hansy ni matumaini Yangu  ni mzima wa afya naomba Mungu uipate barua hii.

Ni Mimi Mwasifa nipo kituo kikuu cha polisi in huku mjini...mama yako amenifungia ili Nisiseme chochote kwako kumuhusu vane.

Vane alitelekezwa lakini bahati Nzuri alipata wasamalia wema ambao walimsaidia akarudi kwao morogoro. Vane yupo kwao naomba usimtupe na pia usiwaambie wazazi wako chunguza huwenda hawana wema kwa vane na kilichompata  vane nawashuku. Nitatumikia kifungo alichonisingizia mama yako lakini naomba msaidie vane usimtupe.".

Hansy mpaka Machozi yalimtoka Ndipo akampa amoni barua ile nae asome.

Amon aliisoma na alipomaliza akamtazama Hansy,

" Pole sana kaka lakini alichokisema huyu kinaweza kuwa kweli Kabisa"
" Sio kinaweza ni kweli? Wazazi Wangu watakuwa wanahusika na kilichompata vane ndio Sababu hata amemkamata huyu ili asiniambie alipo kwa maana nisimuone kabisa Vane.

Sipotezi muda naondoka namfauta vane".
" Naomba nikusindikize Hansy Tafadhali".
" Hapana ofisini unatutegemea hatuwezi kutoka wote wawili.
Bakia wewe hapa angalia majukumu wacha mimi niende.

ila naomba nisaidie kwa sasa twende ukamuwekee dhamana Mwasifa kisha akae pale kwenu kwa muda wakati kesi ikiendelea na nina uhakika Wazazi wangu wakijua sisi ndo tumefanya hivi hawataendelea kesi".

" Hilo wala usijali Hansy Mwasifa nitampeleka kwetu pale atakaa na mama na ukifanikiwa kurudi na vane pia usiende nae pale nyumbani kwenu mfikie kwetu".

Hansy alimkumbatia Amoni hakika nae alikuwa ni rafiki yake wa Karibu sana.

Hansy Alirudi nyumbani Ambapo alichukua vitu vyake vya muhimu akaweka kwenye begi lake na mgongoni na kuondoka pasina kutumia gari pale nyumbani.
Wakati anaondoka mama yake hakuwepo nyumbani ivyo hakuna aliemuona.

Mwasifa nae alipata kawekewa dhamana na Amoni Ambapo barua ya dhamana ilitumia jina la Hansy kwa maana Ndie aliemuwekea dhamana akaweza kutolewa.
" Pole sana Mwasifa barua ilifika kwa mtarajiwa"
" Nimefurahi Asanteni sana....yupo wapi Hansy?"

" Hansy ameanza safari kuelekea morogoro"
" Daaa!!! Nilitamani Kwenda nae maana sina pakwenda".
" Usijali utaenda nyumbani kwetu tumeshazungumza ns Hansy kila kitu. Alafu bado utakuwa unakuja hapa kureport ivyo lazima uwe Karibu".
" Asante sana".
Mwasifa alimtazama na yule askari Alieitwa Baraka.
Alimfuata na kumpa shukran.

"Asante sana kiukweli sina cha kukulipa lakini Mungu akulipe kwa wema ulionifanyia"

"Amiin kila kitu kitakuwa sawa ni furaha ujumbe ulifika ila nahitaji kukuona tena naomba namba zako za simu".
"Sawa".
Mwasifa alimtajia namba za simu askari yule,
"Asante sana naitwa baraka"
"Nami naitwa Mwasifa"
"Karibu".
Ndipo waliagana pale Binti mwasifa alitoka kwa dhamana na kuondoka na amon.

Majira ya mchana mama Hansy alikuwa zake eneo la hotelini akiwa na rafiki yake bi Rose.

"Ujue huyo mfanyakazi wako ni mjinga sana  sasa kwanini amuambie ukweli hansy? Huyo Ndie kasema wala halina mjadala"
"Ndio ivyo lakini tumemfuma pazuri sana ataoezea jela hana ela za kulipa miaka 5 inamuhusu mpaka anatoka hansy yupo kwenye ndoa na ester"
" Umefanya la maana mama Hansy....lakini Hansy mwenyewe ukimuangalia Sasaivi anasemaje?"
" Mhhh anahangaika tu Mwanangu ila jana alijirudi akaniongelesha kwa upole mama yake Mdogo Mdogo atakuwa sawa tu".
" Kweli kabisa".

Sasa Wakati wako hapo wakipata nyama choma ya mbuzi na vinywaji. Mala mama Hansy akapigiwa simu.
" Haloo captain Koba....ehh? Unasemaje? Kawekewa dhamana na nani aliejua yupo hapo kituoni? Ngoja nakuja nakuja hapo".

Mama hansy Ndipo alikata simu,
" Mbona majanga Mwasifa kawekewa dhamana hata sijui na nani? Ngoja niende? "
" Heee kweli majanga haya tumalizie twende wote".
Habari kwao zilibadilika maana walijua kama mwasifa akitoka anaweza kuwasiliana na Hansy.

Walifika mpaka kituoni pale Ndipo kuangalia mdhamini ni Hansy makuka.
Mama hansy alishangaa,
"inamana Hansy amejuaje kama Mwasifa  yupo hapa? Nani kamuambia??".
Polisi hakuna aliekuwa anajua na baraka hakuwepo zamu yake ilimalizika akawa ameondoka.
"Huyu atakuwa ni Erick...maana yeye ndie anajua kila kitu kinachoendelea kaamua kuja kumuambia kaka yake kwanini ananifanyi ivi huyu mtoto?"
"Shoga hao wanao jamani tunaenda mbele tunarudi nyuma".
"Hapa bila shaka mwasifa ameshamuambia Hansy kila kitu na watamfuata vane".

"Athubutu aone safari hii Ndipo nitammaliza kabisa huyo vane nitamaliza historia ya maisha yake".
"Hapa pagumu shoga angu siwezi kuendelea na kesi maana hansy anaweza akamtetea huyo mwasifa Mwishowe kesi ukanigeukia nadhani tuangalie mengine mimi hili nimelinawa".

"Kwamba unaungana na kijana wako asimuoe mwanangu si Ndio?"
" Sivyo lakini nimeishiwa Mipango labda sasa ufanye wewe ila tu msimuathiri mwanangu hansy na huyu erick atanitambua leo".

Mama hansy aliamua kuondoka zake alichanganyikiwa akijua ni erick ndie kafanya hayo yote.

Basi kweli jioni Erick alikuwa zake nyumbani na bibie Ester.
"Ester alifika kwa ajili ya kumuona Hansy Ndipo akakuta nyumbani hayupo badala yake alimkuta Erick.

" Sasa atakuwa wapi maana nimeanzia ofisini kwake nikaambiwa hayupo".
" Ujue kaka ni kama hayupo sawa ivi Usijali atakuwa sawa tu maana huyo vane hatokaa amuone".
" Sawa mimi namsubiri Leo mpaka arudi na nasikia msichana wenu wa kazi hayupo nitaingia jikoni Mimi kupika"

" Ahhh shem akeeeee nakupenda hapo tu hii imeenda wewe wa kwetu"
" Hahaha jamani shem haya basi".
Bibie Ester alikwenda katika chumba cha Hansy akabadili nguo alizokuwa nazo amebeba kisha akaamua kwenda jikoni kupika.

Punde alifika mama hansy na kumkuta Erick Sebleni.
"Mtoto mshenzi sana wewe kwanini umemuambia Hansy kuhusu mwasifa alipo?"
"Mama unazungumza nini?"
"Kwamba haunielewi au?"

"Mimi sijazungumza chochote na kaka Hansy najua unafahamu kuwa mimi na yeye haziifi sana siku  akili yake anaijua yeye mwanao".
" Hansy kaenda kumuwekea dhamana mwasifa na haijulikani wameenda wapi unadhani nini hapo kinafuata kama si kumfuata alipo  vane".

Hata Erick alishtuka na bibie Ester ambaey alikuwa jikoni alisikia ikabidi aende Sebleni.
Mama hansy Ndipo kumuona Ester maana hakujua kama yupo.

" Mama hansy amempata vane au? "

" Ahhhh Usijali Ester kuna mambo yalitokea nadhani mama yako atakuambia kila kitu ila usijali "
" Hansy hayupo ofisini kwake na nyumbani pia kwaiyo ndo kamfuata mwanamke wake".
" Wala usiogope Ester tutajua cha kufanya kama watakuja nae hapa au laa.
Ester mpaka machozi yakimtoka.

"Mama hakika namchukia sana kiumbe anaeitwa vane ni chanzo cha maumivu Yangu".
" Nafahamu hilo mwanangu na wewe wala usijali nakuhakikishia kila kitu kitakuwa sawa".
" Nafurahi mama".

Ester alimkumbatia mama hansy alifurahi kuona bado mwanamama huyo yupo Upande wake.

Basi majira ya usiku kiasi saa3 Ndipo kuna walinzi wawili Ambao walibaki kulinda himaya ya mfalme Mzota baada ya wengine kutumwa Safari.
Walinzi hao walikwenda ndani kwa mfalme mzota.

Mfalme kuna tatizo limetokea?"
" Tatizo gani? "
" Kuna mgeni amevaa mavazi sio kama ya huku kwetu amekuja katika Himaya Yetu... Tumemkamata na kumfungia katika jengo la pale nnje bila shaka ni wanamapinduzi".

" Safi sana muacheni alale humo nitamuona kesho".
Alijibu mfalme mzota Ndipo na walinzi wale wakatoka nnje.

Lakini bibie vane alikuwa Chumbani na chumba alichokuwa ni Karibu na ukumbuni ambapo aliekuwepo baba yake.
Vane alisikia taarifa ile na alijiuliza nae kuwa atakuwa ni mtu gani huyo hakuna aliefahamu.

Palikwenda mpaka Asubuhi Ndipo mtu yule alufunguliwa na kupelekwa eneo la nnje alipokuwa amekaa mfalme mzota na bi malkia.
"Wewe ni nani umekuja unataka nini?"

"Nimekuja kumuona vane mimi ni mpenzi wake".
Mfalme mzota kusikia ivyo alimzaba kibao hansy.

"Umejileta nyie Ndipo mliomfanyia unyama mwanangu sasa wewe utakuwa mfano kwa nitakachokufanyia"
"Hapana mzee nampenda sana vane na yeye pia anajua ningemfanyia hayo ningekuja hapa kufanya nini tafadhali kabla ya yote naomba kumuona vane".
Mfalme mzota akaagiza walinzi wake wamchukue   Tena hansy kwenda kumfungia.

Hansy alianza kupiga kelele,

"Mzee sina hatia mimi... Mzee naomba nimuone vane nipo tayari kwa Chochote Sababu ya vane... Mzee... Mzeee wangu".

Kelele zile mpaka zilimfikia bibie vane ambae alikuwa amejilaza zake Ndani. Bunti aliamka na kusikiliza vizuri sauti ile haikuwa ngeni kwake na aligundua ni Hansy.

Vane akiinuka na kupapasa kutafuta fimbo yake ilipo huku anaita,
" Hansy... Hansy... Hansy wangu amekuja... Hansy..... "

Sijui itakuwaje?
Tukutane sehemu ya 15*ME&YOU*

SEHEMU YA... 15
Na
Mamuh mohd
(0716730000)

Tulipoishia.......

Vane aliinuka na kupapasa kutafuta fimbo yake ilipo huku anaita,
"Hansy.... Hansy... Hansy wangu amekuja... Hansy...".

SONGA NAYO......

Aliinuka Vane na kutoka nnje huku akipapasa papasa Ndipo alifika mpaka Mlango wa nnje kwa maana haikuwa nyumba kubwa ya kumchanganya alishazoea.
Alifika mpaka nnje lakini hakumsikia Tena Hansy akizungumza kwa maana alikuwa ameshakwenda kufungiwa katika chumba nnje kule.

"Ha... Ha... Hansy".
Aliita Vane Ndipo wafanyakazi wa pale walimuona wakaenda kumchukua na kumrudisha ndani.
"Niambie nimemsikia hansy tafadhali niambie walau amekuja nani niambie nakuomba".

" Ni mgeni ndio na amesema anataka kukuona wewe ametokea mjini".

Vane Alizidi kupita kiasi,

" Hansy Wangu jamani amekuja haya niambie baba amesemaje? "

" Amemfungia"

" Kwanini Lakini? Kwanini amefungiwa nipeleke kwa baba tafadhali akamjua kuwa hana nia mbaya kwangu naomba nipeleke nikamuone"

" Hapana siwezi kumbuka mfalme yupo hapa haiwezekani tafadhali tulia ndani dada".

Kijakazi yule aliamua kumfungia mlango vane akamuacha akiwa analia mpaka alianguka chini alitamani sana kuonana na Hansy.

ilikwenda mpaka usiku Ndipo malkia alimfuata mumewe Mfalme mzota.
"Mumewangu muonee huruma binti yetu analia sana na hali yake ile.
Anataka kwenda walau kumsikua Sauti yake mwenzake.
Hatujui maisha yao jinsi yalivyokuwa tafadhali naomba tuwape nafasi".
" Hapana Hapana umefurahia kwa walichomfanyia mwanangu si Ndio?
Hawa ndio wamemsababishia mpaka sasa haoni Binti Yangu.
Sikubali Atarudi kwao akiwa haongei amelala kimya kaa tulia achana na hizi Habari".

" Sawa mmewangu".

Malkia hakuwa na la ziada waliingia zao kupumzika na  mumewe.

Lakini bibie vane alikuwa akihangaika kufungua Mlango akitaka afike alipo mpenzi wake Hansy.
Alikutana na yule kijakazi Ndipo aliangaza akaona mfalme yupo chumbani kwake.
Aliamua kumshika mkono vanena kumtoa mpaka nnje.

Aliekuwepo mlinzi mmoja akilinda alipofungiwa Hansy Ndipo akawaona kijakazi Sophia akiwa na Vane.
" Nyie mnakwenda wapi usiku huu?"
" Samahani tunaomba kuonana na huyu mkaka vane anataka walau kumsikia".

" Hapana mfalme amesema nisifungue Mlango siwezi kwa kweli"
" Nakuomba fanya ivyo haraka sana kesho nitakupakulia chakula kingi"
" Sawa dakika mbili tu".
Mlinzi yule  alifungua Mlango na kumuasha hansy Ambae alikuwa amejikunyata chini usingizi umempitia.

Hansy aliinuka haraka na kutoka Ndipo akamuona vane.
Alimkumbatia hata vane aliposikia harufu akajua ni Hansy nae akanyoosha mikono yake na kumkumbatia.

"Nimefurahi kukuona vane pole sana ipo siku utapona mamaaa".

"Natamani nipone nikuone Hansy Wangu Asante kwa kuja japo naumia kusikia baba Yangu amekufungia nitajaribu kuzungumza nae".
"Usijali vane si kitu Kwangu ila nakuahidi sitaondoka hapa bila wewe. Nimekufuata wewe ikishindikana basi nipo Tayari kwa chochote".
" Nafurahi kusikia ivyo  Hansy Asante...umemuacha hajambo mwasifa bila shaka natamani kumsikia sauti yake rafiki Yangu".
" Hakika ajambo tena katika watu wa muhimu mwasifa namba moja Ndie aliefanya mpaka nikawa sawa na kujua hapa ulipo.
Ni story ndefu lakini usijali ipo siku tutazungumza.

Kubwa nataja kujua aliesababisha mpaka ukapitia haya".

Vane alipoulizwa vile Ndipo alikumbuka alikuwa ni mama Ester lakini alimchimba mkwala mzito sana.

" Hata sijui ni watu gani wale Hansy sijui Kwa kweli?"

" Basi nahitaji kutoka na wewe hapa nitakupeleka india kwa Vyovyote vile".

Basi wakati wanazungumza hapo Ndipo mlinzi yule aliwakatisha kwamba muda umekwisha.

" Sawa ingia ndani nenda kalale kipenzi changu nipo kwa ajili yako nakupenda sana vane".

" Asante nakupenda pia hansy".

Basi waliagana pale Ndipo Sophia akamshika mkono vane na kurudi nae ndani.

Hansy aliingia nae katika anacholalaga Ndipo machozi yalimtoka.
Alivuta picha jinsi alivyomuona vane akiwa katika hali ile ya kushikwa mkono na fimbo aliumia sana.
Hali ile ilimfanya Hansy alie karibia usiku kucha.

Palikwenda mpaka Asubuhi Ndipo Ester aliamka ambapo siku hiyo alilala chumbani kwa hansy.
Palikucha pasina Hansy kurudi.

Ester aliamka na kutoka nnje ambapo alimkuta mama Hansy wakasalimiana vizuri.

Yani mama kumbe Hansy hajarudi jana jamani au ndo yupo na vane wanakula raha zao"
" Kwa raha gani haswaa?? Aliyokuwa nayo vane? Mhhh wala usiwaze hayo mwanangu kwanza achana nae weee muache kama ndo kaenda kumleta kipofu wake tusubiri warudi".
" Sawa mama lakini kiukweli nawaza kwamba ni upendo gani huo aliokuwa Hansy mpaka mpaka anamfuata vane daaah!!!"
" Huwenda hata sio akili yake mwanangu huwezi jua.

Mabinti wa kijijini wanakuwaga wachawi tu yote yanawezekana".
" Sawa mama najiandaa nakwenda kazini na nikitoka nitapitia nyumbani kule tutawasiliana Hansy Akirudi".
" Haya mwanangu usijali mama".
Ester alikwenda zake ndani tena kujiandaa.

Basi upande wa Mwasifa nae aliamka akiwa nyumbani kwa kina Amoni.
Alimkuta amoni yupo akizungumza na mama yake.
Mwasifa aliwasalimia wote,
"Kabla haujaondoka kaka naomba mpigie simu Hansy nataka kuzungumza na vane".

" Kule mtandao hakuna Tokea jana namtafuta aiseee.
Huwa sikai hapa nimepanga nyumba ila nilikuja mapema kuwaona kabla sijaanza majukumu"
" Basi Asante nashukuru sana kaka tuzidi kuwaombea"
" Ni kweli na wewe usijali jisikie upo nyumbani utapata hata kumchangamsha mama hapa".
" Sawa kaka".
Wote kwa Pamoja walifurahi sana.

Basi upande wa mfalme mzota siku ile aliamuru Hansy apelekwe mbele yake tena akiwa amefungwa kamba mikononi.

"Nakukata kichwa chako kisha tutaenda kukitupa Barabarani.
Kama wazazi wako watajua haya wasipojua potelea mbali.
Hii itakuwa fundisho kwa walichomfanyia mwanangu".

Hansy aliishiwa pozi,
" Mzee wangu naomba usiniue tafadhali nampenda kwa dhati Binti yako sijahusika kwa kilichompata na nipo hapa kumfuata nikamtibie.
Naomba nielewe mzee Wangu".
" Kelele wewe huwezi kunipangia nachotaka kukufanyia nakuua nakata kichwa chako".
Hansy alipiga kelele lakini hakuna alienisaidia.

Vane alikuwa ndani amefungiwa akipiga kelele lakini hazikusaidia.
Mfalme mzota aliinua panga Tayari kwa kumkata Hansy.

Lakini kabla hajamkata mala alisikia akiitwa na bi mtama.
"Tafadhali wacha kwanza unachokifanya ... Kuna habari mbaya kuhusu wale vijana uliowatuma njoo nikwambie nilichokiona".
Mfalme mzota alishagaa hiyo Ndio ikawa pona pona ya hansy ikabidi aingie ndani Kwenda kumsikiliza bi mtama.

"Vijana wale inaonesha kuna shida imetokea wangekuwa wamesharudi ni wazi wamefeli mahali inabidi atumwe mwingine alie shujaa"
" Shujaa hao Ndio walikuwa mashujaa sasa nani ataweza? "
Alijiiuliza mfalme mzota kwa muda Ndipo akamfikilia kijana saidy.

" Sawa yupo mtoto wa dada subiri aitwe muandalie ile Ramani yako nahitaji Binti Yangu apone".
Alitoka Haraka mfalme mzota na Kwenda kuagiza saidy aitwe mala moja.....

Sijui itakuwaje?
Tukutane sehemu ya 16*ME&YOU*

SEHEMU YA.... 16
Na
Mamuh mohd
(0716730000)

Tulipoishia.....

"Sawa yupo mtoto wa dada Subiri aitwe muandalie ile ramani yako nahitaji Binti apone".
Alitoka Haraka mfalme mzota na Kwenda kuagiza saidy aitwe mala moja....

SONGA NAYO.......

Taarifa zilimfikia kijana saidy Ndipo haraka Alikwenda kwa mfalme ambae pia ni mjomba wake kuitikia wito.

Wakati huo Hansy alikuwa amefungwa kamba katika mti pale nnje akiadhibiwa kwa namna hiyo.
"Saidy unatakiwa Kwenda kijiji cha saba kutokea hapa kuna majani ya fulani ni dawa unatakiwa kwenda kuyaleta".
"Mjomba nani asiejua kuwa kijiji icho hakuna anaekwenda na kurudi salama? Unataka kuniangamiza mjomba?"
"Hapana ni kwa sababu ya mke wako mtarajiwa Vane nenda kwa ajili yake akipona mtafunga ndoa".

"Mjomba umesahau kama vane alinikimbia hanitaki... Sasa iweje leo nihangaike kwa ajili yake.
Hapana mjomba uwezekano wa vane kupona ni Mdogo sana sio Rahisi.
Nisamehe sana mjomba siwezi kwenda nikamuacha mama Yangu mjane   na mnyonge kwa Sababu ya Mwanamke Ambae alinikataa na kukimbia.
Kule ni Sehemu hatari sana baba".
Mfalme mzota hakuamini kama saidy abhekataa kwenda huko.

Bi mtama ndipo akamuambia mfalme,
" Ni kweli hiyo sehemu ni hatari kama vijana walinzi hawajarudi mpaka sasa basi mtu kama wewe ndo hufiki Kabisa.

Nina imani sana hayo majani ni ya kipekee dawa kubwa sana... Huja madaktari Wengi kwa ndege zao na kuchuma kwenda kutengenezea dawa. Wakishafanikiwa  huwa wanauza bei kubwa sana maana ipo sehemu hatari".

Mfalme mzota machozi yalianza kumtoka,
" Ahhh Binti Yangu jamani inamaana hatapona... Siwezi siwezi namtaka mwanangu apone mimi".
Mfalme alimwaga machozi Ndipo mala akasikia Sauti ya yule mfungwa wake Hansy.

" Nitakwenda mimi naomba niende mimi".

Mfalme mzota alimtazama asikose cha kuzungumza.
Bi mtama Ndipo akajibu,
"Hakika kijana una Mapenzi ya dhati sana na vane.
Pamoja na sifa zote ulizozisikia sehemu hiyo kuwa watu wakienda hawarudi lakini bado umejitoa muhanga".

"Ni Mapenzi nampenda sana Vane naomba mnielewe kwa hili nipo Tayari kwenda".

Mfalme mzota ikabidi aagize Hansy afunguliwe na kweli akafunguliwa.

"Nenda ukishindwa naamini Ndio itakuwa adhabu yako ya kufia huko huko lakini ukirudi na hayo majani ya dawa utampata vane".
"Nipo Tayari baba".

Basi bi mtama alimpatia Ile katarasi aliyochora chora kama ramani.
Hansy licha ya kuwa kijana Shujaa mwenye uwezo wa kupambana na mazingira mbalimbali lakini pia ni msomi Tena anafanya kazi katika taasisi kubwa inayohusu utafiti ivyo hiyo kwake ni kama faida pia.

Alipoitazama Ramani ile alielewa jinsi ya kufanya Ndipo aliondoka kijana huku hata saidy akiwa anamtazama tu wakijua fika uwezekano wa kurudi kwake utakuwa ni Mdogo sana.

Majira ya mchana mwasifa alikuwa zake jikoni akipika lakini huku akiwa anamuwaza Hansy huko kama amefika salama na ameonana na vane au laa. Mala kuna sms iliingia katika simu yake. Mwasifa aliitazama na kugundua imetoka kwa afande baraka.

"Moyo wenye upendo haukumbwi na dhoruba yoyote.

Namuomba Mungu akutunze kwa moyo wako huo".
Mwasifa alitabasamu kisha akajibu ujumbe ule.

"Asante na wewe pia una moyo wa upendo".
Basi walijikuta wanaanza kuchati.
"Kesi itaishia hapa maaana yule mshtaki wako hajaja tena kweli alikuwa anakusingizia pole sana".
"Nafurahi kusikia ivyo afande baraka kiu Yangu nimuone vane Wangu huyo niliekwambia kisha Ndipo nitarudi kijijini kwetu"
"Sitamani Urudi nataka uishi hukuhuku Sababu watu kama nyie ni adimu sana".

"Natamani nami iwe ivyo na ikinibidi hakika nitabaki"
"Sawa natamani kupata wasaa wa kukuona tena nikumwagie sifa nzuri kama jina lako natamani kujua kwanini wazazi wako walikuja jina zuri kama hilo".
" Ni mwasifa... Maana yake mwenye sifa nyingi"
" Basi hizo sifa ni nzuri sana".
Basi waliendelea kuchat wenyewe.

Wakati huo mama Wa kijana Amon nae alikuwa akizungumza na mumewe Ambae ni baba yake amon.
"Yani sio siri baba amoni huyu msichana ana tabia njema anafaa kabisa aolewe na amoni.

Kijana wetu amekuwa mkaka kuoa hataki huyu ni nimemuona tu jana na leo hakika anafaa kuwa mke".
"Sasa kumueleza mwanao aelewe labda tujaribu kumwambia ila naamini kama wewe umemuona huyu msichana anafaa basi hakika anafaa tuzungumze na amoni maana ni kweli muda umefika anatakiwa aoe".

Sasa upande wa bibie Vane alipelekewa chakula ndani Ndipo Kijakazi sophia akamuambia kuwa hansy ameenda kuleta dawa kijiji cha saba.
Vane alishtuka kusikia vile alijikuta anaanza kulia,

" Kwanini Hansy wangu Wangu jamani kule ni hatari sana asingeenda ahhhh hansy".
Alilia sana vane Ndipo Sophia akawa anambembeleza.
" Hupaswi kulia sana vane unatakuwa kumuombea arudi salama japo sio rahisi kabisa maana walinzi waliotumwa jana hawajarudi".
Vane ndo Alizidi kulia na kuinuka akataka Sophia ampeleke kwa baba yake.
Kweli Sophia alimshika mkono na kumpeleka mpaka nnje kwa baba yake.
"Vane mwanangu kaa ndani sitaki watu wakukute hapa watakusema"

" Baba kwanini umemtuma hansy kwenda kijiji cha saba... Hali ya kuwa unafahamu kama  kule ni hatari"
" Mwanangu nipo katika hali ya kuhakikisha unapona nitajaribu na kujaribu hata mimi nitakwenda haijalishi nitapona au laa ila si kukuona unateseka.
Wale ni maadui zako ndio chanzo cha haya yote jaribu kuelewa ".
" Hapana sio kwa hansy hausiki na chochote amekuja huku angekuwa mbaya angekuja kufanya nini inamaana bado hauelewi tu baba".

" Vane Mimi najua kuliko wewe wacha ukaidi wako... Sophia mrudishe ndani haraka".

Vane kweli alishikwa mkono kurudi ndani huku analia sana.

Lakini Wakati huo alikumbuka rafiki yake ambae ni Mwasifa aliwahi kumfundisha kuswali na kuomba.
Alilelewa katika imani za kuamini waganga lakini mwasifa alianza kumfundisha kuhusu Mungu.
Vane aliamua kufanya kama ambavyo Mwasifa alimfundisha kuswali na kumuombea hansy awe salama na pia apone aje kumtazama Hansy kwa macho yake.

Siku ile ilipita ikiwa ni kukesha kwa bibie vane akimuombea Hansy maana anafahamu Huko panasifika kwa wanyama wakali pia.

Palipopambazuka Ndipo Mfalme mzota alitoka nnje na kumuambia bi mtama. "Nimekata tamaa inaonesha hiyo sehemu ni hatari na huyu wa pili amepotelea huko kweli mwanangu atapona siamini kabisa".
Alijiinamia mfalme mzota mpaka machozi yalimtoka kuwa mwanae anaweza asipone maana dawa inayotakiwa ipo mbali na kuipata ni kazi sana.

Basi palikwenda mpaka ilifika saa 4 Asubuhi hata bi mtama alikata tamaa kabisa.
"Hakika ni kweli Sijui itakuwaje juu ya vane na huyu harudi tena jamani na hiyo ndio dawa pekee ya kunisaidia Vane.

Walibaki wote wakiwaza mfalme mzota alibaki ameduwaa kutokana na hali aliyokuwa nayo binti yake.

Basi muda huo huo mala kwa walisikia mtu akiwa anakuja huku anagugumia kana kwamba ana maumivu Fulani.

Ndipo wote waligeuka kuangalia alikuwa ni Hansy akitembea huku amefunga mguu wake mmoja anatembea kama anauburuza.

Mfalme mzota aliagiza haraka mlinzi aende kumpokea kitendo cha kumuona amerudi mpaka imani ilimuingia. Kweli mlinzi yule alikwenda kumpokea na kumleta Karibu ya bi mtama Pamoja mfalme mzota.

Hansy alikuwa ameshika mfuko ambao una majani aliyotakiwa kuyaleta lakini hali yake ilikuwa Mbaya, mwili ulibadilika Ndipo bi mtama alisanuka kuwa alipata ajali ya nyoka.

"Ohhh kijana shujaaa inaonesha ameng'twa na nyoka sijui ni mda gani lakini hajatupa mfuko wake wa dawa... Haya mbeneni haraka mumpeleke ndani nimpatie huduma ya kwanza".
Kweli mlinzi alibaki mmoja akapambana kumuingiza Hansy Ndani.

Bi mtama alimtazama mfalme mzota na kumuambia,
" Hakika huyu ni mwanaume tuombe apone dawa ya vane imefika wacha kwanza nimpatie huduma ya kwanza kisha niandae ya vane".
Mfalme mzota alibaki kimya tu nafsi ulimuuma kwa jinsi alivyokuwa akimdhania awali na kile alichokifanya.

Hata yeye alitikisa kichwa na kukubali kweli anampenda vane.

Mfalme mzota alivua kofia yake na kubaki kimya ameduwaa.....

Sijui itakuwaje?
Tukutane sehemu ya
17*ME&YOU*17_21

SEHEMU YA.... 17
Na
Mamuh mohd
(0716730000)

Tuliposhia......

Mfalme mzota alibaki kimya tu nafsi ilimuuma kwa jinsi alivyokuwa akimdhania awali na kile alichokifanya. Hata yeye alitikisa kichwa na kukubali kweli anampenda vane.

Mfalme mzota alivua kofia yake na kubaki ameduwaa....

SONGA NAYO.....

Palikwenda mpaka usiku Ndipo bi mtama alikuwa akimpaka dawa vane. Baada ya kuiandaa.
Alimpaka na kumtaka afumbe macho tu kwa muda wa masaa kadhaa Ndipo dawa inapata kufanya kazi na a usahihi.

Vane alitaka apelekwe  kwa Hansy maana hakuambiwa kuwa amerudi anaumwa.

Bi mtama alipomsikia vane kuwa anataka aende kwa hansy Ndipo akamuambia,
"Kwa sasa Tayari Una hali hii unatakiwa kwanza kutulie kesho atakuja kukuona Hansy"
" Sawa lakini nataka kumshukuru kwa wema alioufanya Kwangu naomba mruhusu basi aje tafadhali".
" Vane jitahidi kuelewa wakubwa sawa mjukuu Wangu?".
Vane alikubali lakini huku moyo wake akiwa anatamani sana kumsikia walau Sauti yake Hansy.

Hali ya Hansy haikuwa na matumaini Aliendelea kutibiwa na Upande wa bibie vane ilifika mahali alijua ukweli aliambiwa kuwa hali ya Hansy haipo sawa.
Bunti aliumia mno hivyo wote wawili wakawa katika Matibabu.

Zilipita wiki mbili Ndipo siku hiyo majira ya usiku Vane aliamka alishangaa kufumbua macho akakuta anaona.
Aliangaza sehemu zote na kujikuta anaona.

Vane alishangaa akuamini kabisa, alimuamsha yule kijakazi Sophia anaelalaga nae.

"Sophia amka naona naoma hiki kibatari nakiona".
"Weeee kweli?!!! Mimi unaniona?"
"Ndio nakuona".
Sophia alipiga kelele kuwaita watu kuwa vane ameona.

Kelele zile zilimfikia Hata Hansy Ambae nae alikuwa  bado hayupo sawa lakini aliamka na kufumbua macho yake inamaana ni kama nae alipona.

Hansy kuamka Ndipo akasikia kelele zile watu wakiitana,
"Jamani vane anaona vane anaona".
Nae aliamka haraka na kutoka nnje ya chumba alichokuwa.
Hapo alimkuta mlinzi,

"Tagadhali nasikia vane anaona naomba niende kumuona"
"Hata wewe tulikuwa tukisubiri tukuone ukiamka hongera sana shujaa".
Kwa sasa Hansy alikuwa akijibiwa vizuri tofauti na mala ya kwanza kabisa alivyofika.

Basi aliruhusiwa kuingia mpaka ndani Ndipo aliwakuta watu wote wakizungumza na vane.
"Baba siwezi kusubiri nahitaji kumuona Hansy anaendeleaje?".
Aliongea vile vane Ndipo akajibiwa na Hansy,
"Nipo hapa".

Vane alimtazama pamoja na watu wote hadi bi mtama hakuamini leo wote walipona kwa pamoja.

Vane aliinuka na Kwenda kumkumbatia Hansy,
"Siamini unaniona  kweli vane?"
"Nakuona hansy... Pole sana kwa yaliyokupata mpenzi Wangu yote kwa ajili Yangu pole sana dua Zangu zilikuwa kwako siku zote niliitamani hii siku ije itimie".
"Hata mimi vane yani naishiwa hadi maneno ya kusema hakika nakupenda vane tushukuru kwa yote".
Walikumbatiana hapo huku wengine wakiwatazama tu wamalize furaha na shauku walizokuwa nazo.

Basi siku iliyofuata mfalme mzota alichinja kuku, mbuzi aliokuwa nao kama kusherehekea kwa mwanae kupona na pia kuwafungisha ndoa ya kimila Hansy na vane.

Shuhuli hiyo ilifana ambapo alifika pia hadi kijana saidy ambae mpaka alihisi wivu Tena kumuona vane amepona tena yupo salama kabisa.

Watu walicheza ngoma na kufurahi kwelikweli.
Lakini baada ya hapo waliomba udhuru ya kuondoka kwenda mjini kuendelea na Maisha yao.

Mfalme mzota hakuwa na pingamizi kwani kwa wao waliwahesabu kama Tayari ni wanandoa kwa kufunga ndoa ya kimila.

"Nendeni na baada ya mda nami nitakuja huko kuwatembelea kubwa tu mtiachie namba zenu za simu kuna mahali tutakuwa tukienda kuwatafuta". Hansy alimpatia baba mkwe wake huyo namba ya simuna kisha walisindikizwa na kuondoka zao Tayari kurudi Daresalam.

Sasa walipanda kwenye basi kubwa la kuelekea mkoani Ndipo Hansy alimpigia simu Amon kumpa taarifa kuwa wanaenda ivyo amuandalie mahali pakufukia yeye na vane.

Amon alilifanyia kazi jambo lile ambapo alimuambia na Mwasifa kwa siku ile waliwatafutia hotel nzuri wafikie kwanza hapo.
Walipomaliza walikwenda kabisa kuwasubiri stend ya mabasi mpaka walipofika.

Walipokeana kwa shangwe kubwa walikumbatiana haswa vane na Mwasifa mpaka Machozi yaliwatoka kwa Furaha.

"Hatiamae jamani siamini Kabisa ahhh unaona vane Wangu"
"Naona mwasifa sitakaa nikusahau kwa wema wako asante rafiki Yangu nilikukumbuka sana".
"Hata mimi nilikumiss".
Basi walipanda katika Gari la Amon na Tayari Kwenda huko walipoandaliwa kufika.

Huko Maongezi yalikuwa mengi Ambapo ilifika mpaka usiku Ndipo amon na Mwasifa waliondoka na kuwaacha wenyewe Hansy na vane.

"Hansy tumefunga ndoaya kimila lakini si wote wanaoamini na Wazazi wako je watanipokea?"

"Kwa sasa kukupokea kwao siyo hiyali ni lazima tutafunga tena ndoa usijali ila nawaza usalama wako wasije kukuteka tena mkewangu".
Vane kusikia vile alinyamaza tu kimya maana anamfahamu aliemfanyia ivyo ila alikumbuka jinsi alivyomchimba mkwala kama akimtaja.

"Hansy yameshapita hayo kubwa nipo salama inatosha nitakuwa salama tu"
"Basi ok utavumilia kukaa hapa mkewangu kisha kesho nitafika nyumbani na ofisini kuangalia mambo yanavyokwenda tutapanga pakukaa. Na hiyo kesho nitawaambia kila kitu ila wewe bakia hapa kwanza".

" Haina shida Asante sana kwa kuwa na mimi hansy hakika najivunia wewe?"
" Karibu vane".
Walicheka hapo hapo japo bibie vane alikuwa na aibu aibu za hapa na pale lakini Tayari ndo alikuwa katika himaya ya hansy.

Siku iliyofuata mapema Wakati Hansy akijiandaa kutoka Ndipo mala walisikia mlango ukigongwa.
Hansy alienda kufungua Ndipo alikuta ni Mwasifa Ndie alikuja.
Hansy alifurahi kumuona Ndipo akamruhusu kuingia Ndani.

"Mhhh mnisamehe nimewajia Asubuhi subuhi kiukweli bado hamu haijaisha ya kuzungumza na vane nimelala namuota rafiki Yangu".
"Wala usijali umekuja muda muafaka hapa nami najiandaa kutoka ivyo vane atapata kuchangamka safi sana basi mimi niwaache".

Vane alimkumbatia hansy ambapo alimbusu na kuagana Ndipo akaondoka zake.

Walibakia yeye na mwasifa ambapo walikumbatiana tena na kucheka.

"Nimekuja hapa shoga nami kuna kitu kimenikaa moyoni".

Vane Alishangaa kusikia vile,
"Mhh unanitisha Mwasifa kuna nini? "
" Mwenzangu kuna wanaume wawili wananihitaji mmoja polisi ambae alinisaidia sana nadhani hansy alikusimulia  na huyu wa pili ni amon rafiki yake Hansy.
Mama yake kaniambia kuwa nafaa kuolewa na kijana wake isitoshe na amon mwenyewe kaniambia sikufichi nipo njia panda".

" Mhhh kwanza nikupe ho Hongera ni jambo jema... kiukweli raha ni kuwa na mtu Ambae utakuwa umempenda kwa dhat Kwaiyo wewe hapo nani unampenda?"

" Kiukweli alie Ndani ya moyo wangu ni Baraka lakini nawaza amon atalipokeaje hili".
" Basi inatosha hapo ni kumuambia tu ukweli amoni alafu uwe huru kila la kheri rafiki Yangu.. ngoja tuagize chai tunywe".
Walicheka wote kwa pamoja hakika ilikuwa ni Furaha kwa Upande wao.

Hansy alikwenda kazini kureport Ambapo alikutana na mkurugenzi mkuu na kumpa pole kwa matatizo aliyokuwa nayo.
Hansy  alikaribishwa Tena hospital na kukabidhiwa kazi zake Ambazo ataanza nazo.

ilikwenda siku ile mpaka kufikia jioni Ndipo Hansy alikwenda Nyumbani kwao.

Kufika alipokelewa kwa Furaha na bashasha na wazazi wake wote aliwakuta.
Walisalimiana vizuri na kukaa kuzungumza.
"Hakika nimefurahi sana kukuona kijana Wangu tuna mengi hapa ya kuzungumza na wewe lakini kabla ya yote kwanza uonane na mwenzako nadhani nae alikuwa akiisubiri sana hii siku ifike".
Aliongea Baba Hansy ndipo mala alifika bibie Ester kumbe alikuwa Ndani.

Hansy alishagaa kumuona Ester lakini wakati huo Ester alikuwa  alifurahi tu Ndipo akamsogelea Hansy na kutaka kumkumbatia.

Hansy alimzuia hakutaka Ester amguse,
"Ester sina ukaribu huo na wewe alafu imekuwaje unakaa hapa kwetu kama hauna mwenu?".

Mama hansy Ndipo akajibu,
"Hansy mwanangu ungempa nafasi azungumze kwa sasa Ester anakaa hapa na tulikuwa tunakusubiri wewe Urudi tupange habari za ndoa kwa Sababu Ester ana ujauzito wako".

Hansy alishtuka na kumtazama ester,

"Ni kweli Hansy mala moja tuliyokutana nimebahatika kubeba ujauzito nina Furaha haielezeki nakwenda kukuzalia mtoto kitu cha thamani sana naomba nipokee hansy".

Hansy pozi lilimuisha, alishindwa hata azungumze kitu gani pale aliishiwa cha kusema.....

Sijui itakuwaje?
Tukutane sehemu ya 18*ME&YOU*

SEHEMU YA.... 18
Na
Mamuh mohd
(0716730000)

Tuliposhia......

Hansy pozi lilimuisha, alishindwa hata azungumze kitu gani pale aliishiwa cha kusema....

SONGA NAYO....

"Mwanangu wala haina haja ya wewe kuwaza sana jambo la kheri hili baba. Ester ameonesha kama yeye ni Mwanamke kamili mala moja tu imejibu Mwanamke alie kamili Kupata wa namna hii ni adimu sana".
Alizidi kuchochea mama hansy lakini Hansy alimtazama Ester na kumjibu,

"Siwezi kulaumu Sababu ulifanikiwa kucheza na akili Yangu jinsi ilivyokuwa kwa Wakati ule na umefanikiwa.
Hongera lakini ukweli ni kwamba siwezi kukuoa ester.
Tayari nimefunga ndoa mbele ya Wazazi wa vane na kumchukua vane kama mkewangu.
Sawa kama una ujauzito imeshatokea".

Baba hansy aliinuka nae akamsogelea kijana wake.
" Hansy wacha kuzungumza ujinga ujinga lazima umuoe Ester uliempa ujauzito unategemea ni nani Ambae atamkubali akiwa na hali kama hii?
Unataka kumfanyia mwenzako unyama wa namna gani?.

Jibu tunalotaka kusikia kutoka kwako ni kwamba utamuoa Ester hakuna mjadala.

"Hapana baba... Amekataa basi naondoka hapa nitakaa kwetu na kulea ujauzito huu mpaka nitakapojifungua. Nina imani Mtoto atakuwa mkubwa na usije ukamtambua kama mwanao atasikia historia kuwa baba yake alimkataa Sababu ya Mwanamke Mwingine.

Kweli ulinikataa ulikuwa haunipendi Hansy lakini hata kwa sasa nina ujauzito wako bado unanikataa basi kweli unamaanisha sawa endelea na mwanamke wako nami nitabaki na mwanangu sitasumbua tena Asante kwa zawadi hii ya damu yako".

Aliongea kwa uchungu Ester Ndipo akataka kuondoka Hansy akamuita.
"Ester simama".
Binti kusikia vile kweli akasimama.
"Sawa kosa limeshatokea na siwezi kumuhukumu kiumbe asie na hatia Tutakwenda Kufanya vipimo tena vikiendana na ile siku uliyokuwa na mimi basi nitalea huo ujauzito na itabaki kuwa wewe ni mzazi mwenzangu".

"Hapana Hansy wala usijilazimishe fanya kama sina mimba  yako endelea na mkewako".
Ester alikaza kisha akaingia ndani.
Baada ya dakika chache alitoka akiwa na pochi  lenye nguo zake kwa maana anaondoka zake.

Walimzuia lakini Binti alikazania kuwa Hawezi kukaa pale kwa Sababu hansy ameikataa mimba ile.

Erick alimsogelea kaka yake,
"ivi kaka wewe una akili au una matope damu yako unaiacha kisa vane na madawa ya kichawi aliyokupa? Kaka nakuonaga mjanga ila katika hili ni bonge la boya.

Mimi nitaichukua ile mimba kama wewe umeikataa.
Nitailea na mtoto akizaliwa ataitwa jina Langu ukae kwa kutulia ".
Aliongea Maneno hayo erick ambayo yalimuumiza Hansy.

Hali kadhalika wazazi walibaki wakimsema Hansy juu ya kukataa mtoto na madhara yake.
" Unaweza kumkimbilia huyo vane kumbe akawa mbovu hata uzazi hana ndo utamkumbuka ester.. umemshikilia vane Mwanamke mwenyewe mbaya hata kuoga hajui"..

Aliongea kashfa nyingi mama hansy mwisho nae aliondoka hapo na kumuacha Hansy akizungumza na Baba yake.

Ester Alirudi mpaka nyumbani kwao, kufika alimsimulia mama yake kila kitu kilichotokea.
"Huyu vane ananini jamani mpaka hansy asifirahie hata ujauzito uliokuwa nao? Siwezi kukubali mwanangu uwe single mama never".

"Mama naumia sana sielewi huyo vane ana Nini haswa mpaka kaenda kumtibu amepona na wamefunga ndoa"

"Hakuna ndoa hapo kama walikuwa wanajiweza hiyo ndoa wangekuja kufungia huku tuwaone.
Hansy akiendelea na ubishi wake Safari hii atampoteza kabisa huyo vane tena ngoja tuweke watu waanze kumfuatilia tujue huyo vane alipo mbona atacheka".
Alijibu mama Ester mwanamama wa mjini .

Hansy Alirudi kule hotelini alipomuacha Vane na kumkuta mpenzi wake huyo.
Walisalimiana na kula kwa Pamoja.
Hansy hakuonekana kuchangamka jambo Ambalo hata Vane lilimshangaza, "Nikikuangalia nakuona kabisa haupo sawa mmewangu niambie?"

"Ahhh hapana uchovu tu wa kazi nipo sawa mkewangu pia nawaza mahali pakukaa tukishapata nyumba tukahamie nitakuwa ok sema madalali wanatutafutia nataka nyumba Ambayo itakuwa Karibu na ofisini Kwangu".
" Ohhh sawa mmewangu".
Vane alielewa lakini ivyo walipata kujilaza kupumzika.

Lakini Hansy usingizi kwake ulikuwa wa ngama, alikuwa na mawazo yake tofauti.

Maneno yale aliyokuwa akiambiwa na Ester ni kama yalikuwa yakijirudia akilini mwake.

Pia Maneno ya Mdogo wake ambae ni Erick pamoja na wazazi wake yalizunguka kichwani kwake.
Aliona kweli hafai kumtelekeza mtoto asiekuwa na hatia lakini pia hakuwa Tayari kumpoteza vane.

Alimtazama vane ambae kwa Wakati huo alikuwa amelala zake hana hili wala lile.
Alimbusu na kujisemea,
"Na hili pia litapita vane Wangu naomba uwe jasiri siku utakapojua kilichotokea najutia hili".
Hansy mpaka machozi yalimtoka kila akimtazama Vane.

Basi palipambazuka Ndipo siku hiyo hansy alikuwa ofisini kwake na rafiki yake yule amon.
Alimuelezea kila kilichotokea kwa Ester.
"Hili mbona kizaa zaa Hansy na nitakushangaa sana kama utaitelekeza damu yako.
Sawa vane ni wako unampenda lakini mtoto ni habari nyingine just image nawe baba yako labda angekukataa usingesoma ukafikia hapa usimtupe Mtoto wako.
Vane kama anakupenda atalivumilia hili ukipenda boga penda na ua lake".
" Vane sitaki ajue chochote kwa sasa wacha nizungumze kwanza na Ester".
Walikubaliana ivyo na kisha wakaendelea na kazi zao.

Jioni sasa ndipo Hansy alikwenda Nyumbani kwa kina Ester ambapo alimkuta Ester mwenyewe Pamoja na mama yake.
Walisalimiana vizuri.
"Ester kama nilikukwaza jana naomba unisamehe yaliyotokea yameshatokea ivyo tuendelee mbele.
Nitailew hiyo mimba pamoja na huyo mtoto".

Bi rose kusikia vile alimtazama Hansy, "Kiurahisi tu? Umzalishe ataolewa na nani? Wanaume wa siku hizi wanataka kuoa wake ambao hawajazaa waanze kuzaa pamoja unataka kumpa wakati mgumu Binti Yangu au?.

Nataka umuoe Narudia tena nataka umuoe".

Ester akamjibu mama yake,
"Mama Hapana usimlazimishe ana mke atapata watoto huko huyu Wangu kama hataki kunioa basi wacha ajue hana baba katika dunia hii".
" Ester wacha kuongea maneno makali usilazimishe ndoa ikaja kukupa maumivu nitakuwa baba bora kwa Mtoto Wangu".
" Msimamo Wangu ni huo Hansy kama hautaki kunioa basi tena nitahama kabisa hapa hautakaa unione mimi wala Mtoto wako".
Alijibu Ester kisha aliinuka na Kwenda zake chumbani.

Hansy nae aliamua kuondoka pasina hata kumuaga  mama ester maana kila mmoja alichanganyikiwa kwa namna yake.

Basi ilipita wiki moja ambapo Hansy na Vane walifanikiwa kukodi nyumba ndogo yenye vyumba viwili vya kulala, seble, jiko wakahamia na kuanza kuishi hapo. Ulibaki ni mgogoro wanafsi kwa hansy hakumuambia  chochote vane.

Hansy ilibidi akubali Kufunga ndoa Ester japo alimuahidi itakuwa ndoa ambayo Hansy hatolala kwa Ester wala kufanya chochote ni kama kumridhisha tu anachotaka.

Jambo lile alikubali Ester lakini si kutoka ndani ya moyo wake.
Aliamua kumtafuta Amon rafiki wa Hansy Ambapo alimtumia ujumbe wakuonana nae hotelini.
Amon Alikwenda Ndipo akakutana na ester.
Walisalimiana na kuketi mahali kimazungumzo.

"Hatuna ukaribu sana mimi na wewe Amon lakini nimeona wewe ndie rafiki wa Karibu na Hansy.
Nisaidie kama Mwanamke ambae nimepewa ujauzito Mwanaume hanitaki.
Sawa amesema atanioa lakini sivyo navyotaka mimi nisaidie".

"Kiukweli shemeji hiki kitu hata Mimi kimeniuma lakini Hansy hasikii wala haoni kwa vane".

"Naomba nisaidie namuhitaji hansy ili tulee Mtoto wetu.

Napambana kama mama wa mtoto alie tumboni.

Nataka umuambie vane habari hizi kisha hakikisha ananitafuta mimi kuna mpango tumepanga na mama nisaidie kwa hilo shemeji nitakulipa kiasi utakacho".

" Hapo sasa mtihani shem naanzaje kumuanbia vane na je kama Hansy atakuwa ameshamuambia?"

" Hansy aliwahi kunitamkia kuwa hataki vane ajue chochote sasa mimi nataka umuambie kisha mlazimishe aje kwetu siku hiyo Angie katika mtego tuliouweka na mama hautafeli kama utafanya navyomwambia...nataka tumfungulie kesi kuwa alikuja kutaka kuniua".

" Sawa shemeji nitakusaidia mpaka umenitafuta mimi umeona naweza".

" Nitafurahi sana na nitakulipa milioni mbili".

" Sawa haina shida tunampambania mtoto wetu alelewe na wazazi wake".

" Hilo ndilo la Msingi shemeji".

Basi Amon alikubali na hapo Ndipo tunapata kujua licha ya amon kuonesha anamuunga mkono Hansy kuwa na vane lakini baada ya Ester kuwa mjamzito nae alihamia upande wa Ester ndio maana amekubali kufanya kazi Pamoja na Ester.

Basi baada ya mwezi mmoja Ambapo maandazi ya harusi kati ya hansy na Ester yalikuwa yaliendelea, siku hiyo amon alikwenda nyumbani kwa Hansy anapoishi na vane.

Alijua kuwa hansy kamuacha ofisini ivyo nyumbani atakuwepo vane peke yake.

Vane alimkaribisha shemeji yake huyo wakasalimiana vizuri.
"Nilijua nitakukuta na Mwasifa kumbe hayupo?"
"Mhh Mwasifa ana wiki sasa ameenda kijijini kwao kwani hakukuambia? "
" Hapana nilimuhitaji akanikataa basi ndo akaondoka hata nyumbani kwetu".
" Hapana hakukukataa bali ulichelewa kutuma maombi yake shem.
Ameenda kutembea mala moja na kuwaambia wazazi kuwa huyu alie nae anataka kumuoa".
" Ni vizuri namuombea dua".
" Hilo ndo la muhimu".
" Lakini shemeji yanayoendelea unayafahamu? "
" Yapi tena? "

" Mhhh shemeji una kifua? "
" Unanitisha shemeji kwema? "
" Nijibu unakifua cha kustahamili hiki nachokwambia?"

" Nitavumilia niambie ".

" Hansy yupo kwenye maandalizi ya kufunga ndoa na Ester Ambae Tayari ni mjamzito unayajua hayo?".

Vane alishtuka mwili mpaka ulitetemeka kwa mshangao.....

Sijui itakuwaje?
Tukutane sehemu ya 19*ME&YOU*

SEHEMU YA... 19
Na
Mamuh mohd
(0716730000)

Tuliposhia....

Hansy yupo kwenye maandalizi ya kufunga ndoa na ester ambae Tayari ni mjamzito anayajua hayo? "..

Vane alishtuka mwili mpaka ulitetemeka kwa mshangao...

SONGA NAYO.....

"Shemeji unaongea nini? Mbona sikuelewi unasema nini?"
"Kama ambavyo umenisikia shemeji sasa wewe cha kufanya kabla hujamuuliza Hansy kwanza nenda kaongee na Ester.
Nenda nyumbani kwao utakuta maandalizi  ya harusi  pale atakuambia kila kitu na hansy alimuambia kuwa wewe ameshakuacha Ndio maana mpaka Leo hajakupeleka tena kwa wazazi wake, wanajua haupo tena katika maisha ya Hansy.

Shemeji sisi wanaume ni waongo sana tunaongoza katika uongo wa mapenzi.

Hansy anakutafutia tu namna akishamuoa Ester mama kijacho wake basiii kwisha Habari yako".

Vane mpaka alisimama,
" Shemeji Hapana hakuna kitu kama icho ni uwongo shemeji Hapana Hansy wangu hawezi kunifanyia ivyo".
" Shem sikatai ni kweli Hansy alikupenda sana lakini baada ya kumpa Ester ujauzito akawa hana chaguo huo Ndio ukweli nisikilize mimi twende nikupeleke kwa Ester unazungumze nae kama mwanamke mwenzako wala usipanick akuelezee kila kitu Kisha nawe muelezee nakupa hii siri sisi wanaume ni waongo sana".

Vane alibubujikwa na Machozi ndipo aliona kweli alichomuambia shemeji yake alitaka Kwenda kuzungumza na Ester ili ajue ukweli.

Walitoka wote Amon pamoja na vane mpaka nnje Kwenye Gari la amon wakapanda na kuanza safari.
Wakati huo vane alikuwa akilia tu njia nzima haamini kile ambacho Amon amemuambia.

Basi walifika mpaka nnje ya nyumba ile Ndipo amon akamuambia vane.

"Ni hapa sitaingia Pamoja nawe nitabakia nnje nikikusubiri maana Ester akiniona asije kujua nimekuja kukuambia ukweli akajua nipo kundi moja na wewe hali ya kuwa Hansy amenitambulisha kwake ni shemeji".
Vane alishuka kwenye Gari hakutaka hata kuzungumza Mengi akagonga geti na kuruhusiwa kuingia Ndani.

Alimkuta Ester Ndie aliemfungulia mlango mkubwa wa kuingia Ndani.
"Vane umekuja kwa kheri au mbona unalia na unaonekana una jazba"
"Niambie ukweli nini kinaendelea kati yako na Hansy niliyoyasikia ni kweli au?"

"Hansy kwani wewe unamuulizia Hansy kama nani? Mimi najua mmeshaachana na anajiandaa kunioa mimi ameniambia haupo kabisa hata jiji hili".

Hansy ni mumewangu tumefunga ndoa mbele ya wazazi Wangu.

Kwanini amedanganya siamini".

"Vane tafadhali usiniharibie ndoa nataka kufunga ndoa na hansy tulee mimba na mtoto wetu alie tumboni  tafadhali niachie Hansy Wangu sipo Tayari kuwa single mama niachie mwanaume Wangu".

Vane aliumia sana akaamua Kuondoka lakini ile anafika mlangoni mala akasikia sauti ya Ester alipiga kelele kama mtu Ambae ameumia ivi.

"Uwiiii...uwiiiiiiii....uwiiiiiiiiiii
mamaaaa...mamaaaaa".
Vane alisita kuondoka kwanza akabaki anamtazama maana licha ya kuwa kuna uadui kati yao lakini kwa hali ile aliyomuona nayo ilibidi asimame kumtazama.

Ester aliangukia kwenye kochi ikabidi Vane arudi Ndipo alifika msichana wa kazi akiwa na Mama Ester.

Walishangaa kumuona vane na hata vane alishangaa kuwaona kwanza hakujua kama wapo.

"Umefuata nini katika nyumba hii vane? Ulitaka kumuua? Ulikuwa unamkaba mwenzako kwanini?"
"Hapana mama Si ivyo"
"Kelele ulikuwa unamkaba nilikupa onyo umepona sasa umerudia tena sitakuacha nakuangamiza".
"Hapana mama".
Mama Ester alifunga mlango kisha akapigia simu polisi ambae Cha ajabu alifika Ndani ya dkk 5 tu.

"Mkamateni huyu tummemkuta anamnyonga Ester hapa anapatiwa huduma ya kwanza alitaka kumuua".
Vane alibaki anatikisa kichwa asijue cha kusema Ndipo alichukuliwa na kutolewa nnje Tayari kupelekwa kituo cha polisi.

Vane alipiga kelele na alipofika nnje hakumuona hata shemeji yake yule aliemleta hakujua kama ule ulikuwa ni mtego Ambao bibie vane alinasa.

Ester aliamka sasa na kuanza kucheka na mama yake.
"Ahhh mama wewe kiboko una Mipango ta hatari wewe?"
"Bila ivi mwanangu tungesumbuka sasa hapa nimeweka mtu maalum wa Kwenda kuzungumza na Hansy Maneno niliyomtuma amuambie Hansy yatasabisha hansy kwanza kutoka kwa muda kwenda kumtafuta vane.
Wakati huo sisi tutasimamia kesi vane akishafika magereza kwisha Habari yao.

Hansy hatojua kitu atakubali tu kukuoa wewe".
" Yani mama chochote utakachosema mama Yangu mimi sawa maana unaweza mpaka unaweza Tena khaaa".
Walifurahi wote Pamoja mambo kwao yalikuwa mazuri.

Wakati huo vane alipelekwa kituo kukubwa cha polisi ambapo mkuu wa hapo alikuwa rafiki wa bi Rose ivyo walikubaliana kuwa hiyo kesi aisimamue kuhakikisha vane anakwenda jela.

Kweli majira ya jioni Hansy kurudi nyumbani alikuta nyumba ipo kimya. Aliingia mpaka ndani akakuta Vane hayupo na simu aliiacha nyumbani.

" Nampigia  sana hapokei kumbe simu ipo nyumbani sasa kaenda wapi?".
Hansy ilibidi atoke mpaka kwa mlinzi wao getini.
"Umemuona Mkewangu akitoka?"
"Hapana boss nimeingia jioni hii sijaona mtu akitoka nikajua atakuwa ndani "
" Hapana Ndani hayupo... Haya sawa".
Hansy Alirudi ndani akaona Asubiri kwanza huwenda Atarudi.

Lakini muda ukizidi kwenda Ndipo mala kuna kijana Ambae alifika nyumbani pale kwa Hansy na kuomba kuonana na Hansy .
"Habari za usiku brooh"
"Salama Karibu"

"Asante mimi ni boda boda huwa napack pale juu kidogo.
Kuna msichana amesema alikuwa akiishi hapa kanielekeza namba ya nyumba hii.
Amesema nije kukumbua kuwa usimtafute anakwenda mbali na anakutakia ndoa njema na Malezi Bora ya mtoto".

Hansy alishangaa maana alijua kama Vane katuma ujumbe huo basi lazima atakuwa amejua ukweli.
"Ameenda wapi tafadhali niambie?"
"Sijajua kaka ila nimmempeleka hadi stend ya mabasi ndo akanipa ujumbe huo".

Kijana yule alipomaliza kutoa ujumbe akaondoka zake na kumuacha Hansy asijue cha kufanya.

Aliamua kumpigia simu Amon Usiku uleule na kumuelezea kilichotokea. Amon alifika nyumbani kwa Hansy maana aliona hayo si ya kuzungumza kwenye simu tu.
"Ohhh pole sana sasa atakuwa ameambiwa na nani jambo hili na kwanini shemeji anakuwa mwepesi kufanya maamuzi".
"Sijui kiukweli sijui amon hujui tu ila kiukweli nimechanganyikuwa sana hata Sielewi kabisa".
"hata kumtafuta tutamtafutia wapi itakuwa ngumu".

" Kesho nitakwenda Kwao morogoro huwenda ameenda huko na kama hayupo basi nimuambie baba yake kila kitu".

" Aisee sawa Hansy hakika ni mtihani ambao hata sijui tunafanya nini".

Amon alijitia kusikitika nae kana kwamba hajui chochote kunachoendelea hapo" .

Basi siku iliyofuata Hansy Alirudi kijijini kule nyumbani kwa kina Vane Kwenda kumuangalia ambapo alikuta hayupo.

Alieleza kila kitu kilichotokea.

Mfalme mzota alishangaa.

" Ahhh kwanini ufanye ivyo inamana ni kweli una mwanamke mwingine ndio maana binti Yangu kasikia akaumia sana si Ndio?"
" Hapana baba hii ilitokea kipindi vane bado hajaona nilitegewa mtego nami nikanasa na yule mwanamke ndio Sababu akapata ujauzito".
Mfalme mzota alinyamaza kwa muda kisha akataka walinzi wakimkame hansy wakamfungie kwanza.

Walimuweka katika chumba icho mpaka Asubuhi Ndipo akaamuru afunguliwe.
Hansy Alitoka na kuamkuta mfalme mzota akiwa nae amejiandaa.
"Tunaondoka wote mpaka mjini huko nikamtafute Binti Yangu.

Usiku nilikwenda kwa bi mtima ameniambia cha kufanya inaonesha mwanangu yupo hukohuko wala hajaja huku sasa nataka nikamtafute".
" Haina shida Kabisa mzee Wangu tutakwenda na utafikia Kwangu Hapana shida yoyote".

Mfalme mzota aliiacha himaya yake kwa mala ya kwanza tokea awe mtawala na kuamua kwenda  mjini kumtafuta Binti yake.

Bi malkia alibaki akilia sana kwani aliona licha ya yeye pia kubeba ujauzito lakini wapiii mmewake bado alikuwa akimpenda sana Binti yake mpaka kuamua kwenda kumtafuta mjini.

Upande wa bibie Vane siku hiyo alifikishwa magereza akiwa amevaa mavazi ya kifungwa, Mipango ya bi Rose aliongea na wakubwa aliofahamiana nae na kuhakikisha siku ile ya pili vane anakwenda magereza ndicho alichokuwa anakutaka.

Bi Rose alitoa pesa Nyingi sana kuhakikisha anachokitaka basi kinatimia.
Vane alilia mpaka alifika mahali alinyamaza na kukubaliana na hali.

Kwa hayo aliyokuwa pia ameyasikia kuwa  Hansy anatarajia kufunga ndoa na  Ester amempa ujauzito binti ndo yalizidi kumuumiza akaona bola atumikie adhabu ile asiyaone yanayoendelea....

Sijui itakuwaje?
Tukutane sehemu ya 20*ME&YOU*

SEHEMU YA....20
Na
Mamuh mohd
(0716730000)

Tuliposhia.....

Vane alilia mpaka alifika mahali alinyamaza na kukubaliana na hali. Kwa hayo aliyokuwa pia ameyasikia kuwa hansy anatarajia kufunga ndla na Ester amempa ujauzito Binti ndo yalizidi kumuumiza akaona bola atumikie adhabu ile asiyaone yanayoendelea.....

SONGA NAYO.....

Majira ya jioni nyumbani Mr kwa Makuka palikuwa na mjumuiko wa chakula cha jioni kati ya familia hiyo na Familia ya Bi Rose.

Walikuwa mwanzo wakipanga mikakati ya harusi Ambayo Tayari imeshawadia kwani walijua hansy hatokaa ampate vane alipo ivyo kiroho safi atamuoa Ester.
Basi walikuwa wakizungumza Maongezi mbalimbali  huku wakicheka na kufurahi.

Upande wa Hansy alifika nyumbani yeye Pamoja na Mfalme mzota.
"Baba Karibu sana hapa ndo nyumbani jisikie huru kabisa".
"Asante sana Hansy kweli wenzetu mnaishi maisha Mazuri tukiwaangalia nyinyi ndo tunajua sisi kule hatuna raha kama kwenu huku".
" Ni kawaida baba"

" Kwaiyo hapa ndo ulikuwa ukiishi na Vane".
" Ndio baba hii nyumba nilipanga wakati nikijiandaa kujenga kwa ajili yetu".
" Safi sana... Naamini kweli unampenda Binti Yangu. Nenda ukamuoe Huyo Mwanamke Ambae Tayari ni mjamzito na umlete hapa nitaishi nae Wakati namtafuta Binti Yangu"
" Baba Sina hata hamu ya kufunga ndoa ikiwa vane Wangu hayupo.
Na siwezi kumleta eti aje kuishi nyumba hii ambayo palikuwa kwa Vane.
Akalala kitanda ambacho alikuwa akilala Vane siwezi baba.
Patabakia hapahapa utaishi wewe naamini vane atakuja mkewangu"

" Hansy kuna mambo mengine ili ujue yaliyojificha basi lazima uinamishe kichwa chini kwanza wewe muoe na umlete hapa.
Hivyo vitu vya mwanangu nipe mimi nitavihifadhi katika chumba nitakacholala nisikilize mimo Hansy najua nachokifanya".
Hansy alinyamaza kimya kwa muda kisha akamjibu Baba vane.
" Sawa baba nakubali lakini sina Mapenzi kabisa na huyo msichana nitamuoa na akishajifungua sidhani kama nitaendelea kuishi nae".
" Wewe ni Mwanaume mambo kama haya lazima yatokee.
Sikiliza hakuna atakaefahamu kama mimi ni baba yake na vane.

Nimeona kuna chumba pale nnje nitaomba mimi nilale hapo"
" Hapana baba pale huwa analala mlinzi wewe baba Yangu utalala humu ndani "
" Nisikilize Hansy elewa nachokwambia sawa? ili nijue mwanangu alipo sitakiwi kujulikana kama baba yake na Vane nitambulishe hata nafanya kazi ndogo ndogo ndogo Mbele ya huyo Mwanamke akija kwa Sababu yule bibi aliewatibia wewe na vane kule kijijini Ndie kaniambia anahisi vane yupo hukuhuku jijini na kutoweka kwake ni njama za wati".

Hansy Kusikia vile ndo kama vile nae alizinduka,

"Baba hili linawezekanaje? Wao huwenda ndo wanajua alipo vane? Ni kweli baba sikuwahi kumuambia vane kitu chochote kile lakini sijui nani aliemuambia ukweli sielewi baba"

"Ndo nakwambia hatuhitaji Haraka weee Subiri ukweli utajulikana lakini nisije kukuta ni wao wamemdhuru Binti Yangu sitaangalia mala mbili kama ni ndugu zako au laa kwa nitakachowafanya".

"Baba Adui wa vane pia ni Adui Yangu"

"Basi fanya kama navyokwambia kwanza".

Basi Hansy alikubaliana na mzee huyo Ndipo akampeleka kwanza akaoge na kisha hansy akarudi jikoni kuandaa chakula cha Haraka ambacho watakula usiku huo.

Kweli siku iliyofuata baada ya kutoka kazini jioni Hansy Alirudi nyumbani kwao.
Alionesha uchangamfu jambo ambalo hata wazazi wake walishangaa.
Hansy alikuwa ameshaandaliwa kwa namna yake na baba vane ndivyo nae alivyofanya.

Mama Hansy hakujizuia kumuuliza kijana wake,
"Leo nakuona upo tofauti sana mwanangu una Furaha gani baba?"
"Hapana mama Mbona nipo kawaida na nimeamua kurudi kuja kuishi hapa mpaka pale nikishafunga ndoa na ester".

"Hansy ni wewe unayazungumza haya mwanangu? Kweli wewe ni Hansy wangu hata siamini kabisa".
"Usijali mama nipo sawa.
Ester amenishika pabaya sana anakwenda kuwa mama wa mwanangu lazima nimpe kipaumbele sasa".
"Kwaiyo umeachana na vane kabisa?"
"Ahhhh achana nae mjinga yule sijui kapata wanaume mjini hapa wamemtorosha kaondoka.
Nimeamini mama jogoo wa shamba hawiki mjini tuachane na hayo".
Wazazi hao walifurahi siku hiyo kweli kijana wao waliona amepita Ambapo wao wanapataka.

Usiku ule Hansy alikwenda mpaka nyumbani kwa kina Ester akiwa na Mdogo wake yule Erick.
Walikaribishwa vizuri mpaka ndani.

"Nimeona sio vibaya kuja kukuangalia hali yako jinsi ulivyoshinda Ester".
"Hansy ni wewe unayasema haya mbona siamini?"
"Usijali tusahau yaliyopita twende Mbele turudi nyuma wewe sasa unakwenda kuwa mama wa mwanangu una nafasi ya kipekee ester".
"Asante kwa kulifahamu hilo hansy naamini hautanitesa katika ndoa yetu"

" Neno mateso lisahau Ester tutaishi ndoa ya furaha na amani na mtoto wetu atakapozaliwa ataongeza Mapenzi ya dhati kwetu".
Ester alifurahi na kuinuka kumkumbatia Hansy.
Hansy alimtazama Ester na kumuambia,
" Nipe muda kidogo nakuja nakuja".
Hansy alitoka nnje.

Walibakia Ester, mama ester na Erick wakishangaa hawaamini.
" Shemeji umeweza huyo mganga wako kiboko usije kumpeleka mkewangu nami akaja kuniteka".
Aliongea Erick Ndipo wlte wakacheka,
" Yani siamini mmemshawishi nini maana sikutegemea jamani? "

" Sisi wenyewe tumeshangaa kaja kabadilika nadhani baada ya kumtafuta yule mshamba wake akamkosa kaja anatuambia eti huwenda kapata wanaume wamemlaghai".
" Jamani jamani afadhali aamini ivyo".
" Yan shem hii imeenda harusi tunayo".
Walifurahi wote pale na punde Alirudi Hansy Ndani Mule wote wakakaa kimya.

Hansy alimsogelea ester na kisha akatoa kifaa ambacho kilikuwa na Pete Ndani yake inamana ndicho alikifuata kwenye gari.

Hansy aliishika pete ile na kumuuliza Ester,

" Will you marry me ester??"

"Yes yes yes yes iwill".
Alijibu Ester kwa furaha Ndipo akakumbatiana na Hansy hakika ilikuwa ni Furaha kweli ya aina yake.

Mwanamama bi rose sasa walau nae alishasha pumzi,
" Ahhh afadhali jamani Hatimae hansy amempokea Ester mkewe na mama wa mwanae mtarajiwa.
ilibidi kumtoa vane hapa ndo mambo yameenda sawa.
Vane utaoze huko jela ili mwanangu awe na maisha Mazuri na Mumewake".

Alijisemea mwanamama huyo huku akimuangalia mwanae jinsi alivyokuwa na furaha.

Hayawi hayawi hatimae yalikuwa iliwadia siku ya harusi.
Ester alivaa gaoni lake la harusi na kupendeza kwelikweli hakika alipendeza kweli.
Gaoni alilolivaa mrembo huyo lilikuwa la thamani ya milioni 10.
Nguo ilinakshiwa na mapambo ya dhahabu.

Hansy pia alijuandaa kwa kuvaa sare na baba yake pamoja na Mdogo wake Erick wote walikuwa katika muonekano wa nguo saresare na Safari ikaanza kuelekea nyumbani kwa kina Ester.

Huko walifika na kupokelewa na shangwe la haja na kisha ndoa ilifungwa.
Kutokana na hali ya Ester aliyokuwa nayo ya ujazito Sherehe iliishia tu pale nyumbani waliondoka na mumewe kuelekea katika nyumba yao sasa ambayo wataishi.

Walibaki mama Hansy na mama Ester wakisherehekea na kumkumbatia.

"Hatimae tumeweza rafiki Yangu khaaa!!! Siamini kama Hansy Leo Kamuoa Ester"
" Hakuna mwanzo uliokosa mwisho rafiki Yangu nilikwambia mimi ndo Rose hili jambo litakuwa umeniamini sasa?"
" Hakika shoga angu Leo tumwagilie moyo kwa raha zetu".
" Umeonaeeeee".

Hansy Alifika na mkewe mpaka nyumbani kule alipokuwa amepanga ambapo walisindikizwa na ndugu wachache wakawaingiza mpaka ndani na kisha Ndipo wakaondoka.

Walibakia wanandoa wenyewe wakifurahi siku ile.

"Mkewangu kutokana na hali yako naomba nikupikie chakula kisha upumzike tu leo".
"Mhhh unanijali sana lakini Tayari mimi ni mkeo kuwa huru"
"Nafahamu Lakini kukujali ni muhimu weee ukitaka hayo ukishajifungua mbona utafurahi".
"Hahaha... lakini kubwa mimi kuwa na wewe nina Furaha sana".
Walikwenda wote jikoni wakawa wanakaanga kuku na viazi kwa ajil ya chakula chao cha Usiku.

Basi siku iliyofuata Asubuhi Ester aliamka mapema na kuwahi yeye jikoni akamuandalie chai mumewake.

Sasa akiwa jikoni kule dirishani akamuona baba mtu mzima akiwa anafagia fagia.

Ester ikabidi atoke mpaka nnje.
"Wewe ndie mlinzi wa hapa?"
"Hapana mwanangu mimi ni mfanya usafi tu"
"Hansy anawezaje kukuajiri baba kama wewe ufanye usafi ok labda kwa kuwa alikuwa yeye mwanaume hajui mambo ya ndani ila mimi binafsi hapana Sababu nitataka mfanyakazi wa nnje na usafi wa ndani kwa wewe Hapana leo nadhani ndo itakuwa mwisho wewe kufanya usafi".
Aliongea Ester kisha akarudi ndani.

Baba yule Ambae sisi tunamfahamu ni bwana mzota baba mzazi wa Binti vane alibaki akimtazama tu Ester mpaka alipoingia ndani.....

Sijui itakuwaje?
Tukutane sehemu ya 21*ME&YOU*

SEHEMU YA.... 21
Na
Mamuh mohd
(0716730000)

Tuliposhia.....

Baba yule Ambae sisi tunampa ni bwana mzota baba mzazi wa Binti Vane alibaki akimtazama tu Ester mpaka alipoingia ndani....

SONGA NAYO....

Ester kufika ndani alimkuta mumewe nae ameshaamka yupo jikoni akiweka sawa maziwa Ambayo yalikuwa yakimwagika.
"Ohh mmewangu afadhali niliacha mazima jikoni nikatoka kumuangalia yule mzee"

"Ni kama baba Yangu naishi nae hapa hana mahali pakukaa nilimtoaga huko sokoni anaokota okota vitu nikaona nimchukue".
" Mhhh kwaiyo tutaendelea kuishi nae? "
" Ndio mbona hana shida anapenda kazi vibaya utashangaa kakupandia vimchicha".
" Ni kweli Hansy lakini naona kama ni mapema sisi kuanza kuishi na watu hapa labda kwa kipindi hiki tungekuwa wenyewe tu hata dada wa kazi sihitaji mpaka nikishajifungua".

Ester mkewangu sidhani kama kuna ubaya mpokee tafadhali huwa analala kile chumba cha nnje yeye na mlinzi hawana tabu".

"Na chakula inamaama mimi ndo nitakuwa nawapikia?"
"Ohhj sikukuambia baba yule muone vilevile anapika ugali vibaya sana mboga anapika vizuri".
Ester aliona anyamaze lakini hakufurahishwa na uwepo wa mzee yule pale nyumbani.

Basi siku ile walishinda Ndani Hansy na mkewe lakini Hansy alijitahidi kumkwepa Ester kulala nae kama mke kwa Kigezo cha kwamba mjamzito anatakiwa kupumzika.
Ester nae alikubali kubwa alijua tayari Hansy ni wake ivyo mambo Mazuri yatakuja tu.

Siku iliyofuata Asubuhi Hansy alijiandaa kwa ajili ya kwenda kazini.
Ester alionesha madeko kwa mumewe .
"Natamani hata uendelee kukaa mmewangu hatujamaliza fungate yetu"
"Nafahamu mkewangu lakini hapa Katikati nilizunguka sana kazini nikawa siendi ndio maana  wakati huu sijapewa mapumziko  kwaiyo wewe mkewangu kaa ndani kwa ajili Yangu pia".
" Mhh sawa mmewangu lakini basi walau uwe unawahi kurudi ucheze na mwanao tumboni".
" Usijali".
Waliagana hapo ndipo hansy akatoka zake kwa ajili ya Kwenda kazini.

Alipofika nnje hansy alisimama kuzungumza na Baba vane.

" Baba shikamoo"

" Marhaba hongera sana kwa Kupata mke"

" Baba najilazimisha ni kwa vile wewe umeniambia.

Nataka kutafuta safari ya kikazi ili tu niwe mbali na huyu mwanamke kwa muda kwaiyo fanya huo uchunguzi wako kwa Haraka".

" Mhhh!! Usiwe na haraka Hansy mambo mazuri yatakuja tu kuwa kawaida kama ulivyoniahidi".

" Sawa baba lakini sina matumaini tena ya  kumpata vane Wangu "

" Atapatikana tu ni mapema sana kukata tamaa".

Sasa Wakati huo wanazungumza alikuwepo Ester dirishani akiwaangalia. Hakusikia kilichozunguzwa lakini aliwaona tu ukaribu wao.

"Huyu mzee Hapana ukute anamuomba pesa hansy shida ndo zimemjaa". Alijisemea Ester kisha akachukua simu na kumpigia mama yake.

"Haloo mama shikamoo"
"Marhaba mwanangu pole na heka heka za harusi mnaendeleaje?"
"Kiukweli mama naendelea vizuri Kabisa Hansy hana kinyongo kabisa na mimi tumecheka na kufurahi hakika nimepata mume niliekuwa namtaka".

"Hongera mwanangu hii Ndio Furaha Yangu kuona una Furaha".

"Lakini mama kuna mbaba nimemkuta hapa jamani  macho yake kama mchawi eti Hansy kamuokota sokoni huko kaja hapa kuishi nae".
"Heeee!!! Mwanangu usikubali mfukuzie mbali umesikia Hansy akiwa hayupo mfukuze aondoke zake hapo wewe hapo ndo kwake".
"Ni kweli mama nafanya ivyo ivyo Hansy Leo kaenda kazini akija atakuta huyu mzee wake hayupo".
Basi Ester alikubali wazo lile la mama yake na kufurahia kabisa akaona asipoteze muda afanye ivyo haraka.

Siku hiyo katika magereza Asubuhi ulikuwa ni muda wa Kwenda kunywa uji. Wafungwa walikuwa wamepanga foleni na vikombe kwa ajili ya kuchukua uji wa mahindi ndio chakula chao cha Asubuhi.

Walikuwepo askari magereza wawili wakisoga gazeti na kuzungumzia harusi ya Binti wa mwanamama  Tajiri na maarufu nchini Bi Rose.

Walikuwa wakioneshana picha Ndipo binti vane nae akiwa kwenye foleni alifika zamu yake kupewa uji Ndipo akaona na gazeti lile kuhusu harusi ya kitajiri.

Vane alitazama kwa makini Ndipo akaona picha ya Ester kama bi harusi amevaa amependeza.
Vane alikumbuka na vile alivyoambiwa kuwa Hansy anatarajia kumuoa aster Ndipo aliunganisha picha ile akaona yametimia Ester ameolewa na Hansy.

Binti aliumia mpaka alikosa nguvu gafla aliangusha kikombe cha uji ule.
Askari walimsema na kipigo juu pasina hata kupewa uji mwingine.
Vane alilia sana ilibidi arudi  gerezani na kukaa zake akilia sana huku wafungwa wenzake wakiwa wanamcheka.

Ester alitoka mpaka nnje kwa wakati huo mlinzi alikuwa ameshaondoka kama Kawaida Asubuhi anaondoka na kurudi jioni.

Basi ester alifungua geti Kisha akamuita baba vane.

"Weeeee mzeee naomba uondoke hapa sio kwa mwanao.

Kutwa unamsimamamisha hansy kumuomba ela kwani huna watoto? Nyie itakuwa Ndio wale wazee mnaotelekeza watoto wenu wakiwa wadogo mkishakuwa watu wazima ndo mnaanza kutanga tanga kusumbua watu.

Mmewangu kwa sasa anahitaji kuweka pesa kwa ajili ya mwanae ajae sio kuokota okota wazee mtaani haya ondokaaaa".
Ester alimsukuma mzee yule mpaka nnje getini".
"Nisamehe mwanangu sina pakwenda tafadhali"
"Nenda hukohuko sokoni ukaokote au chukua elfu 5 hii itakusaidia ondoka nyumbani Kwangu".
Ester alifunga geti na kumuacha mzee yule akiamini ataondoka.

Siku ilienda Ndipo usiku saa 2 Hansy Alirudi Nyumbani akiwa na baba vane.

Ester alishangaa kuwaona maana anafahamu yeye ni kwamba alimfukuza lakini gafla amerudi.

"Mkewangu mzee Wangu Leo alikuja ofisini Kwangu tumeshinda wote na ameshakula hapa anaenda zake kupumzika tu".

Baba vane nae akaitikia kama vile hakuna kilichotokea.
"Ni kweli mwanangu nilikuwa nae kazini kwake naangalia angalia magorofa haya usiku mwema".
Baba vane alitoka zake na Kwenda katika chumba chake kile cha nnje alichokuwa analala.

Ester alibaki sasa yeye na maswali Mengi kichwani kuwa huyo mzee amemuambia hansy ukweli au laa? Aliona kwa Mpango huo wa kwanza amefeli.

Siku ya pili iliyofuata baada ya Hansy kwenda Kazini ester alimpigia simu mama yake na kumuelezea kila kitu kuwa Mzee yule alimfukuza lakini akarudi tena.

"Mwanangu huyo sio mtu mzuri hata kidogo kwanini umfukuze alafu arudi kama hakuna kilichotokea? Basi katolewa kistaarabu akishindwa niachie mimi.

Namtumia vijana Wangu wanamteka anafilia mbali".
"Mama nakutegemea maana ananiweka roho juu juu jamani khaaa".
"Limeisha ilo leoleo analetwa kwangu ndo atakiona cha moto".
Alijibu mama Ester ambae alikuwa akijali sana Furaha ya mwanae kuliko kitu Chochote.

Basi Majira ya mchana Ndipo kweli Kuna vijana walifika nyumbani hapo kwa Ester.
Walimshambulia mzee yule baba vane kwa kumuwekea madawa puani akapoteza fahamu na kisha wakambeba na kuondoka nae.

Ester alikuwa akiangalia kwa kupitia dirishani akaona afadhali mzee huyo hatokaa arudi tena.

Mzee yule alipelekwa mpaka katika jengo fulani ambalo aliwahi kupelekwa Vane na kupuliziwa matindikali machoni.
Safari hii alipelekwa mzee huyo na kufungwa fungwa kamba kusubiri bossa aje atoe maamuzi.

Jioni Ndipo mama Ester alikwenda katika jengo lile akiwa na silaha nia ammalize kabisa mzee yule.
Alkuta Tayari ameshapigwa mpaka uso umejaa damu na majeraha.

Mama ester alipofika alimcheka.

"Wewe umefuata nini Kwenye maisha ya mwanangu unataka kufanya nini? Kukufukuza ndo lilikuwa onyo na sasa nakupa kali kuliko zote nakuweka mbali na maisha ya wanangu wale waliofunga ndoa.

Mama ester alitoa silaha na kumnyooshea mzee yule Ndipo aliinuka kwa Sauti ya juu mzee yule akamjibu,

"Tagadhali  usiniue mwasike".

Bi rose kusikia jina lile alishtuka maana ni jina lake ambalo alikuwa akilitumia zamani Wakati yupo kijijini na alipofanikiwa kuja mjini alitumia Rose.

"Umeniita mwasike wewe nani?".
Aliuliza madam rose huku akimuangalia kwa ukaribu mzee yule Ndipo alijikuta nae anaita,

"Mzota...."

Sijui itakuwaje?
Tukutane sehemu ya
22*ME&YOU*22_26

SEHEMU YA.... 22
Na
Mamuh mohd
(0716730000)

Tuliposhia....

"Umeniita mwasike wewe nani?"
Aliuliza madam rose huku akimuangalia kwa ukaribu mzee yule Ndipo akajikuta nae anaita,

"Mzota..."

SONGA NAYO.......

Bi rose alichanganyikiwa Ndipo akamsogelea bwana mzota kwa ukaribu,
"Kumbe ni wewe... Hakika ulibadilika sana sikudhania kama ni wewe jamani imekuwaje imekuwaje".

Bi Rose akaanza kumfungua mzee yule Ndipo na wale vijana wake wakamsaidia kumfungua.
Lakini walipomaliza kumfungua kamba mzee yule aliishiwa nguvu akaanguka na kupoteza fahamu.
Ni kutokana na kipigo alichokipata hali ilibadilika.

"Hapana Hapana amka uniambie mwanangu Yuko wapi amkaaaaaaa".
Alilia sana mwanamama huyo Ndipo akawataka vijana wake wambebe Mpaka nnje Kwenye gari amuwahishe hospital.

Njia nzima alikuwa akilia sana huku akiwa anampepea kwani dereva alikuwa ni mmoja kati ya wale vijana.
Kijana mmoja Ndipo akamuuliza bi Rose,
"inaonesha unamfahamu huyu madam?"
"Acheni tu ni mtu wa muhimu sana laiti ningekua nisingeruhusu mumfanyie ivi....amka mzota niambie mwanangu yupo wapi? Uzao Wangu mimi mwanangu".
Alilalamika Mwanamama Huyo mpaka walipofika hospital Ndipo Akapokelewa tayari kwa kuanza Matibabu.

Bi Rose Ndipo alimpigia simu binti yake Ester huku akiwa analia hata kuzungumza alishindwa.
Ester nae alipata hofu..

"Mama unaniogopesha niambie nini kimetokea mama Yangu, niambie tafadhali mama Yangu"
"Njoo hospital ya mgenza hapa Mjini kati njoo"
"Sawa mama inaonesha ni dharura sikawii nakuja Sasaivi".
Ester hakuwa na jinsi nae alianza Safari Kwenda huko hospital.

Kufika alimkuta mama yake ndipo sasa akamuelezea.

Uzuri Ester nae alikuwa akifahamu kuwa bi Rose si mama yake mzazi ila alimlea tokea akiwa Binti Mdogo na hata baada ya baba yake kuondoka duniani bado alimlea vizuri kama mama yake. Ester hakuwahi kuona tofauti kama angekuwepo mama yake mzazi na bi Rose kwa kuwa alipata malezi mazuri sana ya upendo.

Ester pozi lilimuisha,
"Mamaaaaa ungemuuliza mapema ujue wapi mwenzangu alipo sasa itakuwaje? Kweli kila kitu hutokea kwa Sababu mama.

Huyu mzee alikuwa anakaa sokoni maskini watu Wengi walikuwa wakimpita lakini hansy Ndie alimuonea huruma akamchukua kumbe alikuwa anamleta Karibu yako mama kweli kila kitu Mungu hupanga.... Sasa shida tutaanza vipi kukuambia Hansy kuwa huyu mzee yupo Hospital amefikaje fikaje?"

" Fanya unavyojua Ester lakini huyu mzee ni mtu wa muhimu sana sitaki kumpoteza kwa vyovyotev vile".

" Sawa mama nitajua cha kumuambia Hansy  nitamuambia kuwa alitoka nnje akavamiwa kisha wewe ndo ukamsaidia na wewe akiamka muambie ajibu ivyo ivyo".

" Ni sawa".

Bi Rose alimkumbatia Eater Ndipo walipomaliza waliagana na ester akaondoka zake.

Binti alifika kwenye Gari  lake Ndipo akajisemea,
"Sijui Ndugu Yangu utakuwa uko wapi jamani.
Hakika utakuwa umekuja wakati sahihi sana nipo mpweke sina hata ndugu.
Japo hatujazaliwa Pamoja ila naamini ni ndugu Yangu.
Huyu mzee akipata nafuu akapona atatuambia ulipo tutafuata".
Alijisemea Ester kisha Ndipo akawasha gari na Safari ikaanza kurudi nyumbani.

ilikwenda mpaka jioni Hansy Alirudi nyumbani na kumkuta mkewe akiwa nnje.
Alishuka Kwenye gari wakasalimiana vizuri.
"Mmewangu Kuna kitu hakipo sawa"
"Kitu gani?"
"Ni huyu baba tunaekaa nae hapa huyu mzee".

Hansy kusikia vile tu kwanza alishtuka,

"Wewe imekuwaje yupo wapi?"
"Leo alitoka Asubuhi kuzunguka zunguka gafla sijui ilikuwaje akavamiwa huko nakuja kuitwa hapa amepigwa Vibaya vibaya"

"Haiwezekani.... Nani kamfanyia ivyo? Yupo wapi?"

"Usijali nimempeleka hospital na mama nimemuita ndo amebakia akimuangalia".

" Hospital gani? "

" Mmewangu ungeingia kwanza Ndani ukaoga"

" Usijali nimeumia sana niambie ni wapi niende".

Basi Hansy aliambiwa Hapohapo Alirudi kwenye gari na kuanza Safari Kwenda hiyo hospital.

Kufika alikwenda mpaka katika wodi Ambayo alielekezwa na Ester.

ilikuwa hospital private ivyo kwa muda aliokwenda Hansy aliruhusiwa kwenda tu mpaka wodini.

Basi kufika ile Mlangoni akamsikia Bi Rose akiwa anaongea huku analia. Hansy akasimama kwanza mlango  na kumsikiliza.

"Niambie mwanangu alipo mzota... Ulimchukua akiwa Mdogo sana.
Ukaenda nae mbali sana ambapo sipafahamu.
Nimeishi nikimlea mtoto wa mumewangu hali ya kuwa nami nilibeba mimba Miezi 9 na nikazaa kwa uchungu Kabisa.
Mwanangu sikumfaidi ulimchukua amka uniambie wapi alipo mwanangu".

Hansy alishtuka akahisi labda amekosea wodi lakini alipoingia vizuri alimkuta ni mzee yule ndie kalazwa huku bi rose yupo Pembeni yake.

" Shikamoo mama"... Alisalimia hansy Ndipo mwanamama yule akainuka huku akifuta machozi.
" Marhaba mwanangu sijui niseme nini Hansy kwa kumleta huyu  mzee katika maisha Yangu.
Kweli kila kitu hutokea kwa Sababu njoo nikueleze sio siri tena".
" Sawa lakini anaendeleaje?"
" Amechomwa sindano ya usingizi kwani anatumia drip yenye dawa kali aliumia wamesema ataamka baada ya masaa kadhaa".

Basi walitoka nnje na kusimama pembeni Bi Rose alimsimulia Hansy kila kitu juu ya yeye na Mzee mzota.

Hansy kwanza alitoa leso na kujifuta jasho maana kwa Maelezo yake alishajua Mtoto anaezungumziwa hapo ni Vane lakini alishindwa hata aanzie wapi kusema.

"Sawa nipo mimi hapa unaweza kwenda Nyumbani ukaja kesho Asubuhi mimi nitalala nae hapa".
"Siwezi nataka kujua mwanangu amemlea au laa... nitakaa mpaka aamke niongee nae".

"Sawa naamini mwanao atakuwa yupo mzima na atakuwa Binti mkubwa na mrembo pia".
"Na iwe ivyo Hansy".

Hansy aliongea vile kitu Ambacho anakifahamu kabisa huku nae akiwa haamini amini itakuwaje ameshajua Binti ni Vane lakini haijulikani wapi alipo.

Basi ilikwenda mpaka saa 4 Usiku Ndipo Ester nae alifika Hospital hapo akiwa na chakula.
"Najua mtakuwa hamjala na pia siwezi kulala peke Yangu nyumbani kama hansy nawe utabaki hapa nami nitabaki pia maana hili ni jambo zito kwetu".

"Ni kweli mkewangu kwa jinsi mama alivyonielezea kweli aisee Asante kwa chakula".
Basi Walipokea Ndipo wakaanza kula wote pale.

Baada ya kama dakika 10 wakiwa wanaendelea kula Ndipo alifika muuguzi na kuwaambia,
"Mgonjwa wenu ameamka yupo sawa Kabisa na majeraha yamefungwa mnaweza kuonana nae".
Wote walifurahi Ndipo wakainuka na Kwenda wodini.

Walimkuta kweli Mzee mzota ameshafumbua macho yake.

"Nisamehe sana tafadhali nakuomba niambie mwanangu yupo wapi?".

" Ahhh mwasike asante sana kwa kunizalia Mtoto mzuri Ndie nami nipo hapa mjini kumtafuta mwanangu".

" inamaaama amepotea au? Amepoteaje jamani mwanangu? "
Bi Rose alianza kulia Ndipo mzee mzota akamuambia,

" Wewe unaonekana unapesa tunaweza kutumia picha zake kumtangaza tukampata nimemlea vizuri mwanetu na nilimpa jina anaitwa *VANE*.

Bi Rose na Ester wote walishtuka Ndipo Hansy akaona nae azidi kupigilia msumari wa wawili wale.

"Ni kweli mkewangu Huyu si mzee wa sokoni kama nilovyokuambia huyu ni baba wa mwanamke nilimpenda vane. Baada ya vane kupata matatizo ya macho Alirudi kijijini kwao tukamtibia na mala ya pili tena ametoweka Ndipo nilienda kijijini kwao kumuambia mzee akahutaji nae kuja mjini kumtafuta mwanae ivyo ni baba yake na vane huyu".

Mzee mzota nae akaongezea,

"Huyo Vane ndie yetu mimi  wewe mwasike tusaidiane Hansy ana picha zake tumtafute".

Machozi yalimtika bi Ester kumbukumbu zilimjia jinsi alivyomsulubu mala ya kwanza mpaka macho yakaharibika. Kama Haitoshi kamtengenezea kesi Binti anatumikia kifungo na adhabu yote kwa sababu yake.

Bi ester aliangua kilio hata Ester alibaki kimya mikono kichwani.

"Nisamehe mwanangu nitakutazamaje mamaaaa ahhhhh mwanangu mimi nakufuata usiku huu huu mwanangu utoke jela mamaaaaaa".

Hansy na Mzee mzota na wao walishangaa Ndipo Hansy akainuka na kumsogelea vizuri bi rose.

" Unamaanisha nini? Unamaanisha Vane yupo jela mlimfunga jela au?".

Palepale walisikia kishindo binti  Ester aliangua na kupoteza fahamu kwani nae alichanganyikiwa kwa Mengi kwa ukweli ule kujulikana.....

Sijui itakuwaje?
Tukutane sehemu ya 23*ME&YOU*

SEHEMU YA.... 23
Na

Mamuh mohd
(0716730000)

Tuliposhia.....

Palepale walisikia kishindo binti ester alianguka na kupoteza fahamu kwani nae alichanganyikiwa kwa Mengi kwa ukweli ule kujulikana....

SONGA NAYO......

Hansy aliita wauguzi Haraka na kuja kumpatia huduma ya kwanza bibie ambae alipelekwa katika wodi nyingine kwa uchunguzi Zaidi.

Wakati huo Bi Rose bado alikuwa akilia sana akijutia mengi aliyomfanyia binti yake.
"Kwaiyo unataka kusema kwamba mnafauamu wapi Vane alipo si ndio? Nijibuuuu".
Alifoka Hansy Ndipo mama Estee alieleza kila kitu kuwa amemfunga jela.

Hansy machozi yalimtoka, alitoka nnje na Kwenda kujiinamia pembeni hata Mzee mzota alibaki akimlaumu sana Bi Rose na akimsihi kuwa anamtaka Binti yake haraka sana.

ilikwenda mpaka Asubuhi Ambapo mfalme mzota alipata kutolewa hospital kwa kulazimisha ili akaonane na Binti yake.
Walikuwa watatu Mzee mzota, bi Rose Pamoja na Hansy Ambapo walianza Safari Kwenda kituoni kule ambapo anapatikana mkuu wa kitio aliefanya Mpango huo kuhakikisha Vane anakwenda jela.

Kufika aliweza kuzungumza nae wakiwa nnje Kwenye Gari akamuomba vane aachiwe kwa Gharama yoyote ile.

Kiongozi yule alieitwa Mr macky aliwaeleza kuwa Tayari Vane Yupo magereza na kesi waliitengeneza hukumu imeshatolewa ivyo sio Rahisi tena kama wanavyodhania.

"Naomba msaada wako Mr macky ni Binti Yangu huyo mzazi kabisa nakuomba nipo Tayari kwa gharama yoyote nakuomba"
"Bi Rose ngoja nione kama itawezekana ila sio kwa sasa.
Hapa labda ikitokea msamaha wa Raisi tungeweza  kumpenyeza lakini ivi ivi inaweza nami kuniletea shida kazini...
Tafadhali nipe muda kwanza niangalie Kisha nitakufahamisha".

Kauli ya Mr mack ilikuwa Hiyo hali ambayo ilizidi kuwakata maini wanafamilia hao.

Kufikia jioni alikuwepo bibie Ester hospital kule.
Mshtuko alioupata ulipelekea mpaka akaharibu ujauzito wake.
Alishinda kutwa nzima siku Hiyo hamuoni mama yake wala mtu yoyote yule hospital.

Binti Machozi yalimtoka alijua fika watu wapo bize kumtoa vane jela na sio kwa ajili yake.

"Vane... Adui wa mapenzi Yangu eti ndugu Yangu.... Nimepoteza ujazito Wangu kwa Sababu ya hizi Habari sikubali".

Binti Wakati yupo anajiwazia Ndipo mala alifika nurse wodini humo.

" Pole sana unajisikiaje hali baada ya kusafishwa?"

"Bado nina Maumivu kiasi Fulani... Lakini sikiliza kuna Ndugu Yangu yoyote hapo nnje"

"Hapana nadhani hawajarudi tokea Asubuhi walipoondoka.

Lakini usijali walilipia chakula ivyo tulikuwa tunasubiri upate nguvu tukuletee supu ya moto".

"Hapana sihitaji kula ila kuna kitu nikuulize... Hakuna Ndugu Yangu anaefahamu kuwa ujazito umetoka si ndio?"
"Ndipo bado hawajaambiwa mpaka wakishafika".
Ester alimshika mkono M
Nurse yule,
"Naomba iwe siri hakikisha hakuna anaefahamu kuwa nimeharibu ujazito tafadhali niahidi"
"Kuna vitu ni siri baina ya sisi wauguzi na mgonjwa lakini jambo la ujauzito sio siri ni jambo la uwazi kwanini utake iwe siri"
"Nielewe nitakupa Milioni moja Andikeni mtoto tumboni yupo salama ni mshtuko tu Tafadhali".

" Kweli unanipa hiyo milioni moja na itakuwa siri? "
" Ndio fanya ivyo haraka".
Basi nurse yule alikubali kwa dau hilo aliloambiwa na bibie Ester.
" Nalinda ndoa Yangu lazima nifanye ivi huwenda mimba itasababisha hansy asiniache akikutana na Vane".
Alijisemea binti huyo Ambae nae aliamua kutumia akili Hiyo.

Usiku Kabisa Ndipo bi Rose alirudi hospital na kumkuta Ester akiwa ameshakaa sawa yupo tayari kuruhusiwa.
" Pole mwanangu unaendeleaje hali yako?"

" Sijambo vipi nyie za huko?"
" Mr macky amebadilika kabisa amesema kwa sasa itakuwa hatari kwake kumtoa Vane.
Lakini amesema tumpe muda huwenda akafanikiwa mwanangu".
" Mhhh na atafanikiwa mama lakini sikufichi wasiwasi Wangu ni Hansy nani atakuwa na hansy mama? ".

" Ester wacha kuwaza hayo kwa sasa kubwa ni vane kutoka jela kwa sasa nawaza jinsi mwanangu atakavyotoka jela nimekumbatie naumia mimi ahhhh".
Bi Rose mpaka machozi yalikuwa yakimtoka.

Ester alimtazama mama yake jinsi anavyolia na kujisemea kuwa hapo inaonesha wazi kwamba mama yake ni atampenda Vane kuliko hata yeye.

Wakati huo Hansy Alirudi nyumbani kwao na kuwasimulia wazazi wake kila kitu kilichotokea.
Wote walishangaa haswa mama Hansy,
" Mbona siamini yani Vane mama yake mzazi ni bi Rose ohhhh uwiiiiiii".
Alishangaaa mama hansy huku akiyakumbuka mabaya yote Ambayo bi Rose alikuwa akimuelezea na kupanga nae dhidi ya vane kumbe ni mwanae.

"Wazazi wangu   huo Ndio ukweli mbaya Zaidi tumekatishwa tamaa na juhudi za kutoa vane".
"Ataachiliwa tu sema itakuwa ni mlolongo mrefu si kama mwanzo maana kesi kufuatwa ikiwa mtu ameshaenda magereza huwa sio rahisi".
Alijibu baba Hansy kwa mtazamo wake nae anavyoona hiyo hali iliyotokea.

Siku iliyofuata Asubuhi Ester alikuwa zake nyumbani kwake kule Ndipo mama yake alitoka Pamoja na Hansy wote kuendelea kufuatulia Vane awe huru.

Ester alibaki zake nyumbani Ndipo akasikia mtu akigonga nnje.

Ester alimruhusu aingie huyo anaegonga kwani alikuwa bado hayupo sawa ivyo hakuweza kutoka nnje. Kufika Ndipo akamuona mtu huyo ni Mwasifa.

"Habari yako Ester?"
"Nzuri umekuja kumfuata nani hapa vane au?"
"nilikuwa kijijini kwenda kuwaona wakubwa Wangu lakini nilipata mtihani kuuguliwa na bibi Yangu na akatutoka. Nimerudi jana usiku nikakuta hapa kuna mlinzi tu, nikawasiliana na Hansy akanijibu maswali yote niliyokuwa nataka kuyafahamu.

Leo pia kanipigia simu kuomba nije kukaa na wewe kanielezea hali yako Wakati yeye yupo bize kumpambania mkewe vane awe huru".

Ester kusikia vile alicheka kwa dharau na kumjibu Mwasifa huku amebana pua kama kumkejeli,
" Mkewe vane.... ".
Kisha alicheka tena bibie Ester,
" Hansy angekuwa anamjali sana vane sijui kama hata angekumbuka kuwa nahitaji msaada akakuagiza wewe kijakazi uje kiniangalia kajali kiumbe chake pia".
" Mhhh kama ilivyo hatukatai usemavyo una mimba basi nawe usikatae kuwa hansy anampenda vane.

Alafu kuja kwangu hapa sijaja kama kijakazi nilishatokaga huko nipo hapa kuangalia utu kwanza kwa kuwa ameniomba hansy na anachofanya kina umuhimu sama ndio maana nami nikamkubalia... Sio kijakazi mimi kwa sasa ni mchumba wa mtu nitaolewa hivi Karibuni kwa Mwanaume tunaependana sio kulazimisha".

Alijibu mwasifa kisha akaondoka hapo kwa kuwa Binti anafahamu chumba chake zamani kilichokuwa Ndipo akaelekea hukohuko.

Ester alibaki akiumia maana ni kama Mwasifa kamuumiza kusema kuwa haina kubisha kuwa Hansy anampenda sana vane.
Hapo ndo alizidi kujiambia kuwa vane akipatikana hatokuwa na thamani bola aendelee kwanza kudanganya kuwa ana ujauzito inaweza kusaidia.

Harakati ya kumtooa Vane ziligonga mwamba hali iliyopelekea MR Macky mpaka kuwa mkali.
Alijua kama akilazimisha vane atoke inaweza kujulikana kama mwanzo alikula rushwa kesi ikawageukia wao.

Aliwataka wawe wapole wasubiri pakitangazwa msamaha kwa wafungwa ndipo walau wanaweza kumuweka na Vane kutoka magereza.

Basi waliomba nafasi hata ya kwenda kuonana nae Ndipo walipangiwa siku ya kwenda magereza  kuona wafungwa.

Baada ya heka heka ile ya polisi kufuatilia ikashindikana vane kutoka hansy alimuaga Ester kuwa amesafiri kikazi lakini haikuwa ivyo aliamua tu kukaa mbali na ester maana hakumuoa kwa kumpenda.

***BAADA YA MWEZI MMOJA**

Hatiamae ilifika siku ya kwenda magereza kuona wagonjwa.
Mwanamama bi rose alikwenda nyumbani kwa Hansy kwa ajili ya kuungana na wenzake wengine kwenda magereza.

Binti Ester alitafuta Sababu ya kwamba anaumwa ulimradi tu asiende.
Na hansy pia alikuwa hajarudi safari kama ester alivyojua.

Walipika chakula kizuri pale kwa ajili ya kumpelekea Vane.
Walipomaliza Ndipo walikwenda kujiandaa kwa ajili ya kuanza safari.

Ester alikuwa akiwatazama huku nae akiwa na mpango wake wa kuonekana kuwatazama kwa Makini bi  Rose na Mwasifa waliokuwa wakiandaa.

Muda wa chakula ulipowadia Ndipo waliondoka zao huku Ester akiwaaga na kuwatakia wafike salama.
Ester alipomaliza alirudi ndani na kuanza kucheka.
"Hawajui chakula kile nimeweka sumu wakifika sheria za magereza watataka mtu mmoja wapo aonje chakula kile. Najua hansy Wangu hayupo hajarudi Safari inamaana watakaoonja ni kati ya yule baba vane, mama au mwasifa ambao Sina hasara wakila na wale tuu lolote liwakute.

Kisha Vane mwenyewe sasa kwisha Habari yake.
Alijisemea Binti huyo inamanaa alifanikiwa kumbe kuweka sumu katika chakula kile pasina yoyote kujua.

Baada ya masaa3 Ndipo bi rose akiwa na mzee mzota na mwasifa walifika magereza na kumkuta Hansy kumbe akiwa nnje anawasubiri.

Bi Rose alishangaa kumuona Hansy,
"Jamani nikajua haujarudi safari"
"Heshima yako mama... Ndo nimefika Asubuhi hii aisee siku muhimu leo".

Alijibu Hansy huku akikonyezana kwa chini chini na mwasifa anaefahamu ukweli kuwa hakusafiri.

Waliingia mpaka ndani ilikuwa siku ya wafungwa kutembelewa.

Bibie Vane alikuwa zake gerezani ametulia zake anajua hana wa kuja kumuona alikuwa zake ameegemea ukutani.
Mala alifika askari mmoja wa magereza na kumuita.

"Vane... Vane".
"Abee afande"

"Haya changamka ndugu zako wamekuja twende".

Vane alishangaa nani huyo kama si walewale mahasimu wake.
Binti alitembea huku anatetemeka Ndipo alifika mezani walipo hao watu wake.

Vane alishtuka kuwaona hao watu waliokuja kumuona....

Sijui itakuwaje?
Tukutane sehemu ya 24*ME&YOU*

SEHEMU YA.... 24
Na
Mamuh mohd

(0716730000)

Tuliposhia....

Vane alishangaa nani huyo kama si walewale mahasimu wake.
Binti alitembea huku anatetemeka Ndipo alifuka mezani walipo hao watu wake.

Vane alishtuka kuwaona hao watu waliokuja kumuona....

SONGA NAYO.....

Vane alishangaa kumuona Hansy ambae alishuhudia akifunga ndoa na Ester.

Pia alimuona bi Rose ambae Ndie hasimu wake.
Binti alikumbuka kuwa matatizo yote ambayo yanamtokea basi ni bi Rose huwa Ndie chanzo cha yote.

Vane alijikuta anakosa ujasiri na kutaka kurudi gerezani lakini Ndipo akamuona Tena baba yake pamoja na mwasifa.
Vane machozi yalimtoka Ndipo akamsogelea baba yake na kumkumbatia huku akilia sana,
"Baba Yangu jamani umekuja mpaka huku baba.... Hujui tu jinsi gani nilikuwa nakuwaza baba Yangu nilijua sitakuja kukuona tena baba Yangu ahhhh".
Vane alilia sana Ndipo baba yake akawa anamfuta machozi.

" Mungu ametenda mwanangu kaa nakuomba utulie kwa hiki nachokwenda kukuambia".

" Baba unataka kusemaje baba Yangu? "

Mzee mzota aliomba kusogea pembeni kidogo na Binti yake.

" Vane hansy alikuja kijijini baada ya kukutafuta pasina mafanikio.
Alinieleza hali halisi nami nikafanya vile nijuavyo nikabaini kwamba kuna uwezekano mkubwa upo huku mjini.
Bi mtama alinieleza kuwa nimshawishi hansy afunge ndoa na huyo msichana anaelazimishiwa ili tujue kama wanahusika na upotevu wako.

Hisia zetu hazikuwa mbali hansy amemuoa yule Ester mimi nikiwa hapahapa.
Walitaka kunifanyia kama walivyokufanyia wewe Ndipo nilipoonana na mama Ester nimemtambia kuwa Ndie mwasike.
Mwasike Wangu wa kijijini niliemdhurumu kwa kumchukua Mtoto akiwa bado mchanga sana.
Mtoto mwenyewe ni wewe Vane huyu mwanamama unaemfahamu ambae anaitwa kwa jina la Rose mama yako mzazi".

Vane alishuka nusu Kutaka kuanguka lakini baba yake alikuwa amemshika,

" Baba hapana hapana ni afadhali hivi navyoishi nikiwa simfahamu mama yangu kuliko haya unayoniambia baba hapanaaaa".

" Huo ndipo ukweli Vane mwanangu Huyu nilimfahamu kwa jina la mwasike. Aliniteka nami Ndipo nilikutana nae hakika milima haikutani mwanangu. Ametueleza kila kitu kuwa yeye ndie alieyafanya haya yote na tumepambana sana utoke lakini haijawa Rahisi. Nakuomba mwanangu fungua moyo na umpokee mama yako Tafadhali nakuomba sana mwanangu "

" Baba siwezi baba.. siwezi sitaki hata kumuona muambie aondoke baba... Yeye ndie chanzo cha matatizo yangu yote tokea yale ya kwanza mpaka haya ya sasaivi.
Mama gani asiekuwa na huruma ni kweli hakujua mimi ni mwanae lakini walau anajua uchungu wa mtoto asingenifanyia haya aliyoyafanya mama".
Alilia sana Vane huku baba yake akiwa anambembeleza kwani Mzee mzota alijua namna ya kumtuliza Binti yake.
Yeye ndie aliemlea tokea akiwa Mdogo Ivyo kwa kiasi kikubwa anamfahamu vizuri sana namna ya kumbembeleza akiwa katika hali kama hiyo.

Huku walibakia Hansy nae akiwaza Vane hajamchangamkia kabisa nae alikuwa na mawazo yake Mengi sana.
Ndio Mwasifa akamuambia,
" Usijali huwenda hawa walifanya juu chini vane ajue kama umeoa kwaiyo hatakuwa sawa tuache baba amuelezee naamini ana Sababu yake ya kutaka kwenda kuongea nae pembeni".
" Na iwe Ivyo mwasifa".

Wakati huo mwanamama bi Roe nae akiwa kimya tu huku Machozi yanamtoka.

Walirudi mzee mzota na Binti yake.
Vane Ndipo alimsogelea Hansy na kumkumbatia.

Hata Hansy mwenyewe alifurahi sana ndicho alichokuwa anakitaka.
" Vane pole sana kwa yote mpenzi Wangu, tupo hapa hatutakata tamaa mpaka utatatoka"
" Asante sana na pole kwa unayopitia na wewe.. baba amenielezea kila kitu haukuwa na chaguo lingine tuache muda utaongea" .
" Asante kwa hekma yako Vane. Hakika ni mwanamke unaefunzwa kitu na ukaelewa najivunia wewe Vane... Sitazuia furaha Yangu pale itakapofika siku ambayo utakuwa mama wa wanangu ambao watarithi hekma kutoka kwako".

Vane aliishia kutabasamu tu Kisha akamfuata na Rafiki yake Mwasifa wakakumbatiana wenyewe.
" Pole sana vane siku sio Nyingi yatakwisha yote haya endelea kuwa mvumilivu sawa mama"
" Asante sana  kwa faraja yako Mwasifa upo pamoja na mimi siku zote asante".
Vane alipomtazama sasa bi Rose alikosa hata cha kuzungumza.

Bi rose mwenyewe akamsogelea Binti yake na kumkumbatia,

" Naumia sana mwanangu haujui tu naumia sana nashindwa hata niseme nini Ambacho walau kitafanya unielewe jinsi navyojutia... Tafadhali nisamehe sana mwanangu... Mtoto wangu wa pekee jamani mwanangu kabisa Wa kufanana na mama Yangu ahhhhh sijui shetani gani amenipigia naomba msamaha wako vane Wangu nisamehe mwanangu ".

Vane aliishia kumtazama tu Bi Rose ni vile baba yake amemsihi awe mtulivu basi akaamua kunyamaza zake tu.

Mwasifa Ndipo alitoa chakula kile na Wakati huo alikuwepo askari Ambae anamsimamia vane.

Askari yule akawaambia,
" Chakula hicho mnatakiwa kuonja kwanza mmoja wetu anatakiwa akionje Mbele Yangu kisha Ndipo ale mfungwa ".
Hansy alishika chakula kile yeye ndie alikionja na kisha akamlisha vane.

Wengine wote walifurahi sasa vane alijihisi faraja sio ya Kawaida japo bado hakuwa akizungumza chochote na bi Rose haikuwa rahisi kwake kwa mala moja kusahau Ambayo mwanamama huyo amemfanyia.

Muda ulikwisha Ndipo waliagana kila mmoja alimpa neno Vane la faraja na wote wakimuahudi kuwa bado wanapambana kuhakikisha anatoka jela.
Bi Rose kubwa alimuomba Vane ampokee kama mama yake amsamehe kwa yote yaliyotokea.
Watu wale waliondoka huku hansy Machozi yakimtoka akitamani kuendelea kumtazama vane  wake.
Hata vane alijikuta anaangusha Machozi yenye furaha ndani yake kwa kuwaona wapendwa wake.

Vane Ndipo Alirudi zake  gerezani akiwa na zawadi zake Ambazo atazila Polepole alileteewa.

Alianza kuwaza sasa na yeye kwa namna yake kuwa Bi Rose ni mama yake mzazi na Hapohapo ni mama mlezi kwa Ester.
Aliwaza kwa sasa Ester ni mke wa Hansy na ni mjamzito itakuwaje kuhusu yeye.
Binti alikosa majibu ya haraka haraka cha kufanya ila aliona ni mtihani mkubwa.

Baaada ya kama masaa mawili kuna mfungwa mmoja alikimbia kwenda kwa Polisi,
"Vane ameanguka ameanguka mapovu yanamtoka mdomoni".

Haraka ilibidi waende katika chumba anacholala vane na wenzake Ndipo kweli wakakuta watu wamemzunguka Binti katulia tuli huku alama ya mapovu mdomoni.

Polisi magereza haraka alifanya mawasiliano kuomba ambulance Ambayo inatokea hospital ya jeshi iliyo Karibu na hapo.
Huku na wafungwa wenzake walimbeba kumtoa mpaka eneo la nnje na gari lilipofika walimpandisha Tayari Kwenda kupatiwa Matibabu.

Upande wa Hansy nae alikuwa Kwenye gari lake na mzee mzota kwani waligawana.

Hansy alipanda gari moja na mzee mzota, huku bi Rose akiwa na mwasifa lakini Magari yao yalikuwa yakifuatana.

Hansy gafla alisimamisha Gari akilalaka anahisi maumivu.
Bi Rose nae alikuwa nyuma yao kuona Gari la kina Hansy limesimama nae akapack kwa pembeni kuuliza hali.

Ndilo aliitwa na mzee mzota kuwa pana shida imetokea kwa hansy.

Bi Rose akiwa na Mwasifa walishuka na Kwenda kuangalia hali ya Hansy alikuwa akilalamika Tumbo linamuuma.

Bi Rose alipiga mahesabu walipotoka ni mbali kuliko wanapokwenda wanakaribia kufika mjini.
Alifanya mawasiliano na ambulances ya hospital ile aliyolazwa mzee mzota ndio alikuwa na mawasiliano ya huduma kwa wagonjwa.
Aliomba ambulance na kuwaelekeza mahali wanapotokea ili Wakutane njiani.

Walikubaliana Ivyo Ndipo ikabidi Bi Rose aendeshe gari la hansy huku la kwake akifanya mawasiliano na vijana wake wa kazi wakutane njiani awape funguo waende kulifuata.

Waliendelea na Safari na baada ya dakika 20 tu wlaikutana na ambulance Ndipo Hansy na mzee Mzota wakaingia katika ambulance Hiyo huku wengine wakiwa nyuma nao wanaelekea huko hospital.

**********

ilifika mpaka usiku Ndipo ester alipata taarifa juu ya hansy haraka akawahi hospital.
Alimkuta mama yake huyo bi rose,
"Mama Hansy alikuwa wapi imekuwaje jamani?"
"Hansy tulikuwa nae kule magereza lakini Wakati tunarudi Ndipo akaanza kuumwa.

Tumepata majibu ameshafanyiwa kipimo kuwa amekula sumu sasa sijui kaila wapi".

Ester kusikia vile alishtuka Ndipo alijua sasa yeye ndie chanzo.
Binti Machozi yalianza kumtoka kwani hakujua kama hansy nae atakwenda hospital kule.
" Hapana... Hapana... Hapanaaaa Hansy wangu ahhhhh mmewangu jamani lisikupate baya sikujua kama utaenda naumia mimi ahhhhh".
Alilia Binti alichanganyikiwa sio kawaida.

Upande wa Hospital kule alipo Vane yeye ndo hali ilikuwa Mbaya mpaka alipelekwa katika wodi maalum ICU.

" Amekula chakula chenye sumu kali sana.
Tumejitajidi kuipunguza lakini bado ana hali Mbaya nashauri mumpeleke hospital ya mgenza ni hospital kubwa yenye vifaa vya kitabibu vya kila tatizo na madaktari wa pale Wengi wa india".
Polisi aliepewa habari zile alikubali sasa ulianza utaratibu wa kumuhamisha Vane kutoka ile hospital ya magereza kuelekea hospital kubwa ya mjini kujaribu kupambania maisha yake....

Sijui itakuwaje?
Tukutane sehemu ya 25*ME&YOU*

SEHEMU YA... 25

Na
Mamuh mohd
(0716730000)

Tuliposhia...

Polisi alipewa habari zile alikubali sasa alianza utaratibu wa kumuhamisha vane Kutoka ile hospital ya magereza kuelekea hospital kubwa ya mjini kujaribu kupambania maisha yake...

SONGA NAYO.....

Bi Rose alibaki hospital pale akiwa anaomba juu ya afya ya hansy na pia vane ampokee kama mama yake.

Alifika mzee mzota na kukaa Karibu na Bi Rose.

"Usiwaze sana kila kitu kitakuwa sawa Hansy atapata nafuu japo wasiwasi Wangu mkubwa ni kuhusu Hansy na vane wanapendana sana wewe kama mzazi wa Vane utaamua nini"

"Baba Vane kila kitu kipo wazi kinajionesha kama usemavyo Hansy anampenda sana Vane watabakia wenyewe wataoana na kuishi pamoja kwa sasa nitajali furaha ya Binti Yangu naumia mpaka siku atakayonipokea na kuniita mama hakika nitakuwa na Furaha isiyo na kifani".

" Atakuita tu kwa Sababu huo Ndio ukweli"

" Bado nakulaumu wewe mzota kwanini umchukue binti Yangu na kuondoka nae wewe ndie chanzo cha kila kitu mpaka nimefanya mambo ya ajabu sana ahhh".

" Niliambiwa kuwa nimepoteza uwezo wa kumpa mwanamke ujauzito na baba Yangu alinichagua kuwa mfalme wa himaya yetu sikuwa na jinsi kuwa mtawala bila mtoto ".

" Na mwanangu akalelewa na nani? Ulioa mke mwingine hakumtesa mwanangu huyo mkeo? "

" Sawa nilikuwa na mke lakini Vane nimemlea mwanangu kakuwa katika makuzi mazuri.

Hongera kwako uliekuja ukatajirika".

" Mali Zangu kwa sasa ni za Binti yetu akinipokea kama mama yake samahani Yangu kwake ni kumpa urithi Wangu wote.
Baba yake Ester aliniacha sawa na mali lakini nyingi nimezipata baada ya Kuondoka kwake zote hizo zitakuwa za mwanangu vane ila zile alizoniacha nazo ndizo nitampatia Ester".

Basi punde lilifika ambulances lilionekana kabisa limetokea Magereza kuleta mgonjwa.

Eneo hilo la nnje liliposimamia aliekuwepo mwasifa pamoja na Ester wao walikaa nnje Ndipo wakaliona.

Waliona ameshuka askari ambae mwasifa kumuona alikumbuka walimkuta kule magereza wakati wameenda kumuona Vane.

Kutazama wamemshusha mgonjwa ambae bado alikuwa amevalia mavazi ya wafungwa.

Mwasifa alihisi ishara mbaya Ndipo akakimbia kusogea kuangalia Kwa Karibu.

Aliita kwa Sauti iliyoashiria uchungu, "Vaneeeeeeee".

Sauti ile iliwafikia mpaka bi rose na mzee mzota Ndipo kuinuka Kutoka eneo la nnje wakajue beenkuna nini.

Waliokuwepo mpaka watu wengine Ambao Walifika kushangaa nini kimetokea lakini ilikuwa ngumu kwao kuelewa.

Bi Rose na Mzee mzota pamoja na Ester ndipo walifika kwa Mwasifa na kumkuta analia,
"Vane... Vane vaneeee".
Alikuwa akiita mwasifa huku akinyoosha mkono kule akipopelekwa vane.

Punde Alirudi yule askari na kuwakuta bado wamesimama hawaelewi kwani mwasifa alikuwa akilia tu.

"Jamani afadhali tumekutana  tena mtakuwa chini ya ulinzi chakula mlichokileta kwa vane  kilikuwa na sumu amekula sumu huyu".
Bi rose aliweka mikono kichwani hata mzee mzota.

"Ndio maana na sisi yule tuliekuja nae akaonja chakula pia ndo tumemleta hospital ametolewa sumu basi ni ukweli...ahhhh".
Mzee mzota mpaka machozi yalimtoka maana bado hali ya vane waliambiwa sio nzuri.

Wote sasa Ndipo walitafakari  na kugundua ni chakula kile kilikuwa na sumu lakini swali likawa ni nani alieweka sumu.

Bi Rose alimuita Askari yule pembeni na kumuambia,
"Chakula tulikiandaa sisi nyumbani tukisema tufuate sheria kama usemavyo itatuumiza sisi wote naomba funika hili ionekane labda amekula Kulekule alafu kubwa Zaidi naomba niachie mwanangu huru... Hana kesi mwanangu tafadhali nakuomba"
" Mama sio rahisi hapo lazima nami niongee na wakubwa Wangu ngazi za juu Ambapo itakugharimu Sana "

," Usijali kuhusu pesa zipo milioni 100 kwa ajili ya hii kazi naombeni mwanangu akipona anakie huku fanyeni miwezavyo".

Askari yule alibaki mdomo wazi Kiasi kimetangazwa Milioni miamoja hakika haikuwa Rahisi  kwa kila aliesikia kutamani kupitwa na pesa zile.

Basi siku iliyofuata Asubuhi Hansy alipata kuamka na kuwa walau sawa afadhali.
Aliwakuta wazazi wake wakiwa wamefika hospital hapo.

Pia alikwenda Ester kumuona Hansy, "Pole sana mmewangu kwa yote".

Ester alikuwa akiangalia kwa chini  Chini maana aliona aibu hata kumuangalia Hansy kwa kile alichokifanya.

Mala alifika mwasifa wodini humo na kuwakuta Hansy na Ester.

Mwanasifa akamsogelea Hansy na kumjulia hali.

"Vane yupo katika Hospital hii amelazwa nae pia amekula chakula Chenye sumu kama ulichokula wewe.

Tokea jana mama yake na baba yake wapo Karibu nae".

Hansy alishagaa Kusikia vile hata Ester aliumia sio kawaida.

"Unasemaje mwasifa kweli?"

"Siwezi kukudanganya Hansy pata nguvu ukamtazame Vane yupo katika hali mbaya".
Mwasifa alipohakikisha amefanya alichotaka kufanya kumpa ujumbe Hansy ajue kilichotokea akaondoka zake.

Hansy  alitaka kuinuka lakini Ikamuwia vigumu maana bado Anadrip akajikuta hawezi.
Ester Ndipo akamtuliza,
"Hansy angalia na hali yako kwanza sawa  haya pumzika kwanza kumbuka mkeo hapa nipo".

Hansy hakuwa hata na hamu na ester kwani Alikuwa na shauku ya Kutaka kumuona vane wake.

"Hii Sumu alikusudiwa vane Wangu mimi ambae nilikula nae chakula kile ndio maana yametukuta wote.
Nani lakini anataka kumuangamiza vane?"
Alijiuliza Hansy Ndipo Ester alizidi kuumia akaamua Kutoka zake nnje.

Alifika na kuanza kulia kwamba Mbele yake Hansy anaonesha kabisa kumpenda vane.
Ester alilia na kulia Ndipo anasikia mtu akipiga makofi.

Alimtazama mtu huyo na kumuona ni mama yake bi Rose.

"Safi sana Ujanja wako ulioutumia Nimeujua Ester ni wewe Ndie uliweka sumu wakati tunaandaa chakula si Ndio?"

"Mama kwanini unanishutumu mimi?"

"Nani mwingine? Tulikuwa watatu mimi wewe pamoja na mwasifa.

Ni wazi kwamba Mwasifa hawezi kufanya ivyo ni wewe wivu wa mapenzi umekujaa.

Ester wewe ni Mwanangu na hiyo hali yako ndio Sababu nimeizima hii kesi laa sivyo ungeenda jela kupokea nafasi ya Vane unanijua vizuri.

Lakini pia asante umesababisha vane awe huru hatarudi tena jela nimeshapigiwa simu na mkubwa wa magereza ujumbe Wangu kaupata vane ametoka.
Nataka chuki zote uzitoe vane akipona hansy ndie atachagua akae na nani Mapenzi hayalazimishwi".

Ester alizidi kuumia leo mama yake kamtakia. Kauli za kumuumiza sana. Alikumbuka zamani mwanamama huyo alikuwa akimuahidi kuwa atapambana kuhakikisha Binti yake anakuwa na Furaha lakini safari hii anamuambia kuwa Mapenzi hayalazimishwi hakika ester aliumia sana sana.

Mbaya Zaidi aliumia kuona kumbe bi Rose amemshtukia kuwa ni yeye Ndie ameweka sumu lakini kaamua kumsamehe kwa kosa hilo la kwanza na kumpa onyo kuwa asije kurudia.

Baada ya siku mbili Ndipo Vane alitengamaa hatiame juhudi za kutoa sumu zilikamilika na Binti akawa walau ana nafuu.
Aliwakuta wazazi wake pamoja na hansy pia mwasifa wakiwa Karibu yake. Kila mmoja alimlaki kwa furaha na kubwa Zaidi alipata taarifa kuwa amefanikiwa kutoka kwa maana pesa alizotoa mama yake hazijaenda bule Binti ameachiwa.

Vane alifurahi na kumshukuru kwa dhati bi Rose.
"Usinishukuru bali mimi ndie mkosaji kwako natakiwa kulipia... Naomba niite mama mwanangu walau kwanza nifarijike".
Basi vane alitabasamu tu na kumuita bi Rose kama mama yake kwa maana aliamua kuyasahau yaliyopita na kuangalia kwamba kwa sasa yupo salama.

Bi Rose hakusubiri aliagiza shopping za nguo zikanunuliwe kwa saiz ya Vane. Nyumba ilipambwa vizuri ambapo siku ya vane kuruhusiwa kurudi nyumbani alikuta nyumbani kuna maandalizi si ya kitoto.

Vane alipokelewa na wafanyakazi wa bi rose na kukaa sehemu husika kumkaribisha.

Vane alikuwa ni mtu wa kucheka tu moyo wake ulikuwa safi kabisa.
Lakini vane alipokuwa akimtazama ester aliona kabisa hana furaha anajilazimisha tu lakini alionekana hana Furaha ya kutoka moyoni.

Vane alijua shida ni ipi Ndipo kabla ya watu kutawanyika vane alimfuata Ester na kumshika mkono.
Kisha alimuita na  Hansy na kumshika mkono wa pili yeye akawa katikati.

"Wazazi Wangu, rafiki Yangu, wazazi wa Hansy  na wote mliopo hapa.
Nitakuwa mbinafsi kama nitasema niwe na Hansy kwa kuwa tunapendana pasina kumfikilia huyu kiumbe aliekuwa katika tumbo la ndugu Yangu Ester.
Mama yake Ester Ndie mama Yangu itabaki kuwa ivyo kwaiyo nikuombe Hansy kuanzia leo nione kama shemeji yako nami nitakuheshimu kama shemeji yangu.

Wazazi kutengena Ndio ikawa Sababu hata ya mimi kulelewa na mzazi mmoja sio hali nzuri nataka hii familia haijalishi mmeianzisha kwa bahati Mbaya ila imeshatokea.

Naomba muendelee na ndoa yenu nafanya kwa ajili ya Mtoto alie tumboni kwa Ester".

Vane aliunganisha mkono wa Hansy na Ester.
Watu wote walishagaa si mwasifa mpaka wazazi wote.
Hansy alibali ameduwaa hata Ester hakutegemea kama vane angeweza kutoa uamuzi wa kijasiri kama ule.

Vane alionesha kweli hana ubinafsi na anajali Furaha ya mwingine kwa kuikandamiza Furaha yake.

Hansy alitoa mkono wake kwa Ester na kumshika vane akamfokea.

" Wewe unaongea nini ivi unajisikiliza kweli? Kwaiyo mimi naeonesha mapenzi kwako ni mjinga si Ndio? Ni kweli haunipendi vane sema ukweli wako.....vane nakupenda nakupenda elewa neno nakupenda".

" Nachoongea namaanisha Hansy umeanza kutengeneza familia na  Ester na sasa tumejua sisi ni ndugu lazima niwaache mimi ambae bado sijapiga hatua yoyote kwako tafadhali nielewe Hansy huo Ndio msimamo Wangu".

Vane kumaliza alimtazama mama yake kumpa ishara kuwa anaondoka sehemu ile na Kwenda chumba chochote kujipumzisha.

Mwasifa nae aliona kama utani ikabidi amfuate Vane kumuuliza tena vizuri.

Wakati huo wazazi walikuwa kimya kwa muda kisha Ndipo mama Hansy akamuambia baba vane,
" Hakika umelea upewe maua yako sikutegemea kama Vane atakuwa na hekma kiasi hiki katika hili suala zito".

Hansy ndo alizidi kukerwa akaamua kuondoka zake kabisa nyumbani pale huku akiwa na hasira mpaka macho yamekuwa mekundu.

Lakini Binti vane nae kufika chumbani gorofa ya juu alianza kulia Ndipo Mwasifa nae akafika

" Vane umekurupuka ungeomba ushauri hata Kwangu kuombe msamaha Hansy haraka sana umekosea".
" Hapana mwasifa wacha niumie lakini walee mtoto wao nitapata mwingine nitasahau hata kama sio rahisi naomba niunge mkono katika hili sitaki kumtenganisha baba na mwanae".

Aliongea Vane huku akilia sana Ndipo Mwasifa ilibidi kwanza ambembeleze....

Sijui itakuwaje?
Tukutane sehemu 26*ME&YOU*

SEHEMU YA... 26
Na
Mamuh Mohd
(0716730000)

Tuliposhia......

... Hata kama sio rahisi naomba niunge mkono katika hili sitaki kumtenganisha baba na mwanae".

Aliongea vane huku akilia sana ndipo Mwasifa ilibidi kwanza ambembeleze...

SONGA NAYO.....

" Ni kweli usemacho vane lakini umekuwa uamuzi wa haraka sana sidhani kama umemfikilia Hansy.
Hapa mjini naweza kuwa napafahamu kuliko wewe Vane... Wanaume wengi ni waongo sana.
Kumpata mwenyewe Mapenzi ya dhati kama Hansy aliepambana kwa ajili yako wakati wote ukiwa na matatizo ni Wachache sana.... Sawa Vane lakini bado nafasi unayo ya kubadili hili".

" Siwezi mwasifa naomba niunge mkono rafiki Yangu nakuomba kuwa Upande Wangu".

" Katika hili kwa mala ya kwanza tumepishana  Vane haya nakwenda sasa bai".

Mwasifa aliondoka zake huku akionesha kabisa hajapendezwa na maamuzi yale ya Vane.

Basi ilikwenda mpaka usiku Ndipo bi Rose alikwenda katika chumba ambacho alikuwepo Binti yake Vane. Alimkuta akiwa amejiinamia zake.

"Vane mwanangu Najua hali unayopitia ni makubwa kujua mimi ni mama yako Pamoja na yote niliyokufanyia imekupelekea mpaka  kumuacha mpenzi wako.
Sina la zaidi ya kukushukuru mwanangu kunisamehe nikwambie kwamba nakupenda kuliko kitu Chochote hapa ni kwenu utaishi wewe na baba yako pia.
Pumzika Kisha nitaanza kukupeleka Sehemu mbalimbali za Biashara Zangu utachagua wapi patakupendeza mwanangu".
" Asante mama ujue nilikaa nikawaza nikaona haukufanya kwa makosa ulikuwa ukipambania Furaha ya mwanao.

Sikujua upendo wa mama kama upo vile yupo tayari hata kuharibu kwa mtu ili kulinda Furaha ya mwanae".

" Usiseme ivyo mwanangu naumia hujui tu.

Nilikuwa namuumiza mwanangu dahhh!! Sijui hii dhambi nitafanya nini ili ifutike katika moyo Wangu.

Sema kitu vane nitafanya kwa ajili yako mwanangu".

" Mama yameshapita hayo na sina kinyongo kubwa nipo salama mama kuwa na amani nami nafurahi kujua nina mama nimeishi mkiwa kwa miaka Mingi sana".

Bi Rose alimkumbatia binti yake huyo.

*******

Majira ya Asubuhi Vane akiwa zake chumbani amelala Ndipo aliekwenda kuamshwa na mama yake kwa ajili ya kwenda kuagana na baba yake.
Binti alishangaa ndipo Haraka alikwenda Sebleni na kumkuta baba yake akiwa amevaa tayari.
" Baba shikamoo ".
" Marhaba mwanangu vipi hali yako? "
" Salama... Unakwenda wapi baba? "
" Nakwenda kijijini mala moja nikaweke sawa mambo Yangu nitarudi.
Mama yako amebaki akiwa mjamzito lazima kila kitu kikawe sawa.
Nakuacha na mama yako hapa upo mikono salama".
" Sawa baba nikidhania utakaa kidogo ila naamini utarudi "

" Ndio nitarudi pia upate muda uzungumze na Hansy jana uliongea yale kwa hasira mnatakiwa kuyamaliza nyie wawili".

" Baba nimeshafanya Maamuzi Sitarudi nyuma".

" Sikulaumu wewe chanzo ni mimi malezi mazuri niliyokulea Binti Yangu ndio chanzo mpaka umekuwa na moyo huo.

Nikirudi tutazungumza vizuri ila nachojua mimi Hansy anakupenda sana wewe ndie mke wa maisha yake na wewe yule Ndie mume wa maisha yako".

Vane alibaki kimya kwa hapo alikosa cha kujibu Ndipo baba yake huyo aliondoka akisindikizwa na Bi rose mpaka uwanja wa Ndege.

Asubuhi hiyo Hansy alikwenda nae nyumbani kwa Bi Rose na kukuta Mzee mzota ndo akiwa anaondoka ivyo aliungana na Bi Rose kumsindikiza uwanja wa Ndege.

Vane alikaa zake ndani hakutaka Kabisa kuonana na Hansy aliona njia pekee ya kutimiza kile alichokiamua pia ni Kukaa mbali na Hansy.

Upande wa Mwasifa Siku hiyo akiwa zake Nyumbani kule kwa Ester alikuwa akiandaa chai.

Ester Ndipo alimfuata Mwasifa na kumuuliza,

"Umemuona hansy hapa nyumbani?"

"Afuate nini ukiwa moyo wake upo nyumbani kwa bi Rose"

"Unamaana gani kunijibu ivyo mwasifa... Yani wewe upo kwa ajili ya kunikera si Ndio?"

"Sikukeri Ester Tunaambiana ukweli sawa Vane amekubali je na hansy amekubali pia?".

" Atakubali tu pindi pale atakapomshika kwa mala ya kwanza mtoto wake Kutokea katika tumbo langu ".

" Sawa na iwe ivyo".

Mwasifa aliendelea na shuhuli zake huku Ester sasa akiwa anaumia maama anajua kwa sasa hana ujazito jambo ambalo litakuwa gumu kwa Upande wake.
"Hansy utakuwa Wangu tu na utakuwa Wangu natakiwa kuhakikisha napata ujauzito tena kwa ghramaa yoyote ile".
Alijisemea bibie Ester.

Basi Siku ile Majira ya Usiku Vane alikuwa zake ndani Ndipo Mala alifuatwa na mama yake bi Rose huku akiwa amechanganyikiwa.
Vane alimtazama mama yake huyo,
"Mama kuna shida gani?"
"Kuna kitu hakipo sawa jiandae tunaanza safari usiku huu".

"Mama kuna nini?"
"Fanya ivyo vane".
Bi Rose aliondoka chumbani humo hata Vane alibaki nae kwenye sitofahamu.
kweli walijiandaa na baada ya muda alifika Hansy akiwa na dereva Ndipo walipanda gari hilo  na kuanza safari.
Bi rose alipanda
"Mama sielewi nini kimetokea mbona napata wasiwasi mama tunaenda wapi?".
Bi Rose alikuwa kimya tu Ndipo Hansy akamgeukia Vane maana walikuwa wamekaa wote siti za nyuma.
" Vane kuwa jasiri kwa hiki kilichotokea Baba hatunae tena amefika gafla hali ikabadilika.

Uzuri alikwenda na simu mama alimnunulia kuwasiliana kuwa wamefika salama Na punde akapigiwa simu kuwa hali imebadilika"
"Baba!!! Baba yupi mnaemuongelea hapa?"
"Jikaze vane jikaze nakuomba mpenzi Wangu".
Vane aliangua kilio inamaana kumbe taarifa alizopokea bi Rose ni kwamba Mzee mzota amepoteza maisha.

"Nyamaza Mwanangu MUNGU ana makusudio yake baada tu ya kukutambulisha mama yako na yeye ameenda.

Nilimpigia simu kumuuliza amefika salama  akanijibu Ndio gafla tu usiku huu napigiwa simu na namba yake ile naambiwa amepoteza maisha sielewi Jamani.
Cha kwanza nikampigia simu Hansy kama mwanaume awepo katika jambo hili pole sana mwanangu".
Vane alilia sana Huku hansy alimkumbatia Na kumtuliza.

Walifika Asubuhi Kijijini kule Na kukuta kweli hali halisi mzee mzota amepoteza maisha.
Vane alishindwa kujizuia alianguka na kupoteza fahamu.

Malkia Bi muna kumuona bi Rose akamfuata huku analia,
"Wewe ndo mama vane si ndio? Mmemfanya nini mmewangu amerudi tu gafla na kuumwa mpaka hali ikawa ivi nini kimetokea ahhhh?..mmenunulia simu, nguo kumbe ndo mlikuwa kama mnampa mnamuaga kwanini kwanini".
Alilia sana Mwanamama huyo Ndipo bi Rose nae alipokea huku akilia.

" Hakuna kitu ni Wakati maana gafla tu alitaka kurudi Kijijini kumbe ndo ivi ahhhh".
Yalikuwa ni maumivu kwa kila mtu kwa namna yake kupoteza Maisha mzee mzota mfalme wa himaya hiyo.

Alikuwepo pia mganga mkuu ambae ndo akawa kama msimamizi mkuu kuhakikisha shuhuli zinaenda sawa.

Mala alitoka bi Malika na kumuita mganga mkuu pembeni.
"Umeona Binti yake na mkewake wa kwanza wamekuja vipi kama wakitaka madaraka si tutakuwa tumemuua bule mzee mzota".
"Hapana hawa wataondoka inaonesha fika hawatakaa sasa lazima mimi na wewe ndio tubakie mfalme na malkia na Mtoto wetu ajae"

" Sawa alinikera sana kufika eti ananisimulia Amempata mzazi mwenzake nikajua fika huyu si mwenzangu tena Ndio maana nikakuambia"

" Wala usiwe na wasiwasi hili tumeshalimaliza ila hakikisha simu aliyokuja nayo mzee mzota unaificha nitakuwa naitumia mimi mfalme mtarajiwa".

" Sawa tutatumia wote".

Walimaliza mazungumzo yao hapo na Ndipo tunapata kujua kumbe Mzee mzota kupoteza kwake maisha gafla ni mpango wa mkewe na mganga mkuu.

Kufikia jioni walikamilisha Mipango ya kumuhifadhi mzee mzota na kuacha Maumivu makali kwa bibie Vane.

Baada ya siku ile kupita siku iliyofuata Bi Rose alimtaka Vane na Hansy waondoke zao kwani mazingira kwake yalimuwia vigumu kuendelea kubaki.

Vane aliitisha Mkutano kwa wanakijiji wote na kama mtoto wa mfalme walimuitikia kumsikiliza.

"Yaliyotokea tumekubaliana nayo naomba niombe msamaha kwenu kwa kila mtu ambae baba Yangu alimkosea kwa hali yoyote ile.

Mmeishi kama watumwa msiotakiwa kutoka nnje ya himaya hii.
Kuanzia sasa muwe Huru ya kwenda mtakapo kuishi mtakavyo.
Msiamini tena tamaduni hizi zetu Yupo Mungu kila mmoja awe na imani sasa yupo Mungu wa kumtegemea na sio wafalme.

Nadhani Wengi mlidhani kuwa mimi mtoto wake nitakuwa Kiongozi hapana mimi sitaishi huku tena nawaacha muwe huru na msidanyike tena.
Ndoa za lazima ziishe maisha mapya yaanze".

Watu walifurahi kusikia vile japo Malkia na mganga mkuu wao walichukizwa maana wana Mipango yao ya wao kuwa watalawa.

Vane alimaliza na kuagana na watu kisha hakuwa na hiyana waliondoka zao kama walivyokuja sasa amebakia na mama tu pasina baba.

Walifika mpaka mjini ndipo Vane kufika alipitiliza ndani ila Hansy akamfuata na kumuwahi kumshika mkono.

"Sikumbuki kama kuna kosa nimekufanyia Vane mpaka sasa inakuwa kama chuki"

"Nimeghafirika tu lakini samahani na asante kwa kuwa nami katika kipindi kigumu"
"Ni wajibu wangu Nisikucheleweshe nenda ukapumzike lakini sitadharau neno la mwisho aliloniambia baba yako kuwa Niwe na wewe daima... Kwa heri vane".

Hansy aliondoka zake Ndipo vane akababakia amesimama nae alikumbuka kweli Wakati anaagana na baba yake siku anaondoka alimuambia kauli ya mwisho kuwa.

" Wewe ndie mke wa maisha yake na wewe  yule ndie mume wa maisha yako".

Vane aliamua kuingia zake Ndani nae kwa ajili ya kuoga na kujipumzisha.

Baada ya wiki moja Ndipo Vane alikuwa sawa na kuanza kutembea na mama yake katika Maduka na Biashara zake mbalimbali.
Vane alinunuliwa simu ya gharama na mama yake, gari la kutembelea pamoja na dereva wake kiujumla alionekana sasa Binti kutokea katika familia ya kitajiri.

Katika Harakati hizo Vane alijikuta anajuana na watu Wengi kwani alianza mpaka kusafiri nnje ya nchi na mama yake kujua namna ya kufuata mzigo na mambo mengine.

Basi siku hiyo Vane alikiwa amerudi na mama yake Nchini sasa wakiwa uwanja wa Ndege ndipo bibie vane alisimamishwa na mwanaume mmoja.

"Hellow cute how are you?"
Vane alimtazama kisha akatikisa kichwa tu,
"Mhhh poa".
"Ohhh ok inaonesha unapendelea kiswahili ni mwenyeji wa nchi hii?"
"Ndio kwetu"

"Ok nami ni kwetu pia ila nilikiwa masomoni na ndo Narudi leo kama hutojali naomba namba zako za simu uwe hata mwenyeji Wangu".
Vane aliona sawa akampatia kijana yule namba yake.

"Naitwa Hemed"
"Asante naitwa Vane".
"Karibu".
Kijana yule aliondoka zake.
Vane sasa Ndipo akamtazama mama yake na kumuona akiwa pembeni anamtazama tu.

"Mama jamani kumbe unanitazama?"

"Enhee nakuona mwanangu mambo si mabaya kijana wewe lazima vitu kama ivi vitokee".
"Sawa".
Basi walianza kutoka eneo la nnje kwa ajili ya Kurudi nyumbani.

Walifika kwenye gari Ndipo vane kuangalia simu yake akakuta kuna ujumbe namba ngeni,
"Pole kwa Safari bila shaka mmefika salama...niruhusu nije kukuona nyumbani mie Hansy".
Vane Alishangaa ndipo akamuuliza mama yake,
"Mama kwani umempa hansy namba zangu?"
"Ndio aliniomba nikaona sio vibaya".

"Mhhh sawa".
Vane alinyamaza kimya hakujibu sms ile anajitahidi kujiweka mbali na Hansy.

Sasa walifika mpaka nyumbani Ndipo walimkuta Ester akiwa anawasubiri kwani alifahamu kuwa wanarudi.

Ester alijawa na hasira hakuanza hata na salamu,
"Naona sasa mali za baba Yangu unampatia huyu mwanao si Ndio? Vane unataka kuchukua kila kitu changu sawa vyote chukua sina dhiki mie kubwa ni mumewangu naona ulikuwa nae huko safari unatembea nae si Ndio?".

Bi Rose ikabidi ajibu,

" Ester tafadhali upole wa mwanangu isiwe fimbo ya kumpigia.
Vane ameshamuacha Hansy siku nyingi sana kama unaona mumeo haji nyumbani ni wakati wako wa kutenga siku nzima ukae kwenye kioo ujiangalie una mapungufu gani na sio kuja kumtolea maneno Binti Yangu Ambae huyo mwanaume amekuachia".

Ester alijisikia vibaya anaona sasa bi Rose kambadilikia kwa sasa yupo Upande wa Binti yake Vane.
Kabla hajajibu kitu Ndipo mala mlango Sebleni hapo ulifunguliwa wakasikia hodi na kuingia Hansy.

Ester ndo Alizidi kuumia akaona wasiwasi wake ni ukweli kabisa mpaka machozi yalimtoka.....

Sijui itakuwaje?
Tukutane sehemu ya
27*Me&YOU*27_31

SEHEMU YA.... 27
Na
Mamuh mohd
(0716730000)

Tuliposhia.......

Ester ndo alizidi kuumia akaona wasiwasi wake ni ukweli kabisa mpaka machozi yalimtoka...

SONGA NAYO.....

"Mnaona kila kitu kinajieleza Hansy amekuja hapa kumfuata vane mnaona.... Vane wewe ni mnafki unajifanya umemuacha Hansy lakini nyuma ya mgongo wangu mnaendelea na mahusiano yenu.

Wewe ni Mwanamke utapitia kama haya nayopitia mimi nitakuhesabu kama mtu ulienifanya nilee mtoto asiekuwa na baba na ulaaniwe".

Aliongea hayo Ester Kisha akataka kuondoka lakini Hansy akamzuia.
" Punguza ukali wa maneno unaozungumza kwa mwenzio maana yasije kukurudia wewe ikiwa hayupo ivyo unavyomdhania.... Ester unaweza kuwa mama wa mwanangu ila si mkewangu.
Vane hana hatia yoyote nilaumu mimi niliezama katika upendo dhidi ya Vane.
Elewa nampenda Zaidi ya unavyofikilia usiwahi kudhania kwamba labda nitakuja kuwa na wewe".
Ester aliamua Kuondoka zake Huku akilia kwa Maneno yale aliyopewa.

Vane nae aliamua Kuingia Ndani hakutaka kuzungumza kabisa na hansy.

Vane alifika zake chumbani Ndipo kuangalia simu yake alikuta ujumbe ametumiwa na Kijana yule hemed aliekutana nae uwanja wa Ndege.
Vane aliona achati nae walau apoteze mawazo kwa yale yaliyotokea.

Basi ilipita wiki moja Ndipo siku hiyo majira ya jioni Vane alikwenda Hotelini kukutana na hemed.
Walikuwa wakichat na kufikia hapo kuwa waonane.
Vane kufika alimkuta kijana huyo hemed akiwa ameshafika amependeza kwelikweli.
"Karibu mrembo hongera umependeza sana"

"Asante nawe pia umependeza"
"Asante.... Gari la kifahari sana unalotembelea vane bila shaka wewe ni Mtoto wa matawi ya juu sana nazidi Kupata hamu ya kupambana sana kwa ajili yako"
"Mhhh mbona unaongea sana Hemed"
"Ok sorry Karibu tukae".

Hemed alimuongoza vane mpaka eneo la kwenye Kiti akamsogezea na kukaa.
" Asante kwa kuitikia wito Wangu Vane ni tokea siku ile nakuona pale uwanja wa ndege Nilikuwa nikiikumbuka sura yako"
" Mhh asante sana".

" Karibu.... Leo sitajizuia kuzungumza yale yaliyopo moyoni Mwangu naomba agiza utakacho ambacho kitakufurahisha "

" Sawa".

Vane aliaguza  aletewe juice ya matunga na muhudumu alimletea.

"Hautumiagi bia?"

"Mhh hapana sijawahi situmii"

"Kweli wewe ni aina ya mwanamke niliekuwa namtafuta ni kujiheshimu tu maana huna cha kukufanya usinywe bia.

Ok upo Kwenye mahusiano Vane? "

" Hapana kwa sasa sina"

" ila ulikuwa nae? "

" Ndio"

" Kwanini sasa mliachana? "

" Ahhh ni story ndefu hemed tuyaache".
" Ninao muda wa kutosha vane unaweza kunisimulia".
" Hemed acha tu kuhusu hilo"
" Ok sawa samahani nilitaka kufahamu maana nami nahitaji nafasi kwako basi walau nikiipata nisije kufanya kosa kama alilofanya mwenzangu aliotangulia kwa mrembo kama wewe.

Nipatie mimi hiyo nafasi nakauhidi tutaingia kwenye ndoa.
Nimetoka masomoni  huko nilikutana na wanawake wa kila aina lakini Wengi ni waongo hawana vigezo kama Ambavyo nahitaji tafadhali nipatie nafasi Vane".

Binti vane alinyamaza kimya na baada ya muda aliomba apewe muda wa kufikilia kwanza kwa kina kisha atampa jibu Hemed.

Siku hiyo Hansy alikuwa zake nyumbani kwao Ndipo aliitwa na wazazi wake.
"Hansy kiukweli umepoteza kabisa Muelekeo wako... Haijulikani unaishi wapi kwanini lakini?.
Vane amefanya uungwana kukupa Nafasi uwe na ester mjiandae kupokea Mtoto wenu lakini imekuwa haisaidii kitu nyumbani umehama kwanini lakini".
" Mama ni kweli nimepata nyumba ya ofisi naishi huko na Ester nimempangia ataishi pale na kupata mahitaji yote shida nini"

" Shida ni wewe nyumba hata kwao ameiacha lakini amefuata ndoa wewe ni mumewake"

" Hapana sipo Tayari kuishi na Ester kama mkewangu hilo halitatokea kabisa vane kama amenikataa basi Maisha wacha yaendelee tutajuaga huko Mbele ila sio kwa sasa".

" Ahhhh mwanangu unatuweka wazazi wako katika Wakati mgumu sana.

Hujui maneno yanayozungumzwa hapa mtaani".

Hansy aliinuka na kuwaambia wazazi wake,

" Baba, mama nimeshamaliza hilo hayo maneno waambieni waje waniambie mimi na sio Nyingi.

Niliempenda ni vane amenikataa basi wacha maisha yaendelee huwenda huko Mbele nitampata mbadala wake ila sio Ester.
Muwe na usiku mwema".
Hansy aliamua kuondoka zake bado hajabadili maamuzi yake Kabisa.

Basi siku iliyofuata Mwasifa alikwenda nyumbani kule kwa Bi Rose kuonana na Na Vane.
" Nimekumiss rafiki Yangu hauji mpaka nikupigie simu kukuita"

" Acha tu Vane nachoshwa na huyo mama kijacho mala anataka hiki nikipika mala amegairi yani ananipa shida ila namuhurumia mie siku si Nyingi naolewa atakaa na msichana wa kazi sasa".

" Mhhh... Sawa kila la kheri mama nami nina jambo Langu nimekuita "

" Mhhh jambo gani?".

Vane alishika simu yake na kumuonesha Mwasifa picha ya Hemed.

"unamuonaje huyu?"

" Mhhh kwa muonekano hana shida kwani vipi? "

" Huyu mkaka nimekutana nae mda kidogo na ananipenda nahitaji kuingia katika mahusiano mapya".

" Na vipi kuhusu hansy inamaana unamaanisha vane? "

" Mwasifa nampenda sana Hansy na hatakuja kutokea Mwanaume nikampenda kuzidi yeye lakini ni mume na baba wa mtu hivi Karibuni.

Sitaweza kuvumilia eti kesho na keshokutwa Ester anajifungua wapo pamoja.

Nahitaji kijitoa mapema nisiwe mbinafsi, hili ndilo linanisukuma kumpokea huyu kijana walau apooze moyo Wangu nimsahau hansy na hii naamini itakuwa njia sahihi kwa hansy kuniacha mimi alijua tayari nipo Kwenye mahusiano na mtu mwingine".

" Vane ogopa kuingia Katika mahusiano mtu humfahamu vizuri yote kisa kwa ajili ya mtu fulani Hapana.
Vane ni mapema sana kufanya maamuzi Rafiki Yangu wanaume wa mjini huwajui vizuri bahati ulimpata Hansy mwanaume mwema.

Sasaivi mtu akipata mwenza alie mwema hamuachi kiurahisi ni wakumshikilia vane".
" Kwaiyo unamaanisha nini Ester ni kama ndugu Yangu tuchangie mwanaume aliempa ujauzito na mimi nikae Hapohapo si ndo unachokitaka mwasifa?".

" Basi usije ukachukia sitaki nikukere vane ila tu naomba uwe muangalifu sawa?"
"Sawa basi siku nikienda kukutana nae twende ukamtazame vizuri sawa?"
" Hilo halina shida"
" ... Enheee na wewe unaanza kukaa ndani lini kwa ajili ya harusi? "
" Wiki chache zimabakia vane naingia katika ndoa na baraka".
" Nafikilia zawadi kwa ajilu yako jamani lakini siipati njoo nikukumbatie buana bi harusi Wangu ".
Walifurahi wenyewe Ndipo wakakumbatiana kwa furaha.

*****

Siku hiyo alikuwepo Kijana Hemed nyumbani.
Hemed alikuwa akiishi na rafiki yake mmoja alieitwa Kenny.
Wawili hao walikuwa Sebleni wakinywa vinywaji mbalimbali Ndipo Kenny akamuambia Hemed.
"Kwaiyo umerudi na kasi mpya kazi itaendelea maana tilidorora sana".
"Ahhh wee acha tu Wakati wote niliokuwa kwenye Matibabu nilikuwa na shauku nipone na kurudi nchini kwetu. Usijali broo nitahakikisha narudisha kila tulichopoteza tutafanya kazi kama huruma na kila atakaeyakanyaga ugonjwa atauvaa".
"Nakukubali broo kubwa zingatia dawa Ukimwi ni ugonjwa tu wa kawaida".

"Naelewa naelewa sasa basi kufika tu nimemnyaka Mtoto mmoja safi wa kishua namuona kabisa ataingia katika mstari nitahakikisha Narudisha gharama Zangu zote alizonisababishia yule mwanamke mjinga na ugonjwa huu nitautua kwake ahangaike nao huko... Nina hasira sana na wanawake".

" ivyo ivyo kakaaa kama ana mapene basi zichote kama vipi zitusaidie maana huu ujambazi tutakuja kuangukia pua bola tuwe matapeli tu wakutumia akili"

" Kenny wee subirini  huyu mtoto kwao wana  maokoto maana hiyo range aliyokuja nayo acha kabisa".

" Wacha weee"

" Utakuja  umuone siku nikienda kukutana nae tena lakini nataka iigize kabisa kama sisi ni ndugu ambao tupo wenyewe hatuna Wazazi yani atuamini kabisa"
" Ahhh kwa hilo mbona unanijua".
Waligonganisha mikono yao na kufurahi.

Hapo Ndipo tunapata kujua kumbe huyo Hemed sio mtu mzuri ana Mipango yake kutaka kutapeli kwa kumuoana vane kama ni Binti kutokea familia ya kitajiri.
Katika maisha yake inaonesha alikumbana na janga Ambalo bado hajalielezea likampelekea kupata ugonjwa wa ukimwi na sasa yupo kimaslahi Zaidi.

Je atafanikiwa kumuingiza Vane kwenye mtego wake?? .

Basi siku hiyo Majira ya jioni mwasifa alijiandaa kwa ajili ya kutoka.
Alisimama nnje kana kwamba kuna mtu alikuwa akimsubiri Ndipo punde alifika Hansy.

"Mwasifa uko mzima?"
"Mimi mzima tu samahani nimekusumbua"
"Bila samahani unaonekana una mtoko au ndo unarudi?"
"Ndo nataka Kwenda mahali lakini nipo Upande wako siku zote.

Vane ameamua kuendelea na maisha yake na hapa natoka nae naenda kumuona Mwanaume mpya alieamua kumchagua badala yako nikaona si vibaya kukuambia".

Hansy alishtuka kusikia vile,
" Unasemaje?inamaana  vane anamaanisha hanitaki tena si Ndio? Kwanini lakini anasahau yote niliyopitia kwa ajili yake".
" Vane amenitamkia kuwa anakupenda sana ila anafanya haya hana jinsi ili awe mbali na wewe mlee mtoto na ester. Hata mimi nimeumia sana sitaki hili litokee tufanye kitu Hansy".

" Siwezi kukubali niambie mnakwenda wapi sehemu gani nitafika achague mbele yetu wawili Ndipo nitaamini kweli".

" Hansy hiyo itakuwa vurugu sasa naogopa".

" Mwasifa tafadhali haujawahi kuniangusha siku zote nakuomba na hili nambie Vane ni Wangu baba yake ametupa Baraka zote amenisihi kuwa nisimuache mimi ndie mwanaume sahihi kwake".

" Ok fanya ivi tutawasiliana hapa nakwenda kumfuata vane kwao tulifika huko nitakujulisha ni wapi".

" Usichelewe hata sekunde moja wewe ni mtu wa muhimu sana Kwangu kwa hiki ulichokifanya".

" Sawa lakini ingia ndani walau ukamjulie hali Ester".
Hansy hakujibu kitu maana alishachanganyikiwa Alirudi zake kupanda kwenye gari lake na kuondoka.

Wakati huo bibie Vane alimaliza kujiandaa alivaa akapendeza ilikuwa siku ya mtoko anakwenda kuonana na kijana Hemed.
Kumaliza alimsubiri Mwasifa mpaka alipofika Ndipo walipanda wote kwenye Gari na kuanza safari Kwenda huko waendapo.....

Sijui itakuwaje?
Tukutane sehemu ya 28*ME& YOU*

SEHEMU YA.... 28
Na
Mamuh mohd
(0716730000)

Tuliposhia....

Kumaliza alimsubiri Mwasifa mpaka alipofika Ndipo walipanda wote kwenye Gari na kuanza safari Kwenda huko waendapo.....

SONGA NAYO.....

Wakiwa njiani mwasifa alikumbuka kuwa walikubaliana na Hansy kwamba ampe taarifa ya kila kinachoendelea lakini Binti aliamua kuzima simu.

"Utanisamehe sana Hansy lakini Vane atajua hii ni njama na atanichukia sanasana.
Sitamani iwe ivyo hata utanisamehe sana".
Alijisemea mwasifa inamaana aliona hakuna tena haja ya kumuambia Hansy kitu chochote aliamua kumnyamaza zake kimya.

Walifika mpaka huko hotelini Ndipo waliwakuta  hemed akiwa na kenny wamevaa wamependeza kwelikweli.
Wote kuwaona wawili hao walisimama na kuwapokea.
"Umefanya la maana sana kuja na mwenzako na mie nipo na mwanzangu kampani itakuwa ya kutosha".

"Ni rafiki yangu anaitwa mwasifa ila unaweza kumuita sifa"
" Nashukuru kumfahamu".
" Mhhh Mwasifa kutana na Hemed huyu ni rafiki yangu niliekwambia".
Mwasifa alisalimiana tena kwa mala Nyingine na Hemed kisha ndipo walikaa chini na kuagiza kwanza chakula na vinywaji.

Walikula huku wakizungumza mawili matatu na baadae Mwasifa na Kenny walisogea kukaa pembeni na kuwaacha vane na Hemed.

Kenny alionesha kutaka ukaribu wa kumfahamu Mwasifa, lakini Binti hakutaka mazoea sana alikuwa akimkatisha katisha.

Wakati huo vane alikuwa akizungumza na Hemed Ambapo alimpatia jibu kuwa amekubali  ombi lake.
"Kwa muonekano wa kawaida nimekubali naona hauna shida yoyote lakini tutaendelea kuchunguzana kwanza kidogo kidogo"
" Vane kuhusu hilo wala halina shida mama ni wewe tu naamini utajiridhisha kwamba haujakosea.
Japo mimi mkiwa Sina wazazi Zaidi ya huyu Mdogo Wangu tuliachwa tukiwa hivi wawili tunapambana wenyewe.

Nilibahatika Kupata scholarship ndo nikaenda kusoma nnje na sasa nimerudi napambana".

" Ahh poleni sana"

" Asante... Na wewe je Wazazi wako hawajambo?"

" Kwa sasa nina mzazi mmoja tu nae ni mama baba hayupo tena ulimwenguni"

" Pole poa kipenzi changu"

" Asante".

Basi waliendelea kuzungumza maneno kadhaa Ndipo walifika mahali Hemed akaanza kumshawishi vane waende chumbani kupumzika.

" Ni mapema sana hemed tutafikia huko".

" Vane nami ni binadamu nina hisia ulivyo mrembo naumia kukuacha walau kwa leo tuzindue upendo wetu".
" Mhhh... Ahhh unajua..."
" No sina nachojua vane Wangu plzzz naomba usingizi mnono wa leo tuweke alama ambayo itadumu katika mahuasino yetu.

Vane alinyamaza kimya kwa muda huku akijisemea ndani ya moyo wake,
"Kama nikilala na Mwanaume mwingine nadhani Ndipo nitakuwa nimeyavua rasmi mapenzi Yangu kwa Hansy.
Nataka iwe ivyo utanisamehe Hansy lakini nimeamua ubakie na familia yako.
Nitafanya ivi kwa ajili ya kulivunja penzi letu".

Gafla vane machozi yalianza kumtoka Ndipo Hemed akamfuta kwa kitambaa chake.

"Nyamaza plzzz twende chumbani utaniambia nini kinakuliza mumy sawa".

Vane aliinuka na kumuita mwasifa pembeni.

"Nawezakuchelewesha natoka kidogo nimeamua kwenda kuvunja kabisa penzi la hansy Kwangu ni maamuzi ambayo yananiumiza mwasifa".

" Sasa kama yanakuumiA kwanini Vane? Mapema sana... Nipo na baraka tunakaribia kufunga ndoa lakini hatujawahi kulala pamoja.

Ulikaa na hansy Mda gani alishawahi kuweka matamanio ya haraka juu yako kukulazisha? Bado tu haujajua kutofautisha kati ya mwanaume na Mwanaume sahihi?"
Vane wanaume wa mjini Wengi ni waongo wanatamani tafadhali acha twende nyumbani".

"Siwezi Mwasifa tafadhali nauli hii chukua Kodi usafiri na Urudi nyumbani".
Vane aliamua kuondoka na Hemed Ambapo moja kwa moja walielekea jengo la Ndani na kuchukua chumba.

Mwasifa hakuwa na jinsi aliamua kuondoka zake na kumuacha yule kenny akiwa anamtazama tu.

Vane alifika chumbani huku mwili ukiwa unatetemeka Ndipo Hemed kwanza alimbeba,
"Wewe ni mwanamke  mrembo sana Vane hakuna mwanaume anaetoboa kwako hakuna hakika nitakutunza kama mboni ya jicho Langu".
" Asante sana Hemed".
Hemed alianza kumbusu Vane na kumlaza kitandani.

Basi Hapohapo mala gafla Simu ya vane iliita.
Binti aliinuka na kutazama akakuta ni namba ngeni.
" Haloo"

" Haloo dada vane  njoo nyumbani mama hali yake ni Mbaya tunampeleka hospital "

" Unasemaje? imekuwaje nakuja nakuja".

Vane Ndipo kukata simu haraka akaanza kuvaa viatu,

" Mpenzi nini shida? "

" Hemed mama Yangu mwenzio hali yake sio nzuri wacha niwahi"

" Lakini tumalize hili haraka vane? "

" Nielewe Hemed mama yangu hayupo sawa naanzaje? ".

Vane aliamua kuondoka zake na kuwahi mpaka nnje Kwenye gari lake na kuondoka.

Hemed alitoka nae mpaka eneo la nnje alipo mwenzake yule kenny,

" Vipi mbona shem ametoka Haraka hata kuaga hajaniaga? "

" Kapigiwa simu mama yake anaumwa eti kanichomoka Alafu sikuwa sawa kabisaaa hapa nitafute msichana wa bei cheeee nimmalizie hasira".

" Sawa na wewe siku ingine mshawishi azime simu ahhh".

" Yani sema sio mbaya anaonekana sio mgumu kabisa sio kama walivyo watoto wa kishua Wengi hapa mseleleko".

" Acha basi".

Walicheka hapo na kuagiza bia zao wakaanza kunywa.

Vane alifika mpaka nyumbani kwao na Kuingia Ndani.
Kufika alishangaa kumkuta mama yake amekaa Sebleni akiangalia Tv.
" Mama... Mama unaendeleaje mama Yangu?"
" Nikuulize wewe mwanangu za huko? "
" Jamani mama nimepigiwa simu sijui hata na nani kaniambia eti unaumwa hapa unapelekwa hospital nimeshtuka sana"
" Hapana mbona mimi nipo sawa nani huyo amefanya hivyo ebu hiyo namba iliyokupigia".
Vane Ndipo akatoa simu lakini mala akafika msichana wa kazi wa ndani humo kwa bi Rose alieitwa Lucy na kujibu,

" Ni mimi ndie nimekupigia simu dada nisamehe sana?".
Bi Rose alishangaa,
"Lucy wewe ndo umempigia simu umemuambia naumwa kwanini sasa umemmdanganya mwanangu?"
"Nilitumwa Kufanya ivyo halikuwa dhumuni Langu".
Bi Rose na Vane walishangaa na wote wakauliza kwa Pamoja,
"Ulitumwa na nani?"

Kabla Lucy hajajibu Ndipo alifika Mwasifa kumbe alikuwepo amekaa jikoni pasina bi Rose kujua,
"Ni mimi ndo nimemtua mama sikuwa na chaguo jingine.

Nilimtafuta Ester kwa njia ya simu nikamuona namba ya mdada wa kazi yoyote wa hapa nina shida nae na alinipatia ya huyu ndo nikampigia nikiwa bado njiani sijafika hapa.
Yote nilikuwa nakaribu kumfanya Vane Arudi nyumbani sehemu niliyomuacha nahisi sio sahihi.

Nisameheni wote nakwenda lakini nakuambia vane na Sitarudia tena kukuambia Mwanaume sahihi kwako atabaki kuwa Hansy... Hawa wanaume wa mjini unaowaona ni wahuni tu Wengi wanatamani.
Huwenda nikawa nakuzidi kukaa mjini kuwafahamu wanaume.

Nimefanya kazi miaka 5 na chanzo cha kuwa msichana wa kazi za ndani nilitoroka kwetu na kuja mjini nikiwa na mpenzi Wangu.
Kufika alienifanyia makubwana kunitelekeza Ndio Sababu nikaishia kuwa nafanya kazi za ndani.
Najua kuwa wanaume wa mjini si wote wana tabia Mbaya lakini wanahitaji uchunguzi jipe muda uwajue vizuri usikurupuke.... Narudia tena mnisamehe nilipoteleza".
Aliongea hayo kwa uchungu Mwasifa kisha aliamua kuondoka zake.

Vane alibaki ameduwaa hajawahi kumuona mwasifa akimtolea Maneno kwa namna ile .. Ndipo mama yake akamtaka akae chini wazungumze amsilimue kwani ilikuwaje mpaka wakafika pale na mwasifa.

Vane ilibidi amueleze Mama yake kila kitu kwamba alibakia na Hemed.
"Vane mwanangu mwasifa yupo sahihi nitakutafutia elimu mbadala kuna watu watakuelekeza ila kweli mjini umakini usipende kuamini vitu kiurahisi sawa... Anaweza kuwa mzuri au mbaya yote yanawezekana inahitaji uchunguzi".

"Mama ni kweli lakini mwasifa namjua anafanya haya ili niwe na hansy kitu ambacho hakiwezekani tena hansy amempa ujauzito ndugu Yangu naanzaje".
"Nakuelewa mwanangu basi".
Bi Rose Ndipo ikabidi amkumbatie Binti yake kumfariji kwanza katika hilo.

Upande wa hotelini  eneo la nnje aliekuwepo Hansy akiwa ameagiza bia za kujaa meza nzima kuanza kunywa.
"Hatakuwa maisha Yangu haya lakini ni wewe Vane ndo umeyataka sasa niwe mtu wa kulewa mpaka nalewa tena.

Mwasifa nae kanidanganya hajaniambia chochote amekuunga mkono basi kuanzia leo siamini hata mashemeji bola ninywe pombe tu".
Alijisemea hansy huku akianza kunywa chupa moja moja.
Mala gafla aliesikia sauti ya kelele kutokea eneo la nyuma alipokuwa amekaa.
Hansy kwanza alinyamaza lakini akaona kelele zimezidi Ndipo akainuka kwenda kuangalia shida nini.

Kufika alikuta ni Mwanamke mmoja akiwa anasukumana na mwanaume akudai ela yake.
"Utanilipa nasema utanilipa elfu 20 Zangu weee mkaka nipe ela Zangu".

Mwanaume huyo aliekuwa anadaiwa alionekana kuwa amelewa na hakuwa mwingine bali ni Hemed lakini kwa hansy alikuwa mgeni machoni mwake.

" Sikulipi ela sina fanya chochote".
Basi waliendelea kusukumana pale huku hansy akiwa anawatazama Mwisho akaamua kuondoka kabisa na bia zake akaziacha mezani.
Aliona sehemu ile sasa sio ya hadhi yake kabisa yeye si mtu wa kulewa namna ile basi akapanda zake kwenye gari na kuondoka zake.

Mwasifa Alirudi zake Nyumbani kule kwa Ester  basi akiwa analipia usafiri aliokodi Ndipo kuna Mwanaume alimuona akitoka nyumbani kule kwa Ester na kuingia Kwenye gari lake Kisha akaondoka.

Mwasifa alishagaa aliposhuka kwenye usafiri aliokuwepo akawa anajisemea,
"Huyu ni Erick kama sikosei sasa amefuata nini usiku huu hapa? Au Ester ana hali Mbaya?"
Alijiuliza Binti Ndipo ikabidi haraka aingie ndani.

Alikwenda mpaka mlangoni katika chumba cha Ester akamuita,
"Dada Ester upo mzima?"

"Ahhh  mwasifa umerudi nilijua hauji leo ulivyonipigia simu kusema Kuna dharura nikajua hauji"

"Hapana nimerudi na kupishana na Erick alikuwepo humu"

"Ndio nilimpigia simu maana nilizidiwa gafla ila sasa nipo sawa nimelala sasa".

"Sawa basi pumzika na ukihisi hali tofauti utanipigia simu nipo chumbani".

" Sawa".

Mwasifa alikwenda nae Chumbani kwake lakini bado alikuwa akijiuliza Erick kweli alikuja kumjuli hali Ester alizidiwa au vipi???.

Wakati huo Erick nae alikiwa kwenye Gari lake Akirudi nyumbani huku akiwa kama mtu Ambae hayupo sawa Kabisa.

Erick mpaka machozi yalimtoka,
"Ester kwanini umenifanyia ivi? Jamii itatuchukuliaje ahhhhh sielewi sielewi".
Alijisemea nae Erick ni wazi kuna kitu kimetokea hakipo sawa....

Sijui itakuwaje?
Tukutane sehemu ya 29*ME&YOU*

SEHEMU YA.... 29
Na
Mamuh mohd
(0716730000)

Tuliposhia.....

Erick mpaka Machozi yalimtoka,

"Ester kwanini umenifanyia ivi? Jamii itatuchukuliaje ahhhh sielewi sielewi".

Alijisemea Nae Erick ni wazi kuna kimetokea hakipo sawa...

SONGA NAYO....

Bibie Ester nae alibaki kitandani akiwa amekaa usingizi uligoma kabisa.
Alionekana nae kujutia kabisa,
"Ndo nini sasa? Nimefanya nini mimi ahhhh? Erick nitamtazamaje kuanzia sasa uwiiiiiiii nimeharibu kila kitu".
Alijilaumu Ester huku akishika kichwa kuonesha anajutia Ndipo akakumbuka ilivyokuwa ni kwamba.

Ester usiku huo alimuita Erick akiwa na nia ya kumuomba azungumze na kaka yake juu ya kutokurudi kukaa Pamoja nae.
Erick alifika akiwa anatokea matembezi na rafiki yake amekunywa bia mbili tatu zilikuwa zikiingia na kutoka.

Sasa Wakati wakiendelea na mazungumzo Ndipo Ester lilimjia wazo la harakaharaka kuwa anajijua hana ujauzito na niia ya kumuweka walau Karibu na Hansy ni yeye kubeba ujauzito kujifungua.
Aliona Hapana Ana kila Sababu ya kutafuta ujauzito kwa nguvu.

Ester alianza gafla  kumtega shemeji yake mala akipandisha nguo juu kumuonesha maeneo mbalimbali ambayo ni nyeti kwa mwanamke.
Mwishowe alimsogele Karibu kuonesha nini anahitaji.
Erick nae kwa hali aliyokuwa nayo akajikuta akili inahama kabisa na hisia kuchukua nafasi yake wote wakajikuta wamekutana kimwili hata Erick alishindwa kujizuia kwa majaribu yale ya Ester.
Walipomaliza Ndipo kuangalia pale palikuwa ni Sebleni hakuna walichokizungumza Erick aliondoka hata Ester kwa aibu alikimbia chumbani.

"Hapana Hapana nimeharibu nimefanya maamuzi ya haraka sana.
Ni kweli leo ilikuwa siku ya kubeba ujauzito lakini sikafuata ushauri wa daftari kuwa nipumzike kwanza nimefuata hisia Zangu najuta mimi ester".
Alijilaumu mrembo huyo alilia kupita kiasi.

Basi Siku iliyofuata Asubuhi Vane alikuwa zake katika duka moja wapo la mama yake linaliuza nguo zawatoto na vifaa vya watoto kwa ujumla.
Lilikuwa ni duka kubwa lililovutia wateja wengi.

Mala alifika kijana Hemed dukani hapo kwani alikuwa akiwasiliana na vane kwenye simu akimuelekeza sehemu hiyo.

"Hongera duka lenu zuri sana tena lipo classic"
"Asante pole sana kwa kilichotokea jana"
"Usijali vipi lakini hali ya mama?".
Vane aliona asimuambie ukweli hemed kuwa alikuwa akimdanganya ivyo akazuga tu.

"Nashukuru alikaa sawa baada ya muda"
"Ohhh utu uzima tena wazazi wetu"
"Yah.. Karibu ukae nakuagizia Kinywaji"

"Ok Asante"
Hemed alibaki amekaa na vane akatoka katika Restaurant iliyokuwa eneo la Karibu na pale dukani kuagiza juice na bite kwa ajili ya Hemed.

Kweli binti Alirudi akiwa na vitu hivyo akampatia Hemed nakumkaribisha.
"Asante sana japo natamani tutoke kidogo Nina hamu na wewe Vane naona kama bado hatujawa wapenzi"
"Usijali leo tutatoka nipo kwa ajili yako"
"Kweli?"
"Ndio".
Walicheka wenyewe Ndipo alifika Hansy nae dukani hapo.

Hansy aliwakuta vane akiwa amekaa na hemed kwa ukaribu Zaidi.
Hansy alimtazama vizuri mwanaume yule alikumbuka kuwa ni jana tu ametoka kumuona eneo la bar akiwa anagombana na mwanamke Ambae amejiuza kwake hajampatia malipo yake.

"Vane huyu ni nani?"
Aliuliza Hansy kwa hasira Ndipo kabla Vane hajajibu hemed aliinuka,
"Broo vipi mbona unamuuliza ivyo kwani wewe nani?"
"Mimi ni mume wa Vane and you?".
"Vane hana mume na mimi ndie mpenzi wake na mume mtarajiwa".

Vane alibaki kimya alijikuta anakosa kabisa ujasiri wa kumjibu hansy chochote Ndipo akamuambia hemed, "Tafadhali naomba uondoke nitakutafuta".
"Kisa huyu? Unamuogopa? Kweli ni mmewako si ulisema haujaolewa?"
"Ni story ndefu nitakueleza ila kwa sasa naomba uende hemed".
Basi Hemed hakuwa na jinsi aliondoka Ndipo sasa Vane akamgeukia Hansy.

"Unataka nini katika maisha Yangu hansy? Niseme mala ngapi kuwa baki na Ester ndoa Yangu mimi na wewe tulifunga kijijini alietufungisha ni baba Yangu ambae kwa sasa hayupo kwaiyo na ndoa imeishia hapo.

Anatarajia kujifungua Ester lazima utakuwa nae Karibu mimi nitabaki naumia si Ndio? Natafuta amani Yangu sasa naomba usinifuatilie hansy".

Hansy alimtazama Vane machoni na kumuambia,

" Naomba usipepese macho nijibu ukiwa unanitazama ni kweli haunipendi tena?"

" Hansy maswali gani hayo nikuchukie kwa sababu ipo labda?"

" Ok nikurahishie swali unanipenda? Kama mpenzi wako au unamaanisha haya Maamuzi yako? "

" Hansy acha ni dukani hapa ondoka tafadhali ".

" Najua unanipenda nami nakupenda sana na siwezi kukuacha upitie mikono kwa watu wabaya.

Kwanza huyu mwanaume hafai hata kukusogelea na iwe mwanzo na mwisho nimemshuhudia kwa macho Yangu ananunua wanawake anashindwa kuwalipa wa nini sasa? Sihitisha haya mambo yako".

" Siwezi hansy siwezi tena nimeamua na msimamo Wangu utabaki kuwa huo. Niambie Maneno mengi utakayo kuhusu huyu mwanaume lakini Ndie nampenda kwa sasa kama mwanaume Wangu". Vane aliamua kutoa Maneno hayo Ambayo alijua kabisa yatamuumiza Hansy.

" Vane unaongea nini? Unasikia unachokisema".

" Ndio nimesema na Narudia tena kaa ulee mimba ya mkeo kwa Sababu mimi nampenda hemed na kero zako ndo zitanifanya nifanye maamuzi ya haraka kuzaa nae au kuolewa kabisa".
Hansy aliumia kwa Maneno yake alitamani asiwe ni vane aliyeyaongea vile Taratibu aliondoka zake.

Vane nae alibaki sasa akilia huku akinyoosha mkono kutaka kama kumshika Hansy kumzuia asiendoke lakini alishindwa.
Aliingia eneo la pembeni na dukani hapo panapohifadhiwa Nguo zingine akaanza kulia bibie Vane.

" Nisamehe hansy Wangu nakupenda sana kukusahau nashindwa ndio maana naingia katika mahusiano mapya Walau nikutoe moyoni.
Ahhhu naumia naumia hansy Wanguuu".
Alilia Binti huyo.
Hali kadhalika Hansy nae akiwa kwenye gari mpaka chozi lilimtoka.
Maneno ya Vane yalikuwa yakijirudia na kumuumiza sana.

Majira ya jioni siku hiyo Hansy alikuwa katika apartment aliyokuwa akiishi Ambapo kuna kijana alimuita na kuna kazi alimpatia.

Kijana yule alieitwa mogar akamuuliza Hansy,

" Boss kwanini unafanya ivyo ikiwa umesema amekiri kuwa hakutaki tena? "

" Kuachana sio vita mogar sitasahau kuwa tuliishi kwa upendo Hilo linatosha kufanya hili wewe fanya kazi nayokupa na utabaki ukiishi hapa kwa sasa narudi nyumbani Kwangu kujaribu kuulazimisha moyo juu ya Ester".

" ila kweli boss Utaendelea kuteseka mpaka lini? Mwanaume wewe anazingua huyu unashika huyu naamini akijifungua utajikuta unampenda "

"Sawa".

Basi Hansy alijiandaa na kubeba nguo zake kweli akaondoka zake.

*********

Majira ya Asubuhi kiasi saa4 Ndipo Vane aliamka akaingia zake bafuni kuoga na kisha akatoka Sebleni na kumkuta mama yake.

"Mama shikamoo"

"Marhaba upo sawa vane?"

"Ndio mama kwanini?"

"Jana haukuwa sawa Kabisa ulirudi umepooza mpaka nikamuuliza yule muuzaji wa pale dukani kwako akaniambia tu ulikuwa unalia kuanzia dukani baada ya kijana mmoja kuondoka ni nani?"

"Ni Hansy mama jana nimeamua kumpa Maneno ya kumkatisha tamaa kabisa na alinikuta nipo na Hemed".

"Mhhh kwaiyo wewe ndo umempa Hayo Maneno bado unaumia wewe hata kula hujala kweli yametoka moyoni usije kukonda hapa mwanangu? "
" Mama nina imani nitasahau tu".
" Mhhh haya".
Basi waliendelea kunywa chai pale pamoja Ndipo Majira ya mchana mwasifa alifika nyumbani kule kwa bi Rose.
Mwasifa alikwenda kuwasalimia na kupeleka mualiko rasmi kuwa zimebakia wiki 2 kufunga ndoa.

Bo rose alimpongeza mwasifa na kuahidi kumpatia milioni 10 kabla ya harusi.
Hata Vane pia alimpongeza mwasifa.

" Nakuombea na wewe Vane uingie katika ndoa na yule umpendae hakuna ndoa nzuri kama mwanaume umpende naona raha sio siri".
" Amiin Asante Kwaiyo sasa ndoa itafanyika palepale nyumbani kwa Hansy unapoishi sasa au? "
" Hapana leo ndo nimehama pale rasmi nahamia  nyumbani kwa kina baraka ametaka iwe ivyo nilimuomba nikae huku labda lakini akasema niende tu kwao kwaiyo ndoa utafanyika ukumbini tutatokea pale kwao".

Bi Rose aliitikia akamuuliza Mwasifa,

" Ni sawa pia kwaiyo huyo mwanangu Ester mama kijacho amebakia peke yake au kashapata msichana wa kazi? "
" Hapana Jana usiku kaka hansy amerudi rasmi nyumbani na kuahidi ataishi nae pale ndo maana kanipa ruhusa nikatulie bi harusi".

Vane kusikia vile alishtuka yani jana usiku Hansy karudi kuishi na Ester. Hiyo baada ya yeye kumtolea kauli za maumivu mchana akajua fika Hansy ameshaamua kuachana nae.

Vane aliinuka na kukimbia chumbani hadi mama yake na mwasifa wakabakia wanashangaa hawajui imekuwaje gafla.

Vane machozi yalimtoka, aliyakumbuka Mapenzi ya Hansy, upendo, ucheshi vile akiwa nae na sasa atafanyiwa Ester hapo ndo aliyaona sasa maumivu.

"Siwezi siwezi Hansy ni Wangu nisamehe mpenzi Wangu ahhhhh nakupendaaaaaa".
Alipiga kelele vane huku mwasifa  na mama vane (bi Rose)wakiwa wamesimama mlangoni katika chumba cha Vane kumsikiliza tu pasina kumsemesha kitu chochote.

Asubuhi hiyo Hansy alikuwa zake ofisini akizungumza na rafiki yake Amon.
 Ndipo  kuna ugeni ulifika nae alikwenda mdogo wake wa kuitwa Erick.

"Vipi kaka niaje?"
"Safi  safi dogodogo za siku za nyumbani mko fresh".
"Ahhh wote wazima aisee kaka kitambo sijakuona"
" Nipo mdogo Wangu harakati tu"
" Ni kweli ila kuna kitu nataka kukuambia aisee".
Amon kusikia vile ikabidi atoke nnje kuwapisha ndugu wazungumze.

Hansy alimtazama Mdogo wake na kumjibu,
"Kitu gani?".
Kabla Erick hajazungumza mala gafla....

Sijui itakuwaje?

Tukutane sehemu ya 30*ME&YOU*

SEHEMU YA... 30
Na
Mamuh mohd
(0716730000)

Tuliposhia....

Hansy alimtazama Mdogo wake na kumjibu,
"Kitu gani?"
Kabla Erick hajazungumza mala gafla...

SONGA NAYO.....

Mala gafla mlango ulifunguliwa ofisini humo akaingia mrembo bibie Ester.
"Ohhh mmewangu nikaona nikuletee chai ofisini nikuwahi kabisa vipi mpo wazima?"
"Yah tuko poa lakini haikuwa na haja ya kuangaika ungetulia tu"
"Yote ni shukurani kwa kurudi nyumbani mmewangu na kunipokea Mimi kama mkeo haujui furaha niliyokuwa nayo".
Erick aliamua kuinuka na kuondoka zake hadi Hansy alishagaa kumuona Mdogo wake ametoka gafla bila hata kuaga.

"Ebu Subiri nimfuate Erick kuna kitu alitaka kuniambia naona kaondoka gafla nahisi hayupo sawa nisubiri nakuja".

Hansy aliinuka na kutoka Ndipo haraka Ester akachukua simu na kuwahi kumpigia Erick.

"Wewe Mwanamke muhuni unanipigia unasemaje?"
"Unataka kumuambia nini hansy? Kwa kile kilichotokea au? Tuliteleza wote na kulijikuta tumefanya icho kitendo kwaiyo funga bakuli lako mimi sawa nitaachana na hansy ila nitajifungua mwanae atanisamehe na wewe je? Si mtamvunja undugu na ukizingatia kwa sasa amerudisha Mapenzi kwangu".
Erick akaamua kukata simu tu Ndipo na papo hapo hansy Alirudi ofisini.
" Erick ameshaondoka kumbe sijui ana shida gani? "

" Ahh Labda alitaka kukusalimia tu". Ester alianza kumuwekea chai Mumewake huyo huku akifurahi kwelikweli.

Basi Vane alipokaa sawa Ndipo Mwasifa akamuuliza,
" Haya leo imekuwa unampenda tena Hansy mpaka unalia? Rafiki Yangu wewe ni kigeu geu".
" Ni mazoea mwasifa nimemzoea Sana Hansy Wangu ila sawa niliyataka mwenyewe Wacha niteseke".
" Na utateseka vane kama hutakuwa Muwazi kwake mapema".

" Niwe muwazi kuvipi? Tayari nimeshafanya Maamuzi nyie wacheni yaniyese kadri yatakavyo ila sirudi nyuma hemed atanisahaulisha haya".
" Mhhh haya kila la kheri".

Basi zilipita siku tatu Ndipo Siku hiyo Vane akiwa  zake dukani kwake Ambapo mama yake amempa duka kubwa  la vifaa vya watoto.
Alikiwa akiuza Ndipo alifika Hemed akiwa amebeba maua kwa ajili ya mrembo huyo Vane.

"Karibu sana mpenzi Wangu"
"Asante mzima wewe?"
"Hakika hofu kwako haukuniambia kama unakuja leo".

"Nimeghafirika vane kuna kitu hakipo sawa".
"Kitu gani?"
"Kuna mama yetu mkubwa alietulea anaumwa sana.
Ametoka kijijini na kufikia kwetu.
Mambo kwangu kwa sasa sio mazuri kazini nimesimamishwa basi sieleweki kabisa".
"Mbona una matatizo lakini haujaniambia  hemed ulisimamishwa kazi Kwa Sababu zipi?"
"Kuna upotevu wa milion 10 nikapewa Muda wa wiki moja nizirudishe laa sivyo nafunguliwa kesi.
Sijakaa sawa ndo mgonjwa amekuja yani niponipo tu vane".

"Pole matatizo tumeumbiwa sisi binadamu kama hukuchukua hizo ela ipo siku MUNGU atafungua kila kitu ila kwanza Urudi kazini".

" Ndo ivyo vane lakini kuja hapa na kuliona tabasamu lako najiona mpya kama sina matatizo".

" Asante sana Hemed kwa sifa zako".

" Nakupenda vane sio kwamba nakusifia tu no... Ni kitu kinatoka moyoni kabisa".

" Sawa basi tukatafute uwezekano wa mgonjwa aende hospital kwanza".

" Vane mgonjwa nishamchukulia dawa anaendelea nazo hapa napambania kurudi Kazini hiyo kesi iishe tu".

" Basi sawa nitajaribu kushuhulikia hilo mama alinipa pesa za kuendeshea duka hili naweza kuchukua hicho kiasi cha pesa nikakupatia".
" Sijui hata niseme nini Vane utakuwa umenisaidia sana na nakuahidi nikirudi kazini Miezi mitatu tu zinarudi hizo pesa zote"
" Sawa Usijali kuhusu hilo wewe ni Wangu ".

Vane aliguswa na matatizo hayo ya Hemed Ndipo kweli baada ya siku mbili alitoa kiasi cha Milioni 10 bank na kumpatia Hemed.

Kama haitoshi Siku hiyo walikwenda hotelini Ambapo walikula na kufurahi.

Hemed alikuwa akimlazimisha Vane kunywa pombe Ndipo Kweli Binti alijikuta ameionja na kumbadilisha kabisa.

Hemed alimbeba Vane kiulaini na kuchukua chumba kwa ajili ya kwenda kufurahi nae.

Lakini Wakati wanaendelea chumbani mala walipamiana na mtu eneo la kordoni kabla hawajaingia Chumbani. Hemed alikasirika Ndipo akaimshika yule mtu aliepamiana nae,
"Wewe unatembea huoni watu mpaka utupamie ona mpaka mpenzi Wangu anataka kuanguka".

" Oyaa brooo niache nyie pombe zenu mnatembea hamuoni".
Basi Hemed kujibiwa vile saa ngapi asikasirike akamvaa mvulana yule.
Nae yule mvulana hakubaki nyuma alikuwa na chupa yenye bia akaipasua na kumkata Hemed mkononi damu zikaanza kumtoka kisha kijana yule alikimbia.

Vane sasa akiwa hayupo sawa pombe inamsumbua kichwani aliweza kupiga kelele zikawafikia wahudumu Ambao haraka walifika kutoa huduma ya kwanza.

Waliitwa walinzi na kukodi usafiri kumuwahisha Hemed hospital maana damu zilikuwa zikimtoka alikatwa mkononi katika mshipa mkubwa ivyo zilitoka nyingi licha ya kuwahi kumfunga vitambaa.

Vane mpaka pombe zilimuisha kichwani alikaa sawa wakiwa hospital Ambapo watu walitawanyika akababakia yeye sasa peke yake.

Usiku huo Hansy alikuwa zake nyumbani na mkewe Ester Ndipo mala alisikia simu yake ikiita.
Kutazama aligundua ni mogar ndie amempigia.
Haraka akaipokea simu ile.

"Haloo mambo vipi?"
"Kaka nipo nnje kwako hapa njoo mala moja".
Hansy ilibidi atoke nnje na kweli akamkuta mogar akiwa na pikipiki yake.

"Vipi kwema?"
"Si kwema hapa mda wowote naweza kukamatwa na polisi maana nishaharibu huko nisaidie maokoto kiongozi Wangu nitimkie mbali".
"Shida nini niambie".
"ile kazi ulinipa siku ile unaondoka kwenye apartment nimfuatilie Vane na yule jamaa yake.
Kweli nilifanikiwa mimi nilikuwa nadili na vane alipo nami nipo Leo si ndo wakatoka kwenda hotelini.

Nikawa nawapimia nikamuona jamaa anamchanganyia vane bia za kutosha".

Hansy alishtuka kusikia vile,
"Unamaanisha vane amekunywa bia na huyo mwanaume umekubali vipi nilikwambia mlinde vane yule broo nilishamuona amna kitu na vane aelewi"
.

" Mkuu nisikilize  niliwapimia nikaona jamaa anaenda kuchukua chumba nikawahi mimi kwenda ndani ile wanakuja nikawatafutia Kona nzuri nikapita kuwapamia kibabe.
Jamaa akawaka nami nikasema yes ndo nilikuwa nataka nikampasulia chupa hapa nimeacha Damu zinamvuja".

" Ohhh Afadhali sijui Vane atanielewa lini ameniambia  maneno makali sana kiasi kwamba nashindwa hata kumfuata tena nikaona nitumie njia hii".

" Brooo kweli una Mapenzi ya kweli yule mwanaume anaonekana kabisa hamna kitu basi ndo ivyo"

" Ok sawa Subiri Nina pesa ndani kama laki3 nakupatia sasa zingine nitakutumia kesho".

" Amna neno nakukubali kiongozi ".

Kweli hansy alifanya Ivyo kisha kijana yule mogar akapanda pikipiki na Kuondoka zake.

Hapo Ndipo tunapata kujua kumbe Hansy alimtuma mogar kumfuatilia vane na Hemed, pia Mogar kupamiana na kina hemed hotelini ulikuwa ni Mpango kama Kutaka  kuwaharibia wawili hao.

ilikwenda mpaka Asubuhi Mwasifa alifika hospital baada ya kupigiwa simu na Vane.
"Pole sana sasa ana hali gani?"
"Acha tu mwasifa mkosi tu hata sielewi jana nilikunywa bia nikashtukia tu ugomvi amevuja damu nyingi sana Hemed sielewi
itakuwaje"

" Jamani vane mpaka umekunywa bia? Yani imebidi nivae nikabu nije maana na mimi bi harusi sikuruhusiwa kabisa Kutoka... Haya ngoja tuone ".

Walikaa hapo Ndipo Alipofika daktari alimuita vane kuzungumza nae.
" Mgonjwa hana damu anatakiwa kuongezwa damu na tumemfanyia vipimo hakuna budi kuficha maana hali imefikia pabaya...wewe umesema ni mkewake kwaiyo mnaishi kwa matumaini si Ndio? ".
Vane alishtuka kusikia vile,
" Hapana Hapana nilijibu tu jana sikuwa sawa nililewa sijafunga nae ndoa ni mpenzi Wangu tu".

" Ohhh basi uwe unatoa taarifa zilizo sahihi".
" Anaishi kwa matumaini una maana ana virusi vya ukimwi au? "

" Ndo nilishaanza kukuambia mwanzo hakuna jinsi Ndio ni Muathirika Wengi huwa hawasemi wazi kwa wenzao sasa nawe nakushauri kama ushawahi kushiriki nae tendo la ndoa unatakiwa kufanya vipimo ili muingie kwenye ndoa mkiwa mnajuana".

" Hapana hapana hapana sijawahi ndio maana mala nyingi alikuwa akilazimisha tushiriki kumbe alitaka kuniambukiza".
" Ohhh pole sana kama Mungu amekuepusha na hili ni kumshukuru.

Nisamehe sana nilijua wewe ni mkewe Ndio maana nikajua unajua lakini huo Ndio ukweli ishi nao moyoni mwako kwa sasa tuhangaikie damu apone".

Vane alitoka kwa daktari akiwa analia akafika mpaka kwa Mwasifa na kumkumbatia.
Hata mwasifa alishangaa,
" Vane nini kimetokea mgonjwa amepatwa na nini unaniogopesha".

Vane alishindwa hata kuzungumza kitu kwanza alibaki akilia tu, amenusurika mala mbili kwanza ni Mwasifa alimkwepesha  kutembea na Hemed na pili ni Hansy lakini hakujua kama ni yeye.

Vane alilia mpaka Mwasifa ikabidi ampige pige mgongoni alihisi yametokea matatizo Zaidi huwenda Hemed hayupo nao Tena.

"  basi Vane pole kipenzi Changu hakuna wa kupinga hili ulimpenda sana lakini ndo yameshatokea jikaze jikaze tujue tunaanzia wapi jikaze swahiba".

Vane Ndipo alimtazama Mwasifa na kumuambia,
" Ulisema... Ulisema.. ahhh ulisema".
Mwasifa alizidi kubakia njia panda akamkazia macho Vane kumsikiliza nini anataka kusema..

Siijui itakuwaje?
Tukutane sehemu ya 31*ME&YOU*

SEHEMU YA..... 31
Na
Mamuh mohd
(0716730000)

Tulipoishia......

Vane Ndipo alimtazama Mwasifa nae kumuambia,
"Ulisema... Ulisema... Ahhh ulisema".

Mwasifa Alizidi kubakia njia panda akamkazia macho vane kumsikiliza nini anataka kusema....

SONGA NAYO........

"Vane tulia na uniambie kitu gani kimetokea?"
"Hemed... Hemed ni muathirika kumbe na hakuwahi kuniambia hata siku moja alikuwa akinilazimisha tukutane kimwili hakuwa na nia njema na mimi naumia mimi".
Mwasifa Alishangaa,
"Subiri... Umeshatembea nae?"
"Hapana hapana ni kama bahati tu kila nikitaka kwenda nae inatokea Sababu.

ile siku ya kwanza ni wewe uliniokoa Mwasifa Wangu na mala ya pili jana ule ugomvi uliotokea ndo ikawa pona Yangu.
Alikuwa ameshanipa vilevi sio mtu mzuri kabisa".

" Basi shukuru Mungu kwa kukuepusha na hili usilie vane sawa?. Madaktari wanasemaje sasa? "
" Damu nyingi zimemuishia anatakiwa Kupata damu kama yupo wa kumchangia aje au ilipiwe awekewe".
" Basi lipia Kisha chukua simu yake tumpigie yule Sijui Ndugu yake aje hapa sisi tuondoke achana nae"
"Nitamsubiri mpaka atakapoamka na kukaa sawa Ndipo tutaondoka".

Mwasifa alimbembeleza Vane na mpaka akaacha kulia na kukaa pale hospital.

ilifika mpaka jioni Ndipo Hemed alifanikiwa kuongezewa damu akapata ma afuheni.

Vane na mwasifa walipata kwenda kumuona,

" Vane nilijua tu uko hapa mpenzi Wangu huwezi kuniacha peke Yangu".

" Ndio nilikuwa nasubiri uamke shika simu yako hii mpigie huyo ndugu yako kenny atakuja kuendelea kukuangalia nimeshalipia kila kitu.

Asante MUNGU kanifungua macho juu yako haukunipenda bali ulitaka kuniua kwa maradhi uliyo nayo Asante sana haukuwa mtu mzuri.

Sahau kila kitu kuhusu mimi hata pesa nilizokupatia sahau kunilipa nimekusamehe endelea na maisha yako nami niache maisha Yangu".
Mwasifa nae hakubaki nyuma akamsogelea Hemed.
" Wewe ni aina ya wale wanaume washenzi sana matapeli wa mapenzi ulitaka kumlaghai rafiki Yangu.
Sasa kaa mbali na Vane kuanzia sasa".
Kisha mwasifa alimshika mkono vane na kuondoka zao.

Hemed alibaki ameduwaa na kujiuliza Vane amejuaje kuhusu maisha yake?.
Alitikisa kichwa na kupiga kelele, kuashiria majuto kwa upande wake.

Palikwenda mpaka usiku Ndipo Vane Alifika nyumbani akiwa na Mwasifa wake.
Mama vane kumuona Binti yake alimshangaa,
"Tangia jana mwanangu nilipata wasiwasi sana ila Mwasifa alinipigia simu kuniambia nisijali yupo na wewe. Nakuona sasa haupo sawa nini shida?"
Vane Ndipo alikaa chini na kumueleza mama yake kila kitu kilichotokea baina yake na Hemed.

"Mjaa laana mkubwa huyo nitamuweka jela alitaka kukuharibia maisha.
Pesa si tatizo naumia vipi kama angekuharibia maisha? Atakaa jela iwe fundisho".

Aliongea kwa hasira bi Rose Ndipo vane akamzuia hilo mama yake.
"Hapana mama kubwa nimeshajua ukweli hajafanikiwa alichokitaka basi inatosha ".
"Mwanangu ukweli mwanaume wako wewe ni Hansy haya yote yametokea ili kukuonesha kuwa Hansy Ndie mwanaume sahihi kwako.
Kwanini unamlazimisha awe na Ester ikiwa alishasema anakupenda wewe Ester atabakia kuwa Mama wa Mtoto mbona huwa inatokea hii sio ajabu".

" Mama nakiri mbele yako nampenda sana Hansy na nilikuwa najaribu kuudanganya moyo Wangu lakini kwa sasa siwezi tena".

Mwasifa Ndipo kwanza alicheka kisha akamuambia vane,
" Sasa ni Wakati wako na wewe kumuonesha kuwa unampenda.
Hansy amepambania sana Mapenzi yenu lakini ukajifanya huoni huu upendo sasa muoneshe.
Mtafute wewe sasa na ukazungumze nae ajihisi anapendwa.
Hichi naamini ni kitu ambacho Hansy anakihitaji Zaidi kwa sasa".
Vane alimtazama Mwasifa akaona kabisa jambo lile kama kwake ni gumu.
" Mwasifa naanzaje ikiwa mala ya mwisho nilimtamkia Maneno mabaya sana atanielewa kweli".

" Kuhusu kukutana nae niachie mimi nitasawazisha hili kesho nakukutanisha nae hakikisha unabaki nae muombe msamaha na usisahau kumuambia jinsi gani unampenda na kukiri daima na ni wewe na yeye".

" Ahhh Mwasifa buana ujue unanipanga mpaka nahisi aibu"

" Ndio nataka siku ya harusi Yangu mje mkiwa Pamoja na nitarajie taarifa za ndoa".

Basi walifurahi wote kwa Pamoja pale hata Vane alijihisi ujasiri sasa wa kumkabili Hansy kumueleza Maneno hayo".

Basi Siku iliyofuata majira ya Jioni Hansy Alirudi nyumbani kwake kule Ndipo akakuta mkewe Ester ameandaa vyakula amepamba seble.
ilikuwepo shampeni na keki kiujumla alijiandaa.
Hansy alipokelewa Vizuri.

"Hansy mmewangu Leo nimeandaa yote haya nahitaji kumaliza tofauti baina yetu.
Umerudi kuishi hapa hapo hatulali kitanda kimoja naumia sana mimi ni mkeo naetarajia kuwa mama wa mwanao.

Naumia sana huwa najiangalia na kujiuliza nina kasoro gani Sijioni, tafadhali hansy naomba unipende na kuikubali hii ndoa yetu nitakuwa mke mwema  kwako.

Hii keki nahitaji uikate wewe ikiwa Utanipokea Leo na kunikubali kama mkeo.
lakini kama bado moyo wako hautaki sitaendelea kulazimisha nitaondoka na kurudi kwetu nitajisemea kuwa nimeshindwa.
Naomba nidhihirishie leo kata keki hii na unilishe endapo umenipokea ila kama bado acha nitaelewa".

Aliongea Ester huku akilia sana hata Hansy alibaki njia panda.
Hansy alikumbuka Upendo wake kwa vane na hapohapo akakumbuka kauli ambayo Vane alimtamkia kwa mala ya mwisho kuwa anampenda sana huyo mwanaume wake.

Alikumbuka pia jinsi Vane alivyo mkali kila mala anapomfuata Binti anasimamia msimamo wake kwamba hansy abakie na Ester mzazi mwenzako mtarajiwa.

Alimtazama na Ester Ambae ameanza kumpenda muda na anafahamu kuwa Binti ni mjamzito.

Hansy aliisogelea keki ile na kujisemea ndani ya moyo wake,
"Naempenda hanipendi basi wacha upendo Wangu wote kwa sasa niuhamishe kwa mwanangu ajae ndie atakuwa kipenzi Changu nakubali kwa niaba yake".

Hansy alishika kisu Tayari kukata keki ile hata Ester hakuamini alijikuta anafurahi kupita kiasi inamaana akikata hiyo keki amekubali hata kulala watalala pamoja.

Hansy akaanza kuikata keki ile lakini gafla simu yake iliita ikabidi aache na kuweka kisu pembeni akapokea ile simu.

"Haloo mwasifa.... What?? Pole uko wapi? Nakuja nakuja nakuja". inaonesha Hansy alipewa Taarifa Ambazo zilimfanya aache zoezi alilokuwa anafanya na kumuaga Ester akaondoka zake.

Ester alikasirika mpaka keki yote akaitupa ikamwagika alishaona amefeli kuunganisha upendo baina yake na Hansy Ndio maana dharura imetokea ikiwa anakaribia kufanikiwa.

Hansy alifika mpaka sehemu Fulani ambapo palikuwa ni katika uwanja mmoja alafu kuna nyumba Ambayo haijamalizwa kujengwa.

Alikumbuka kuwa Mwasifa alivyompigia simu alimuambia kuwa ametekwa na watu wamemleta sehemu hiyo aende na pesa akamuokoe".

Aliingia mpaka ndani na nyumba ile huku ameshika Jiwe kubwa kujihami,
" Mwasifa.... mwasifa... mwasifa".
Alisikia akijibiwa na mtu kutokea nyuma yake.

" Nipo hapa".
Ndipo kugeuka alimuona bibie Vane hata hansy alishangaa.

" Ni mimi vane ndie nimekuita hapa nisamehe sana kama umeshtuka".

"Vane ulikuwa na haja gani ya kutumia njia hii kuniita?"
"Hansy sijui hata niseme nini".
Binti alipiga magoti huku amemshika hansy miguu.
"Naomba unisamehe mpenzi Wangu nilikuwa naulazimisha moyo nikajisahau kuwa siwezi bila wewe.
Nakupeleka sana Hansy nakuomba nisamehe mpenzi Wangu mpaka sasa mimi ni wako niko salama kabisa naomba msamaha wako".
Hansy alimuinua Vane na kumshika mashavuni.

"Asante kama nawe umeligundua hili nimepambana mpaka kusikia hili neno mdomoni kwako kuwa unanipenda...nami pia nakupenda na unajua hilo...umekuja leo muda muafaka asante vane kwa kuikamilisha Furaha Yangu iliyopotea".

" Yaliyotokea ni  makubwa sana Hansy kuhusu yule kijana Hemed si mtu mzuri alitaka kuniharibia maisha Yangu".
" Nafahamu nilikutana nae kuna siku anagombana na mwanamke anaejiuza kuanzia hapo niliona sio sahihi kwako ndio maana kuna kijana nilimuweka kuhakikisha anakufuatilia nadhani juzi kuna tukio limetokea kwa huyo hemed".
" Unamaanisha nini hansy?"

" Najua kuna kijana alimjeruhi Hemed yule nilimpa kazi ya kukulinda wewe na katika hali hiyo akajikuta amemjeruhi".

" Ahhhh siamini!!!! Kumbe ni wewe Hansy basi uliniepusha na ugonjwa kumbe yule kaka ni muathirika baada ya Tukio lile kwenda hospital nikajua ameathirika Asante sana Hansy naamini unanipenda nami kwa sasa sitaacha kukuonesha upendo sijali tena chochote Hansy".
Walikumbatiana pale Ndipo Hansy alimbeba  Vane mpaka nnje Kwenye gari lake.

" Hansy tunaenda wapi sasa? "

" Unadhani tumemaliza mazungumzo siku ya muhimu kama hii usijali upo salama".
" Najua kwako niko salama".
Hansy aliendesha gari Ndipo wakaondoka zao.

Sasa usiku huo Hemed ndo alipata kupona akaruhusiwa kurudi nyumbani.
Alikuwa na Rafiki yake kenny.
" Aisee broooh kila kitu kimeharibika yule mwanamke tushampoteza.
Milioni 10 hizi tumezichezea kulewa na kubadili wanawake tukijua tutaendelea kupata tujipongeze lakiji amekushtukia mapema".

" Weee acha tu kwanza yule doctor alikuja kuchukua vipimo akamuambia vane ukweli nimeshamjua yule tumfyeke walau ndo hasira Zangu zitatulia.
Kisha vane Atarudi kwangu kilazima atatoa ela nitakavyo.

Tutamteka sasa Nitamuambukiza ukimwi na ela atatoa"
" Hilo ndo la msingi kaka hatushindwi na kitu wa kishua yule sisi tunataka ela lazima Arudi kwetu kilazima".
" Hilo wala usijali kesho waite wenzetu Chunda na Kiza  tujenge mishe hapa".
" Sawa brooh kwa sasa weee kunywa dawa ulale mimi natoka kwanza kunywa kidogo nikae sawa".

Walizungumza wawili hao inamaana mpango wao sasa ni kumpata vane hawajakubali awaache kirahisi......

Sijui itakuwaje?
Tukutane sehemu ya
32*ME&YOU*32_36

SEHEMU YA... 32
Na
Mamuh mohd
(0716730000)

Tuliposhia.....

"Sawa brooh kwa sasa weee  kunywa dawa ulale mimi natoka kwanza kunywa kidogo nikae sawa".
Walizungumza wawili hao inamaana mpango wao sasa ni kumpata vane hawajakubali awaache kirahisi....

SONGA NAYO.....

Siku ile Asubuhi Ndipo Hansy aliamka na kumkuta vane pembeni yake inamaana usiku ule walikuwa Pamoja.
Hansy alitabasamu kwanza na kuinuka akakaa pembeni ya bibie vane.
"Niambie mpenzi Wangu mbona umekaa haujaniasha?"

"Hansy sitaki Tena haya maisha ya kukutana kwa wizi kwa sasa nahitaji kuishi na wewe tufunge ndoa ambayo watu wote wanaotujua na wasiotujua wataitambua".

" Vane laiti ungejua Hiyo kauli yako inavyousisimia moyo Wangu acha tu. Nakuoa kipenzi nenda kamuambia mama na kila ndugu yako kwamba tunakwenda kufunga ndoa.
Hapa natuma talaka kwa Ester Leo Leo pale atabaki akiishi ila suala la ndoa mimi na yeye nilishindwa tokea zamani. Ndoa ya ndoto Yangu ni yetu me&you".

" Asante sana Hansy kwa sasa nimeingia mazima kwenye Mapenzi yako Sitarudi nyuma tena na sitafanya makosa Ambayo nilitaka kuyafanya mwanzo.

Naomba nisamehe sana Tafadhali".

" Hayo yameshapita kipenzi tusonge Mbele Kadri muda unavyozidi kwenda ndo nazidi kukupenda Vane hakika wewe ni Wangu.

Uliniokoa katika yale maji  kwanini nikuache kama sitozama mie".

" Asante hansy nashukuru kwa maneno matamu yasiyoisha hamu kukaa na kuyasikiliza.

Sitamani hata uwepo mbali na mimi".

Hansy alimkumbatia Vane na kumbusu mfululizo ulikuwa ni upendo wa dhati kabisa kutoka moyoni.

Siku ile majira ya  mchana Ester akiwa Nyumbani Ndipo alisikia geti likigongwa. Alikwenda kufungua akakuta ni ujumbe umeletwa na amon rafiki yake na Hansy. Ester Ndipo alifungua kuusoma ujumbe ule akakuta ni  barua za talaka.
Ester machozi yalimtoka mpaka nguvu zilimuisha alikaa chini.
" Kwanini lakini? Kwanini Hansy ananifanyia ivi kumpenda ndo naadhibika ivi ahhhu ndoa imekuwa ya mateso sijawahi Kupata upendo wa Hansy naumia mimi".

" Kiukweli hata mimi sijui hata nikusaidiaje maana juhudi zetu zimegonga mwamba.
Hansy amerudisha Mapenzi kwa Vane utadhania ndo wamekutana leo.
Vane ni mnafki huko kusema alikuachia hansy mlee mtoto hana lolote nimuongo kabisa.
Wewe sawa umepoteza lakini hakikisha mnakosa wote Usikubali ashindwe utakuwa sio mtoto wa mjini".
Amon alimuambia hayo Ester na kumpandisha Binti hasira.
" Sawa nakubali Hansy hanipendi lakini kama usemavyo shemeji katika kuanguka tutaanguka wote".

" Hayo ndo Maamuzi  ya kijasiri shemeji Yangu najua unaumia lakini jikaze sawa kuwa jasiri sasa kwa Sababu ya mtoto unaekwenda kumzaa".

" Sawa shameji mziki wangu wataucheza nasema wataucheza Subiri tu naondoka Narudi nyumbani kwetu kupambana na vane na Kwenye nyumba ya baba Yangu ataondoka".

" Hapana Adui ili umtafune  vizuri awe Karibu yako na sio mbali.

Nenda Vane baki nae ili upate kumfanya utakavyo kimya kimya maana mtakuwa Karibu".

" Sawa shemeji Asante na ukamuambie Hansy Asante.

Kama kubembeleza nimembembeleza sana hansy lakini moyo wake haujanipokea kabisa basi sawa nakubali sasa".
Walimaliza kuzungumza hayo Ndipo Amon akaaga na kuondoka.
Ester alibaki analia sio Kawaida.

Siku ile Hansy alikwenda Nyumbani kwao jioni hiyo na kuwakuta wazazi wake.
Walimpokea na kusalimiana pale vizuri.
"Ester amesema kuwa sasa umerudi kuishi nyumbani hakika ni jambo la furaha sana"

" Mama sivyo mnavyodhania kwa nimekuja kuwaambi kwamba nimempa talaka rasmi Ester na badala yake najiandaa kumuoa vane rasmi".

Baba hansy yeye hakuonesha pingamizi lakini mama hansy Alishangaa,

" Kwani mbona mnabadilika kama kinyonga? Huyo vane alisema anakuacha uwe na ester mlee mtoto wenu ajae sasa imekuwaje amekuwa mbinafsi?"

"Mama Vane sio mbinafsi kabisa ni mwanamke stahiki na liniepukalo lina kheri naamini vane ndie mke sahihi kwangu  rasmi nimempa talaka Ester najiandaa kumuoa Vane nadhani baada ya ndoa ya mwasifa inafuata ya kwetu".

" Hansy Mwanangu inamaana unaitelekeza hadi damu yako Sababu ya Mwanamke kweli? "
" Si kweli mama Mtoto nitamlea na vane amekubali hilo namuona kabisa atakuwa mama mzuri".
" Uwongooo... Anaongea Sasaivi tu kukudanganya ila Hawezi kukaa na mtoto wa mwanamke mwenzake kaa jifikirie tena hansy".

Sasa Wakati wanaendelea kuzungumza hapo mala Alifika Erick ambae alikuwa eneo la chumbani sasa ndo alitoka Sebleni.

"Erick alipiga makofi na kumtazama kaka yake akamuambia,

"Safi sana kwa Maamuzi haya kaka. Nami nimeamini Ester sio mke sahihi kwako mke ni Vane apewe maua yake". Hata wazazi wa hansy walishangaa maana wanajuaga Erick huwa hampendi vane badala yake anamteteaga Ester lakini leo kwa mala ya kwanza kamuunga mkono kaka yake kumuoa vane.

Hansy alifurahi hadi aliunuka na kumkumbatia Mdogo wake Huyo,
"Asante sana kwa kutambua hisia Zangu Erick"
"Nakuelewa kaka ipo siku utajua yaliyojificha ya yule Ester hafai hata kidogo kuitwa mke wa mtu si kwa wewe tu bali mtu yoyote".

"Asante Mdogo Wangu".
Mama hansy alibaki kimya ni kama nguvu zilimuishia peke yake ndo alikuwa anapinga Mwishowe akaona aridhie japo kwa shingo upande.

Basi usiku huo Vane nae alikuwa nyumbani kwao akimuelezea mama yake kuwa anatarajia kufunga ndoa na Hansy.
Bi Rose hakuwa na hiyana maana anafahamu kati ya hansy na vane Ndipo upendo ulipo ni suala la muda tu.
"Nitakuandaa mwanangu ukawe mke bora huko alete posa ukimaliza tu harusi ya Mwasifa nawe uwekwe ndani".
"Sawa mama natamani haraka jamani khaa".

Wakicheka wenyewe wakiwa hapo Sebleni.

Mala gafla wakaona mfanyakazi akiingiza mabegi ndani kama vile kuna mgeni amekuja.
Walinyamaza kimya Ndipo aliingia bibie Ester.

Ester kufika alimtupia talaka zile Vane, "Hongera umeshinda mama nimepewa talaka nimerudi kwetu zamu yako sasa Kwenda kuishi katika ile nyumba.
Kaa ukijua jambo unalomfanyia mwenzake vane basi nawe litakukuta tu weka akilini hilo".

Vane hakubaki nyuma nae akajibu,

"Sio mimi bali ni upendo.
Hansy ameshindwa kukupenda kwanini niendelee kumtesa.
Nilikupa nafasi umeshindwa kuitumia basi Siwezi kujificha pengine tena Chaka langu ni Hansy".
"Sawa".
Alijibu Estar Kisha akaelekea zake chumbani hata bi Rose alibaki kimya tu kwanza akiwasikiliza mabinti wale mpaka walipomaliza mazungumzo yao.

Vane hakuoneshwa kuwa na uwoga wowote alijiamini Binti kupita kiasi.

******

Basi siku kadhaa zilipita hatimae ilifika siku ya ndoa ya bibie Mwasifa.
Kuanzia saloon Bi harusi alikwenda Pamoja na Vane waliandaliwa na kupendeza kwelikweli .

Walipomaliza Ndipo Walirudi nyumbani Tayari kwa ndoa kufungwa.
Mwasifa alifanikiwa kufunga ndoa na mpenzi wake Ambae ni baraka.

Shuhuli ile ilihudhuriwa ma watu Wengi vyakula vilikuwa vya kutosha hapo.

Sasa Wakati shuhuli inaendelea Vane alianza kuhisi kama usingizi alijikuta anatamani kulala.

Binti alishindwa kujizuia Ndipo akaamua aelekes sehemu yenye utulivu ajiegeshe maana usingizi ulimzidi mno hali Ambayo sio ya kawaida.

Basi Wakati anaelekea huko ndani kabisa mala alishtukia amezibwa puani na mtu Ambae hakumfahamu ni nani. Vane palepale alipoteza fahamu.
Mtu yule alimsukuma kumficha katika kona nyingine ili asiweze kuonekana na mtu...

Sijui itakuwaje?
Tukutane sehemu ya 32*ME&YOU*

SEHEMU YA.... 33
Na

Mamuh mohd
(0716730000)

Tulipoishia......

Vane palepale alipoteza fahamu.
Mtu yule alimsukuma kumficha katika kona nyingine ili asiweze kuonekana....

SONGA NAYO.....

Sherehe ilikuwa ikiendelea ndipo alionekana mtu mmoja  akiwa amebeba gunia analiburuza na kutoka nalo nnje.
Hakuna mtu aliemfuatilia  watu walijua huwenda ni mfuko tu wa taka taka.

Alikuwepo bibie Ester eneo la hapo nnje lakini amefunikwa na majani ngumu mtu kuonekana.
alikuwa anazungumza na simu haijulikani alikuwa anaongea na nani.

Ester aliangalia mtu yule ambae alitoka nnje na gunia akaweka katika toroli lililokuwa eneo la nnje pale.
Lakini kabla hajaanza kuondoka alipokea simu na kuongea,
"Haloo ndo natoka na mzigo nipo naelekea mlandege chimbo niwakute hapo".
Ester alishangaa Ndipo kutazama vizuri akaona  ni kama katika gunia lile kuna kitu kinafurukuta furukuta.

Aliyaacha maana nae habari alizokuwa anazungumza kwenye simu ni za siri sasa baada ya mtu yule ambae walimfahamu kama mzoa uchafu kuondoka akaendelea kuongea na simu.

"Ndio kesho nitawapa Njia zote za kumpata huyo hasimu wangu mfanye kazi kweli nawaomba kama ambavyo huwa mnamfanyiaga mama na iwe siri... Haya... Haya".
Bibie Ester alimaliza mazungumzo hayo kisha Ndipo akatoka kurudi eneo la shuhulini.

Hansy alikuwa zake na amon wamekaa meza moja.

Amon alikiwa akinywa bia tu zilimchakaza mpaka akaanza kuongea kuwa alitaka kumuoa yeye Mwasifa lakini amezidiwa kete.
Hansy yeye alikuwa akimcheka tu.

Muda wa shuhuli ulimalizika ma tayari ni usiku watu walikuwa wameshaaanza kutawanyika.
Bi Rose Ndipo akamfuata Hansy,
"Vane upo nae maana namtafuta simuoni na simu yake hapokei"
The"Hapana sijamuona muda nikadhania labda hekaheka za harusi au bado yupo ndani? "
" Basi huwenda bado huyo ndani na bi harusi ila sawa mimi Narudi nyumbani kupumzika aiseee"

" Sawa mama Vane nipo nae akitoka nitamleta Mimi nyumbani"
" Haya".

Bi Rose akaondoka zake na watu Wengine Wengi waliondoka.
Sasa Hansy alikuwa akimpigia simu Vane lakini simu ilikuwa ikiita tu pasina kupokelewa.
Alizidi kumpigia Ndipo mwisho ilipokelewa,
"Haloo mimi muhudumu wa Harusini hapa nimeokota hili pochi hapa Ndani kordoni nikasikia simu inaita naipeleka kwa mama mwenye nyumba hii sijui ni ya nani?"
"Ok sawa nielekeze hapo ulipo nije"
"Ni hapa kordoni kama unaingia ndani"

"Haya".
Hansy alifika pale kwa Haraka Ndipo akamkuta mtu huyo kashika pochi ambayo alikuwa nayo vane.

Aliyatazama maeneo yale ambayo ameambiwa kwamba Ndipo Pochi ilipokutwa pale  alipata wasiwasi.
"imekuwaje mpaka aache pochi sehemu hii?
Alijaribu kumuita pale mpaka familia walitoka wakiwemo maharusi.
Hansy aliwaelezea hali halisi ambayo iliwashtua wote.

" Uwiii!!! Vane rafiki Yangu jamani uwiiii Mungu Wangu weee!!!".

Machozi yalianza kumtoka Mwasifa ikawa sasa ni hekaheka pale.

Baraka  ambae ni mume wa Mwasifa ilibidi afanye mawasiliano na askari wenzake kureport kuwa kuna tukio inasadikika linetokea la utekaji.
kwa mazingira yale huwenda Vane ametekwa.
Alikuwepo mtoto mmoja ambae ni Mtoto na ndugu yake na baraka mwenye umri wa miaka 10 aliitwa Betty akamuambia bibi yake mama wa Baraka.
"Bibi mimi nilimuona kuna mtu kabeba gunia ni mchafu kama anazoa taka ametokea huku ndani au ndo yeye kamchukua Anty vane".

Wazo hilo wote waliliafiki na ubize wa shuhuli wakajikuta hawafuatilii mtu yule.

Basi Baraka hakuwa tena bwana harusi wa kulala ndani na mkewe, ilibidi atoke na Hansy safari Kuelekea kituoni kupanga nàmna ya kuanza upelelezi wao.

Usiku huo bi Rose alikuwa amelala kitandani Ndipo akapigiwa simu na hansy kupewa habari zile.
Zilimshtua kupita kiasi aliamka huku amechanganyikiwa.

Bi rose moja kwa moja alienda mpaka Chumbani kwa Ester.

"Weeee mjaa laana niambie mwanangu umemfanya nini? Vane yupo wapi?"
"Mama!!!! Sijui chochote kwani imekuwaje?"
"Vane ametekwa inasemekana kuna mzoa taka alikuwa amebeba gunia la uchafu anashakiwa kuwa Ndie alimchukua vane ni nani kama sio wewe Ester utakaa ndani niambie mwanangu Yuko wapi?"
"Mama niamini sijafanya ivyo niamini mama".
"Hujanishawishi subiri".
Bi Rose alifanya mawasiliano nae na askari anaemfahamu baada ya nusu saa tu Ester alikuja nae kukamatwa bi Rose alimshuku Ester kwani Ndie hasimu wa Vane.

Polisi walianza kwa kutembelea dampo zote za pale mjini ambapo huwa uchafu unamwagwa na kuwapeleleza wanaolala sehemu hizo.
Walikataa na kusema hawajui Chochote.
Mpaka usiku unakuwa mkubwa Hawakupata mafanikio yoyote.

ilikwenda mpaka Asubuhi sasa Ester akiwa ndani hajazoea maisha yale Ndipo alibanwa na kueleza kile alichokisikia.
"Ni kweli nilimuona huyo mzoa taka akazungumza na simu alisema.... Alisema.... "Naelekea mlandege chimbo niwakute hapo".

Aliongea hayo kisha akasukuma toroli lake akaondoka huo Ndio ukweli sihisiki na Chochote Kingine mimi".
Binti alilia Ndipo Polisi wakafanya mawasilino kuzungumzia kile ambacho alikisema Ester.

Basi Safari ya maaskari watatu pamoja na Baraka akiwemo wakiwa wamevaa mavazi ya kawaida walianza kwenda sehemu hiyo waliyoambiwa kwa ajili ya upelelezi.
Walifika eneo hilo lililoitwa mlandege wakakutana na nyumba kubwa Ambayo haijamalizika nnje pamechorwa chorwa kuonesha wanaioishi hapo ni wahuni wahuni.

Walificha silaha zao na kuanza kuingia polepole katika jengo hilo.
Walifika mahali wakasikia Sauti ya mtu akiwa anahema  analia sio kawaida.
Walianza kwenda kwa tahadhari mpaka wakafika kwa kunyata wakakuta kundi wa Wahuni wamekaa huku wamemzunguka Binti ambae ni Vane kwa maana walimpata.

Risasi zilianza kutembea sehemu hiyo, "Askari wote walishika Risasi tofauti na wale watekaji aliekuwa na Risasi alikuwa ni mmoja tu Ambae ni Kenny.
Askari waliwashambulia wote na wa mwisho kupigwa Risasi alikuwa ni Kenny rafiki kipenzi wa Hemed.

Kenny nae katika hali ya Kuanguka chini akajikuta ameachia Risasi ikampata Baraka eneo la begani kwani hawakutegea.
Walijua pale walivyompiga ameshaishiwa nguvu anaanguka lakini kumbe kenny nae alijiweza kuachia Risasi.

Basi watekaji wote wale sita waliokuwepo pamoja na Kenny walipoteza maisha palepale kwa Risasi zile hali Mbaya ikawa kwa baraka.

Vane alipiga kelele kumuona shemeji yake mume wa rafiki yake ambae hata ndoa hajaifaidi aliingia kazini Kwanza.

Askari wawili walimfanya kwanza jitihada za kumtoa Risasi mwanzao walikuwa na utaalamu huyo kisha wakambeba kutoka nae nnje Kwenye Gari.
Huku mwingine akiwa anamfungua kamba kamba Vane alizokuwa amefungwa na kuondoka nae.

Wakiwa Kwenye Gari walikuwa wakipiga honina kuwasha taa za hatari kuomba njia kwa Haraka kumuwahisha baraka hospital.
Vane alikuwa nyuma akiwa na baraka ambae sawa alitolewa Risasi lakini ilionekana kuwa imejeruhi alikuwa akiugulia sana.

"Shameji Yangu jamani utapona shemeji shemejiiii ahhhuhh ahhh".
Baraka alimshika mkono Vane na kumtuliza.
"Usijali usijali lakini ne... Nenda.... Ka... Ka ka.. kamuambie.. sifa... Na.... Na... Nampenda sana.. nitaishi nae.. nitaishi nae nitaishi nae hata... maisha baada ya haya....".
" Hapana Hapana Hapana".
Walifanikiwa kufika hospital ya eneo hilo ikabidi waingie hapo dharura kitanda haraka kililetwa kwa ajili ya kumpokea mgonjwa/majeruhi.

Lakini wakati wanamtoa kwenye gari wanampandisha kwenye kitanda baraka alilegea na akiwa ametulia tuli.

Askari mmoja akamsogelea na kushika kufuani alishtuka  na kuweka mkono mdomoni kwa mshangao, hadi wote waliokuwa pale walishangaa kuonesha kuna Hatari imetokea.....

Sijui itakuwaje?
Tukutane sehemu ya 34*ME&YOU*

SEHEMU YA....34
Na
Mamuh mohd
(0716730000)

Tuliposhia......

Askari mmoja akamsogelea na kushika kifuani alishtuka na kuweka mkono mdomoni kwa mshangao, hadi wote waliokuwa pale walishangaa kuonesha kuna Hatari imetokea....

SONGA NAYO......

Askari yule alipiga saloot na kuwaambia wengine,
"Afande Baraka anetuacha".
Wauguzi waliompokea nao kumgusa walijiaminisha kwamba kweli amewaacha amepoteza maisha.

Vane alibaki ameduwaa kwamza alimfikilia mwasifa atalipokeaje hili? Ni kwa Sababu yake ndio kaleta shida yote Hiyo.
Binti alipooza akabaki kimya Machozi yakimtoka.

Basi kwa kuwa ilikuwa ni hospital ya njiani waliyoingia kwa dharura ilibidi waubebe mwili wa Baraka na kuurudisha kwenye gari wote wakapanda kuelekea sasa mjini.
Vane alikuwa akimtazama baraka huku analia sana.
"Nitamnyamazisha vipi mwasifa ahhh shem umeniweza ni Afadhali lingenipata vane mie na sio wewe uhhhhhh".

Bunti alilia sana Ndipo askari yule mwingine alikuwa alimtuliza huku akifanya mawasilino kituoni kwao pale kuwapa taarifa kamili.

Hansy alikuwa na bi Rose pamoja na ester kituoni bado wanasubiri majibu ya upelelezi ambao walikwenda askari wale watatu kwanza.
Alitoka mkuu wa kituo mpaka eneo la nnje walipo watu hao.
"Vane amefanikiwa kuokolewa Ni kweli huko aliposema Ester Ndipo aliekuwepo ivyo wapo njiani wanarudi atataueleza kwa kina nanu alimteka.
Ester kwa kuwa ametaja sehemu hiyo basi ataondelea kuwa chini ya ulinzi.

Wote walishusha pumzi  Ester alilia sana,
"Nieleweni..mama ongea nao sijui chochote nilimsikia tu yule mzoa taka akizungumza nisaidie mama Yangu ahhhh".
Bi Rose  akamuomba kweli yule mkuu wa kituo.
"Basi huyu pia ni Binti Yangu madam mwenzie ameshapatikana tumuache kwanza vane akija akimtaja huyu anahusika Atarudi jela nakuomba".

"Sawa ila kuna tatizo lingine limetokea katika Harakati za kumuokoa Vane tumepoteza askari shujaa na mpambanaji amepigwa Risasi na mateka waliowakuta huko na sasa wanarudi nae hapa tumpe heshima zetu kisha tumpeleka hospital ya Jeshi kuhifadhiwa wakati taratibu zingine zikiendelea".

Wote walishangaa na kupata majonzi...lakini hakuna alieweza kuhisi Kama atakuwa baraka ni kama walipigwa na wimbi na upofu hawakuwaza ivyo kabisa.

Punde lilifika gari la askari wale Ndipo walishuka askari wale wawili pamoja na vane akiwa ameloa machozi usoni.
Hansy kwanza alikwenda kumkumbatia vane sasa Wakati anamkumbatia Ndipo akajikuta macho yake yanatazama ile seat ya nyuma ulipo mwili wa aliepoteza Maisha.

Hansy alishtuka akamtazama vane analia binti kuangalia wale askari wawili waliofika akakumbuka kuwa wa tatu kwenda alikuwa ni baraka.
Hansy taratibu alisogelea gari lile na kumtazama mtu yule.

Hansy hakuamini macho yake moyo ulipiga pigo moja la mshtuko paaaaaaaaaaaaaah!!!! Mwili wote ulisisimka muasho si muasho, ubaridi si ubaridi.
Alitazamana na bi Rose na wengine wote ndo kusogea kumuona ni baraka.

"Uwiiiii mwasifa Wangu jamani uhhhhhh mamamaa mamaaaaa mmamaaaa yeeeeee uwiiiiii".
Alipiga kelele bi Rose Ndipo askari wakawazuia kwani eneo la usalama lile waliwataka wawe wapole kwanza.

Kwa kuwa wanafahamu kuwa Baraka ana uhusiano na Familia ile waliwaruhusu kurudi nyumbani na kuwaeleza familia ya Baraka wakimaliza Ndipo kesi itaendelea kubwa walijiridhisha kuwa Wameshambuliwa Watekaji wote.

Walitoka pale Ambapo bi Rose alipendekeza kwanza vane kupelekwa hospital kwa ajili ya checkup na huduma za dharura kama kuna chochote limetokea.
Bunti alibaki huko hospital na Hansy, Ester bi Rose walikwenda nyumbani kwa Kina baraka sasa.

Kufika sasa waliingia mpaka ndani nyuso zikiwa ni za majonzi.
Mwasifa alikuwa Chumbani ila kusikia wageni kina hansy alitoka Haraka.

"Vane amepatikana? Eti?".
Hansy kama Mwanaume alilibeba lile kuzungumza Mbele ya familia,
"Vane amepatikana lakini  katika harakati hiyo tumepoteza".

Wote walishtuka mama baraka alimtazama Hanys,
" Kwani nini kimetokea? "
Hansy alimshika mwanamama huyo mikono,
" Baraka ametutoka amepigwa Risasi".

Mwanamama huyo alibaki ameduwaa hata mwasifa moyo ulimdunda hakuamini yote hayo.
Bunti alijikuta anaanguka na kupoteza fahamu.
Haikuwa rahisi kwake hata baadhi wa wageni walikuwa bado hawajaondoka baada ya Harusi kuisha na sasa wamesikia taarifa hizo zenye maumivu ndani yake.

Baadhi ya wanafamilia walitoka na Kwenda mpaka hospital ya jeshi ambapo ulipelekwa mwili wa Baraka kujiridhisha ni kweli Ndipo Taratibu zilianza kufanyika.

Yalikuwa ni majonzi yasiyoelezeka kwa watu Wengi waliguswa sana na tukio hilo.

Siku ile Majira ya usiku Ndipo Vane alitoka hospital na moja kwa moja alikwenda nyumbani kwa kina baraka kuungana na Wanafamilia katika majonzi yale.
Mwasifa alikuwa zake ndani amevalishwa nguo  nyeusi kama mjane, Ndipo alifika Binti vane wakakumbatiana.
"Vane....vane Wangu mmewangu kaondoka mwenzio ahhhh".
Alilia sana Mwasifa huku vane akiwa hana la kusema Zaidi ya kulia kwa uchungu sana.

Siku iliyofuata baraka aliweza kuhifadhiwa katika makazi yake ya milele na kuacha majonzi kwa Familia na watu wote kiujumla.

Vane alibaki anajiona kama ni mwenye hatia,
"Nisamehe Mwasifa Mimi ndio Sababu ya haya yote naumia mimi".
"Hapana ni Mipango Ambayo hakuna mwanadamu wa kupangua.
Mmewangu amepoteza maisha Wakati anatumikia kazi yake aliyokula kiapo amekufa kishujaa akiwa amepata ushindi.
Kukutana kwetu mimi na baraka ni kwa Sababu yako pia sitasahau hilo.

Nilimueleza kuhusu wewe ndipo akanisaidiaga tukajuana kuanzia hapo. Kila kitu kina Sababu vane hatuna uwezo wa kupinga".
Aliongea Mwasifa hakika alikuwa ni Binti mwenye imani ya kukubali hali yoyote inayomkabili.

********

Upande wa Hemed nae siku hiyo majira ya usiku walikuwa msituni yeye na watu Wengine wanne jumla watano.
Walichimba shimo na kumstiri kenny.
Walipomaliza Ndipo Hemed alibaki akilia kwa uchungu Ambapo wenzake wale wengine walitawanyika na kutangulia Barabarani.

"Annn kenny... Nina uchungu moyoni mwangu.
Naumia sana sana sijui kama haya maumivu yatakuja kupoa hata iweje.
Nitalipa kisasi Cha maumivu kwa kila mtu wa Karibu wa vane bila shaka Ndio waliosababisha mpaka Kenny Wangu akaniacha.
Nitalipa kisasi na mpaka nchi hii itanitambua Hemed ni nani kwa matukio nitakayoyafanya".
Aliongea huku machozi yakimtoka Hemed hakika nae alipata pigo la namna yake.

*************

Basi Baada ya wiki moja kupita ndipo Siku hiyo vane alikuwa nyumbani kule kwa Mwasifa kaenda kumtembelea.

"Nimeogopa sana vane unavyosema kuwa yule hemed ndo alikuteka lakini hajakufanyia kitu chochote kibaya?"

"Acha tu Mwasifa hakufanikiwa kwani siku ile sikuwa sawa kama mwanamke ivyo alishindwa akawa amepania nikikaa sawa anifanyie icho kitendo"

" Basi kwa sasa umakini unahitajika kuwa makini Vane yasije kukukuta na wewe majonzi".

" Sawa".

Vane alikuwa alishinda hapo kwa Mwasifa  mpaka jioni Ndipo anarudi nyumbani kwao.

Bi Rose nae baada ya kusikia kuwa Binti yake alitekwa na vane Ndipo aliweka vijana wa kazi kuwatuma wahakikishe wanamtafuta Hemed. Kwaiyo hemed sasa alikuwa akiwindwa na Polisi pia kundi la watu wa bi Rose.

Siku hiyo ingine Ester alikwenda kule kwa mwasifa kwenda kumuona. Alimkuta Mwasifa akiwa amekaa zake ndani kama mfiwa wa Mumewe.

" Nitakuona mtu wa ajabu sana kama utaendelea kumuamini vane wakati ndo amesababisha mpaka umekuwa mjane alafu yeye anaponda raha.

Uhuni wake Ndio umemfikisha hadi kuanza kuwindwa akaja kukuponza wewe.
ingekuwa mimi ni wewe nisingekubali ningemchukulia mwanaume wake kama fidia".

Mwasifa Alishangaa kusikia vile,
" Ester unamaanisha nini? ".....

Sijui itakuwaje?
Tukutane sehemu ya 35*ME&YOU*

SEHEMU YA.... 35
Na
Mamuh Mohd
(0716730000)

Tulipoishia.....

ingekuwa mimi ni wewe nisingekubali ningemchukulia mwanaume wake kama fidia".

Mwasifa Alishangaa Kusikia vile,
" Ester unamaanisha nini? "...

SONGA NAYO....

" Kwa sasa huwezi kunielewa nachomaanisha  mwasifa lakini ipo siku utanielewa....haya kwa  heri nakwenda".

Ester aliamua kuondoka zake na kumuacha Mwasifa akiwa ameduwaa bado hakuelewa nini ambacho ester anamaanisha.

Ester alitoka mpaka nnje Kwenye gari lake.
Binti alipanda huku akijisemea,
" Nina kazi mbili kwanza kumtafuta huyu aliemteka Vane hakika ananifaa kabisa. Pili ni kumfanya Mwasifa Amchukie vane atake kulipa kisasi japo sitampa nafasi Hiyo maana nami nampenda sana Hansy siwezi kukubali achukuliwe ni mtego tu nataka kumtega".
Alijisemea Binti huyo kisha Ndipo akaamua kuingia kwenye gari lake na kuondoka.

*********

Basi Ester alikuwa Karibu sana na mwasifa kana kwamba kila mala alikuwa akienda kumtembelea na kumpa Maneno ya chuki dhidi ya vane.

Pia hapohapo Maneno ya chini chini kutokea familia ya Baraka yalianza wakimsema mwasifa kuwa amempa mkosi kijana wao ndio maana Kapoteza maisha.
Hali ile ilizidi kumuweka katika Wakati mgumu Sana mwasifa mpaka ilifika mahali akafukuzwa kabisa pale nyumbani kwa kina baraka.

Mwasifa hakuwa Na kimbilio Zaidi ya nyumbani kwa bi Rose Ndipo alipokelewa na kuanza  kuishi huko.

Vane alikuwa akiendelea kwenda dukani kwake kuendelea na biashara zake. Wakati huo Ester aliutumia kuwa nyumbani kuzungumza na Mwasifa ili amchukie vane.

Mwasifa hakuliafiki kabisa jambo lile. "Ester vane hausiki na chochote kuhusu Mmewangu amepoteza maisha akiwa katika kutekeleza majukumu yake sina cha kufanya Zaidi ta kukubaliana na hali tu".

Ester aliona mwasifa haelewi somo
Ndipo akaamua kuachana nae na
Kuondoka kabisa hapo nyumbani.

Sasa ile anatoka Ester nyuma kuna mtu
ambae alikuwa akimfuatilia pasina Binti
kujua.

Ester nae alikwenda siku hiyo katika
biashara zake kwani nae aliachana na
kazi za kuajiriwa na kubase katika
biashara zake.
Alipokuwa anashuka kwenye Gari Ndipo
mala alishtukia amepishana na mtu
Ambae amempulizia dawa puani mpaka
Binti akabaki hajielewi.

Ester alisimama Ndipo mtu yule aliepishana nae akamuambia njoo Binti akajikuta anamfuata yani ni kama alipumbazika.
Waliingia mpaka Kwenye Gari ndipo kufika Ester alipoteza fahamu na kuchukuliwa kwa namna ile.

Alipelekwa mpaka nyumbani kule anapoishi Kijana Hemed inamaana kumbe alikamatwa ma watu wa hemed Ndio leo waliagizwa kumteka bibie Ester.
Kufika Ndipo Ester aliteremshwa kwenye Gari na kuingizwa mpaka ndani.
Alimwagiwa maji ya baridi na Haraka akaamka.

Ester alianza kuangaza sehemu ile ambayo ilikuwa Ngeni kwake.
Alivuta kumbukumbu za yeye kufika pale hakujua Zaidi alikumbuka alikuwa anakwenda zake dukani kwake baada ya kushuka Kwenye Gari sasa hajui ilikuwaje.
"Nipo wapi hapa wewe nani kwanini umenikamata mimi?"
"Nyamaza nina hasira na familia yenu kuliko kitu Chochote kile.
Tumemuwinda vane mala mbili zote tukagundua analindwa kuna watu wanamfuatilia Ndipo nikaagiza ukamatwe wewe ndugu yake kupona kwako ni kunipa ushurikiano wa kupata nachotaka".

" Unataka nini? Kwanini unifanyie haya?"
" Nimeshakujibu kwa Sababu nimejua una ukaribu na Vane ni ndugu yako mnaishi Pamoja shida Yangu ni vane ameleta matatizo makubwa sana Kwangu.
Usiponipa ushirikiano nakuangamiza".
" inamaana ni wewe Ndie ulimteka kwa mala ya kwanza si Ndio? "
" Ndio na katika harakati za kuokolewa nikampoteza mtu Wangu wa muhimu sana roho inaniuma nashindwa kulipokea hili mpaka nilipe kisasi".

Ester kwanza alicheka sio kawaida.

" Kwanini unifanyie yote haya? Laiti ungejua sina hata upendo na huyo mtu ungenifuata nistaarabu sana tukazungumza.
Vane amemchukua mumewangu anataka kufunga nae ndoa namchukia sana nina kisa nae utakuwa umenisaidia".
" Muongo wewe unadhania nitakuamini kirahisi nikuache uondoke ukaniitie polisi?.
Ahhh wapi hutoki ivi ivi mpaka nijiaminishe.
Alafu sheria Yangu Mwanamke haingii ndani Kwangu pasina kutembea na mimi".

" Sema chochote utakacho nipo Tayari kukuhakikishia kuwa sina upendo na Vane na nipo Tayari chochote kibaya kimkute utakacho wewe fanya nipo Tayari".
Hemed Alishangaa aliona zali tena kwake kujipatia mrembo Ambae hana kizuizi kwa siku ile moja kukutana kimwili.

Basi walikwenda chumbani Na kufanya kitendo hicho hadi Ester alijisikia raha kabisa.
Baada ya pale Hemed aliingia bafuni kuoga ndipo Ester alibaki amekaa kitandani.

"Nimetoa utu Wangu yote Sababu ya chuki niliyokuwa nayo kwako Vane nimeunganisha chuki yenye Upendo kwa huyu kaka Basi hautapona Vane".
Basi baada ya hemed kutoka kuoga ndipo akarudi na kumtazama ester,

" Wanawake wa aina yako nimekutana nao Wengi sana.
Wanaojitambua na kujthamini ambao sio warahisi kama wewe.
Kiasi umchukie vane Sababu sio wa sawa yako.
Nimekuwa katika mahusiano na vane kwa Zaidi ya miezi miwili lakini hatujawahi kukutana si kwa Mapenzi yake hata wakati nikimuandalia mitego haikuwezekana.

Nina kisa nae kwa Sababu ya kumkosa pia ndio maana nina hasira".
Ester alichukia Kusikia vile,
" Unamaana gani? Unanichukulia poa? Sikiliza mimi ni msomi kuliko hata huyo vane ambae hajaenda shule na nimefanya kitu ambacho sijutii.
Katika maisha Yangu nimekosa upendo tu Ndio maana na usinichukulie mimi kama changudoa tafadhali".
" Ok  sasa nimekuamini naitwa Hemed"
" Nami naitwa Ester"
" Karibu".
" Karibu na wewe pia".

" Haya namtaka vane tunaanzia wapi? "
" ila isiwe kwa Mapenzi naomba umuangamize".

" Najua mimi cha kumfanya nitamtorosha na Kwenda nae mbali pasina yeye kujua hatokaa Arudi nchi hii kamwe.
Natumia madawa ya nnje ya nchi katika kazi Zangu Ndio maana nikimtega mtu rahisi kutegeka kama wewe ivi.
Kuna dawa ya kumfanya mtu apoteze fahamu zake licha ya kuwa anatembea yupo Macho kwa muda wa siku nzima.
inanitosha kabisa kumchukua vane na kusafiri nae na hatokaa Arudi sasa ni maamuzi Yangu nikamtupe huko au laa ila lazima nimfanyie kitu mpaka dunia isimame.
nataka ifanikiwe ikishindikana nitawaua ukoo wenu wote".

" Mhh kazi Ndogo sana hiyo nipe hiyo dawa hata Sasaivi na matumizi yake".

" Kwa sasa haipo mpaka nifanye mawasiliano na pesa pia iletwe".

" inagharimu kiasi gani? "

" Milioni 5".

" Pesa ndogo sana hiyo nitaitoa mimi"

" Kweli unamaanisha nakuamini Ester"

" Asante  lakini nikuombe kitu Wakati kazi yetu inaendelea Nitaomba uwe burudani Yangu ya siri nilimiss sana hii hali uliyonifanyia leo usinichukulie kama muhuni".

" Mhhh wakati wowote Ester unakaribishwa siwezi kufanya kazi na mwanaume pasina hii kazi Nyingine kuendelea kila ukija".

" Sawa niachie niondoke sasa".

" Ruhusa utapelekwa kuanzia pale ulipokutiwa kwanza nipate mawasilino yako".
Basi walibadilishana mawasiliano na kisha bibie Ester aliondoka zake.

Majira ya jioni vane alirudi nyumbani na Kwenda mpaka Chumbani kwa Mwasifa kwani bado hajamaliza eda Ivyo anakaa ndani.

"Rafiki Yangu Hansy amependekeza wiki hii niende nyumbani kwao Wazazi wake wakanikaribishe maana mwanzo hawakunipokea ndoa imekaribia".

Mwasifa alinyamaza kimya alijikuta nae anatamani mumewake anvekuwepo,

"Sawa nendeni bahati yako ila si kila kitu uje kuniambia vane mengine endeleeni tu naona kama unaniumiza moyo".
Vane alijisikia Vibaya hakutegemea kama mwasifa angemjibu vile.

"Basi nisamehe nimefanya kosa kukuambia yaishe".
Vane aliamua Kuondoka zake chumbani humo na mwasifa alibaki akilia sana.

Aliyakumbuka Maneno ya Ester aliyokuwa akimuambia mala kwa mala kuwa asikubali atafute furaha, vane kasababisha mpaka mumewe apoteze maisha na sasa anakula bata tu".
Maneno yale yalimuumiza yalijirudia kichwani kwa Mwasifa.

Alikumbuka pia jinsi ukweni kwake walivyomfukuza kuwa amemuua kijana wao ana mkosi.
Binti ndo Alizidi kuumia.

" Furaha nitaitoa wapi mimi? Wenzangu wana furaha mimi ni kilio tu.
Kweli Ester ulivyosema wameniharibia ya kwangu kwao yanawaendea tu.
Wema Wangu unaniponza mimi sikubali".
Alilia kwa Sauti Mwasifa haikujulikana anamaanisha nini kutokana na Maneno yale...

Sijui itakuwaje?
Tukutane sehemu ya 36*Me&You*

Sehemu ya... 36
Na
Mamuh Mohd
(0716730000)

Tuliposhia.....

Kweli Ester ulivyosema wameniharibia ya kwangu kwao yanawaendea tu.
Wema Wangu umeniponza mimi sikubali.
Alilia kwa Sauti Mwasifa haikujulikana anamaanisha nini kutoka na na Maneno yale....

SONGA NAYO....

Mwasifa alikosa raha siku ile Ndipo Ester aliporudi nae akaenda kumuona mwasifa chumbani kwake.

"Vipi upo sawa mwasifa za tokea nimekuacha?"

"Salama tu sijui wewe huko utokako?"

"Nzuri pia haya nilikuwa nakusalimia tu haya nakwenda chumbani Kwangu kupumzika".

Ester wakati anatoka Ndipo Mwasifa akamuita.

"Ester njoo mala moja nikwambie jambo".

"Mhhh jambo gani?"

"Najikuta moyo unaniuma sana mwenzio hata sielewi.

Vane amekuja kuniambia hapa kuwa kesho anakwenda nyumbani kwa kina hansy kutambulishwa kwa mala nyingine tena najikuta naumia na mimi"

" Mhhh nilikwambia Mwasifa japo uliniona mimi mbaya lakini najua uchungu wake.

Bila Vane kutafuta balaa huko mumeo angekuwepo unafurahia ndoa yako.

Angalia sasa wakwe zako wanakuita Vibaya bado mume umekosa huku mwenzako anavinjari kwa raha zake.

Kazi ya Vane ni kuharibia wenzake maisha.

Aliniambia ananiachia Hansy kutokana na hali yake kiko wapi?  Chunguza utagundua ni mbinafsi.

Shauri yako".

Ester alipomaliza kuzungumza hayo akaondoka zake na kumuacha Mwasifa akiwa analia kupita kiasi.

Siku iliyofuata Majira ya mchana Vane alikwishajiandaa Tayari kwa Kwenda ukweni kwa mala nyingine tena kutambulishwa.
Alitoka chumbani kwake na kutaka kwenda katika chumba cha mwasifa lakini alipofika mlangoni akasita.
Alikumbuka jana mwasifa alivyoonesha kutokuchangamka kabisa.
Alisita akaona aache kwanza kwani akienda kumuambia ataona tena kama anamkosea.

Kumbe Wakati huo mwasifa nae alikuwa amekaa akitazama dirishani akipunga hewa.
Punde Ndipo akamuona Vane akufunguliwa mlango wa gari na dereva akiingia na kuondoka.
Mwasifa Machozi yalimtoka,
"Una furaha sasa lakini Kwangu ni kilio.
Sina bibi wala sina mwanaume wa maisha Yangu nimeambulia kubaki mjane.
Huwazi hata jana kukuambia vile umeamua kushuhulika na yako vane.
Nimepambana sana na kujitoa kwa ajili yako, lakini wewe haujawahi kujitoa kwa ajili Yangu.

Basi inatosha sijazaliwa kuwa mtu wa kuwatafutia watu furaha nami kuambulia Maumivu napambania nami sasa niwe na furaha".
Aliyasema hayo mwasifa huku akilia sana ni wazi alidhihirisha maumivu makubwa sana moyoni mwake.

Nyumbani kwa Wazazi wa Hansy siku hiyo walijiandaa na kumpokea Vane rasmi kama mwanamke aliechaguliwa na kijana wao.
Pingamizi zote walizokuwa nazo juu yake siku hiyo waliziweka kando na kuruhusu rasmi kama ni ndoa basi wafunge wazazi wapo Tayari.

Walikubaliana kuwa Ester alishajifungua mtoto atatuzwa na baadae atalelewa na vane kama ndie mama yake.

Vane alifurahi sana kwa mapokezi yake alijihisi furaha isiyoelezeka.
Hansy nae hakusita kumvalisha Pete mbele ya wazazi wake kuashiria sasa ajiandae Wakati wowote atamuoa.

Walikula chakula kwa Pamoja pale na kufurahi mpaka Usiku Ndipo bibie Vane alirudi zake nyumbani ikiwa hansy mwenyewe ndie aliemrudisha kuhakikisha usalama wa mpenzi wake huyo.

Siku kadhaa zilipita ambapo mwasifa hakutaka kuzungumza chochote na Vane kila Wakati vane alimfuata chumbani lakini hakuonesha kutaka kuzungumza nae kabisa.

Vane alipoona hali ile imezidi ilibidi amfuate mama yake na kumuelezea.
"Mhhh kweli hata mimi namuona mwasifa amebadilika lakini sio yeye bali ni matatizo aliyopitia.
Ujue amepitia matatizo makubwa sana kiasi asiwe sawa nadhani tumpe muda sawa"
" Sawa mama lakini sio Kwangu mimi mwasifa namfahamu vizuri sawa huwenda hayupo sawa lakini sio Kwangu mimi".

" Basi hii hali ni nzito mwanangu ebu wacha mawazo unaelekea kufunga ndoa sasa usiwaze sana mwanangu usije ukakonda gaoni la harusi likakosa kukupendeza".

" Mhhh basi mama wewe zungumza nae hii harusi Yangu bila mwasifa sioni hata raha yake zungumza nae mama".

" Sawa usijali mamaeeeh".

Basi walikubaliana walau vane alipata afuheni  ya moyo.

Majira ya usiku siku hiyo Ester alikuwa zake amekaa nnje akipunga upepo.

Mala alitoka bibie vane akiwa ameshika Karatasi na kumuambia Ester,

"Huu ni ujumbe wako Kutoka kwa hansy unatakiwa kuusoma na kujibu mahali ambapo panafaa kujibiwa".
"Na kwanini amekutuma wewe unileteee kama nani?"
"Kama mkewake mtarajiwa na mama wa mwanae ajae".
"Mhhh sahau Vane eti mwanangu kuja kulelewa na wewe tena sahau. Umeamua kumchukua baba mtoto its okay nakuwa single mama ila usitegemee mwanangu akuite wewe mama never".
"Sijamchukua bali amekukataa ni mimi ndie nilianza kwa hansy wewe ukaniingilia na bado hata nilipomuacha hakukubali wewe hakutaki.

Kama mwanao atamuita hansy baba basi nami ni mama yake soma yaliyomo katika Karatasi hiyo na ujibu".

Ester alikunjua barua ile akaisoma na kisha akaichana chana.
"Hansy nimelala nae na tulipeana mahaba mpaka yakajibu sio wa kunitumia ujumbe kupitia wewe kikaragosi akinitaka baby mama wake atanitafuta Kama anakudanganya kwa njia hii amka usingizini utajikojolea my dear".
Alifyonza Ester kisha akamuacha vane amesimama hapo na kuondoka zake.

Vane alibaki akimtazama tu wala hakushtuka kwani anajua hayo yote lazima yatatokea kubwa sasa wameamua kusimamia upendo wao.

Basi siku iliyofuata Hansy alimfuata Ester dukani kwake akiwa na jazba kwelikweli.
"Wewe nimekuletea  mkataba usome ujue sheria zako umekataa si Ndio? Ok nakuambia kuwa umevunja mawasiliano baina yetu.
Nahesabu umebakia miezi 4 ujifungue sasa huduma zote ni vane ndie atakuwa akiwasilisha sio mimi na usipotaka pia basi".

"Hansy nimeshakubali bola iwe basi nitalea mwanangu wewe kaa na mwanamke"
"Sawa sawa".
Hansy aliondoka zake na Wakati huo Ester alionekana Kabisa kuwa  na kitumbo kama kiasi kama mjamzito japo haikujulikana ni kweli mjamzito au kuna namna gani imetokea.

Mwezi mmoja ulipita Ambapo Mipango ya harusi ilikamilika.
Mwanamama bi Rose alimuandalia Binti yake  kitchen part cha hadhi.

Basi siku hiyo ilikuwa Ndio siku ya Kitchen part.

Vane alikuwa zake saloon akiandaliwa lakini hakuwa sawa kabisa alikuwa alimuwaza mwasifa tu.
Hakuwa na maelewano. Mazuri na Rafiki yake huyo.

Vane aliamua kushika simu na kumuandikia ujumbe mwasifa wenye Maneno mazuri kuonesha jinsi gani hana furaha alimuomba hata kama hawezi kwenda ukumbuni kutokana na Hali yake ya eda  lakini  walau ampe baraka zake.

Mwasifa alijibu ujumbe ule akaandika, "Kipo kitu cha kunipa furaha vane ukinipatia icho kitu basi nitaamini nawe unaweza kujitoa kwa ajili Yangu".

Vane kuona sms ile akapiga kabisa maana aliona kama sms zinachelewa kwenda.
"Mwasifa niambie kitu gani nitakupa na kama sina nitakununulia mwasifa Wangu nataka  uwe na furaha".
"Usijali nenda Shuhuli ukirudi tutazungumza".
Kisha mwasifa akakata simu.

Kweli Shuhuli ilikwenda  vizuri Ambapo Binti Vane alifundwa akafundika zawadi zilimiminika kwa ajili yake na Kwenda nazo kwa mume wake.
Lakini Wakati wote huo Vane alikuwa anatamani shuhuli iishe akazungumze na mwasifa ili akae sawa.

Kufikia saa 7 usiku kweli walimaliza shuhuli na kurudi nyumbani.
Watu walifikia kupumzika lakini Vane alipomaliza kuoga akaenda Chumbani kwa Mwasifa akiwa na shuka kabisa kwa maana walale wote.

Alimkuta Mwasifa amekaa tu hana hata lepe la usingizi.
"Macho yako yanaonesha hauna Usingizi kweli Kuna kitu nipo Tayari niambie nikufanyie nini utakuwa sawa? "
Mwasifa machozi yalimtoka Ndipo akamtazama Vane na kumjibu,
" Hicho kinachokupa Furaha wewe ndicho nami nakitaka bila shaka kitanipa furaha nipatie".

Vane alibaki ameduwaa ni kama alibaki njia panda.
" Sijakuelewa unamaanisha nini? Usiniongelee kwa mafumbo tafadhali niambie".
" Mumewangu ameniacha kwa Sababu yako nataka mume nipatie hansy awe mumewangu Ndipo walau litapoa jeraha la moyo Wangu".

Vane alishtuka mpaka mwili ulimsisimka hakutegemea kama angeambiwa jambo kama lile.....

Sijui itakuwaje?
Tukutane sehemu ya
37*ME&YOU*37_41

SEHEMU YA.... 37
Na
Mamuh mohd
(0716730000)

Tuliposhia......

"Mumewangu ameniacha kwa Sababu yako nataka mume nipatie hansy awe mumewangu Ndipo walau litapoa jeraha la moyo Wangu".

Vane alishtuka mpaka mwili ulimsisimka hakutegemea kama angeambiwa jambo kama lile...

SONGA NAYO.....

"Mwasifa unasema nini? Unajisikiliza kweli? Hansy ni mchumba Wangu wewe ni shemeji yako unawezaje kusema eti nikupe nakupaje labda kwa mfano"

" Wewe ndio chanzo mpaka Mumewangu akaniacha mjane.

Ulishakosea tokea zamani kukutana na huyo  hemed ukaleta mkosi wako mpaka mmewangu hayupo.

Unataka nikae nachekelea kukuona wewe mnaishi vizuri na hansy umefanyiwa kitchenparty unaolewa hongera kwa kuharibu maisha Yangu na kutengeneza maisha yako.

Vane mimi nimejitoa sana katika maisha yako wakati umeharibika macho nilipambana mpaka hansy akajua ulipo na akaja kukusaidia.
Huyu hemed wako nimepambana mpaka umebaki mzima hajakuambukiza Chochote lakini wewe hujawahi kujitoa kwa Sababu Yangu.
Kwa sasa Ndipo nitaamini kuwa wewe ni mtu mwema au mbaya kwa hili nililokuambia.
Fanya juu chini Hansy anioe Mimi naitaka ndoa Yangu laa sivyo nitakuwa adui yako milele nitakuhesabu kama mtu ulieharibu furaha Yangu".

Vane pozi lilimuisha.

Alibaki ameduwaa hata hakujua aseme nini taratibu aliondoka chumbani humo na kuelekea chumbani kwake.

Kufika aliangua kilio jamani alilia kwa hisia aliumia sio kawaida.

Wakati huo Mwasifa nae alibaki analia chumbani kwake Ndipo aliingia bibie Ester.
Ester alikuwa akicheka huku anapiga makofi.

"Safi sana umefanya kama nilichokuambia mwasifa".
Mwasifa kumtazama Ester Ndipo akakumbuka ilivyokuwa ni kwamba,

Majira ya asubuhi siku hiyo mwasifa alikuwa zake chumbani kwake analia sana Ndipo ester aliingia na kumkuta.
"Unalia nini shoga badala  ufurahi leo shoga ako anafanyiwa kitchenparty?"
" Nina maumivu makubwa sana moyoni mwangu.
Anaingia katika ndoa ikiwa mimi hata sijaifaidi.
Vane hajali kuhusu mimi kabisa hataki kuzungumza na mimihanijali"

" Mhh mimi mbona nafahamu hili tokea siku nyingi kwamba vane ni mbinafsi anajiangalia yeye tu.

Mhhh usikubali sawa hansy alinikataa mimi lakini huwenda wewe akakukubali muambie vane akupe hansy akuoe kama fidia kwa mume wako aliemtoa kafara huyo vane ili apone yeye".

" Naanzaje jamani Kumuambia ivyo Vane na hansy atalipokeaje hili? "

" Vane akiamua kila kitu kinawezekana wee muambie kumpima tu ndo utakapoona tabia halisi ya Vane mimi nakwambia  fanya ivyo".

Mwasifa alijikuta anakubali na hivyo ndivyo ilivyokuwa.

Basi Ester alisogea na kukaa kitandani kwa Mwasifa,

" Nimewasikia wakati mnazungumza nimemuona vane katoka ana hasira nilijibanza sehemu ila nakwambia hawezi kukubali huyu ni mbinafsi sana".

" Nimeamini lakini  namaanisha Ester namtaka mmewangu naitaka ndoa Yangu hakika nimechanganyikiwa mimi".

" Nakuelewa sana Tena sana simamia huo msimamo wako Nipo Upande wako Sababu hata Mimi ni muathirika wa huyu vane lala zako kwa sasa tutaongea kesho".

Ester Ndipo alitoka nae chumbani humo na kumuacha Mwasifa peke yake.

Basi no ilikwenda mpaka Asubuhi Ndipo vane kuamka tu Alikwenda Tena kuonana na mwasifa.

" Nina uhakika umebadili hayo Maamuzi yako ya ajabu bila shaka".

" Maamuzi Yangu ni Yale yale kupona kwako kumefanya mumewangu aangamie sitakubali muambie hansy anioe kama fidia".

" Sikiliza mwasifa hilo pepo chafu likuondoke  huwenda kweli nikawa nina hatia kwako lakini si malipo ya kukupa mchumba Wangu unadhania hata Hansy akiyasikia haya maneno atasemaje iwe mwanzo na Mwisho usije ukarudia haya maneno mwasifa kwa sasa nitajifanya kama sijasikia ulichosema jana".

" Usinifokee vane nilichokisema nimemaanisha na kama haiwezekani basi sawa Asante ondoka mbele ya macho yangu".
" Sawa lakini Hicho unachokitaka hakitawezekana ni Afadhali unifanye utakavyo Mimi kupooza hasira zako ila sio kumtaka Hansy".
Alimaliza kwa kuzungumza hayo Vane Kisha akatoka nnje ya chumba Icho.

Mwasifa alishika simu yake akampigia Ester ambae kwa Wakati huo alikuwa dukani kwake.
Alimuelezea kila kitu kilichotokea Ndipo kuna jambo Ester alimtaka mwasifa afanye.

Zilipita kama nusu Saa vane akiwa chumbani kwake Ndipo akasikia akiitwa kwa nguvu na mama yake.
Vane alishtuka Ndipo haraka akainuka na kutoka mpaka Sebleni.
Kufika alimkuta mama yake amemshika mkono mwasifa ambae amebeba nguo zake akisema anataka kuondoka.

"Vane njoo zungumza na mwenzako mbona gafla jamani anaondoka huku analia imekuwaje kwani umemkera au?"
"Hapana mama sijamfanya chochote Mwasifa mimi".
Alijibu Vane huku nae alimsogelea mwasifa.
"Kwanini lakini umedilika kiasi hiki kosa letu sisi ni lipi?.

Tafadhali naomba usiondoke Jiji hili utakwenda Wapi?".
" Siwezi vane mimi ni mtu wa kuteseka wacha nikateseke wewe ponda raha zako".
Mwasifa alikuwa mkali kabisa mwishowe akaondoka zake.

Vane mpaka machozi yalimtoka wakati huo mama yake amebaki njia panda hajui Sababu ya mwasifa Kuondoka gafla ni ipi.
Vane hakutaka kumueleza mama yake maana ni jambo zito kwa mtu yoyote atakaelisikia.

Mwasifa alikwenda mpaka sehemu ambayo alipewa Maelekezo Ndipo akakutana na ester ambae alimpeleka katika hotelini Fulani.
"Nimelipia hapa utakaa hapa kwa Muda Wakati napanga nyumba utakayokaa kuwa na amani mwasifa".
"Asante sana Ester kiukweli wewe una moyo wake wa huruma nashukuru sana".
"Usijali nipo na wewe bega kwa bega nafuatilia nyumba nipange utaishi wala usiwe na wasiwasi.

Kwa yote hayo mwasifa alikubali na kubakia hotelini pale.

Baada ya wiki moja kweli ester alipanga nyumba na mwasifa akahamia kuishi huko.
Mala kwa mala Ester alikuwa akienda kumtembelea mwasifa na kuzidi kumpandikiza chuki ili amchukie vane.
Mwasifa kweli Alizidi kukasirika na Tokea pale alimchukulia Vane kama mbinafsi na chanzo cha kumpoteza mumewake.

Basi Siku hiyo Ester alikwenda nyumbani kule alipo mwasifa akiwa na Hemed.
Mwasifa kumuona hemed Alishangaa sana,
"Ester huyu umetoka nae wapi?"

"Usijali huyu ni rafiki Yangu yani ni mwenzetu.
Bado siku moja kufikia ndoa ya vane na hansy tunatakiwa kuiharibu  sisi watu watatu.
Wewe sasa upo upande Wangu fuata Maelekezo mwasifa.
Wewe ulikuwa Karibu Zaidi na vane kuna dawa tunahitaji ale leo ili apumbazike umlete huku aondoke hatokaa aonane na hansy.
Jifanye kama umesahau yaliyopita na umerudi kusherehekea nae harusi tufanye hii kazi.
Nimechunguza pale nyumbani hajamuambia mtu yoyote uliyomuambia basi katufanyie hiyo kazi mwasifa tutakuwa tunakuelekeza kila kitu".

Kwa kuwa wakati huo Mwasifa kiasi Fulani alikuwa ameshakunja moyo dhidi ya vane alijikuta anakubali kuungana na ester na Hemed akasahau unyama wote wa watu wale kila mmoja kwa nafasi yake.

Ester kusikia  vile alipiga  makofi na kutoa nguo Ambazo kazitengeneza huwa anaweka tumboni.

Mwasifa kuona nguo zile alishtuka inamaana kaijua siri kuwa Ester hana ujazito.

"Ester hauna mimba kumbe?"

"Ndio nimekuonesha kwa kuwa wewe sasa ni mwenzangu sasa kazi kwako ukitoa hii siri sitakuacha salama mwasifa kwa sasa tufanye kazi".
Mwasifa alitikisa kichwa kukubali maana mpaka alijawa na uwoga  Tena gafla na kubaki na hamaki kugundua jambo lile...

Sijui itakuwaje?
Tukutane sehemu ya 38*ME&YOU*

SEHEMU YA.... 38
Na
Mamuh Mohd
(0716730000)

Tuliposhia.....

Mwasifa alitikisa kichwa kukubali maana mpaka alijawa na uwoga Tena gafla na kubaki na hamaki kugundua jambo lile....

SONGA NAYO......

Mwasifa alikabidhiwa  dawa ambayo anatakiwa kuhakikisha anampatia  Vane Mapema sana na kumtorosha kutoka nyumbani mpaka kwa kina Ester.
Dawa ambayo iligharamiwa kutokea nnje ya nchi kabisa kwa ajili ya kazi hiyo maalum.

Mwasifa alikumbuka kweli jinsi alivyotoka mbali na Vane tokea wakiwa Vijakazi wa ndani na urafiki wao ulizidi kukuwa hata baada ya kutoka nyumbani kwa Kina Hansy.
Kitu ambacho kilimkwaza*ME&YOU*

SEHEMU YA.... 39
Na
Mamuh Mohd
(0716730000)

Tuliposhia.....

Ester ndo akifanya amepewa ramani kumbe anajua kila kitu ila kaamua kumlipua mwasifa...

SONGA NAYO....

Baada ya muda mfupi kufika walifika mpaka nyumbani kwa kule ambapo Ester alifahamu kuwa amemuacha mwasifa akibakia pale.
Kufika tu kwanza wakalikuta gari la Vane ushahidi Tosha kama kweli vane amepelekwa pale.
Waligonga mlango Ndipo Mwasifa kuangalia dirishani ni watu wale Hansy, mama vane, mapolisi pamoja na watu wengine.
"Nasema Nini Mimi uhhhh sielewi sielewi"
Binti alishtuka mwisho uwoga ulimzidi akaamua kwenda kufungua Mlango.

Mwasifa alikuwa anatetemeka mpaka aliona aibu akainama chini na kujifunika usoni.
Hansy ndo akawa wa kwanza kunsogeje,
"Mwasifa Nini kimetokea niambie Vane ampetwa na Nini yupo wapi? Usiogope niambie nini kimetokea".
Hansy kwa Haraka haraka yeye alidhania kwamba huwenda mwasifa alikuja pale na vane na kuna tatizo labda limetokea hawakujua bado kama ni  Mwasifa Ndie aliefanya tukio  hilo.

Binti mwasifa alikuwa  analia tu mpaka ikabidi watu waingie ndani kwenda kukagua huwenda vane yupo ndani Kuna tukio limetokea au laa.

Walitafuta sehemu zote vane hakuonekana.
Polisi walimzungumza mwasifa kumuhoji lakini Binti kwanza aliishia kulia tu Ndipo alichukuliwa na polisi kwa ajili ya kwenda kutoa maelezo wapi vane alipo.
Hansy alilitazama gari la Vane lilikuwa wazi kabisa funguo zilikuwa mlangoni hazijatolewa.
ilibidi Hansy apande lile Gari kulirudi nalo kituoni Cha polisi kama ushahidi waliokuta.

Walipofika kituoni. Mwasifa alifunguwa ndani na kupewa kibano aseme wapo vane alipo.

Mwasifa alipigwa ndio Ndipo akaamua kusimulia  ukweli wote ulivyokuwa na watu alioshirikiana nao.

Alieleza yote kuwa Vane ameondoka na Hemed hajasema walikwenda wapi ila wameenda sehemu ya mbali sana.

Ester nae alikuwa hatiani  japo alimchoma Mwasifa akamatwe lakini na yeye pia alikuwa hatiani kwani mwasifa aliongea ukweli wote mpaka kuhusu Ester kuwa hana ujauzito yote aliyaongea.

Ester hakuwa na hiyana alikubali kufungwa pingu  Ndipo kabla hajapelekwa ndani akawaambia watu wote,

"Huu Kwangu ni ushindi najua Hansy hanipendi na wala Hawezi kunipenda Tena lakini walau tumekosa wote yeye na mimi hakuna atakaekuwa na Hansy.

Nina amani na kama nastahili kufungwa nifungwe tu lakini na nyie hamtakaa kumpata vane hamtajia ni wapi amepelekwa abadani hasirani".

Ester aliingia nae ndani pamoja na mwasifa na kumuacha mwanamama bi Rose akiwa analia sana alihisi huwenda yeye Ndie chanzo.

Alijilaumu maisha aliyomlea Ester ya kuwa na mambo ya kijambazi kuwateka watu ndio yaliyopelekea nae Leo kamfanyia njama hizo Vane.
Alijiwazia kama Laiti nae angemlea Ester maisha ya kuwa Binti mwema basi asingefikilia kabisa kumfanyia mwenzake ubaya yote yale alijilaumu ni makosa yake.
Alilia sana mwanamama huyo lakini hakuwa na WA kumbembeleza mwenzake kwani kila mtu alikuwa na maumivu kwa upande wake.

Hapakuwa na matumaini ya kumpata vane mpaka ilibidi taarifa zisambae katika  Viombo vya habari lakini pia Hapakuwa na matumaini.

Hansy mpaka alikonda aliona sasa basi Vane sio fungu lake kwa Sababu kila Wakati wanapokuwa sawa basi lazima litokee tatizo na kuwatenganisha.

Siku hiyo majira ya usiku akiwa chumbani kwake alikuwa na madawa mengi sana ameamua liwalo na liwe. "Basi nimekubali matokeo Vane wewe sio fungu Langu huwenda tumepangiwa kuwa wote maisha baada ya haya ya sasa wacha basi tukutane huko. Hansy wako nitakuwa nakusubiri wewe...umepelekwa mbali haijulikani ni wapi ningepajua haijalishi ni wapi ningekufuata.

Basi inatosha nashindwa kuendelea kuhimili haya maumivu ya kukuwaza siku zote sijui ni mzima au laa.
Sina ujasiri wa kuja kupokea habari Mbaya juu yao siwezi siwezi...basi Nakubali matokeo haya".

Aliongea Hansy Ndipo akashika madawa yale pembeni kukiwa na Kinywaji bia Kali ndo aliamua kutumia hayo kama maji ya kusukumia hizo dawa.

Alikunywa Hansy pasina kujihurumia aliamua liwalo na liwe kuliko maumivu anayopitia kwa sasa.

Wakati huo alikuwepo  Erick chumbani kwake nae Ndipo kuna taarifa alitumiwa mtandaoni zilimshtua kwelikweli.
Erick aliinuka haraka na Kukimbia mpaka Chumbani kwa kaka yake amuoneshe habari zile lakini kufika hakuamini alichokikuta.

Erick alipiga kelele na kutoka mbio kwenda kuwagongea wazazi wao.
Wote waliamka na kuwahi kukuta hali halisi Hansy akiwa anaangalia juu huku mapovu yanamtoka mdomoni.

Haraka walimbeba mpaka nnje eneo la packing wakaingia kwenye Gari Safari ni speed kuelekea hospital huku mama Hansy akiwa analia sio kawaida.

Walifika  katika Hospital ya private Ambayo ilikuwa Karibu na kwao Ndipo Hansy alipokelewa Tayari kwa uchunguzi.
Hakuna alieweza kuzungumza chochote kila mmoja alibaki kimya amepigwa na bumbuwazi hawajui Nini kinafuata.

Baada ya kama dakika 10 Ndipo alitoka daktari na kuwafuata Wanafamilia.
Aliwatazama Ndipo akamuambia,
"Hali yake ni Mbaya sana tumempatia huduma ya kwanza lakini naona bado Tumeita ambulance inakuja awahishwe hospital ya Taifa".

Erick alitikisa kichwa hadi machozi sasa yalianza kumtoka Ndipo akarudi kuwapa Habari zile wazazi wake.

Walikubali na kusubiri pale mpaka ambulance ilipofika wakamuhamisha Tena Hansy kuelekea sasa hospital kubwa.

Huko walifanikiwa kufika na Hansy alipatiwa Matibabu Ndipo mpaka panakucha Asubuhi walau walifanikiwa kumtoa sumu aliyokuwa nayo lakini hali yake haikuwa nzuri alikuwa wodi ya ICU kwa uangalizi wa Karibu Zaidi.

Baada ya siku ile kupita Ndipo waliambiwa kuwa Mbali na simu Mgonjwa anakabiliwa na Msongo wa mawazo ambao umeathiri afya yake ivyo hata akipona Kuna hati hati akawa sio mzima kiakili.

Erick aliwaita Wazazi wake baada ya taarifa hizo na kuwaambia,
" Nami nilikuwa natangaza upotevu wa Vane sehemu mbalimbali na ile jana Usiku Kuna mtu aliniambia amemuona Kuna rafiki Yangu anakaa kisiwani kasema amemuona naombeni niende Vane pekee ndie wakumuweka kaka katika hali nzuri tusije kumpoteza niombeeni awe ni yeye kweli".

Wazazi wa Hansy hawakuwa na hiyana walikubaliana Erick Kumbe hata taarifa aliyokuwa anataka kumpa kaka yake ni kuhusu kupewa taarifa za kuonekana kwa vane kisiwani Ndipo akakuta Hansy ameshakunywa sumu.

Erick aliwasiliana Tena na rafiki yake huyo na kuanza Safari Kwenda kuangalia kama ni yeye vane au laa...

Siijui itakuwaje?
Tukutane sehemu ya 40*ME&YOU*

SEHEMU YA.... 40
Na
Mamuh mohd

(0716730000)

Tulipoishia.....

Erick aliwasiliana Tena na rafiki yake huyo kuanza safari Kwenda kuangalia kama ni yeye vane au laa..

SONGA NAYO......

Palikuwa ni kisiwani ambapo palichukua masaa takriban 10 kufika.
Erick alifika ikiwa ni usiku sana kiasi saa 9.

Aliposhuka alimkuta huyo rafiki yake Ambae Ndie anawasiliana nae alikuja kumpokea na wakaelekea sasa mpaka nyumbani Ambapo Hapakuwa mbali sana na pale feli.

"Kaka Yangu ana hali Mbaya sana anampenda sana huyu mwanamke Yani Leo usalama Wake ni kurudi na Huyu msichana nahisi huwenda kaka Yangu walau atapona".
" Nimemuona Haishi mbali na hapa lakini anaishi na mtu wake Ndio maana hata sikuamini uliponiambia unamtafuta imekuwa kama bahati tu nami huku nimemuona".

Erick alifurahi kusikia vile akaona afadhali hakutaka hata kulala aliamua tu kukaa zake huku akiisubiri pakuche.

Kweli palikwenda mpaka Asubuhi Ndipo safari ilianza Erick akiwa na huyo Rafiki yake alieitwa Emmanuel.
Walifika katika nyumba moja Ndipo Emmanuel akamuomeshea Erick.
" Ni pale Ndipo anakaa huyo Msichana sasa sijui utafika vipi au unakwenda kusemaje  lakini Ndio pale mimi mpaka naogopa".
" Asante sana Usijali  nitakwenda wewe nisubiri hapa".
Erick alikwenda mpaka katika nyumba ile na kugonga mlango kwanza palikuwa kimya.

Baada ya muda Ndipo mlango ulifunguliwa na alikuwa si mwingine ni Hemed.

Hemed alimtazama Erick na kumuuliza,
" Wewe ni nani? Mbona huendani na watu wa kisiwa hiki bila shaka haukai hapa?"
" Ndio nimetoka Daresalam nimefuata Vane umempeleka wapi Vane? ".
Hemed alimtazama Erick na kisha akamjibu,
" Sawa Karibu ingia ndani".
Erick alipoingia tu mala alishtukia amepigwa na kitu kizito kichwani mpaka akaanguka.

Vane alikuwa zake katika chumba kimoja Ndipo akashtuka kusikia Kuna mtu kama amepiga kelele.
Binti aliinuka na kutoka Nia aangalie Kuna nini Ndipo akamkuta ni Hemed anamburuza Erick ameahamzimisha.

"Haaa!!! kwanini Hemed kwanini unadhuru watu wasiokuwa na hatia nimeshakwambia kama ni unataka kuniangamiza niangamize sio watu wasiokuwa na hatia".
" Ameyataka yeye amekuja anakuulizia ametokea Daresalam bila shaka ametumwa sasa atataja  wenzake aliokuja nao na watashuhudia nafunga ndoa na wewe"

" Siwezi kufunga ndoa na wewe Hemed nifanye utakavyo".
Hemed akampeleka Erick katika chumba kimoja wapo Ndani hapo na kumfungia.

Vane alibaki anajiuliza Erick amekujaje hapo? Na vipi kama atakuwa na Hansy anakuja pia.
"Hansy wangu sijui wamekuja wote huyu anaweza kuwauwa jamani siwezi kukubali Leo lazima nifanye kitu Kuwalinda wengine wacha kama kuniangamiza aniangamize Mimi ila sio watu wasiokuwa na hatia".
Vane aliamua kwenda kuchukua kisu na kupiga kelele mpaka Hemed akaenda sehemu ile aliyokuwepo.

" Leo namaliza hizi shida zote Hemed. Hautaki kuniangamiza bali unataka kunitesa wacha nijimalize Mimi mwenyewe nitajimaliza Mimi mwenyewe".
Vane alijiwekea kisu katika mkono wake mahali ambapo akipakata damu Nyingi zitatoka hatochukua muda mrefu kupoteza Maisha.

Hemed Alishangaa Binti aliemteka Ndani akiwa dhaifu Leo kaonesha ujasiri na yote kwa kuwa vane alihisi huwenda na kina Hansy wanakuja sasa hakutaka kuona Hemed anakutana na Hansy akijua amempania atamuangamiza.

Hakujua kumbe kwa Wakati huo Hansy hali yake ni Mbaya sana anapambania maisha yake.

Vane alipiga kelele hakuamini Akimtazama Hemed damu zinamtoka Shingoni Ndipo alipiga kelele kuomba msaada huku akiweweseka.

Hadin Erick alipata kuzinduka kwa kelele zile za Vane akaamka na kusukuma Mlango Ndipo Vane akamfungulia.

Erick  alitoka na kukuta hali halisi lakini akimtazama Vane alikuwa mzima tu.

Watu walianza kugonga Mlangoni kelele zile za Vane ziliwaita watu kujaa walihisi kwamba huwenda pana tatizo.

Erick akajua ile ni kesi Ndipo akamuita vane katika chumba kingine na kumuambia,
"Hii ni kesi na sijui kitatokea watu wameshajaa lazima nikabiliane nalo ili wewe uwahi nyumbani hali ya kaka Hansy ni mbaya sana.
Kaa utulie nitawafungulia mlango watajua Mimi ndie muhusika watanipa tuhuma tukitoa na wewe chukua akiba hii ya pesa Anza Safari Rudi Daresalam hospital ya Taifa kaka Hansy hali yake ni Mbaya kwa ajili yako vane.

Utawaleza wazazi Wangu kilichotokea najua baba atakuja watanisaidia ila kwa sasa wewe Urudi Daresalam".

"Vane alikuwa akilia Binti aliangua kilio Ndipo Erick akamtaka azibe mdomo asisikie kisha akaenda kufungua Mlango liwalo na liwe kumpa Nafasi vane arudi nyumbani.

Kweli watu walikuta damu zimeenea Ndipo wakaanza kelele,
"Muuaji... Muuaji huyo muuaji....".
Erick aliingia hatiani Kwa kuituwa polisi wa eneo lile na kuubeba mwili wa Hemed ambae alikuwa Tayari ameshapoteza maisha.

Wakati huo vane alikuwa amejificha na bahati chumba alichokuwepo hakuna aliekwenda kukagua ivyo ikawa salama kwake Ndipo akatoka na Kukimbia huku Binti akiwa analia sio Kawaida.

Safari ilianza kuelekea feliz na bahati alikuta meli Ndogo ikiwa inapatia abiria Kutoka kisiwani hapo kuelekea jijini Daresalam.
Binti alilipa nauli pesa ambazo alipatiwa na Erick na kukaa sasa Safari kuelekea Daresalam kwanza akajue hali ya Hansy inaendeleaaje na pia kutoa Taarifa Kwa kile kilichompata Erick.

Walianza Safari ikiwa ni Jioni mchana kiasi saa8  na walilifika majira ya saa5 Usiku.
Usiku huo Vane alikodi usafiri Hapakuwa mbali sana pale Bandarini waliposhushiwa mpaka Hospital ya Taifa Uzuri mjini pale watu Bado waliokuwa macho ivyo hakupata shida Bibie.

Kufika eneo la packing ya magari alikuta Magari mengi yamejipanga lakini kama bahati aliliona gari la mama yake Bi Rose Hilo Ndo lilikuwa jepesi kwake kulitambua japo yalikuwa pamoja na magari ya Wazazi wa Hansy.

Vane alipigwa sasa na bumbuwazi hakujua aelekee wapi, hospital ni kubwa aliwaza pengine aombe simu kwa walinzi wa pale eneo la packing ampigie mama yake maana ameshapata uhakika kuwa yupo pale kwa kuliona gari lake.

Kweli Binti akili ilimchemka akaenda mpaka kwa mlinzi mmoja wapo na kumsalimia,
"Habari yako kaka... Samahani naomba niazime simu nimpigie mama Yangu nijue alipo ndani ya Hospital hii"
"Kwanza muda huu Mbona hakuna mtu yoyote anaeruhusiwa kuingia ndani labda wenye dharura maalum.

Hawa wenyewe waliopack magari haya wamekuja dharura nahisi pengine mgonjwa wao amepoteza maisha wamekuja kuhakiki kumuhifadhi laa sivyo haruhusiwi mtu kuingia".

Vane Alishtuka kwa jibu lile Mpaka kigugumizi kilimshika Binti.
" ila usijali simu hii hapa mpigie dakika moja".
Mlinzi yule alitoa simu lakini Vane akajikuta hadi anakuwa kuoga hakuwa Tayari kusikia kitu chochote kibaya dhidi ya Hansy wake.

Vane Alichukua simu ile na kuweka namba ya Mama yake Kisha akaiweka Sijioni ikawa inaita tu.

Baada ya muda mfupi Ndipo ikapokelewa akasikia Sauti ya watu wakiwa wanalia hata mama yake alipokea huku akionekana kuwa analia.

"Haloo nani mwenzangu?"
"Mama Mimi vane nipo hapa  hospital"
" Vane mwanangu uko sehemu gani nakuja mwanangu niambie uko sehemu gani"
" Nipo hapa lilipo gari lako lakini Nini kimetokea mama Yangu naogopa sana".
Bi Rose alikata simu Ndipo haraka akawahi eneo la nnje kweli lilipo gari lake na kumkuta mwanae.

Kwanza alimkumbatia na kuangua kilio,

" Mwanangu jamani siamini umerudi mwanangu ulikuwa wapi mama ahhhh"
" Mama Mimi nipo mzima Niambie usiku huu mpo hapa Nini kimetokea mama Yangu? "
" Tumepoteza naomba ujikaze vane Wangu kuwa jasiri"
" Mama .. mama... Mama hansy amepatwa na nini mama ahhhh"...

Vane aliangua kilio pale uso wa mama yake ulieleza kabisa kuwa Kuna tatizo limetokea...

Sijui itakuwaje?
Tukutane kuhitimisha....*ME&YOU* (41)

Na

Mamuh mohd
(0716730000)

Tulipoishia....

Vane aliangua kilio pale uso wa mama yake ulieleza kabisa kuwa kuna tatizo limetokea...

SONGA NAYO....

Walikuwa wakilia pale wote wawili mama na Binti yake ndipo bi Rose akawa analia huku analalamika.
"Ester Wangu jamani, nilishakusamehe kwa yote yaliyotokea kwanini lakini umeamua kufanya haya ahhhh Ester wangu jamani Mimi naumia".

Vane alishangaa ndipo akamtazama mama yake.

"Mama unamaanisha nini mama Ester... Ester".
Bi rose alishindwa hata aongee Nini Zaidi aliishia tu kulia nguvu za kuzungumza zilimuisha.

Mala walitoka wazazi wa Hansy Ndipo wakamkuta vane akiwa nnje anazungumza na mama yake.

Mama hansy alimsogele vane na kumkumbatia.
"Vane mwanangu jamani ahhh ulikuwa wapi jamani.

Japo tuna huzuni Ester ametutoka lakini Kupata wewe imekuwa afuheni mwanangu njoo njoo".
Mama hansy alimshika  Mkono vane na Kwenda nae mpaka wodini kule alipolazwa Hansy.

Alimkuta nurse wa wodi hiyo Ndipo akamuuliza mama hansy,
" Mmerudi Tena? Lakini ilibidi mje kesho?"
" Huyu Ndie Vane ambae mwanangu alikuwa akimuimba kuwa anamtaka vane naomba  umruhusu".
Hata nurse alimtazama Vane na kumuambia,

" Kama wewe ndie Vane basi ingia pengine unaweza kuwa msaada kwa mgonjwa huyu Ambae kuamka kwake ni kutaja jina lako".
Kweli vane aliingia wodini kule na kumkuta Hansy wake amelala huku anahema kwa Mipira.

Binti alimshika Hansy wake katika paji la uso na kumbusu.
" Amka Hansy... Amka mume Wangu najua haukuwa sawa ilibaki kidogo tu niwe mkeo.. nipo hapa tafadhali amka tufunge ndoa".

Binti Machozi yalimtoka akamshika Hansy mkononi ambapo aliamini Atapata ishara kuwa ni yeye hata mama hansy aliambiwa atoke nnje kwa maana alibakia  vane amemshika mkono Hansy mpaka aamke.

Kweli mpaka palipambazuka Hansy aliamka na kufumbua macho yake ndipo akamuona Vane yupo Pembeni yake akiwa  amejiinamia nae kapitiwa na usingizi.

"Vane... Vane".
Aliita Hansy Ndipo vane aliamka na kumtazama Hansy wake.
"Hansy Hansy wangu uko mzima?"
"Ulikuwa wapi vane mzima na wewe?"

"Hakika Mimi ni mzima nipo hapa amka Hansy".
Hansy alipata afuheni kabisa akataka hadi kutoa mpira ule uliowekwa puani mwake Ndipo vane akamuita nurse haraka akafika na kumtazama Hansy maendeleo yake.

Wakati huo waliokuwepo wazazi wa Hansy na bi Rose eneo la nnje wakipanga.
Baba Hansy akamtaka bi Rose Arudi nyumbani kwani watu wameshakusanyika taarifa imesambaa kuwa ester amepoteza Maisha.

Wakiwa wanajadili Ndipo mala wakamuona Vane anatoka akiwa anamsukuma Hansy aliekuwa kwenye kiti wanaonekana kucheka na kufurahi.

Wote walishagaa hawakuamini kwa muujiza ule.
Wazazi waliwapokea kwa furaha wazazi wa Hansy hawakuamini kabisa.

Alitoka na daktari wa Hansy na kuwaambia,
"Aisee tunapaswa kumshukuru Mungu kwa muujiza aliotutendea Hansy wa jana na wale ni tofauti kabisa.

Ameonekana hajambo Kabisa ni furaha kwetu kwa hakika.... Dawa imepatikana kwake tunajiridhisha tu kama ni kweli ametengamaa atakuwepo hapa kwa Leo pia".
Wazazi walikubali Ndipo daktari akawaacha wanazungumza.

Vane sasa Ndipo akamsogelea mama yake aliekuwa Amelia mpaka macho yamekuwa mekundu.
Binti alitaka kujua imetokea Nini Ndipo akahadithiwa kuwa Ester amejiua.
"Sikutaka mwanangu aende jela nilimsamehe kabisa na kuwatoa kwa gharama yeye na mwasifa.

Lakini wakiwa njiani wanarudi Ester aliamua kufungua Mlango wa Gari na kutoka Wakati gari linatembea ameanguka vibaya amepoteza maisha". Zilikuwa taarifa zenye kusikitisha kwao hata Hansy alizipokea kwa masikitiko taarifa zile.

Basi hiyo ndio hali ambayo ilitokea kwamba bi Rose aliamua kuwasamehe Ester kwa kuwa ni mwanae pia pamoja na mwasifa aliamini wameshapata fundisho.

Alitumia gharama kuhakikisha wanakuwa huru lakini siku ambayo walitoka wakiwa njiani Ester aliteremka kwenye Gari likiwa bado linakwenda hali iliyopelekea kuanguka vibaya na kupoteza maisha.

Taratibu za mazishi zilipangwa na siku iliyofuata Ester alihifadhiwa na kuacha majonzi kwa watu.

Mwasifa aliekuwepo nyumbani pale kwa bi Rose Ndipo baada ya kwenda kumuhifadhi Ester nae aliamua kwenda kumuangukia vane kuomba msamaha.

"Nisamehe Vane halikuwa kusudio Langu ibilisi alinichanganya.

Niliteleza kama mwanadamu tafadhali nakuomba Vane.
Ester hayupo tena tukiwa kwenye gari alijiona hafai Tena nilipomuambia kuwa Hemed alikuwa nimuathirika alijiona ameshaangamia ndio Sababu nisamehe vane".
"Naelewa  mwasifa haukuwahi kuwa mbaya Wangu ni ibilisi kama ulivyosema.
Sina kinyongo na wewe Wala Ester namuombea apumzike salama.
Wanaadamu tunakosea na tunahitaji nafasi ya kusahihisha makosa yetu sisi wote yameisha mwasifa Wangu".
Basi walikumbatiana pale hata Mwasifa alijihisi amani moyoni.

" Vipi Hemed hajakudhuru? "
" Nashukuru hajanifanyia chochote alichokuwa anataka ni ndoa kwanza. Nilipambana pia Nashukuru nimetoka salama mikono mwake".
" Amiin tuswali kushukuru Mungu vane Wangu".
" Ni kweli".
Basi walifurahi wenyewe.

Vane alipoona baba yake Hansy amerudi Kutoka malaloni kumuhifadhi Ester Ndipo nae alimfuata na kuzungumza nae.
Alipata kumuelezea kile ambacho kimemkuta Erick.

"ohhh Vane kwanini haukuniambia mapema mwanangu? Nami ndo nilikuwa nataka kukuuliza Erick alikufuata amebakia wapi? "
"Nilighafirika baba kwa matatizo niliyoyakuta juu ya Ester".
"Sawa nitakwenda Leo ngoja tujiandae utanipa Maelekezo vizuri mpaka ile sehemu aliyokamatwa watakuwa wanafahamu alipopelekwa".
Kweli baba Hansy muda uleule alianza kushuhulikia jambo lile la kijana wake Erick.

*********

Baada ya miezi mitatu kupita Ndipo Hansy alipona Kabisa na kuruhusiwa kurudi nyumbani pia Erick alikuwa huru baba yake alifanikiwa kushirikiana na wanasheria wake Erick akawa huru na Kurudi nae Nyumbani kwao.

*******

Basi siku hiyo majira ya Asubuhi bibie Vane aliamka na kulitazama gaoni lake la harusi Ambalo lilikuwepo chumbani hapo.
Binti alitabasamu na punde aliingia mama yake bi Rose.
"Haya mpambaji amekuja oga haraka wanakuja kuoa saa4 Asubuhi hii mkwe Wangu shauku yake ni akuoe ndoto zake zitimie"

"Mama hata mimi ndio ndoto Zangu tumetoka Mbali na kupitia Mengi sana".
"Haya kaoge Haraka tunaendelea tulipoishia kipindi kile".
Kweli vane alikwenda kuoga haraka na kisha akanywa chai na kukaa Tayari kwa kuandaliwa.

Kufikia majira ya saa 4 na nusu Asubuhi waowaji walifika akiwa ni Hansy amevaa sare sare na Mdogo wake Erick Pamoja na rafiki yake amon.
Yupo baba yake na watu Ambao waliongozana nao.

Walipokelewa mpaka ukumbini kwani Hapakuwa na watu Wengi sana Asubuhi ile kwenye ndoa.

Hansy alikaa na kutulia Ndipo ndoa ilianza kufungwa.

"Hansy makuka nakuozesha Vane Mzota kwa Mahari ya makubaliano. Awe mke wako katika nyakati zote za maisha je umekubali kumuoa?"
"Nimekubali"
"Nimekuozesha"
"Nani nimemuoa".
Palifurika shangwe na vigelegele na pasina kupoteza muda Hansy alielekea sehemu ambayo alikaa mkewe bibie Vane akiwa amependeza kwelikweli. Alifungua mtandio wake na kumkumbatia, huku akimbusu hatimae wamekuwa wana ndoa.

Shuhuli ile ilifana kuanzia pale nyumbani na mpaka Jioni ilienda ukumbini huko Ndipo watu Wengi waalikwa walikuwepo kusheherekea nao kwa Pamoja.

Siku ile iligeuka na kuingia siku nyingine majira ya saa8 usiku Ndipo maharusi walikwenda nyumbani kwao.
Hansy alitimiza azma yake ya mkewe afikie katika nyumba aliyoijenga na kweli yalitimia.

Usiku ule haukuwa wa kulala kwao bali ni story mahaba wakikumbuka mbali walipotoka.

"Leo umekuwa mkewangu vane Sina zawadi kubwa kwako Zaidi ya kukuahidi upendo wa dhati katika maisha Yangu yote.
Tuanze maisha yetu kwa furaha tuwe wachamungu, tuwe na upendo kwetu sisi hata wa wageni wetu.
Pia tuwe wazazi bora Kwa watoto tutakaobarikiwa".
"Asante sana Hansy nami naahidi kukupenda mumewangu.
Dua zisirudi nyuma... Alafu leo ukumbini umemuona Amon alikuwa Karibu sana na Mwasifa".
" Haaa!! Nina Habari zao Amon Kuna kitu kaniambia sema sio Wakati wake kwa Sasa kazime taa mkewangu Leo ni ME&YOU"

Vane aliinuka huku wakiwa wanafurahi mpaka Binti akahisi aibu.

*******

Maisha yao mapya ya ndoa yalitawaliwa na upendo na amani. Baada ya Mwaka mmoja walibahatika Mtoto wao wa kwanza wa kiume.

Upande wa Amon nae baada ya mwaka mmoja alituma ombi kwa Mwasifa Kutaka kumuona kwani alikuwa akimpenda siku nyingi na sasa aliona wakati muafaka.

Nae mwasifa hakuwa na hiyana alikubali.

********

Alhamdulilah..Naam nimefikia tamati wa simulizi hii.
Nawashukuru nyoote wapenzi tuliokuwa pamoja mwanzo mpaka Leo tamati.

Mazuri tuyachukue penye mapungufu tusameheane.

Huwa siwaachi ivi ivi mwisho wa simulizi hii basi ni kwanzo wa Simulizi nzuri inayokwenda kwa jina la SULINA.

SI YA KUKOSA SHUKRAN MINGU AWABARIKI TUKUTANE WAKATI MWINGINE.

❤️❤️❤️

MWISHO.